

30 APRILI, 2013

30 April, df 01

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Tano - Tarehe 30 Aprili, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Randama za Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria
kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 120

Kijiji cha Kitopeni Kukosa Huduma za Kijamii

MHE. ZAYNAB M. VULLU aliuliza:-

Kijiji cha Kitopeni kilichopata hadhi ya Kijiji mwaka 2010
katika Jimbo la Bagamoyo kimeshajenga Ofisi kwa michango
ya wananchi, lakini kimekosa huduma muhimu za jamii:-

30 APRILI, 2013

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea wananchi wa Kitopeni huduma muhimu za jamii zikiwemo shule ya awali, shule ya msingi, zahanati na barabara za uhakika zinazounganisha vitongoji vyake?

(b) Je, ni lini Serikali itawajengea Zahanati wananchi wa Kijiji Kongwe cha Buma, Kata ya Kiromo ili kuwaondolea adha ya ukosefu wa huduma hiyo wananchi hao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kijiji cha Kitopeni kilianzishwa mwaka 2010 na kinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa huduma muhimu zikiwemo shule, zahanati na barabara. Miradi ya ujenzi wa zahanati na shule katika Kijiji kwa sehemu kubwa huibuliwa na wananchi wenyewe na kwa mantiki hiyo asilimia kubwa ya gharama za utekelezaji wa miradi iliyoibuliwa na wananchi zinatokana na wananchi wenyewe. Halmashauri huchangia kiasi kidogo kwenye miradi hiyo hasa kwenye ununuzi vifaa kama saruji, mabati, mbao, nondo na kutoa ushauri wa kitalaam na kusimamia ubora wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Serikali iliidhinisha shilingi milioni 39.4 kwa ajili ya matengenezi ya barabara ya Mataya - Kitopeni, yenye urefu wa kilomita 4.5.

Aidha, katika mwaka 2013/2014 Serikali imeidhinisha shilingi milioni 277.5 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa kiwango cha changarawe ambapo shilingi milioni 35 zitatumika kutengeneza barabara za Kitopeni.

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za shule na zahanati, wakazi wa Kijiji hiki wanapata huduma hizo kutoka katika kijiji mama cha Kiromo ambacho kiko umbali wa kilomita mbili na nusu(2.5km) kutoka Kijiji cha Kitopeni. Hata hivyo, Serikali inawashauri wananchi wa Kitopeni kuweka katika mipango yao ujenzi wa Zahanati na shule kwa kuzingatia mpango wa fursa na vikwazo katika Maendeleo. Serikali iko tayari kushirikiana nao katika ujenzi wa miundombinu hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kongo kina shule moja ya msingi na Zahanati moja. Kijiji cha Buma hakina zahanati na wananchi wa kijiji hiki hupata huduma za afya katika kijiji cha Kiromo kilichoko umbali wa kilomita 7. Serikali inawapongeza wanakijiji wa Buma ambao wamekwisha fyatua tofali na kutenga eneo la ujenzi wa zahanati katika kijiji hicho. Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imeshauriwa kuangalia upya vipaumbele vyake ili kuhakikisha kijiji cha Kitopeni kinapatiwa huduma muhimu za kijamii.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kabla sijauliza maswali hayo napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Kijiji cha Kiromo kwa juhudi zao za kushirikiana na kutaka kujiletea maendeleo.

Swali la kwanza. Kwa kuwa majibu ya msingi yameeleza kwamba wananchi wenyewe wanatakiwa waibue miradi wanayoitaka ikiwemo hiyo hospitali na Zahanati, wananchi wa kijiji cha Kiromo kutokana na adha wanayoipata ya watoto wao kutembea zaidi ya kilomita tano kwenda na kurudi kwa ajili ya kwenda shule, wameamua kutenga eneo la hekari saba kwa ajili ya ujenzi wa shule wameshafyatua tofali elfu tatu.

Je, Serikali iko tayari kuwasaidia katika kujenga hiyo shule?

Swali la pili; kwa kuwa huduma ya zahanati pia wanaipata kutoka kijiji jirani, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wananchi hawa wanaopenda maendeleo na wanajitolea wenyewe kuanza kuwajengea zahanati?(*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza sisi tunashukuru kwa sababu tatizo la ardhi pia nalo ni kubwa na sasa kama anasema eneo limepatikana na kwamba wananchi wenyewe wameonesha hizo jitihada za kufyatua matofali kwa ajili ya kazi hii.

Mimi nadhani kubwa hapa tutakachofanya ni kuwasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kuzungumza nao kwa sababu sasa wananchi wameshajitoa kiasi hicho ili tuweze kuona jinsi ambavyo itakuwa inajitokeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili ambalo linahusu zahanati ambayo wanatumia huduma ya jirani. Kwa msimamo wetu sasa hivi wa kiserikali ni kwamba pale ambapo inaonekana vijiji viko karibu wanaweza wakachangia katika huduma hiyo pale katika kijiji hicho.

Lakini natambua kwamba Mheshimiwa Vullu anafuatilia sana kwa karibu haya matatizo na huenda ikawa kuna wananchi wengi ambao wanatakiwa kwenda mbali zaidi.

Kwa kifupi tunachoweza kusema hapa ni kwamba sisi tutafuatilia hii mipango, hili jambo ni lazima lizungumzwe katika *Ward Development Committee* na wao wenyewe waoneshe kwamba kweli kuna haja ya kufanya hivyo, halafu tutasaidiana nao kuhakikisha kwamba wanapata zahanati katika kijiji hiki. (*Makofi*)

MHE. MWIGULU L. M. MADELU: Mheshimiwa Spika ahsante sana. Maeneo mengi sana hapa nchini ambayo wananchi wamejitolea, wamejenga madarasa, wamejenga zahanati na maeneo mengine wanafunzi wanasafiri umbali

30 APRILI, 2013

mrefu kwenda shuleni na majengo yote yameshakamilishwa isipokuwa yanakosa walimu kwa upande wa madarasa na yanakosa wataalam wa afya kwa upande wa huduma za afya.

Je, Serikali sasa itakuwa tayari kutoa tamko kwamaba itatoa vipaumbele kwa majengo ya aina hiyo ili na watu wangu wa Igugulya na Ipuma waweze kupata walimu kwa sababu tayari walishajenga madarasa?

SPIKA: Ahsante sana, umeliuliza vizuri, Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa kifupi ushauri huu anaoutoa Mbunge ni ushauri mzuri, kwa hiyo tutazingatia ushauri wake. *(Makofi)*

Na. 121

Tangazo la Mipaka-Ukonga

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA aliuliza:-

Hii ni mara ya tatu nasimama Bungeni kwa tatizo la mipaka kati ya Nzasa Msitu wa Kazimzumbwi, Kitunda na ardhi ya Jimbo la Ukonga:-

(a) Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kwenda kuonyesha mipaka ili kuondoa migogoro?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua migogoro ya ardhi katika Kata za Msongola, Pugu, Chanika, Kivule na Majohe?

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eugen Elishiringa Mwaiposa, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwa na tatizo la migogoro ya Ardhi kati ya Kata ya Nzasa, Msitu wa Kazimzumbwi, Kitunda na ardhi ya Jimbo la Ukonga.

Mgogoro katika Kata ya Nzasa unatokana na mwingiliano wa mipaka kati ya Kata ya Nzasa na eneo la Msitu wa Kazimzumbwi ulioko Wilaya ya Kisarawe. Katika hatua za kutatua mgogoro huu, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Manispaa ya Ilala na Wilaya ya Kisarawe waunde timu ya uchunguzi wa mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, timu iliyoundwa imekamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa Serikalini. Serikali baada ya kupitia taarifa hiyo ya Tume inakusudia kutoa uamuzi kuhusu mipaka ya eneo la hifadhi ya msitu huo na eneo la makazi ya wakazi wa Kata ya Nzasa.

(b) Mheshimiwa Spika, mgogoro uliopo kati ya Kata ya Pugu na Kata ya Chanika unatokana na Kata ya Pugu kujenga shule ya msingi ya Viweje ndani ya mipaka ya Kata ya Chanika. Hii ni kufuatia uchunguzi uliofanywa na wataalam wa ardhi pamoja na Madiwani wa Kata za Pugu na Chanika. Hitaji la Kata ya Pugu ni Serikali kuwajengea shule nyingine ili kuondoa utata uliopo.

Ili kuondokana na utata huo Halmashauri ya Manispaa ya Ilala katika bajeti ya mwaka 2013/2014 imeweka kipaumbele na kutenga shilingi milioni 280 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba kumi vya madarasa, kati ya fedha hizo shilingi milioni 70 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa shule ya Msingi

30 APRILI, 2013

Pugu Kajiungeni ili kuondoa utata huo ambao nimeutamka hapo juu.

Mheshimiwa Spika, mgogoro mwingine ni kati ya wakazi wa Kata ya Kivule na Umoja wa Vijana wa Kikristo Tanzania (UVIKIUTA) ambao unatokana na wakazi wa Kata ya Kivule kuvamia eneo la shamba linalomilikuwa na UVIKIUTA. Mgogoro huu uko katika ngazi ya mamalaka ya mahakama ambapo wakazi wa eneo la Kivule baada ya kutoelewana na umoja huo kwenye shamba hilo walifungua kesi katika Mahakama Kuu ya Ardhi. Kwa kuwa suala hili linaendeshwa na muhimili wa kisheria, Serikali inawashauri walalamikaji wasubiri ili tuweze kupata maamuzi ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, ipo migogoro ya mara kwa mara katika Kata za Pugu, Chanika, Kivule na Majohe, inayotokana na uvamizi wa maeneo unaofanywa na makundi ya watu kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam. Serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ilala imetoa maelekezo kuhakikisha uvamizi huo unadhibitiwa. Aidha, wananchi wametakiwa kuheshimu sheria za ardhi zilizopo ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na jitihada nzuri ambazo zimefanywa na Serikali katika kutatua tatizo la mpaka kati ya msitu wa Kazimzumbwi na wananchi wa Nzasa na kwa kuwa, mpaka sasa hivi imebakia tu kutoa uamuzi.

Je, Serikali sasa inaweza ikanihakikishia kwamba sitasimama tena mbele ya Bunge hili kwa mara ya nne kuzungumzia jambo hilo? Nikimaanisha kwamba uamuzi huo utatoka mapema ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za kiuchumi badala ya kuendelea kuishi kwa wasiwasi?

Swali la pili; kwa kuwa, migogoro mingi imechangiwa sana na Watendaji wa Kata pamoja na Watendaji wa Mitaa. Lakini pia wenyeviti wa Serikali za Mitaa pamoja na Kata wakiwa wasimamizi wa maeneo hayo wanakuwa wanauza maeneo hayo ya watu lakini saa nyingine wanakuwa pia ni mashahidi wa kuuza maeneo ya wananchi bila ridhaa yao.

Je, Serikali sasa inatoa tamko gani kwa watendaji ambao siyo waaminifu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mbunge kwamba ameona jitihada za Serikali. Jambo hili tumelifuatilia kwa karibu sana, tumekwenda nalo na wadau mbalimbali wamekwenda pale na *version* mbalimbali zimetolewa pale.

Matumaini yangu yeye hataki tena asimame hapa ndani, matumaini yangu ni kwamba anachofanya Waziri Mkuu akipata ripoti kama hii ni lazima arudi kwenye *field* akaangalie uhalisia wa jambo lenyewe, aangalie wanasema nini kwa sababu unaweza ukatoa tamko pale na tamko la Waziri Mkuu ni tamko la Serikali. Namwomba tu kwamba tuna hakika kwa hapa tulipofika sasa huenda hatatakiwa tena kurudi hapa na kuanza kuuliza swali hili kwa sababu mgogoro utakuwa umekwisha na tamko la Serikali litakapokuwa limetolewa pale sisi tutasimamia kuhaikisha kwamba linatekelezwa kama lilivyosemwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ambalo ndilo tatizo kubwa zaidi ni hili la Watendaji wanaozungumzwa hapa. Mimi siwezi kusimama hapa nikasema si kweli. Hapa na pale baadhi ya Watendaji wetu wamehusika katika jambo hili. Tamko la Serikali ni nini? Ni kwamba mtu wa namna hii anakwenda pale anachukua *open space* ambayo watoto wanatakiwa kwenda akubembea halafu anagawa na kuuza lile eneo ni kufukuzilia mbali. Unakaa naye wa nini huyu kwa maana ndiyo anatuletea haya matatizo yote yanayozungumzwa hapa.

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, hili litizameni midomo yangu na macho yangu, Mtendaji wa Kata au Mtendaji wa Kijiji au wa Mtaa amekwenda amegawa eneo linajulikana ni kwa ajili ya shule ya msingi au kwa ajili ya zahanati anagawa, baada ya hapo likifika kwetu sisi na Waziri yupo hapa tunamwondoa tu, hatufai hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri Mkuu kwa sababu hili ni tatizo kubwa, Watendaji wetu wengine baadhi yao wameingia katika hali hii, tutachukua hatua. *We shall never leave any stone unturned*, mtu ametoa kiwanja hapa anajua hiyo ni *open space* tutashughulika naye. (*Makofi*)

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Spika ahsante. Kwa kuwa hili tatizo la migogoro limekuwa likituathiri sana sisi watu wa Mkoa wa Pwani, mimi hasa wa Kisarawe na Kaka yangu pale Malima maeneo ya Mkuranga, lakini kwa mgogoro huu naishukuru Serikali kwa sababu imefanya kazi kubwa sana, lakini kwa bahati mbaya mpaka juzi watu wa Ilala wameingia Kisarawe katika maeneo ya Maguruwe na kilichobakia sasa hivi ni ofisi ya Waziri Mkuu kuja kule tukatathmini kwa pamoja kuonesha kwamba kwa mujibu wa makubaliano tuliyofanya na timu kubwa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, naomba kujua ni lini sasa timu ile itakuja Kisarawe tuungane na wenzetu wa Wilaya ya Ilala kwenda ku-*identify* ile mipaka ili tuweze kumaliza huu mgogoro?

SPIKA: Hilo ni swali lingine, lakini Waziri jibu tu kama unalifahamu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) Mheshimiwa Spika, mimi naomba tu tupate nafasi kidogo. Nitakwenda kukaa na Mheshimiwa Jafo ili niweze kujua jambo hilo. Kama lipo *connected* na hili ambalo limeulizwa au kama lipo nje ya hapo. Kama nilivyosema matatizo haya ni mengi sana.

30 APRILI, 2013

Kwanza utatuzi wake unaanzia kule kwenye Halmashauri zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, migogoro mingine ambayo umeisikia hapa ni migogoro kati ya Kata moja na nyingine ambazo zipo katika Halmashauri hiyo hiyo. Kwa hiyo, nitakaa na Mheshimiwa Jafo ili anielimishe vizuri kuhusu tatizo hili halafu baadaye sisi tutachukua hatua kama atakavyokuwa ametushauri.

SPIKA: Ahsante sana, yeye ameuliza swali jipya kabisa. Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Mfugo na Uvuvi.

Na. 122

Ruzuku kwa Sekta ya Mifugo.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY (K.n.y. MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI) aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya pembejeo kwenye sekta ya kilimo tu na kuacha sekta ya ufugaji na uvuvi ambayo nayo inachangia pato la Taifa la nchi yetu;

Je, ni lini Serikali itaanza kutoa ruzuku kwa wafugaji na wavuvi ili kuendesha shughuli zao za kila siku kwa ufanisi mkubwa zaidi kama inavyofanya kwenye sekta ya kilimo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, Mbunge wa Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku katika sekta ya mifugo na uvuvi kama ifanyavyo katika sekta ya kilimo.

30 APRILI, 2013

Katika Sekta ya mifugo Serikali kupitia Mipango ya mendeleo ya *PADEP* na *DADPS*, imetoa ruzuku kwa ujenzi na ukarabati wa majosho 1,278 kwa gharama ya Tshs. 14,822,310,970/=.

Aidha, ruzuku imetolewa ya lita 99,505 ya dawa ya kuogesha mifugo katika mikoa 21 dawa zilizogharimu Tsh.15,315,893,584/=. Kutoka mwaka 2000/2001 – 2012/2013 Serikali imetoa ruzuku ya kununua dawa za chanjo dhidi ya homa ya mapafu ya ng'ombe, dozi milioni 47,825,800 zenye thamani ya shilingi 4,698,469,283/= zilizotumika kuchanja jumla ya ng'ombe 36,790,517 katika mikoa 17.

Pia dozi 6,566,666 za chanjo ya Bonde la Ufa zilizotolewa kwa ng'ombe 2,868,068, mbuzi 1453,103 na kondoo 570,862 katika mikoa 11 dozi zilizogharimu Tsh. 4,119,999,600/=.

Mheshimiwa Spika, Serikali, pia imetoa ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa minada 10 ya mipakani na minada 12 ya upili, pamoja na mabanda ya ngozi na viwanda vya maziwa pamoja na machinjio, ikiwemo ile ya Sakina na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Uvuvi, kuanzia mwaka 2007/2008 Serikali, imefuta kodi ya ongezeko la thamani kwenye nyavu, injini za maboti ya uvuvi za kupachika, nyuzi za kushonea nyavu na vifungashio.

Aidha, chini ya makubaliano ya soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki, ushuru wa malighafi zinazotumika kutengeneza zana za uvuvi zinazonunuliwa kutoka nje ya eneo la Afrika Mashariki, hizi zimekuwa zinapewa punguzo la kodi 5%.

Mheshimiwa Spika, injini za uvuvi na malighafi za kutengenezea zana mbalimbali za uvuvi na viambatanisho vyake, vimefutwa kodi kabisa na kodi yake imekuwa ni *zero rating*.

Aidha, Serikali, kupitia mradi wa usimamizi wa mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani – *Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP)*, pia imewawezesha wavuvi jumla ya 3,827,176,793/= kutekeleza miradi 240 ya ujasiriamali ikiwemo ununuzi wa zana za kisasa za uvuvi na kunufaisha jumla ya wananchi 4,000.

Vilevile jumla ya shilingi milioni 339 na senti 35 zilitolewa kwa wananchi 198 kutoka hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia na wananchi 436 kutoka hifadhi ya Ghuba ya Mnazi na maingilio ya Mto Ruvuma, kutekeleza mpango wa kubadilishana zana haribifu kwa zana zinazoruhusiwa Kisheria. (*Makofi*)

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, wafugaji wengi wanshindwa kununua dawa za mifugo kwa sababu, ya bei iliyo juu inayosababishwa na kodi. Serikali, ina mpango gani wa kupunguza kodi hiyo, ili wafugaji wengi waweze kununua madawa na kufuga mifugo bora?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, minada mingi, barabara za kuendea ni za lami na hakuna *cattle routes*. Serikali, ina mpango gani wa kuagiza Serikali za Mitaa za Halmashauri, ili kutengeneza *cattle routes* kwa kusaidiana na *TANROADS*?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Akunaay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna baadhi ya madawa ambayo yamepewa ruzuku na kodi imepunguzwa na Wakala kadhaa wamechaguliwa.

Mikoa imehusishwa katika kuwachagua Wakala watakaosambaza baadhi ya dawa hizi. Lakini tunaelewa kwamba, kiasi kilichopunguzwa hakitoshi na bado kwa ujumla gharama ya dawa za mifugo bado ipo juu.

30 APRILI, 2013

Lakini hili tunalifanyia kazi kuhakikisha kwamba, dawa zitakuwa zinapatikana kwa bei wanayoimudu wafugaji, ili waweze kumaliza tatizo la magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la minada, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, *stock routes* nyingi ama zimezibwa na maendeleo ya miundombinu ama na kilimo ama matumizi mengine ya ardhi.

Katika *frame work* ile ya matumizi bora ya ardhi na mipango yake, maelekezo yapo kwamba, moja kati ya vitu muhimu katika *zoning* ni kuhakikisha kwamba, kila Kijiji, kila Wilaya na kila Mkoa, unajiwekea taratibu za kutenga maeneo ya makazi, maeneo ya huduma, maeneo ya kilimo maeneo ya ufuigaji, maeneo ya hifadhi, lakini kubwa pia kati ya haya ni kuhakikisha kwamba, *stock routes* zote zinafunguliwa kuhakikisha kwamba, mifugo inaweza ikafikia maeneo ama ya maji, ama ya chumvi, ama ya malisho pamoja na minada. *(Makoff)*

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, ni vigezo gani vinatumiwa na Wizara, kugawa hizi dawa za pembejeo na hasa dips? Ni vigezo vya wingi wa mifugo katika Mikoa au inatolewa tu *flat rate* kwa ajili ya Mikoa yote?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanining'o Kaika Telele, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika; tuna takwimu za mifugo katika maeneo yote Tanzania, maana katika Sekretarieti ya kila Mkoa na katika kila Wilaya, ama katika kila Halmashauri, tunao watu wetu wanaotuongalia takwimu. Na wanatuongalia pia *pattern* ya magonjwa kwa hiyo, utakuta kwamba, dawa hizi zinapotolewa na kugawiwa, kigezo kikubwa ni hicho cha idadi ya mifugo na msongamano wa mifugo katika kila eneo.

Lakini pia kutegemeana na magonjwa ama ya mlipuko ama magonjwa yanayowapata mifugo mara kwa mara katika kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hivi ndivyo vigezo vya msingi. Na *ofcourse*, kigezo kingine ni uwezo wetu wa mfuko, kama Serikali.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, kuna mlipuko ya kila wakati kwa ajili ya magonjwa ya mifugo.

Je, Serikali, itafanya utaratibu gani kuanzisha mfuko wa wafugaji wa mifugo, ili kuweza kununua madawa wakati wowote inapohitajika? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longodo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari kama Wizara, Sekta ya Mifugo, tayari tuna mpango mkakati na pia tuna programu ya kuendeleza hii sekta. Kwa kadiri tulivyojipanga kuanzia mwaka kesho, Sekta vya mifugo na yenyewe itakuwa ni kati ya sekta zitakazopewa kipaumbele kama hizi 6 zilizopewa kipaumbele mwaka huu.

Tunatarajia kwamba, kwa njia hiyo, kutakuwepo na uwezekano wa kuwa na mapendekezo ya kuanza huo mfuko utakaotunishwa, ili utumike kwa uwezeshaji wa wafugaji na sekta ya mifugo kwa ujumla. (*Makofi*)

30 APRILI, 2013

Na. 123

Mgao wa Fedha za Rada

MHE. AMINA A. AMOUR K.n.y. YUSUFU HAJI KHAMIS
aliuliza:-

Je, Sekta ya Elimu ya Msingi Zanzibar, imetengewa kiasi gani cha fedha kutoka katika fedha za Rada?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yusufu Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu litakumbuka kwamba, fedha za rada ni marejesho ya fedha za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zilizotokana na udanganyifu uliofanywa na Kampuni ya *BAE Systems* ya Uingereza, wakati wa kuiuzia Serikali ya Tanzania Rada ya kuongozea vyombo vya usafiri wa angani.

Fedha hizi sio msaada bali ni sehemu ya mapato ya Serikali, ndio maana zikzingizwa kwenye bajeti ya Serikali ya Mwaka huu wa Fedha 2012/2013. Kiasi hicho kilichoingizwa kwenye bajeti ya Serikali, kupitia *addendum*, kilikuwa ni shilingi bilioni 72.3. Aidha, Bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kulipia masuala ya Muungano na Elimu ya Msingi Zanzibar, sio suala la Muungano.

Mheshimiwa Spika, kutokana na makubaliano yaliyofikiwa baina ya Serikali na *BAE Systems* ya Uingereza kupitia Idara ya Maendeleo ya Nchi za Nje ya Uingereza (*Department for International Development – DFID*), fedha zote zilizorejeshwa kutokana na mauzo ya rada, zitapelekwa sekta ya elimu kugharamia mahitaji muhimu.

30 APRILI, 2013

Kwa utaratibu wa Kibajeti uliopo kila Wizara ndani ya Sekta, hubainisha mahitaji yake kutokana na vipaumbele vya kimkakati Kitaifa na vikishaidhinishwa na Bunge, ndipo fedha hutolewa na Hazina.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, pindi Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, wanaohusika na masuala ya Elimu Nchini, watakapokamilisha mchanganuo wa mahitaji muhimu yanayotakiwa na kukamilisha taratibu za ununuzi, ndipo fedha za mahitaji hayo zitakapotolewa na Hazina.

MHE. AMINA A. AMOUR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, jibu lako la msingi umesema kuwa, Shule za Msingi sio suala la Muungano. Kwa kuwa, Zanzibar, kuna shule za Elimu ya Juu, ambapo ni shule za Muungano. Je, Shule hizo wamepata mgao kiasi gani?

Mheshikiwa Spika, fedha za rada ni fedha ambazo zilitokana na mapato ya nchi mbili, yaani Zanzibar na Tanzania Bara. Je, kwa nini, katika marejesho Zanzibar hawapati mgawo wowote?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa fedha, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khamis, yaliyoulizwa na Mheshimiwa Amina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mgawo, kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kuwa, mpaka sasahivi hiyo fedha haijagawiwa kwa sababu, bado ule utaratibu haujakamilika.

30 APRILI, 2013

Kuhusiana na mgao wa Zanzibar, kuhusiana na mgawo mzima wa masuala ya fedha, kuna *formula* ambayo huwa inatumika kugawa pesa kati ya Tanzania Bara na Tanzania Muungano; ninatumaini huo ndio utakaotumika katika mgao, wakati utakapofikia. (*Makofi*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, tayari zipo taarifa kwamba, Wizara ya *TAMISEMI* ambayo, iko chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, imeshatoa zabuni kwa baadhi ya Makampuni kwa ajili, ya kutumia fedha hizo za rada kwenda kununua vitabu na hatimaye Serikali, itavitawanya kwa mujibu wa utaratibu wake.

Mheshimiwa Spika, ni sababu gani ambazo leo hii zinaifanya Wizara ya Fedha, iwe na kigugumizi kulieleza Bunge lako, ni kiasi gani ambacho kitabaki kwa upande wa Tanzania Bara (Tanganyika), ikiwa ni pamoja na upande wa pili wa Zanzibar? Naomba ufafanuzi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Machali, lakini pia ufafanuzi wa swali la awali la nyongeza, lililoulizwa na muuliza swali.

Mheshimiwa Spika, fedha za rada, ambazo pia tumezizungumza katika Bunge hili mara nyingi na mimi kutoa jibu hili wiki iliyopita kama swali la msingi la namna mgao ulivyofanywa kwa ajili ya matumizi ya elimu. Fedha yote iliyotengwa kwa marejesho ya rada imetengwa kwa ajili ya kuboresha elimu ya msingi. Na mgawo wa fedha ile ni kama ifuatavyo:-

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 55.2 zimetengwa kwa ajili ya kununua vitabu kwa ajili ya Shule za Msingi Tanzania Bara. Shilingi bilioni 18.9 zimetengwa kwa ajili ya madawati na fedha hizi zitagawiwa katika Halmashauri zote nchini. Hayo ni makubaliano ambayo tuliyafanya hapahapa Bungeni kwa hiyo, hayo ndio majibu yangu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, zabuni zimeshaandaliwa. Makampuni 9 yatafanya kazi ya kusambaza vitabu vyote nchini na vitafika katika kila Halmashauri na taratibu za zabuni zimeshakamilika, makampuni yamepatikana, wakati wowote kazi ya usambazaji itaanza mara moja. Wakati vitabu vinasambazwa na fedha nazo zitapelekwa katika halmashauri zetu.

SPIKA: Tunaendelea na Swali linalofuata, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Albert Obama?

Huwezi kukaimu nafasi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Mheshimiwa Ntabaliba Obama? Kwa niaba yake, Mheshimiwa Genzabuke? (*Kicheko*)

Na. 124

Ruzuku kwa Zao la Kahawa

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE K.n.y. MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

Je, kwa nini zao la Kahawa halipati ruzuku? Na ni lini ruzuku hiyo itaanza kutolewa?

30 APRILI, 2013

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali, imekuwa ikitoa ruzuku ya zao la kahawa tangu mwaka 2007/2008, ambayo inahusisha uzalishaji na upatikanaji wa miche bora ya kahawa inayouzwa kwa wakulima kwa bei nafuu. Aidha, miche bora ya kahawa inazalishwa na vikundi vya wakulima katika maeneo yote yanayozalisha kahawa hapa nchini, kupitia Kituo cha Utafiti wa Kahawa – *TaCRI (Tanzania Coffee Researching Institute)*. Ili kuhakikisha miche hiyo inawafikia wakulima wa Wilaya ya Kasulu, hususan Jimbo la Manyovu, Taasisi ya Utafiti wa Zao la Kahawa (*TaCRI*) inatumia Kituo Kidogo cha Mwayaya, ambacho kinazalisha miche bora na kutoa huduma kwa wakulima wa Wilaya za Kigoma, Kibondo na Ngara. Uzalishaji wa miche bora ya kahawa hadi kufikia tarehe 31 Desemba, mwaka jan 2012 ni kama ifuatavyo:-

(a) Kikundi cha Kitambuka, wanakikundi wamezalisha na kugawa miche 90,000 waliyoipanda katika mashamba yao.

(b) Bustani ya *TaCRI* – Mwayaya, imetoa miche 11,500 ambayo imepelekwa vijijini kwa ajili ya kuanzisha bustani mama (*Mother Seed Farms*). Aidha, miche mama 10,300 inaeendelea kukuzwa kwenye kitalu cha Mwayaya.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyomjibu Mheshimiwa Mbunge, wakati nikijibu swali lake Namba 318, Tarehe 3 Agosti, 2012 Serikali, inaendelea kuboresha mfumo wa uzalishaji wa kahawa nchini, ili kuongeza tija, kuongeza uzalishaji, ubora wa kahawa yetu na masoko kwa kushirikiana na taasisi zilizotajwa na wadau wengine kadiri Bajeti itakavyoruhusu.

30 APRILI, 2013

Kwa kuzingatia haya, Serikali, itaongeza wigo wa kutoa ruzuku za pembejeo kwa zao la kahawa, ili wakulima waweze kupata pembejeo nyingine, kama vile mbolea na madawa. Aidha, kwa kuwa, mahitaji ya miche bora ya kahawa ni makubwa, nitoe wito kwa Halmashauri katika maeneo yanayolimwa kahawa, kutenga fedha kwa ajili, ya uzalishaji wa miche kupitia vikundi vya wakulima.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Jimbo la Manyovu na Jimbo la Kigoma Kaskazini kuna Makampuni yamenunua kahawa ya wakulima bila ya kuwalipa na sasa ni zaidi ya mwaka mzima na wakulima wameendelea kupata tabu kwa sababu ya ukosefu wa fedha ambayo wameuza kahawa yao kwa makampuni hayo.

Je, Serikali, haioni umuhimu wa kuchukua kesi hii, ili wananchi wapate haki yao kwa kulipwa pesa yao?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo baina ya Vyama viwili vya Msingi, kuna *Kalinzi Organic Coffee Farmers* na *Kalinzi Coffee Farmers*. Walichukua kahawa yao ikaenda kukobolewa Kilimanjaro, ilipofika kule baada ya kukobolewa, ilipouzwa baadhi ya kahawa ya *Kalinzi Organic* ikatathminiwa kama kahawa ya *Kalinzi Coffee*. Kwa hiyo, kilichotokea ni kwamba, pesa ya mmoja ikaenda kwa mwingine.

30 APRILI, 2013

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Spika, sasa sijui kwa nini hili limekuwa ni tatizo kwa sababu thamani ya kahawa iliyochukuliwa inajulikana na pesa tu ilikuwa inatakiwa itoke kwenye akaunti ile iliyopelekwa kwa makosa ije huku.

Iko kwenye Halmashauri ya Kigoma nadhani pia Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Obama wote wamekuwa wameliulizia hili suala sijui kwa nini lakini halipati ufumbuzi lakini naomba niwahakikishie tu kwamba sisi pamoja na nyinyi pamoja na Halmashauri yenu tutasimama tumalize tatizo hili maana yake lina miaka miwili sasa *its just dragging too long* tutalipatia ufumbuzi kwa pamoja. *(Makofi)*

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru wananchi wa kata za Boshia, Mhinduro, Malamba na Kigongoi wameonyesha hamasa kubwa sana ya kufufua zao la kahawa ambalo walilima kwa mafanikio makubwa sana katika miaka iliyopita.

Je, Serikali iko tayari kuwashauri *TaCRI* waweze kupeleka miche bora na huduma za ugani kwa wananchi hawa ili waweze kufufua zao hili?

SPIKA: Ni swali jipya lakini la maendeleo haya naomba ujibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kitandula kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye tutaongea na *TaCRI* lakini tatizo la kahawa ambalo ndiyo zao namba tatu nchini siyo tatizo tu hilo ni kwamba tunazungumzia kwa maeneo yote mkakati uliokuwepo ni kwamba tunakuombeni sana wakulima wa kahawa tumieni miche, miche mnayotumia ina miaka arobaini wastani wa miche mibuni ni miaka ishirini na tano ndiyo *maximum physisibility*.

30 APRILI, 2013

Kwa hiyo tunakuombeni sana wakulima wa kahawa kwamba tuzingatie kanuni bora hizi za kilimo na hayo maeneo mapya kama haya ya Lushoto mpaka Mara huko kuna wakulima wanataka kulima kahawa tunaomba sana wazingatie kanuni bora ili kilimo hiki kiwe na tija zaidi kuliko kilivyo sasa hivi. *(Makofi)*

Na. 125

Kiwanda cha Chai cha Lupembe Kufunguliwa

MHE. DEO K. SANGA aliuliza:-

Wananchi wa Lupembe ni wakulima wakubwa wa chai na tangu Kiwanda cha Chai cha Lupembe kifungwe uchumi wa eneo hilo umeshuka sana;

(a) Je, mgogoro wa kiwanda cha chai cha Lupembe utakwisha lini ili kiweze kufunguliwa?

(b) Je, Serikali itaruhusu lini kuuzwa kwa chai iliyokwisha sagwa iliyomo kwenye kiwanda hicho ili wananchi walipwe haki yao?

(c) Je, ni lini wananchi watalipwa fedha zao zitokanazo na chai hiyo iliyosagwa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasanyenda Sanga Mbunge wa Njombe Kaskazini, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo.

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha Chai cha Lupembe kilibinafsishwa kwa kampuni ya *Dhow Mercantile (E.A) Limited* kwa asilimia 70 na asilimia 30 ya hisa zinamilikiwa na wakulima wa Chai wa Lupembe chini ya Muungano wa vyama vya Ushirika Lupembe (MUVYULU).

Mheshimiwa Spika, baada ya ubinafsishaji kulitokea kuto kuelewana kati ya kampuni ya *Dhow Mercantile (E.A) Limited* na mwekezaji mwenza MUVYULU hali iliyopelekea kufungwa kiwanda hicho mwaka 2008. Wadau wa Chai ikiwemo Serikali kupitia uongozi wa Wilaya na Mkoa wa Iringa pamoja na Wizara yangu imefanya jitihada mbalimbali kwa nyakati tofauti za kushawishi pande husika kumaliza mgogoro huo nje ya Mahakama bila mafanikio.

Aidha ili kuwa wezesha wakulima kuwa na soko la majani ya chai, Serikali ilihamasisha ujenzi wa kiwanda kingine cha kusindika chai katika eneo la Lupembe. Kiwanda hicho kimeshajengwa na kuanza uzalishaji tangu mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya utangulizi sasa napenda kujibu swali kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, (a) mgogoro wa kiwanda hicho upo mahakamani na kesi hiyo imeshaanza kusikilizwa katika mahakama kuu kitengo cha ardhi, hivyo kumalizika kwa mgogoro huo kunategemea uamuzi wa mahakama.

Aidha ni matarajio yetu kuwa kesi hiyo itamalizika mapema ili kuwezesha kiwanda hicho kufunguliwa na kuwawezesha wananchi wa Lupembe kuuza chai yao katika kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, (b) kama nilivyosema katika sehemu (a) kuwa suala hili lipo mahakamani hivyo suala la kuuzwa kwa chai iliyokwisha sagwa kiwandani hapo linasubiri maamuzi ya mahakama.

Mheshimiwa Spika, (c) suala la wakulima kulipwa fedha zitokanazo na chai hiyo iliyosagwa nalo linasubiri maamuzi ya Mahakama. Hata hivyo kutokana na chai hiyo kukaa muda mrefu kuna uwezekano wa kupoteza ubora wake hivyo kutokufaa kwa maana ya kupelekwa sokoni. *(Makofi)*

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili.

Mheshimiwa Spika, Lupembe katika tarafa ya Lupembe ni wakulima wengi sana wanaozalisha chai na pamoja na kiwanda ambacho kimejengwa hakikidhi chai kila siku inamwagwa.

Je, Serikali itakuwa tayari kwenda kujifunza kule Kenya, Kenya kuna viwanda vidogo vidogo vinavyowasaidia wakulima angalau waweze kujenga viwanda vidogo vidogo viweze kukidhi kule Lupembe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kule Lupembe kuna mkulima mmoja mkubwa ana mashamba makubwa sana anaitwa Msambwa anahitaji kujenga kiwanda. Serikali itakuwa tayari kukaa na huyu Msambwa ili kuona namna gani ya kutusaidia kujenga kiwanda kule Lupembe?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Deo Sanga, *Jah People* Mbunge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hili tatizo la tarafa ya Lupembe ni tatizo ambalo limekaa kwa muda mrefu kama nilivyosema matarajio yetu ni kwamba hii kesi ya mahakani inaweza ikapata ufumbuzi ndani ya muda mfupi ili kiwanda hiki cha zamani pamoja na hiki kipya viendeleo kuzalisha chai hii ya wakulima inayozalishwa.

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, hili swala *specific* la kwamba Kenya kuna viwanda vidogo vodogo ni kweli Mheshimiwa Spika na wewe unafahamu tumelijadili kwenye Bodi ya Chai ni kweli viwanda vidogo vya Kenya vinafanya kazi vizuri sana lakini msingi wake kwa upande wa Tanzania ni vyama vya Ushirika, vyama vya msingi.

Kwa hiyo kuna *combination* hapa ya kwamba kuna vile viwanda vidogo vya Kenya na *efficiency* zake na utekelezaji na ufanisi wa vyama vya ushirika hivi vya msingi. Nakubaliana naye kwamba tutafanya kazi kwa kushirikiana na Bodi ya Chai na Tashfida ambayo ni Umoja wa wakulima wadogo wa chai kwa pamoja ili tupate ufumbuzi wa namna ambavyo wakulima wadogo hawa wanaweza ku-*engage* kwenye *processing activities* kwa *model* hii ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, swali la pili hili la mkulima huyu anayeitwa Msambwa anahitaji kujenga kiwanda, Wizara ya Kilimo ilishasema kwamba tumeongea na taasisi za fedha kuangalia kama tunaweza kupata mfuko wa kuongeza thamani kwa mazao yote na kwa maana hiyo tunatarajia kwamba mfuko huo ambao utahusisha *NSSF*, *PSPF* na *PPF* na taasisi nyingine za fedha za nchini mwetu.

Hapa wamekubali na tunatarajia kwamba wakina Msambwa kama hawa ndiyo watakuwa watumiaji wakuu wa mfuko huu kwa hiyo naomba niseme tu kwamba nitashirikiana na Mheshimiwa Sanga na Msambwa ili tuone kwamba na yeye anaweza kuwa *pioneer* katika mfumo huu ambao tunataka kuanzisha. (*Makofi*)

SPIKA: Jamani muda umekwisha maswali bado manne dakika kumi na tano haiwezekani Wizara ya Nishati na madini Mheshimiwa Modestus Kilufi atauliza swali kwa niaba yake Mheshimiwa Mwijage.

30 APRILI, 2013

Na. 126

Usambazaji wa Umeme Katika Kata- Mbarali

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE (K.n.y. MODESTUS D. KILUFI) aliuliza:-

Umeme ni nyenzo muhimu sana katika kutoa ajira kwa wananchi hasa vijana.

(a) Je, Serikali itasambaza lini umeme katika Kata za Madibira, Rulwa na vijiji vya Ilongo, Igalako, Utoro na Ukwavila?

(b) Je, kwa nini wananchi wasipatiwe huduma hiyo wakati nguzo za umeme zimepita katika baadhi ya vijiji hivyo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Modestus D. Kilufi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kata ya Madibira pamoja na vijiji vya Saadani, Ikoga, Igalako, Utoro, Ukwavila, Ilongo, Rulwa, Ubaruku, Isongole, Ilengaitekela, Itambo, Rugelele, Ihai, Sonyanga, Utengule, Imalilo, Mwaindi, Igava, Ipwani, miyombweni, Usangu na Luhanga vimejumuishwa katika mpango kabambe wa umeme vijijini awamu ya pili.

Zabuni ya kumpata mkandarasi wa kazi hizi ilitangazwa mwezi Desemba 2012 na kufunguliwa mwezi Machi, 2013. Kazi za mradi huu zitajumuishwa.

30 APRILI, 2013

Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa *KV 33*, Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa *KV 0.4*, Ufungaji wa *transfoma* na kuwaunganishia umeme wateja. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza wakati wowote mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuvipatia umeme vijiji vyote ambavyo vimepitiwa na misongo ya kusafirisha umeme kwa kufunga transfoma za kupoozea umeme katika vijiji hivyo. Kwa sasa Serikali inatayarisha *program* maalum ya kushusha umeme kwenye maeneo yote ambayo yamepitiwa na misongo mikubwa ya kusafirishia umeme.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, asante katika jibu lako Mheshimiwa Waziri umezungumza kazi ambayo umeifanya kwenye Kata ya Madibila na kwa kufanya hivyo umetekeleza kikamilifu ahadi ya Mheshimiwa Rais mwaka 2010 nakupongeza. Napenda kuuliza.

Je, Wilaya nzima sasa utaiweka katika mpango wa *REA*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili umezungumzia msongo wa umeme unakopita ningependa kujua na mimi katika jimbo langu kata za Mafumbo na vijiji vya Vigaga vitaweza kufaidika na kushushiwa umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwijage kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa awamu ya kwanza tutatekeleza miradi katika vijiji hivyo tulivyovitaja lakini tunaandaa tena awamu ya tatu ambayo itakuja baada ya kukamilika awamu hii basi tutazingatia haya anayoyasema na pengine tunaweza tukafikia lengo hili la Wilaya nzima. Dhamira ya Serikali hapa ni kuhakikisha nchi nzima vijiji vyote vya nchi nzima vinakuwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ameuliza kuhusu Kata za Jimbo lake Mheshimiwa Mwijage za Mafumbo na Igaga nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vijiji hivi na kata hizi zipo katika *REA* ya *Phase Two* ambayo tutakwenda kuitekeleza baada ya kukamilisha taratibu na zitaanza kutekelezwa mwaka huu. (*Makofi*)

Na. 127

Fidia kwa Wananchi Walipisha Mradi wa EPZ

MHE. AMINA M. MWIDAU aliuliza:-

Umeme ni nyenzo muhimu sana katika kutoa ajira kwa wananchi hasa vijana.

Wananchi wakazi wa eneo la Neema katika jiji la Tanga wamefanyiwa tathmini maeneo yao kwa muda sasa ili kupisha utekelezaji wa mradi wa *EPZ* lakini hadi sasa hawajalipwa.

Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi hao kwa kutumia sheria ya malipo ya sasa?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina M. Mwidau Mbunge wa viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008 Wizara yangu kwa kushirikiana na mamlaka ya kutenga maeneo maalum kwa ajili ya uzalishaji wa mauzo nje yaani *EPZ* pamoja na Halmashauri ya jiji la Tanga walibainisha eneo lenye ukubwa wa hekta 1,363 sawa na hekari 4000 kwa eneo la Neema Jijini Tanga kwa ajili ya matumizi ya mradi wa *EPZ*.

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, mwishoni mwa mwaka 2009 wathamini kutoka Halmashauri ya jiji la tanga walifanya zoezi la uthamini wa mali na maeneo katika eneo zima la mradi na kukamilisha zoezi hilo mwaka 2010. Baada ya kukamilisha uthamini huo Halmashauri iliandaa jedwali la fidia ambalo lilithibitishwa na mthamini Mkuu wa Serikali lenye jumla ya shilingi bilioni 4.2 ikijumuisha riba ya ucheleweshaji.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zimetengwa katika bajeti ya EPZA ya mwaka wa fedha 2012/2013 na kiasi hiki cha fedha kitalipwa pindi zitakapotolewa na hazina. Aidha malipo haya yatafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 ambayo ndiyo inayotumika kuthamini fidia hivi sasa.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Amina swali la nyongeza.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, asante pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake ya msingi ameanisha kuwa fedha hizo zimetengwa katika mwaka wa fedha huu 2012/2013 na zitalipwa mara tu zitakapotolewa na Hazina.

Kwa kuwa mwaka huo wa fedha 2012/2013 unakaribia ukingoni namuomba Mheshimiwa Naibu Waziri anihakikishie mbele ya Bunge hili kama kweli pesa hizo zitalipwa ndani ya mwaka huu kabla ya kWisha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa kulikuwa na malalamiko mengi sana miongoni mwa wananchi waliopisha mradi huo katika yale maeneo na malalamiko yao makubwa ni mwongozo wa ardhi uliotumika ni ulitumika wa nyuma wa 2004 badala ya ule wa 2008 ninamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri afafanue ni muongozo gani ambao ulitumika wa ardhi katika kuthamini maeneo yao na mali zao.

30 APRILI, 2013

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa lile jibu la kwanza la kutaka uhakika kwamba sasa hivi mwaka wa fedha wa 2012/2013 unaishia Juni. Je, fedha hizi zitapatikana?

Napenda nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba bado miezi mitatu ili mwaka wa fedha huu ambao unaishia mwezi Juni uweze kuisha na nimhakikishie Mbunge kwamba fedha hizi kwa miezi mitatu hizi tunategemea kwamba tutapokea Hazina na endapo tutapokea Hazina fidia hii italipwa na kama miezi mitatu hii itakuwa bado mwaka wa fedha unaokuja itapewa kipaumbele cha kwanza ili fidia hii iweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, na swali la pili ni kwamba uthamini wa fidia hii kwa vigezo vya nyuma vya 2004/2008 napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Tanga wakiwemo Wabunge kina Mheshimiwa Pamba, Mheshimiwa Kitandula, Mheshimiwa Nundu kwamba wawaeleze wananchi kwamba fidia inayolipwa inatokana na Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 na si vinginevyo wala si maagizo au maazimio ya nyuma ni Sheria namba 4 ya Ardhi ya mwaka 1999 ndiyo inayotumika hivi sasa. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante twende Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo bado wana maswali mawili, Mheshimiwa Iddi M. Azzan atauliza swali hilo.

30 APRILI, 2013

Na. 128

Kuwaenzi Wanamichezo

MHE. IDDI M. AZZAN aliuliza:-

Serikali imeshindwa kuwaenzi baadhi ya wanamichezo walioliletea Taifa sifa kubwa.

Je, ni kwa nini Serikali inashindwa kumpatia matibabu Nahodha wa zamani wa timu ya Taifa Jellah Mtagwa?

Je, Serikali ina mkakati gani wa maisha ya baadaye ya wachezaji wa Timu za Taifa?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Azzan Mbunge wa Kinondoni lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali hajaweka utaratibu rasmi wa kuwaenzi baadhi ya wanamichezo walioliletea Taifa sifa kubwa. Utaratibu unaotumika kwa sasa na ambao siyo rasmi ni ule ambao viongozi wa juu wa Serikali na Sekta binafsi kuwapa zawadi wachezaji waliofanya vizuri kwenye mashindano mbalimbali na wengine hupewa tuzo zinazotolewa na asasi zisizo za Kiserikali kama vile Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo (*TASU*).

Hata hivyo tunaangalia uwezekano wa kuanzisha utaratibu wa kuwaenzi wanamichezo mahiri na pindi tutakapopata namna bora inayotekelezeka tutawafahamisha wananchi.

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kutompatia matibabu nahodha wa zamani wa timu ya Taifa Ndugu Jellah Mtagwa ningependa ifahamike kwamba mchezaji huyu amepatwa na matatizo akiwa amekwisha kustaafu kucheza mpira katika klabu aliyoichezea mwishoni ya *Pan Africa* baada ya kuchezea timu ya Taifa mchezaji huyo wa zamani aliendelea kuichezea Pan Africa na kuifundisha timu ya Pan.

Kimsingi Wizara yangu haina utaratibu wa kugharamia tiba ya wanamichezo wanaoumia wakiwa michezoni au wakiwa wamestaafu. Inapotokea wanamichezo hao wakaoumia wakiwa na timu ya Taifa hugharamikiwa moja kwa moja na vyama vinavyosimamia michezo husika au kupitia Bima walizowekewa.

Mheshimiwa Spika, kwa wachezaji wanaoumia wakiwa na klabu zao hugharamiwa tiba na klabu zao zenyewe. Hata hivyo panapokuwepo na uwezo na kwa maombi maalum Wizara yangu imekuwa ikisaidia gharama za wanamichezo wanaoumia wakiwa na timu za Taifa.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Azzan swali la nyongeza.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya kuwakatisha tamaa wana michezo ngojeni wafe mkasome wasifu mrefu na pengo lake halitazibika nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwa kuwa matatizo haya yamejitokeza kwa wanamichezo wengi ni kwa nini Serikali isiweke utaratibu maalum wa kuhakikisha wale wanaochezea timu za Taifa ama vilabu ama wanakuwa wamekatiwa Bima za ajali au za maisha ama wamejiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii ili baadaye iweze kuwasaidia kwa mafao hayo?

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa Jellah Mtagwa ni kielelezo cha Wanamichezo wa Tanzania alichezea timu ya Taifa zaidi ya miaka kumi na tano akiwa *Captain*, picha yake ilibandikwa kwenye *stamp* zilizouzwa kwa mamilioni hapa Tanzania na kukusanya pesa nyingi na hivi sasa anaumwa kutokana na kushiriki kwake kwenye michezo hiyo Serikali haioni umuhimu wa kutoa gawio la *stamp* hizo zilizouzwa ili ziweze kumsaidia katika maisha yake?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, naomba ujibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Idd M. Azzan, kama ifuatavyo:-

Kwanza, niungane naye kwamba yeye mwenyewe mchezaji na mimi ni mchezaji na wachezaji wengine. Kwamba Serikali haikatishi tama wachezaji, zaidi Serikali itaendelea kuwatia moyo na kuwapa *support* wachezaji.

Sasa nijibu maswali yake yote mawili, kwanza ni kwamba upo utaratibu ambao wachezaji kama wachezaji wanacheza katika vilabu vyao, hiyo ni ajira katika kilabu anachocheza, na anazo haki zote kutoka kwa mwajiri wake.

Lakini kanuni za ligi namba 11 na 12, kuanzia ngazi ya daraja la nne mpaka Taifa, zinazitaka *club* hizo kuwakatia Bima wachezaji wake na kuziambatanisha hati ya bima katika mkataba wake anaposajiliwa na timu hiyo.

Kwa hiyo, wachezaji hawa wanazo Bima kutoka katika virabu vyao, wanazo haki za kupata matibabu na kila aina ya msaada kutoka kwa mwajiri wake. Pia, Serikali kwa maombi maalum iko tayari na imeshawasidia akina Laurence Mwalusako, akina Juani Akwale na wachezaji wengine mbalimbali kwa maombi maalum.

Kwa hiyo, siyo kweli kwamba sisi Serikali hatuliangalii suala hilo. Lakini lingine ni kwamba nakubaliana naye kwamba Jella Mtagwa anasifa kubwa, lakini wachezaji wa Taifa wakiwemo pia wakina Leodgar Tenga na wengine wengi huchaguliwa. Kwa hiyo tunakuwa na idadi kubwa ya wanamichezo ambao leo atachaguliwa timu ya Taifa, mechi inayofuata hatachaguliwa, tutatukuwa na wachezaji wengi ambao kama Serikali itabeba gharama hizo zote ni kwamba tutakuwa na msululu wa kusaidia wachezaji wengi sana wa Taifa.

SPIKA: Ahsante, tunaendelea na Wizara ya Mawasalano Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Cecilia D. Paresso atauliza swali hilo kwa niaba ya Mheshimiwa Joshua Nassari.

Na. 129

Minara ya Simu Katika Makazi ya Watu

MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. JOSHUA S. NASSARI) aliuliza:-

Wananchi wamekuwa na malalamiko juu ya minara ya simu kuwekuwa katika makazi ya watu na kudai kuwa ina madhara ya kiafya kwa binadamu:-

- (a) Je, kuna ukweli wowote juu ya hilo?
- (b) Je, kunafanyika tathimini yoyote ya mazingira (environmental impact assessment) kabla ya kuwekwa kwa minara hiyo?
- (c) Je, Kijiji kinapata asilimia ngapi ya mapato kutoka katika minara hiyo?

30 APRILI, 2013

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA
TEKNOLOJIA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joshua S. Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki lenye sehemu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Kamati maalum iliyoungwa kwa ushirikiano kati ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Tume ya Mionzi ya Taifa (TAEC) imefanya utafiti wa awali wa athari za mionzi katika Mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Dodoma, Mwanza, Mjini Magharibi, Kasini Unguja na Kaskazini Unguja.

Utafiti ulifanyika ukihusisha minara yote yenye kurusha masafa ya FM, VHF,TV, UHF TV, GSM 900 Cellular, 1800 GSM cellular na UMTS. Maeneo yaliyofanyiwa utafiti ni yale yenye watu wengi kama vile shule na makazi ya watu ambapo kwa kuanzia, jumla ya minara 70 ilikaguliwa.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti huo yalionyeshwa minara kukidhi viwango vya kutokuwa na madhara kwa binadamu vinavyotakiwa kitaalamu na vinavyotambuliwa na "*International Commission on Non-Ionizing Radiation Protection – ICNIRP*".

(b) Mheshimiwa Spika, tathimini ya mazingira "*Environmental Impact Assessment*" hufanyika kabla ya mnara wowote wa mawasiliano kujengwa katika eneo lolote nchini. Tathimini hii inasimamiwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Baraza hili ndilo hutoa vibali vya ujenzi pindi mwombaji anapokidhi vigezo vinavyotakiwa kimazingira katika ujenzi wa minara.

(c) Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu imepokea

malalamiko mbalimbali kuhusiana na utaratibu na viwango vya asilimia ya tozo inayotakiwa kulipwa na wanaotoa huduma za mawasiliano katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Kwa kipindi kirefu sasa, Wizara imefanya majadiliano mbalimbali na kampuni za simu, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ili kuweka mfumo madhubuti utakaoongeza ufanisi wa malipo kwa Halmashauri na vijiji kulingana na kiwango cha matumizi ya huduma za mawasiliano katika eneo husika.

Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI inaendelea kuandaa mwongozo wa tozo hizo utakaowasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya uchambuzi zaidi na pale utakaporidhiwa, utatumiwa na Serikali za mitaa zote na hivyo kupunguza ukiukwaji wa utozaji na ulipaji wa tozo hizo katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, mwongozo huu utainisha kiwango cha mapato ambacho kila kijiji kitapata kutoka katika minara ya simu. *(Makofi)*

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali inakili kuwepo kwa malalamiko ya wananchi kuhusiana na utaratibu wa tozo za minara ya simu katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo vijiji vya Nshupu, Maleu, Maji ya Chai Wilayani Arumeru Mashariki.

Je, ni lini sasa Serikali itatoa muongozo hapo?

Je, ni lini Serikali itatoa tamko kwa wamiliki wa minara hiyo kuwezesha kuimarisha na kuboresha miundo mbinu iliyopo minara husika?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

30 APRILI, 2013

Kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kwamba tumeunda timu ambayo sasa hivi inafanyia kazi suala hili, na tunajua ni suala muhimu ingawaje hivi sasa kuna baadhi ya Halmashauri zinapata tozo hizo kupitia mauzo ya *voucher* ambazo ni asilimia 0.3%. Sasa kwa upande wa vijiji ambavyo havina maduka ya simu au maduka ya kuuzia *voucher* hili tunalifanyia kazi na wakati tutakapo kuwa tayari tutamuarifu mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

Pili, kwenye mpango wetu wa *UCAF* tumetayarisha mpango ambao kwa vijiji vyote vile ambavyo havina mawasiliano tutavipelekea mawasiliano. Kwa sasa tumeanza na awamu ya kwanza, tunaenda awamu ya pili halafu awamu ya tatu, na nitahakikisha Mheshimiwa Mbunge vijiji ulivyovitaja vitapata mawasiliano bila matatizo vyote.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tupo nje ya muda, naomba nitangazie shughuli za kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Anna M. Abdallah ameomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 mchana watakuwa na kikao kwenye Ukumbi Namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundo Mbinu, Mheshimiwa Peter Serukamba, ameomba niwatangazie wajumbe wa kamati yake kwamba, leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao katika ukumbi mkubwa wa Msekwa, wajumbe wote wanaombwa wahudhurie.

Ofisi ya Bunge, imeomba niwatangazie kwamba, kampuni ya *African Assurance* ipo kwenye viwanja vya maonyesho vya Bunge kutoa elimu juu ya Bima mbalimbali ambazo Wabunge na wananchi kwa ujumla wanaweza kunufaika nazo.

Kwa hiyo, Wabunge wanakaribishwa kutembelea eneo hilo. Katibu tuendeleee!

30 APRILI, 2013

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali 2013/2014
Wizara ya Maliasili na Utalii

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Mheshimiwa Hamad R. Mohamed!

HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, naomba muongozo wako kwa mujibu wa kanuni ya 68 (7), wakati Naibu Waziri wa Fedha akijibu swali la Mheshimiwa Mheshimiwa Yusufu H. Khamis, swali namba 123, alisema kwamba, fedha za RADA siyo fedha za Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba, nyongeza ya kwanza, Ibara ya 10, kodi ya mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika na ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania inasimamiwa na Idara ya Forodha ambayo ni ya Muungano. Ibara ya 17, usafiri na usafirishaji wa anga ni mambo ya Muungano. Kwa hiyo, chanzo cha mapato yenyewe kinatokana na mapato ya Muungano. RADA yenyewe iliyonunuliwa ni ya Muungano. Kwa hiyo, bakaa ya fedha iliyorudisha inatokana na fungu la Muungano.

Naomba Mwongozo wako, kwa kuwa Bunge lako linatakiwa kusimamia Katiba na Sheria, na kwa kuwa Ibara ya 133 ya Katiba inayozungumzia mfuko wa pamoja wa fedha hakijatoa fomula rasmi ya mugawanyo wa mapato, huoni kama ni busara kwa Serikali kukaa kuzingatia hasa ikielewa kuwa watoto wote hawa ni watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maana hiyo wanahaki ya kupata mgao huu ili ilwasaidie katika suluhu.

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako katika hili.

SPIKA: Wizara inayohusika na mambo ya Muungano itajadili suala hilo. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla!

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Uwe na uhakika kuwa ni mwongozo, na isiwe hotuba nyingine.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, bila shaka! Nasimama kwa mujibu ya 68(7) ili kuomba jambo ambalo linahusiana na muongozo lipatiwe ufumbuzi wako, kwamba wakati Serikali ikitoa majibu ya swali namba 128, lilioulizwa na Mheshimiwa Iddi M. Azzan, Mbunge wa Kinondoni, swali lake la pili la nyongeza halikupatiwa majibu.

Kwamba, Ndugu Jella Mtagwa, ambaye alikuwa *captain* kwa miaka 12 mfululizo katika timu ya Taifa, na kwa maana hiyo, akajijengea umaarufu mkubwa na kuwa *iconic* kiasi cha kuwekwa kwenye *stamp*.

Sasa hivi anaumwa na Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwasaidia baadhi ya wachezaji wengine ambao hata hawakufikia umaarufu wa ndugu Jella Mtagwa.

Ninaomba Mwongozo wako, kwamba Serikali sasa itupatie majibu ya swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi M. Azzan ambaye alisema, mapato mengi yalipatikana kutokana na kukusanywa kwa mauzo ya *stamp* ambazo zilikuwa zinapicha ya Ndugu Jella Mtagwa na hivyo alistahili angalau kupatiwa chochote kutokana na mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba muongozo wako kwamba Serikali itoe majibu ya swali hilo au ikubaliane tu na mapendekezo ya mwuliza swali kwamba Ndugu Jella Mtagwa anastahili kulipwa mafao kiasi fulani ili aweze kupata matibabu katika ugonjwa unaomsibu.

SPIKA: Naomba usome kifungu cha 68(7) chote.

MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA: Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika, kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili spika, atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa hapo hapo au baadaye kadri atavyoona inafaa.

SPIKA: Sasa mnaona, mwongozo ndiyo unaotakiwa, kwamba je hilo jambo lilikuwa sahihi au siyo sahihi. Sasa tatizo la humu ndani watu wanasema hakutoa majibu, wanataka ajibu anavyotaka yeye; mimi nafikiri alijibu, sasa kama hamkuridhika nitoe tofauti hiyo. Mtoa hoja!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wake Mhe. shimiwa James Daudi Lembeli, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Taasisi zake kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuniwezesha kuiongoza Wizara hii yenye dhamana ya kusimamia Rasilimali za Maliasili na Malikale na kuendeleza Utalii.

Nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu, nikishirikiana na viongozi wenzangu ndani ya Wizara na wadau wote wa sekta hii kuhakikisha kuwa ulinzi na matumizi endelevu ya rasilimali hizo ni kwa manufaa ya Watanzania na dunia nzima.

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka 2012/2013 na Mpango wa Bajeti wa Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014. Nalihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na wenzangu kutoa pole kwako Mheshimiwa Spika na kwa waheshimiwa Wabunge kutokana na kuondokewa na aliyekuwa mbunge mwenzetu Mhe. Salim Hemed Khamis Mbunge wa Chambani - CUF. Vilevile, natoa pole kwa familia za marehemu na watanzania wote kwa ujumla kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea nchini. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, Hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya pili inazungumzia Utekelezaji wa Mpango wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010 - 2015. Sehemu ya tatu ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango kazi wa mwaka 2012/2013 ambao umezingatia utekelezaji wa ahadi pamoja na maelekezo yaliyotolewa Bungeni na maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali. Sehemu hii inazungumzia pia changamoto ambazo Wizara ilikabiliana nazo katika utekelezaji.

Sehemu ya nne ni Mpango wa Utekelezaji na Malengo ya Wizara kwa mwaka 2013/2014, na sehemu ya tano ni hitimisho ambapo bajeti inayoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2013/2014 inawasilishwa.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Ilani ya uchaguzi ya ccm ya mwaka 2010-2015, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 - 2015. Utekelezaji umezingatia maeneo yaliyoainishwa katika Ilani hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kuwezesha jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi kunufaika na rasilimali za wanyamapori na misitu. Katika mwaka 2012/2013, jumuiya moja ya hifadhi ya wanyamapori ya Randilen katika wilaya ya Monduli imeidhinishwa na hivyo kufanya idadi ya Jumuiya zilizoidhinishwa kufikia 18.

Katika mwaka 2012/2013, jumuiya kumi zimepata mgawo wa jumla ya Sh.164,908,467.75, ikiwa ni sehemu ya mapato yaliyotokana na uwindaji wa kitalii katika sehemu husika. Aidha, Halmashauri za wilaya 32 zenye vitalu vya uwindaji wa kitalii zimenufaika na mgawo wa jumla ya Sh.1,162,199,512.52.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za misitu. Kupitia Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu (*PFM*), maeneo ya misitu yenye jumla ya ukubwa wa takribani ekari milioni 7.7 katika vijiji 2,285 kwenye wilaya 77 za mikoa 21 ya Tanzania Bara yamehifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo umewezesha kurejesha uoto wa asili katika maeneo ambayo awali yalikuwa yameharibika. Aidha, baadhi ya misitu imeanza kuvunwa na vijiji kuongeza mapato yao na hivyo kuweza kugharimia miradi ya maendeleo. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri za wilaya za Chunya na Kiteto, ni ujenzi wa vyumba vya madarasa, ofisi nne za vijiji, nyumba sita za watumishi, zahanati moja, visima viwili vya maji na ukarabati wa madarasa matatu, nyumba tano za walimu na zahanati moja.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia Hifadhi za Taifa 16, Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba 28, Mapori Tengefu 44 na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) 38 zimesajiliwa, kati ya hizo 18 zimeidhinishwa kutumia rasilimali za wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Kuweka utaratibu shirikishi wa

30 APRILI, 2013

upandaji miti, uvunaji na udhibiti wa moto katika misitu. Utaratibu wa kushirikisha wananchi kulinda na kudhibiti moto katika misitu umeendelezwa kwa kutoa elimu ya uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za Misitu na Nyuki. Mikutano 360 ya uhamasishaji ilifanyika kwa jamii zinazozunguka misitu ya hifadhi katika Kanda saba za Wakala wa Misitu. Aidha, wilaya na mikoa imeendelea kuadhimisha siku ya upandaji miti kufuatana na hali ya mvua. Kitaifa siku hii huadhimishwa tarehe 1 Aprili kila mwaka. Mwaka 2012, miti 145,156,884 ilipandwa katika mikoa 17 ya Tanzania bara. Kati ya miche ya miti iliyopandwa, asilimia 74.5 imestawi.

Kuboresha Miundombinu ndani ya Mapori ya Akiba, Hifadhi za Wanyamapori na Misitu. Kazi ya kuimarisha miundombinu imefanyika katika maeneo mbalimbali ya hifadhi za Wanyamapori na Misitu. Ukarabati wa barabara zenye urefu wa kilometa 71 katika Mapori ya Akiba ya Moyowosi, Kigosi, Lwafi na Maswa na kilometa 386 katika Hifadhi za Taifa za Katavi, Ruaha, Mikumi na Saadani umefanyika.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya misitu, jitihada zimefanywa kuboresha miundombinu kwa kujenga barabara mpya zenye urefu wa jumla ya kilometa 48 na kukarabati barabara zenye urefu wa kilometa 487 katika mashamba 15 ya miti ya kupandwa.

Mheshimiwa Spika, Kuwezesha uanzishwaji wa hifadhi za nyuki. Wakala wa Misitu Tanzania umeandaa mwongozo wa kuandaa mipango ya usimamizi wa hifadhi za nyuki. Aidha, hifadhi mbili za ufugaji nyuki za Kang'ata hekta 1,439.16 na Kwenyunga – Magiri hekta 138.62 katika Wilaya ya Handeni ziko katika hatua za awali za kutangazwa baada ya kupata ridhaa ya wananchi katika vijiji husika na mamlaka ngazi ya Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Kukuza muamko na kuendesha kampeni za kuwashawishi Watanzania kujenga utamaduni wa kutembelea vivutio vya utalii. Kupitia maonesho na

maadhimisho mbalimbali, Wizara imeendelea kuwahamasisha Watanzania watembelee vivutio vya utalii. Wakati wa maonesho hayo, Wizara huweka wanyamapori hai pamoja na vivutio mbalimbali vya utalii katika banda lake ambavyo huvutia wananchi wengi na hivyo kuhamasisha utalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, punguzo la gharama (*Offer*) limekuwa likitolewa kwa wananchi kutembelea maeneo ya vivutio kwa gharama nafuu. Kwa mfano, katika maonesho ya Sabasaba safari za kutembelea Hifadhi ya Taifa Mikumi zilikuwa Sh.10,000 kwa mtu mzima na Sh.5,000 kwa mtoto. Kiasi hicho kilijumuisha usafiri, kiingilio na maelezo mbalimbali kutoka kwa wataalam wakati wote wa safari.

Mwitikio ni mzuri kwani mwaka 2011 watalii 770 walishiriki na 790 mwaka 2012. Aidha, vikundi vya utalii wa utamaduni vya Chilunga na Mto wa Mbu vilishirikishwa katika maonesho ya Sabasaba ili kuonesha mafanikio ya utalii wa kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 51 ya uhuru, Bodi ya Utalii ilidhamini tukio la kupanda Mlima Kilimanjaro. Tukio hilo lilihusisha washiriki 38, ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira (8), Askari wa Jeshi la Wananchi Tanzania (5), Kampuni ya bia ya Serengeti (7), Wajumbe wa Mamlaka ya Utalii Zimbabwe (4) na watu wengine (14).

Mheshimiwa Spika, kupanua wigo wa aina za Utalii kwa kuendeleza Utalii unaohusisha huduma za utamaduni, mazingira na makumbusho. Wizara imeanzisha utalii wa

30 APRILI, 2013

kutembea usiku katika Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kuhusu utalii katika maeneo ya kihistoria hususan michoro ya miambani katika Wilaya ya Kondoa na magofu yaliyoko Kilwa Kisiwani na Songo Mnara.

Pia, Wizara ilishiriki tamasha la Utamaduni kwa nchi za Afrika Mashariki (JAMAFEST) lililofanyika Kigali, Rwanda, tarehe 11 hadi 18 Februari 2013. Lengo la tamasha lilikuwa ni kutangaza utamaduni wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia ubunifu wa soko la bidhaa na huduma za kiutamaduni ikiwemo malikale.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa onesho la kudumu kwenye Ubalazi wa Tanzania *Washington* DC Marekani. Onesho hilo linahusu vivutio vya bonde la Oldupai na nyayo za binadamu wa kale (*Zamadamu*) za eneo la Laetoli, Ngorongoro. Onesho hilo limewavutia watalii wa nje kutembelea maeneo ya malikale yaliyopo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuongeza msukumo wa ufugaji nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali na nta kibiashara. Maonesho maalum ya asali yalifanyika sanjari na kongamano la kujadili maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki nchini katika viwanja vya Mwalimu Nyerere (Saba saba)- Dar es salaam tarehe 4 hadi 7 Oktoba, 2012. Pia, siku ya kutundika mizinga imezinduliwa rasmi na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 4 Machi, 2013 katika Wilaya ya Manyoni.

Kuzinduliwa kwa siku hiyo ambayo itakuwa inaadhimishwa kila mwaka kutaongeza hamasa na msukumo katika ufugaji nyuki kwa kuongeza idadi ya mizinga na hivyo

30 APRILI, 2013

kuongeza uzalishaji wa asali. Vilevile, Mizinga 5,000 na mavazi ya kinga 200 yamegawanywa kwenye vijiji vilivyoko kandokando ya hifadhi za Misitua katika kanda saba za Wakala wa Huduma za Misitua.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa ahadi zilizotolewa wakati wa bunge la bajeti mwaka 2012/2013, sekta ndogo ya wanyamapori. Utekelezaji wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyaamapori.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kutoa Amri ya Wanyamapori wa Taifa (*National Game Order*) na Leseni Maamum ya Uwindaji yanaendelea. Aidha, Amri ya Matumizi ya Silaha za kiraia zilizoidhinishwa kwa uwindaji wa kistalii imeandaliwa. Vile vile rasimu ya Kanuni za Uanzishaji wa Kikosi cha Ulinzi wa Wanyamapori inapitiwa na Kanuni za Matumizi ya Silaha za Kiraia zimejadiliwa na wadau na kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, rasimu ya Kanuni za Uchimbaji Madini ndani ya Mapori ya Akiba imejadiliwa na wadau wa ndani na nje na kutolewa maoni. Rasimu hii itapelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupitiwa kwa mara ya mwisho kabla ya kutangazwa.

Aidha, rasimu ya Kanuni ya Ushoroba, Maeneo ya Mazalia na Mtawanyiko wa Wanyamapori itawasilishwa kwa wadau mwezi Juni, 2013 kwa ajili ya kupata maoni.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa Rasilimali ya Wanyamapori. Katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali ya wanyamapori, siku za

30 APRILI, 2013

doria 59,338 zimefanyika ndani na nje ya Mapori ya Akiba.

Watuhumiwa 1,215 wamekamatwa kwa makosa mbalimbali na jumla ya bunduki 85 na risasi 215 za aina mbalimbali zimekamatwa. Kesi 670 zimefunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini. Kati ya hizo, kesi 272 zimekwisha kwa washitakiwa 247 kulipa faini ya jumla ya Shilingi 175,002,420 na washitakiwa 71 kupewa adhabu ya vifungo vya jumla ya miezi 1,192. Aidha, kesi 398 zenye jumla ya washitakiwa 897 bado zinaendelea katika Mahakama mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya operesheni za kiintelijensia katika Wilaya za Liwale na Tunduru ambazo ziliwezesha watuhumiwa 354 kukamatwa na kufunguliwa jumla ya kesi 283 ambazo zinaendelea katika mahakama za Liwale na Tunduru.

Bunduki 435 za aina mbalimbali, risasi 1,129, maganda 514 ya risasi, mbao 10,332 na nyara mbalimbali zenye thamani ya Shilingi 855,013,701.20 zilikamatwa.

Vilevile, Wizara inaendelea na mikakati ya kuzuia, kudhibiti, na kukabili wimbi la ujangili nchini awamu kwa awamu katika maeneo mbalimbali kwa kufanya operesheni kama hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama imeunda kamati ndogo inayoandaa Mpango Kazi wa kuzuia na kudhibiti ujangili. Utekelezaji wa mpango kazi huo utatumia Teknolojia ya kisasa kama vile "*unmanned air vehicles (UAV)*" inayobaini uwepo wa majangili katika maeneo yenye wanyamapori na kuchukua hatua zinazostahili kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua mchango mkubwa wa wananchi katika mapambano dhidi ya ujangili. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wanaosaidiana na Serikali kuwafichua wahalifu na kuwaomba waendeleo na moyo huo wa kizalendo. Natoa rai kwa wananchi wengine wote washiriki mapambano hayo ya kulinda maliasili zetu. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wote kwa ujumla katika juhudi za kuhifadhi wanyamapori kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watu kutoka ndani na nje ya nchi wamekuwa wakifanya ujangili ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa na kuchukuliwa hatua stahiki pale wanapokamatwa. Katika kutekeleza majukumu yao, baadhi ya Wahifadhi na Maafisa Wanyamapori wamekuwa wakiuawa au kujeruhiwa na majangili. Kati ya mwaka 1997 na 2012, Wizara imepoteza watumishi 17 kutokana na kuuawa na majangili. Aidha, kumekuwepo na matukio mengi ya wananchi kujaribu kuwazuia wahifadhi wanyamapori kutenda kazi zao.

Mheshimiwa Spika, yapo matukio mbalimbali ya kuingiza mifugo ndani ya Mapori ya Akiba ambayo yamekuwa yakisababisha mapambano kati ya wafugaji na wahifadhi hasa wafugaji wanapolazimisha kuchukua mifugo kwa nguvu ambayo imekamatwa kisheria kama kielelezo. Mapambano hayo yamesababisha baadhi ya askari na wananchi kuuawa au kujeruhiwa wakati wa tukio.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa wananchi kutambua mchango mkubwa unaotolewa na Watumishi wanaolinda wanyamapori. Hivyo, Jamii inatakiwa kutimiza wajibu wake kwa kuunga mkono na kuwapa moyo Watumishi hawa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufuatilia suala la utorohaji wa wanyamapori hai uliofanyika tarehe 26 Novemba, 2010. Kutokana na uchunguzi uliofanyika hapa nchini, watu sita (6) walituhumiwa kuhusika na usafirishaji huo haramu na walikamatwa na kufikishwa katika Kituo cha Polisi

cha *K/A* na kufunguliwa kesi ya Uhujumu Uchumi Na. EC.4/2011. Maelezo ya awali ya kesi hiyo yamepangwa kutolewa tarehe 7 Mei, 2013.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano yameendelea kufanyika kati ya Wizara na Serikali ya Qatar ili kuruhusu Tanzania kufanya uchunguzi nchini Qatar. Awali, ilipangwa timu ya uchunguzi kutoka Tanzania kwenda Qatar tarehe 27 Januari, 2013. Hata hivyo, uchunguzi nchini Qatar haujafanyika kutokana na ushirikiano hafifu kutoka Serikali ya Qatar.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ulinzi dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya iliendesha siku za doria 3,339 kwa lengo la kulinda uhai wa watu na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu. Halmashauri za Wilaya 26 zenye matatizo hayo zilikusika na kufanikiwa kudhibiti tembo na viboko dhidi ya uharibifu wa mazao na kuwarejesha wanyama hao kwenye maeneo yao ya asili. Aidha, kunguru weusi 185,179 waliuawa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Tanga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali katika kulinda maisha ya watu na mali zao dhidi ya wanyamapori, bado matukio ya uharibifu wa mazao na vifo vinavyotokana na wanyamapori hao yameripotiwa. Kwa bahati mbaya, watu 30 walipoteza maisha na tisa walijeruhiwa. Jumla ya ekari 1,896.7 za mazao ziliharibiwa.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kutoa pole za dhiti kwa wote waliofikwa na majanga hayo. Serikali imetoa kifuta machozi kwa familia za walipoteza maisha na wale waliojeruhiwa cha jumla ya Sh. 31, 800,000/=. Vile vile, wananchi 776 walioharibiwa mazao wamelipwa kifuta jasho jumla ya Sh. 93,573,750/=.

Mheshimiwa Spika, ushirikishaji jamii katika uhifadhi wa wanyamapori; kufuatia mafanikio yaliyopatikana kutokana na kuanzishwa kwa *WMAs*, juhudi zimeendelea kwa kuwezesha wananchi kuanzisha maeneo mengine. Katika

mwaka 2012/2013, Jumuiya sita za Hifadhi zimo katika hatua mbalimbali za kuidhinishwa, ambapo Jumuiya ya Randilen (Monduli) imekamilisha mchakato wa kuanzisha *WMA* na imetangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 21 la tarehe 1 Februari, 2013.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya ILUMA (Kilombero na Ulanga) ipo kwenye hatua za mwisho za kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Aidha, Jumuiya za WAGA (Iringa vijijini, Mbarali na Mufindi), UMEMARUWA (Njombe na Mbarali), MBOMAMINJIKA (Kilwa) na JUHIWANGUMWA (Rufiji) zinaendelea kukamilisha taratibu za kuidhinishwa. Pori jipya la Akiba Piti limeanzishwa katika Wilaya ya Chunya kwa kushirikisha wananchi kwa lengo la kuimarisha uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, miundombinu katika Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba. Katika kuboresha miundombinu, matengenezo ya barabara katika Hifadhi za Katavi (kilomita 119), Ruaha (kilomita 124), Mikumi (kilomita 58) na Saadani (kilomita 85) yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mapori ya Akiba, barabara zimekarabatiwa katika Mapori ya Moyowosi/Kigosi (kilomita 21); Lwafi (kilomita 30) na Maswa (kilomita 20). Vilevile, Kilomita 81 za mipaka zimesafishwa katika Mapori ya Akiba ya Moyowosi/Kigosi (kilomita 31) na Lwafi (kilomita 50).

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania. ili kuwezesha uanzishwaji wa Mamlaka, Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya 2009 inafanyiwa marekebisho ili kutenganisha majukumu ya urekebu na uratibu na yale ya usimamizi. Shughuli za usimamizi zitafanywa na Mamlaka na zile za urekebu na uratibu zitabaki Wizarani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hayo, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria yameandaliwa, rasimu ya muundo wa usimamizi na majukumu ya Mamlaka (structure and functions) pia imeandaliwa. Hatua inayofuata

ni kupeleka rasimu hizi kwa wadau kwa ajili ya kujadiliwa na kuridhiwa. Muswada wa kuanzisha Mamlaka unatarajiwa kuwasilishwa Bungeni mwezi Novemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukusanyaji Maduhuli. Katika mwaka 2012/2013 hadi mwezi Machi 2013, Wizara kupitia Idara ya Wanyamapori imekusanya Sh. 10,761,228,343/= sawa na asilimia 42.75 ya lengo la Sh. 25,175,381,917/=. Mapato hayo yanatokana na uwindaji wa kitalii, utalii wa picha na biashara ya ndege na wadudu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Tanzania ulikadiriwa kukusanya Sh. 12,631,413,244/=. Makusanyo hadi Machi 2013 yamefikia Sh. 13,296,278,179/= sawa na asilimia 105.26 ya makadirio. Fedha hizo zimeendelea kutumika kwa shughuli za kulinda wanyamapori, utafiti na mafunzo, kutoa elimu kwa umma na kukarabati miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Taaluma ya Wanyamapori. Katika mwaka 2012/2013, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka kimedahili wakurufunzi 502 badala ya 550. Lengo halikuweza kufikiwa kutokana na waombaji kukosa sifa za msingi za kujiunga na Chuo pamoja na ada ya kulipia mafunzo. Aidha, katika kujenga uwezo kwa wakufunzi, Chuo kiligharimia mafunzo ya wakufunzi sita kwenye ngazi ya Shahada ya Uzamili na wakufunzi tisa katika ngazi ya Uzamivu.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori, Pasiansi ilifikia lengo la udahili wa wakurufunzi 324. Katika kuboresha miundombinu, ujenzi wa maabara umekamilika na imebakia kuweka samani na mfumo wa gesi. Vile vile, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu- Sekamaganga kimedahili wakurufunzi 110.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (*TAWIRI*) ilifanya tafiti za magonjwa yanayoambukizwa kati ya wanyamapori, binadamu na mifugo. Magonjwa hayo ni kichaa cha mbwa, homa ya

bonde la ufa, kifua kikuu (*TB*) na homa ya vipindi katika ikolojia ya Serengeti. Matokeo ya tafiti hizo yamebainisha kuwa kifua kikuu ni tatizo. Wastani wa asilimia 2.4 ya ng'ombe 1,103 waliochunguzwa kutoka kwa wafugaji 32 walionekana kuwa na kifua kikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wanyamapori, ilibainika kuwa asilimia 10 ya nyumbu 101 waliochunguzwa walikuwa na maambukizi ya *TB*. Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu vyanzo mbalimbali vya maambukizi ya kifua kikuu. Chanzo kimojawapo ni watu kunywa maziwa yasiyochemshwa pamoja na kula nyama isiyopikwa na kuiva.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kichaa cha mbwa, matokeo ya utafiti yameonesha kuwa kuna aina moja ya kirusi cha kichaa cha mbwa (*Africa 1b*) ambacho huathiri mifugo, wanyamapori na binadamu. Kirusi hicho kinatokana na mbwa wa kufugwa. Matokeo ya tafiti hizo yatapelekwa kwa wadau husika ili kuwezesha hatua stahili kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ilifanya sensa nne za kuidadi wanyamapori katika mifumo ikolojia ya Burigi-Biharamulo-Kimisi, Moyowosi-Kigosi, Katavi-Rukwa na sensa ya mamba kwa nchi nzima. Matokeo ya sensa hizo ni kuwa wanyama walioonekana kwa wingi katika mfumo ikolojia wa Burigi-Biharamulo-Kimisi walikuwa takriban swala 1,512, pundamilia 223; Moyowosi-Kigosi tohe 509 na nyati 277; Katavi-Rukwa nyati 18,652 na pundamilia 499. Aidha, idadi ya mamba kwa nchi nzima ilikuwa takriban 5,253.

Mheshimiwa Spika, Taasisi iliendelea kuchunguza tuhuma za uwepo wa sumu ya tumbaku (nikotini) katika asali ya Tanzania ambapo sampuli 24 za asali zilikusanywa kutoka vijiji 13 katika Wilaya za Same, Kongwa, Sikonge, Tabora Mjini, Uyui na Urambo. Matokeo ya uchunguzi huo yalibaini kuwepo kwa kiwango kidogo cha nikotini (chini ya 0.005 nikotini), ambacho ni cha kawaida kwa mahitaji ya mwili wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, utafiti huu ni endelevu. Aidha,

Wizara inakamilisha maandalizi ya ujenzi wa maabara ya kisasa ya utafiti wa nyuki katika eneo la Ofisi za *TAWIRI*, Arusha ambao utakamilika katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Hadi Machi, 2013 watalii wa kimataifa 507,984 walitembelea eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na kukusanya jumla ya Sh. 47,610,714,532/=. Aidha, Mamlaka imekarabati barabara zenye urefu wa jumla ya kilomita 350 ndani ya hifadhi. Vile vile, Mamlaka imenunua magari manne ya doria ili kuimarisha shughuli za ulinzi wa rasilimali za Hifadhi. Kuhusu ujenzi wa jengo la Kitega uchumi Mjini Arusha, tathmini ya awali (*pre-qualification*) katika taratibu za kumpata Mkandarasi imefanyika na ujenzi unatarajiwa kuanza kabla ya mwisho wa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imekamilisha ukarabati wa majosho manne ya mifugo (Alailelai, Embulbul, Meshili na Ndian) pamoja na kujenga bwawa la maji katika eneo la Ngairish kwa ajili ya kuimarisha afya ya mifugo. Mamlaka ilinunua madume bora ya ng'ombe 40, ya mbuzi 20 na ya kondoo 20. Aidha, majike 87 ya ng'ombe yalihalilishwa. Jumla ya mitego 2,500 ya kudhibiti mbung'o iliwekwa katika Kata ya Kakesio mpakani na Pori la Akiba Maswa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilitoa chanjo ya mifugo kama ifuatavyo: Mbuzi 177,965 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na mbuzi 66,088 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa kimeta. Ng'ombe 24,087 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu, ambapo ng'ombe 15,595 walichanjwa dhidi ya Ndigana kali. Vile vile magunia 3,300 ya chumvi ya mifugo yalinunuliwa na kusambazwa katika vijiji vilivyopo ndani ya Hifadhi. Aidha, hadi Machi, 2013 jumla ya Sh. 1,050,000,000/= zilitolewa kwa Baraza la Wafugaji kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na uhakika wa chakula kwa jamii zinazoishi ndani ya eneo la Hifadhi, Mamlaka ilinunua jumla ya magunia 16,100 ya mahindi na kuyasambaza katika vijiji vilivyopo ndani ya Hifadhi. Aidha, magunia ya mahindi

560, sukari kilo 11,050 na kilo 450 za siagi ziligawiwa kwa shule zote za msingi zilizoko ndani ya eneo la Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013, Mamlaka ilichangia utekelezaji wa miradi ya ujirani mwema kama ifuatavyo:- Hifadhi Mazingira Karatu (HIMAKA) Sh. 4,000,000/=; ujenzi wa bweni la wasichana katika shule ya Sekondari ya Wasichana Slahamo Sh. 40,000,000/=; ujenzi wa darasa Sekondari ya Mang'ola Sh. 5,000,000/=; ujenzi wa Wodi ya Wanawake Kijiji cha Kambi ya Simba Sh. 40,000,000/= na madawati 135, kabati nne, meza 12 na viti 12 vya ofisi vilinunuliwa na kukabidhiwa shule ya msingi Jema Oldonyosambu.

Mheshimiwa Spika, aidha, vikundi vinane vya ujasiriamali vilifadhiliwa jumla ya Sh. 40,000,000/=. Miradi sita ya ufugaji kuku ilianzishwa na vikundi 12 vya kutengeneza sanaa kwa kutumia shanga vilifadhiliwa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. 10,000,000.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha ulinzi wa wanyamapori katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, doria za kawaida ziliendeshwa ambapo majangili 43 walikamatwa kwa makosa mbalimbali na jumla ya bunduki nne na risasi 11 zilikamatwa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa, Tanzania. Kufuatia Bunge lako Tukufu kupitisha Azimio la kuanzisha Hifadhi mpya ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane, taratibu za kukamilisha zoezi hili ziko katika hatua za mwisho. Aidha, taratibu za kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Gombe kwa kuongeza eneo la ukanda wa maji katika Ziwa Tanganyika na kupunguza eneo la makaburi, mashamba na nyumba ziko katika hatua za mwisho. Lengo la marekebisho ya mpaka huo ni kulinda rasilimali ya wanyamapori na mazingira yao pamoja na kutatua mgogoro wa ardhi baina ya hifadhi na wananchi wa Vijiji vya Mtanga na Mwamgongo.

Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2013 watalii wa Kimataifa 750,797 walitembelea Hifadhi za Taifa ambapo

jumla ya Sh. 105,139,608,440/= zilikusanywa. Katika kuboresha miundombinu ndani ya Hifadhi za Taifa, jumla ya Kilomita 6,526.5 za barabara zilikarabatiwa katika Hifadhi za Arusha (236.7); Katavi (425); Kilimanjaro (114.5); Kitulo (75); Ziwa Manyara (160); Mikumi (549.1); Mkomazi (615); Ruaha (1,435.2); Rubondo (96); Saadan (422); Serengeti (1,577); Tarangire (746) na Udzungwa (75).

Mheshimiwa Spika, aidha, njia za watembea kwa miguu zenye jumla ya kilomita 41.6 zilikarabatiwa katika Hifadhi za Kilimanjaro (kilomita 30.6), Udzungwa Kilomita sita na Kitulo Kilomita tano. Vile vile, njia ya kurukia ndege katika Kiwanja cha Ndege Seronera imeongezwa kutoka Kilomita 1.5 hadi Kilomita 2.2. Upanuzi huo umewezesha ndege za ukubwa wa kati kama vile aina ya *Fokker* kutua kwenye uwanja huo.

Mheshimiwa Spika, Mikataba ya ujenzi wa nyumba 12 za watumishi katika Hifadhi za Ruaha, Serengeti na Tarangire imekamilika na wakandarasi wapo kwenye maandalizi ya ujenzi utakaoanza mwezi Septemba, 2013. Katika kuimarisha ulinzi Askari Wanyamapori 40 walijiriwa, magari sita ya doria yalinunuliwa na taratibu za ununuzi wa magari 10 zimekamilika, magari hayo yatapatikana mwezi Mei 2013. Aidha, siku za doria 95,283 ziliendeshwa ndani ya Hifadhi za Taifa ambapo jumla ya majangili 2,523 walikamatwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki; Sera na Kanuni. Taratibu za kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ufugaji nyuki ya mwaka 1998 zimeanza ambapo warsha ya kwanza ya wadau imefanyika Desemba, 2012 Dar es Salaam. Warsha nyingine za wadau zitafanyika kuanzia mwezi Mei 2013 kwenye kanda saba za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki. Wizara imeendelea kuviwezesha vyuo vya misitu na ufugaji nyuki kutekeleza majukumu yake. Katika mwaka 2012/2013, jumla ya wakurufunzi 218 wamedahiliwa kama

ifuatavyo:- Chuo cha Misitu Olmotonyi, Arusha 146; Chuo cha Nyuki Tabora 41 na Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi 31. Kati ya wakurufunzi 218 waliodahiliwa, 76 ni kwa udhamini binafsi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa soroveya na ukadiriaji wa gharama za ujenzi wa jengo la Maktaba na Maabara katika Chuo cha Viwanda vya Misitu, Moshi, taratibu za kumpata mkandarasi zinafanyika ili kazi ya ujenzi ianze. Aidha, Chuo cha Ufugaji Nyuki, Tabora kimekarabati majengo mawili, mifumo ya maji machafu ya nyumba mbili za watumishi, kukamilisha ujenzi wa bwalo la chakula na utayarishaji wa ramani ya chuo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania umeendelea kutekeleza majukumu ya kiutendaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuendeleza ufugaji nyuki. Katika kuimarisha ufugaji nyuki, eneo lenye ukubwa wa hekta 56,290 kwa ajili ya kuanzisha hifadhi ya nyuki limeainishwa katika Kanda ya Ziwa. Aidha, makundi ya nyuki 631 kwenye manzuki tatu zenye mizinga 882 yalitunzwa katika Wilaya za Bukombe, Biharamulo na Maswa.

Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa wafugaji nyuki 162 yalitolewa katika vijiji 23 na maeneo matatu kwa ajili ya kuanzisha hifadhi za nyuki yaliainishwa huko Geita, Biharamulo na Nyantakala. Mizinga 500 ya nyuki ilisambazwa kwa wafugaji Kanda ya Kusini (Ruangwa, Mtwara, Newala, Tunduru na Namtumbo).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa kudhibiti mabaki ya kemikali katika asali nchini, sampuli 54 za asali zilikusanywa na kufanyiwa uchambuzi wa kemikali katika maabara nchini Ujerumani. Matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha kuwa asali ya Tanzania ni nzuri na inakidhi viwango vinavyokubalika katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Spika, pili, elimu kwa umma na uhamasishaji. Uhamasishaji kuhusu elimu ya uhifadhi wa misitu na ufugaji nyuki ulifanyika kupitia vipindi 78 vya Redio, saba vya Televisi, mikutano na semina 83. Aidha, vipeperushi na machapisho mbalimbali yalisambazwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara ilitoa elimu kuhusu njia sahihi za kufuga nyuki kwa wafugaji 979 ikijumuisha vikundi 72 katika Vijiji 67 vya Wilaya za Kanda za Kaskazini na Mashariki. Vikundi 52 na mafundi seremala 52 walipatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki katika Wilaya za Njombe, Ileje, Mbozi, Chunya, Rungwe, Kilolo na Ludewa.

Mheshimiwa Spika, tatu, ushiriki wa wadau katika kuendeleza misitu. Katika jitihada za kuendeleza ushirikishwaji wa sekta binafsi kupanda miti kibiashara, vikundi 16 vya wakulima wa miti vimeundwa na kufanya jumla ya vikundi 37. Vikundi hivi vyenye jumla ya wanachama 2,369 vimewezeshwa kupanda miti 2,530,144 katika eneo lenye jumla ya hekta 2,277 katika Wilaya za Tukuyu, Njombe, Kilolo na Mufindi. Aidha, vikundi hivyo vimewezeshwa kutayarisha mipango ya utekelezaji wa kilimo cha miti ya matunda.

Mheshimiwa Spika, nne, usimamizi wa mashamba ya miti. Miche 12,956,354 ya miti laini ilikuzwa na kupandwa kwenye eneo la hekta 3,756, ikiwa ni asilimia 90 ya lengo la kupanda miche 14,440,000 katika mashamba 15 ya miti. Aidha, tathmini ya miti imefanyika katika mashamba 14 kwa ajili ya kupata takwimu za kuandaa mipango ya usimamizi. Vile vile, eneo la mashamba ya miti ya kupandwa lenye jumla ya hekta 3,756.04 limesafishwa na hekta 14,655.42 zilipogolewa.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mipaka na kuzuia moto ndani ya misitu, barabara za kuzuia moto zenye urefu wa jumla ya kilomita 1,649.3 zimesafishwa katika mashamba ya Sao Hill (kilomita 1,147); Matogoro (kilomita 52); Shume (kilomita 101); Ukaguru (kilomita 26); Kiwira (kilomita 27.6); Kawetire (kilomita 94.7); Rondo (kilomita 50); Rubya (kilomita 25); Mtibwa (kilomita 68) na Longuza (kilomita 58).

Mheshimiwa Spika, tano, usimamizi wa Misitua ya Hifadhi. Uihakiki wa mipaka yenye jumla ya kilomita 2,563.42 umefanyika katika Kanda ya Kati (kilomita 60.92); Kanda ya Magharibi (kilomita 1,117.60); Kanda ya Mashariki (kilomita 100.30); Kanda ya Ziwa (kilomita 142.30) na Kanda ya Kaskazini (kilomita 1,152.30). Aidha, Mipango 15 ya usimamizi wa misitu iliandaliwa pamoja na kusimika maboya 479 katika Kanda za Ziwa na Kati. Vilevile, ramani nane zilichorwa na mabango 255 ya tahadhari yaliwekwa kwenye misitu ya Kanda za Magharibi na Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, katika kuongoa maeneo yaliyovamiwa, wavamizi wa hifadhi za misitu na mazingira asilia waliondolewa katika misitu ya Mkwani Hills, Nyahua Mbuga, Uyui, Kigwa-Rubuga, Goweko, North Ugalla, Mpandaline, Mbeya Range, Kilimanjaro, Chome, Rufiji Delta, Amani, Magamba, Nilo, Mkingu, Geita, Biharamulo na Sayaka.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Kanda ya Magharibi, wahalifu 98 walikamatwa, kati yao 48 walitozwa faini ya Sh. 201,920,000/= na watuhumiwa 50 kesi zao zipo Mahakamani. Vile vile, wavamizi 516 waliondolewa katika hifadhi za misitu zilizopo Kanda ya Kaskazini na kesi 34 zipo Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, siku za doria 109,522 zilifanyika ndani na nje ya maeneo ya misitu. Kutokana na doria hizo mazao mbalimbali ya misitu yaliyokamatwa yalitaifishwa na kuuzwa ambapo jumla ya Sh.1, 588, 549,727 zilikusanywa.

Mheshimiwa Spika, sita, kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli. Wakala umewezesha Halmashauri za Wilaya 26 kufanya vikao vya Kamati za Uvunaji za Wilaya pamoja na kutayarisha mipango 10 ya uvunaji. Aidha, Mfumo wa ukusanyaji wa maduhuli umeimarishwa kwa kufanya ukaguzi na uhakiki katika maeneo mbalimbali. Hadi Machi 2013, Sh. 33,182,997,357 zilikusanywa sawa na asilimia 56.51 ya lengo la kukusanya Sh. 58,718,747,409/=.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Misitu Tanzania. Hadi

Machi, 2013 Mfuko ulikusanya Sh. 2,229,097,230/= ikiwa ni asilimia 63.7 ya lengo la mwaka 2012/2013 la kukusanya Sh. 3,500,000,000/=. Katika mwaka 2012/2013, Mfuko unatarajia kuwezesha miradi 70 ya wadau mbalimbali wa misitu na nyuki kwa kutoa Sh. 1,940,810,000/=. Jumla ya miradi mipya 48 na 52 inayoendelea iliwezesha kwa kupewa jumla ya Sh. 1,380,478,612/=.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa katika miradi hiyo ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu manufaa na umuhimu wa matumizi ya nishati mbadala; ushirikishaji jamii katika uanzishwaji wa hifadhi za misitu ya jamii na hifadhi za nyuki; upandaji miti na ufugaji nyuki. Vile vile, Mfuko uliwezesha tafiti mbalimbali kwa ajili ya kuboresha usimamizi wa misitu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mbegu za Miti. Hadi Machi, 2013, kilo 5,103 za mbegu za miti zenye thamani ya Sh. 169,309,385/= ziliuzwa nchini na kilo 297 zenye thamani ya Sh. 40,511,100/= ziliuzwa nje ya nchi. Hadi Machi 2013, Wakala iliiza miche 24,789 yenye thamani ya Sh. 24,249,600/=. Vile vile, vyanzo vinne vya mbegu bora za miti ya Mkaratusi, Mkorimbia, Mfudufudu na Miembe vilianzishwa. Halikadhalika, Wakala uliendesha mafunzo ya muda mfupi kuhusu utunzaji wa miche ya miti kwa washiriki 43 kutoka Mikoa ya Morogoro na Iringa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Taasisi ya Utafiti wa Misitu, Tanzania imekamilisha ujenzi wa majengo ya utawala na maabara ya Makao Makuu katika eneo la Kingolwira, Manispaa ya Morogoro na kuhamia. Aidha, Taasisi inaendelea na utafiti wa mahusiano kati ya miti ya kupandwa na udongo, kazi hii imeanzia katika mashamba ya miti Meru/ Usa. Matokeo ya awali yanaonesha uwepo wa upungufu wa rutuba unaosababishwa na uondoaji wa mabaki ya miti.

Mheshimiwa Spika, Taasisi imefanya utafiti wa familia 98 za miti ya misindano (*Pinus maximinoi*) katika Mkoa wa Iringa na matokeo ya awali yameonesha kuwa miche

michache katika familia 16 kati ya 98 imeota na imepandwa kwenye arboreta (Kihanga arboretum) kwa uangalizi ili kuwa chanzo cha mbegu hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, pia, Taasisi inaendelea kushirikiana na Taasisi za Utafiti za Afrika Mashariki pamoja na Shirika la Kimataifa liitwalo Central American and Mexico Coniferous Resources (CAMCORE) la Kuhifadhi na Kuongeza Ubora wa Miti. Matokeo ya ushirikiano huo ni kuandaa mpango mkakati wa kuboresha miti ya kupandwa katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ikishirikiana na Wakala wa Misitu inaendelea kufanya utafiti wa uoteshaji na ukuzaji wa familia mbalimbali za Mitiki na Mikaratusi kwa lengo la kusambaza kwa wadau. Aidha, mashamba darasa manne ya miti ya kuni na mkaa yenye ukubwa wa hekta moja kila moja katika Wilaya za Morogoro (Kata ya Mikese na Gwata) na Bagamoyo (Kata ya Msata na Mbwewe) yameanzishwa. Kutokana na elimu waliyoipata wakulima wameweza kuzalisha miche 28,000 ya miti ya kuni na mkaa. Taasisi inaendelea kutoa elimu ili kuwezesha wakulima kuanzisha mashamba makubwa.

Mheshimiwa Spika, Taasisi imehamasisha utengenezaji na utumiaji wa majiko banifu ya kuni katika Vijiji vya Gwata na Lubungo, Wilaya ya Morogoro na Vijiji vya Kihangaiko na Kwang'andu katika Wilaya ya Bagamoyo. Jumla ya familia 50 katika vijiji hivyo zimenufaika na teknolojia hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta Ndogo ya Utalii; Sera na Sheria. Wizara imeanza kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 ambapo rasimu ya awali ya Sera hiyo imeandaliwa. Sera mpya ya Taifa ya Utalii itakamilika mwaka 2013/2014. Vile vile, Wizara imekamilisha Kanuni za Tozo ya Maendeleo ya Utalii (GN. No. 218 ya mwaka 2012) na ukusanyaji wa Tozo la Kitandasiku (bed night levy) utakaoanza rasmi Julai, 2013 kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa utalii; zoezi la kupanga hoteli katika daraja limeendelea ambapo mwaka 2012/2013, zoezi hilo limefanyika katika Mkoa wa Manyara. Kati ya huduma za malazi 17 zilizohusika, mbili zimetunukiwa nyota nne ambazo ni *Lake Manyara Tree Lodge* na *Kikoti Safari Camp*; 11 zimetunukiwa nyota tatu na nne zimetunukiwa nyota mbili. Sambamba na jitihada za kuboresha huduma za malazi, idadi ya watalii wanaofika nchini imeendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizokusanywa zinaonesha kuwa idadi ya watalii wa Kimataifa imeongezeka kutoka 867,994 mwaka 2011 kufikia 1,077,058 mwaka 2012. Takwimu hizo zinaonesha kuwa takriban asilimia 61 ya watalii wa Kimataifa wanatoka katika nchi za Marekani, Italia, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, na Hispania.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa maduhuli; katika mwaka 2012/2013, Wizara ililenga kukusanya Sh. 11,091,246,108/= kutokana na Tozo ya Maendeleo ya Utalii na leseni mbalimbali za biashara ya Utalii. Hadi Machi, 2013 jumla ya Sh. 2,696,571,256/= zilikusanywa. Makusanyo hayo ni asilimia 24.3 ya makisio ya mwaka 2012/2013. Hata hivyo, ifikapo mwishoni mwa mwaka 2012/2013, huenda lengo la makusanyo halitafikiwa kutokana na kuchelewa kuanza kwa Tozo ya Maendeleo ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii Tanzania. Mkakati wa miaka mitano wa kutangaza utalii wa Kimataifa 2012/2013 - 2016/2017 ulizinduliwa mwezi Novemba, 2012. Mkakati huo unalenga kuelekeza juhudi za utangazaji katika masoko machache zaidi yenye tija ikiwa ni pamoja na masoko yenye uwezekano mkubwa wa kukua kwa utalii ambayo ni masoko ya India, Afrika Kusini, Brazil, Urusi, China, Uturuki na Nchi za Ghuba.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mkakati huo unazingatia mbinu za kisasa za kutangaza utalii zinazojumuisha matumizi ya TEHAMA; ziara za utangazaji utalii; misafara ya Waandishi

wa habari na Mawakala wa Utalii kutoka nje; kutumia Mabalazi wa Hiari (*Tourism Goodwill Ambassadors*) na wawakilishi wa kutangaza utalii katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mkakati huo umeanza kwa kufanya mikutano mitano katika Mikoa ya Dar es Salaam (2), Iringa (1), Morogoro (1) na Arusha (1) ili kuutambulisha Mkakati na kuhamasisha wadau kuutumia.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii kwa kushirikiana na Shirika la Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, imeweka matangazo katika kiwanja cha Seattle Sounders nchini Marekani ambacho kinatumika kwa soka na mpira wa miguu wa Kimarekani. Matangazo hayo yalianza kuoneshwa Mei, 2012 na yataendelea hadi Aprili, 2013 ambao ni mwisho wa msimu.

Mheshimiwa Spika, Bodi kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Utalii Tanzania (TCT), ilipokea mapendekezo 319 yaliyotolewa na wadau kuhusu kuunda utambulisho wa pekee (*Tanzania Destination Brand*).

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo yalichambuliwa na kupatikana matano bora ambayo yatawasilishwa tena kwa wadau ili kupigiwa kura kwa lengo la kupata pendekezo moja litakalotumika kwa utambulisho wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Bodi iliendelea kuhamasisha uanzishwaji wa miradi ya utalii wa kiutamaduni ambapo vikundi jamii vya utalii wa utamaduni vimeongezeka kutoka 41 mwaka 2012 hadi 47 mwezi Machi, 2013 kati ya 50 vinavyotarajiwa kufikiwa mwezi Juni, 2013. Mwongozo wa uanzishaji wa miradi ya utalii wa kiutamaduni upo na utaendelea kusambazwa kwa wadau ili kuhamasisha uanzishwaji wa miradi nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi na wadau mbalimbali wa ndani na nje kwa kushiriki kupigia kura vivutio

vitatu vya utalii Tanzania vilivyoingizwa katika shindano la kutafuta maajabu saba ya asili ya Bara la Afrika lilokamilika Desemba, 2012. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vivutio vyote vitatu yaani Hifadhi ya Serengeti, *Crater* ya Ngorongoro na Mlima wa Kilimanjaro, vilitangazwa rasmi na Taasisi ya *Seven Natural Wonders* kuwa kati ya maajabu saba ya asili ya Bara la Afrika. Kuingia kwa vivutio vya Tanzania katika orodha hiyo ni heshima kubwa kwa nchi yetu. Hadhi hii mpya ya vivutio hivyo vya utalii itaongeza umaarufu wa nchi yetu na kuongeza idadi ya watalii wanaokuja nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Watanzania kuvitembelea ili kuvifahamu na kuvifurahia vivutio hivyo na kuvitangaza kila wanapopata fursa ya kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii umeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada katika tasnia ya Ukarimu na Utalii. Katika mwaka wa masomo 2012/2013, Wakala umedahili wakurufunzi 249 kati ya hao, 72 wapo Kampasi ya Bustani, 92 Temeke na 85 Arusha.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Chuo kimedahili Wakurufunzi 249 badala ya 315 waliotarajiwa. Upungufu huo umetokana na waombaji wengi kukosa sifa za kujiunga. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Chuo kitaanzisha programu za awali (*Foundation Courses*) ili wasio na sifa za kutosha wafikie kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo, utaratibu wa kuwatembeza watalii katika Jiji la Dar es Salaam umeanza. Utaratibu huo umelenga kukuza utalii wa ndani na kuongeza mapato ya Chuo. Tangu kuanza utaratibu huo mwezi Januari, 2013 hadi mwishoni mwa mwezi Machi, 2013 jumla ya watalii wa ndani 280 wametembezwa katika vivutio mbalimbali vilivyoko Jijini Dar es Salaam na Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale; Sera na Sheria, kufuatia Sera ya Malikale 2008, Wizara imeendelea na marekebisho ya Sheria ya Mambo ya Kale, Sura 333 ya Sheria za Tanzania kwa kuendesha mikutano mitatu ya kukusanya maoni ya wadau. Uchambuzi wa maoni ya wadau utatumika katika kuandaa mapendekezo yatakawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, uhifadhi na uendelezaji wa Rasilmali za Malikale; ukarabati wa magofu ya kihistoria ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara umefanyika kwa asilimia 80. Aidha, Wizara imeanza taratibu za ujenzi wa kituo cha Kumbukumbu na Taarifa Amboni katika Mkoa wa Tanga. Kituo hicho kitaonesha kumbukumbu za urithi wa utamaduni katika eneo hilo na maelezo yanayotoa historia ya chimbuko la eneo hilo. Taratibu za kukarabati nyumba ya mtumishi katika kituo cha Kaole, Bagamoyo zimeanza.

Mheshimiwa Spika, Wizara katika kupanua wigo wa vivutio vya urithi wa utamaduni na kuhifadhi nyayo za binadamu wa kale za Laetoli, imetangaza zabuni ili kumpata Mtaalam Mshauri wa kuandaa michoro ya jengo la Makumbusho ya kuhifadhi nyayo hizo ambapo kampuni saba za ushauri zimejitokeza kuomba kufanya kazi hiyo. Kati ya kampuni zilizojitokeza, mbili ni za nje na tano ni za hapa nchini. Kazi ya kuipata kampuni ya ushauri inatarajiwa kukamilika Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeboresha miundombinu katika vituo vya Isimila, Lugalo, Ujiji na Tongoni ili kuimarisha uhifadhi wa malikale. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa uzio na mfereji wa maji ya mvua kwa ajili ya kuzuia mmonyoko wa ardhi katika kituo cha Isimila; ukarabati wa Mnara wa Lugalo katika Mkoa wa Iringa; kukamilisha ukarabati wa jengo la ofisi Tongoni, kukamilisha ujenzi wa jengo la Kumbukumbu na Taarifa Kituo cha Ujiji, Kigoma na kuweka vioneshwa katika Makumbusho hiyo.

Mheshimiwa Spika, utangazaji na ushirikishwaji wa

jamii; elimu ya uhifadhi shirikishi na uendelezaji wa malikale kwa jamii zinazozunguka maeneo yenye rasilimali za malikale ni endelevu. Wizara imetoa elimu ya uhifadhi wa malikale kwa wakazi wa Vijiji vya Pahi, Mnenia na Kolo katika Wilaya ya Kondoa kupitia vikundi vyao vya kulinda na kuhifadhi maeneo yenye Michoro ya Miambani.

Mheshimiwa Spika, aidha, elimu imetolewa kwa wananchi wa Kilwa kuhusu uhifadhi shirikishi wa Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara na kujengewa uwezo katika kuyahifadhi na kuyakarabati. Wananchi hao wamehamasishwa kuunda na kujiunga na vikundi mbalimbali vya kijamii ili kutumia fursa zilizopo za utalii wa utamaduni kujiongezea kipato na hivyo kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara kwa kutumia njia ya Televisheni na Redio (*TBC1, ITV na Channel 10*) imeendelea kuelimisha umma juu ya Sera ya Malikale, uhifadhi endelevu wa malikale, maendeleo ya urithi wa utamaduni na Tamasha la Kumbukizi la Vita vya Majimaji na Utalii. Vipindi nane kuhusu maeneo ya wapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika yaliyoko Wilaya ya Nachingwea katika Mkoa wa Lindi vilitangazwa.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa Malikale; Wizara kwa kushirikiana na Kitengo cha Hifadhi ya Mazingira ya Bahari na Maeneo Tengefu (*Marine Parks and Reserves*), Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Shirika la Bandari Zanzibar, Idara ya Mambo ya Kale, Makumbusho na Nyaraka- Zanzibar na Kituo cha Urithi wa Utamaduni cha Uholanzi ilifanya soroveya baharini katika eneo la Kisimani Mafia na kubaini kuwepo kwa mabaki ya meli, masalia ya vigae na sarafu za karne ya 11 na 12. Aidha, kazi ya utambuzi na uwekaji wa kumbukumbu za urithi wa utamaduni uliomo baharini katika Kisiwa cha Mafia inaendelea.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa maduhuli; Katika mwaka 2012/ 2013, Wizara kupitia Idara ya Mambo ya Kale hadi kufikia Machi, 2013 imekusanya Sh. 1,124,048,564/=, hivyo kuvuka lengo la kukusanya Sh. 750,000,000/= . Ongezeko hili

ni sawa na asilimia 149.87 kutokana na kupanda kwa ada za viingilio katika maeneo ya vivutio vya utalii wa kitamaduni.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kisheria ya kutafiti, kuhifadhi, kutunza na kuelimisha umma kuhusu Urithi wa Taifa. Kwa mwaka 2012/2013, tamasha la Kumbukizi ya Vita vya Majimaji na Utalii limefanyika katika Mkoa wa Ruvuma tarehe 25 hadi 27 Februari, 2013 na kujumuisha Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Morogoro, Iringa, Njombe, Ruvuma, Simiyu, Kilimanjaro, Mbeya na Pwani.

Mheshimiwa Spika, katika kuhifadhi urithi wa Taifa, Shirika limeendelea na ujenzi wa uzio katika Makumbusho ya Taifa ya Majimaji, Songea katika Mkoa wa Ruvuma na Makumbusho ya Mwalimu J. K. Nyerere, Butiama, Mara.

Mheshimiwa Spika, katika kutoa elimu kwa umma, Shirika limeandaa na kusambaza vipeperushi 10,000 katika shule, taasisi, hoteli za kitalii na wadau wengine. Aidha, jamii wakiwemo watoto na wanafunzi wamehamasishwa kutembelea Makumbusho kupitia vipindi vya televisheni vinavyoendeshwa na Shirika la Makumbusho ya Taifa kwa kushirikisha wataalam wa makumbusho na Nyumba ya Utamaduni, *TBC1* na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, huduma kwenye Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni zimeimarishwa na kuboreshwa. Shirika limekamilisha Mradi wa Maktaba kwa Ajili ya Watu Wazima (*Thank You Small Library for Adult*) na Maktaba kwa Ajili ya Watoto (*Thank You Small Library for Children with Smart Tree*) ili kukuza ubunifu wa watoto.

Mheshimiwa Spika, Maktaba ya watoto imewekewa *computer* 12 maalum kwa ajili yao zenye lengo la kuwafundisha lugha na maarifa anuwai.

Maktaba hizi zimekamilishwa kwa kwa ushirikiano wa Shirika la *UNWTO Step Foundation* pamoja na Taasisi ya Wanawake na Maendeleo (UWAMA). Natoa shukrani kwa

Taasisi hizo kwa msaada huu mkubwa wa nchi yetu na kutoa rai kwa Watanzania kutembelea makumbusho hii ili kujifunza.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uratibu, utawala na maendeleo ya rasimali watu; Mpango Mkakati wa Wizara 2010-2013 umefanyiwa mapitio na kuandaa Mkakati mpya kwa kipindi cha Julai, 2013 hadi Juni, 2016. Mkakati huo umeainisha maeneo sita ya vipaumbele ambayo ni kuhifadhi maliasili na malikale; kuendeleza na kutangaza utalii; kuboresha mifumo ya ukusanyaji maduhuli; kushirikisha wadau katika uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii; kujenga uwezo wa Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kudumisha ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika kutoa elimu kuhusu uhifadhi na uendelezaji utalii, Wizara iliandaa na kurusha vipindi vinne vya redio na 16 vya televisheni, kuweka taarifa za matukio mbalimbali ya Wizara kwenye tovuti na mitandao ya kijamii pamoja na kuchapisha na kusambaza nakala 4,000 za Jarida la Maliasili, nakala 1,500 za kalenda. Aidha, mikutano nane ya Waandishi wa Habari ilifanyika pamoja na kutoa taarifa 15 kwa umma. Pia, kipindi maalum kuhusu mafanikio ya Awamu ya Nne kiliandaliwa na kurushwa kupitia vituo vitatu vya televisheni.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013, katika jitihada za kukabiliana na upungufu wa watumishi, Wizara imepewa kibali cha kuajiri watumishi 617 na taratibu za kuajiri zinaendelea katika Mamlaka husika. Wizara imepandisha vyeo watumishi 197 wa kada mbalimbali na watumishi sita wamebadilishwa cheo.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi na kuboresha utendaji, Wizara imewezesha watumishi 103 kuhudhuria mafunzo mbalimbali. Kati ya hao, watumishi 72 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na 31 mafunzo ya muda mrefu. Aidha, watumishi 68 wameshiriki Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara (SHIMIWI) katika Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea pia kuwahudumia watumishi waliojitokeza na wanaoishi na virusi vya UKIMWI kwa kutoa fedha kwa ajili ya kununulia virutubisho na lishe bora. Vile vile, Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi ulifanyika mwezi Machi, 2013 ili kudumisha utawala bora na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara; pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali katika juhudi za kulinda, kuhifadhi, kuendeleza na kusimamia maliasili, malikale na uendelezaji utalii.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizo ni uhaba wa fedha, watumishi na vitendea kazi katika kutekeleza baadhi ya programu za Wizara hasa katika Sekta za Wanyamapori, Misitu na Malikale; mwamko mdogo wa Watanzania wazawa kutembelea vivutio vya utalii; ushirikiano hafifu wa wadau katika uhifadhi wa maliasili na malikale; kubomolewa kwa majengo ya kihistoria hususan mijini; uchomaji moto misitu; kukabiliana na ujangili na ubovu wa miundombinu katika maeneo yaliyohifadhiwa na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za maliasili na malikale.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kukabili changamoto. Katika kukabiliana na changamoto hizi, Wizara imepanga mikakati mbalimbali kupitia Mpango Mkakati wake 2013 – 2016. Mikakati hiyo ni kuendelea kuajiri watumishi wapya kulingana na ikama iliyopitishwa; kuongeza ushiriki wa wadau mbalimbali katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili, malikale na shughuli za utalii; kukuza utalii wa ndani kwa kuhamasisha jamii kutembelea vivutio vya utalii; kufanya mapitio ya Sera na Sheria; kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji maduhuli na kuongeza bajeti ya ulinzi, uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za Maliasili na Malikale.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa utekelezaji na malengo kwa mwaka 2013/2014. Sekta Ndogo ya Wanyamapori; ulinzi, usimamizi wa wanyamapori na

ushirikishwaji jamii. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za wanyamapori kwa kuendelea kufanya doria ndani na nje ya Mapori ya Akiba kwa kuendesha siku za doria 100,000.

Mheshimiwa Spika, vile vile, miundombinu, vitendea kazi na huduma zitaboreshwa kwa watumishi katika vituo 27 kwenye Mapori ya Akiba na Kanda nane za Kikosi Dhidi Ujangili. Aidha, Wizara itafanya mapitio ya Kanuni mbili (2) na kuandaa kanuni mpya tatu (3) za Kikosi cha Ulinzi wa Wanyamapori; Ushoroba, Maeneo ya Mazalia na Mtawanyiko wa Wanyamapori na Matumizi ya Silaha za Kiraia.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza ushiriki wa wadau katika usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itakamilisha uanzishaji wa maeneo matatu ya *WMAs*.

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo ni WAGA katika Wilaya za Iringa Vijijini, Mbarali na Mufindi; UMEMARUWA Wilaya za Mbarali na Njombe na ILUMA Wilayani Kilombero na Ulanga. Aidha, Wizara itaendelea kutoa gawio la asilimia 25 ya fedha zitokanazo na uwindaji wa kitalii kwa Halmashauri za Wilaya 42 na *WMAs* 16 ili kuziongezea uwezo wa kusimamia rasilimali za wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za wanyamapori na kuboresha uwezo wa kukusanya maduhuli, Wizara itakamilisha uanzishwaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania ifikapo Novemba 2013.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutekeleza mikataba na makubaliano ya Kikanda na Kimataifa ya *RAMSAR*, *AEWA*, *CMS*, *Lusaka Agreement Task Force* na *CITES*. Wizara pia itaendelea kushiriki katika maonesho mbalimbali ndani na nje ili kujiimarisha katika masuala ya uhifadhi endelevu wa wanyamapori nchini na kuboresha ushirikiano katika masuala ya uhifadhi wa rasilimali ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Vyujo vya Taaluma ya Wanyamapori vinatarajia kudahili wakurufunzi 1,020 ambapo Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka kinatarajia kudahili wakurufunzi 496 pamoja na kugharimia mafunzo kwa wakufunzi watano kwenye ngazi ya Uzamili na tisa katika mafunzo ya Uzamivu.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Chuo kimepanga kuendelea kuimarisha miundombinu ya maji chuoni na kujenga madarasa mawili pamoja na kumaliza mapitio ya Mpango Mkakati (*Strategic Plan*) wake ikiwa ni pamoja na kuandaa Mpango wa Biashara (*Business Plan*).

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori, Pasiansi kinatarajia kudahili wakurufunzi 324 na kukamilisha ujenzi wa maabara kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Aidha, Kituo cha Mafunzo ya Usimamizi wa Maliasili kwa Jamii cha Likuyu- Sekamaganga kinatarajia kudahili wakurufunzi 200.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania litajenga nyumba 29 katika hifadhi za Arusha (2), Katavi (3), Kilimanjaro (2), Mikumi (2), Mkomazi (6), Ruaha (10), Rubondo (1), Serengeti (2) na Udzungwa (1) na barabara mpya zenye urefu wa jumla ya Kilomita 115. Aidha, ukarabati utafanyika katika barabara zenye jumla ya kilomita 6,026; viwanja 12 vya ndege na Kilomita 41.6 za njia za kutembea kwa miguu katika hifadhi za Ruaha na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma katika hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, Shirika litajenga mahema kwa ajili ya kulia chakula, vivuli vya kupumzikia na kuboresha malango ya kuingilia. Vile vile, Shirika litanunua magari 43, ndege mbili za doria na *excavator, low loader, low bowser, roller compactor, dumper truck, tractor, water bowser* kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro itajenga nyumba moja ya familia sita

za wafanyakazi pamoja na kuweka uzio kuzunguka nyumba za wafanyakazi eneo la Kamyn, ujenzi wa jengo la mapokezi uwanja wa ndege Ndotu, ujenzi wa jiko kwenye kambi ya kulala wageni ya Simba A pamoja na ujenzi wa nyumba moja ya askari eneo la Lositete. Pia kuendelea na ujenzi wa jengo la kitega uchumi (kwa ubia) lenye ghorofa 10 Mjini Arusha.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2013/2014, maeneo ya kihistoria na urithi wa kitamaduni ambayo yamo kwenye eneo la hifadhi ya Ngorongoro, yatasimamiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kuhakikisha uwepo wa uwiano wa viwango vya maeneo ambayo yametangazwa kuwa Urithi wa Dunia. Maeneo hayo ni pamoja na Oldupai, Laetoli, Ziwa Ndotu pamoja na maeneo mengine ya urithi wa utamaduni yaliyopo Ngorongoro. Hata hivyo, maeneo hayo yataendelea kusimamiwa kwa kutumia Sera na Sheria ya Mambo ya Kale.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imepanga kununua mitambo miwili (*grader na excavator*) ya kutengeneza barabara, magari mawili kwa ajili ya kuimarisha doria, basi moja kwa ajili ya utalii wa ndani, gari moja kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa, basi moja la wafanyakazi na gari moja kwa ajili ya kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli kwenye lango la Naabi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mamlaka itaendelea kusaidia miradi ya maendeleo ya jamii kwa kujenga jengo kwa ajili ya kuhifadhi na kuchakata asali Endulen, kuendeleza mradi wa wenyeji waliohamishiwa Jema Oldonyosambu, kuchangia gharama za matibabu kwa ajili ya wenyeji Hospitali ya Endulen, pamoja na ujenzi wa majosho na kuboresha mifugo Ngairish.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori itaendeleza utafiti wa wanyamapori nchini pamoja na kuidadi wanyamapori katika maeneo mbalimbali ya nchi na kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa kuhifadhi Tembo na Faru.

Mheshimiwa Spika, aidha, Taasisi kupitia Kituo cha Utafiti wa Wanyamapori Njiro itaendelea na ujenzi wa maabara ya utafiti wa nyuki. Vile vile, kituo kitaendelea na utafiti wa mahusiano kati ya nyuki na mimea, maadui wa nyuki aina ya *varroa destructor* na kukamilisha maandalizi ya Mpango Mkakati wa Utafiti wa Ufugaji Nyuki Tanzania (*Beekeeping Research Master Plan*).

Mheshimiwa Spika, Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki; Sera, Sheria na Kanuni, ili kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu na nyuki, Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Misitu ya mwaka 1998 na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya mwaka 1998 na kuzisambaza kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatarajia kufanya mapitio ya kanzi ya misitu na nyuki nchini (*NAFOBEDA*) na kuendesha mafunzo ya matumizi ya kanzi hiyo kwa Maafisa Misitu na nyuki 120 kutoka Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Morogoro. Aidha, Wizara itafanya tathmini ya Asasi zinazojihusisha na uhifadhi wa misitu na ufugaji nyuki hapa nchini ili kurahisisha uratibu katika usimamizi wa rasilimali hizo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kuwezesha uanzishwaji wa misitu 15 ya hifadhi za vijiji katika Mikoa ya Morogoro, Tanga na Ruvuma, pamoja na hifadhi tano za nyuki za vijiji katika Mikoa ya Rukwa, Kigoma na Tabora.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki vinatarajia kudahili jumla ya wakurufunzi 296 katika mwaka 2013/2014 kama ifuatavyo:-

Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora 63; Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi 30 na Chuo cha Misitu Olmotonyi 203. Vile vile, Wizara itaendelea kuwezesha Vyuo vya Misitu na Ufugaji Nyuki kutekeleza majukumu yake. Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi kitaanza ujenzi wa maktaba. Chuo cha Ufugaji Nyuki, Tabora kitakarabati nyumba mbili za Walimu; kuweka samani katika ofisi za Walimu, kufunga mtandao wa mawasiliano na kuweka samani na majiko katika bwalo la chakula.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, utaelekeza juhudi katika utekelezaji wa sheria, kuimarisha mipaka ya misitu, ukarabati wa maeneo yaliyoharibika na vyanzo vya maji, uendelezaji mashamba ya miti na ufugaji nyuki na usimamizi wa rasilimali ya misitu na nyuki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa sheria. Ili kudhibiti biashara na uvunaji haramu wa mazao ya misitu na nyuki, jumla ya siku za doria 20,700 zitaendeshwa katika maeneo ya nchi kavu na majini (baharini). Vile vile, katika kudhibiti viwango na ubora wa mazao ya misitu na nyuki Wakala utakusanya sampuli 60 za asali kutoka maeneo mbalimbali ya nchi kwa ajili ya uchambuzi wa kimaabara.

Mheshimiwa Spika, aidha, mafunzo kuhusu ubora wa mazao ya nyuki yatatolewa kwa vikundi/vyama 150 vya wafuga nyuki. Wavamizi wa hifadhi za misitu na hifadhi za mazingira asilia wataondolewa kwenye hifadhi za Biharamulo, Geita, Nyantakara na Minziro.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa migongano ya kiutendaji na kuongeza ufanisi, Wizara itaanzisha mchakato wa kufanya mapitio ya Tamko la Uanzishwaji wa Wakala wa Misitu (*Establishment Order No. 269 of 2011*) ili kuihuisha na Sheria ya Misitu (Sura 323) ya mwaka 2002 na Sheria ya Nyuki (Sura 224) ya mwaka 2002 na nyaraka mbalimbali za kitaalam katika usimamizi wa misitu ya hifadhi, hifadhi za nyuki, manzuki na mashamba ya miti.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha mipaka ya misitu; Wakala utafanya soroveya, kufungua na kusafisha mipaka ya misitu yenye urefu wa kilomita 2,714. Aidha, maboya 200 na mabango 530 yatatengenezwa na kusimikwa kwenye mipaka ya misitu hiyo ili kutoa tahadhari kwa jamii juu ya hifadhi za misitu. Vile vile, mgawanyo wa viunga (*compartmentation*) utafanywa kwenye mashamba sita ya miti ya Sao Hill, Kawetire, Wino, Rubare, Buhindi na Rubya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa maeneo

yaliyoharibika; Wakala utakarabati vyanzo vya maji kwa kuondoa mimea isiyofaa kwenye eneo la ukubwa wa hekta 889 katika shamba la miti *Sao Hill*; kupanda miti hekta 772 kwenye maeneo yaliyoharibiwa ndani ya misitu ya hifadhi; kuongoa hekta 300 za maeneo ya misitu yaliyoharibiwa katika Wilaya 12 pamoja na maeneo ya *Delta* ya Rufiji kwenye mikoko.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji Mashamba ya Miti na Ufugaji Nyuki. Kazi zifuatazo zitafanyika katika mashamba 15 ya miti:-

Kupanda miche 16,296,000 ya miti kwenye maeneo yenye jumla ya hekta 8,648; kupogolea miti kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 5,314.83; kukagua na kusimamia uvunaji wa miti yenye mita za ujazo 833,955 katika maeneo ya uvunaji ya ukubwa wa hekta 2,133; na kuongeza maeneo mapya yenye jumla ya hekta 43,000.

Mheshimiwa Spika, manzuki 40 zenye makundi ya nyuki 6,000 zitaanzishwa na kuendelezwa katika Kanda saba za Wakala; mizinga 10,000 ya nyuki itasambazwa katika Misitu ya Hifadhi ya Sayaka (1000), Kinzi na Lowasi (2000) Wilaya ya Njombe; Nkasi (2000) Wilaya ya Nkasi; Patamela (1000), Lupa (1000) na Mbiwe (1000) Wilaya ya Chunya na Hifadhi Asilia ya Kilombero (2000) Wilaya ya Kilolo.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya shughuli za ufugaji nyuki kwa jamii zinazoishi kandokando ya misitu ya hifadhi ya New Dabaga, Iringa na Kalambo river, Rukwa yatatolewa.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji jamii katika usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki; ili kuendeleza dhana ya usimamizi shirikishi wa misitu, Wakala utafanya Tathmini ya rasilimali za misitu Kanda ya Magharibi ili kuandaa mipango ya usimamizi na mikataba ya makubaliano kwenye msitu mmoja utakaoteuliwa; kutoa mafunzo kwa Kamati nne za misitu za vijiji kuhusu mwongozo wa usimamizi wa misitu wa pamoja katika Wilaya za Bagamoyo, Kisarawe, Kilosa na Kilombero na kuhamasisha shughuli mbadala za kuongeza

kipato kwa jamii kwenye vijiji saba vinavyozunguka hifadhi za mazingira asilia na hifadhi za misitu Kanda ya Kaskazini. Aidha, mapitio ya mipango miwili ya usimamizi yatafanyika na kutengeneza mipango mingine minane kwenye hifadhi za misitu na hifadhi za nyuki.

Mheshimiwa Spika, kuboresha miundombinu katika hifadhi za misitu. Ili kuhakikisha kuwa watumishi wanafanya kazi katika mazingira mazuri, Wakala unatarajia kujenga nyumba 10 za watumishi na ofisi tatu katika kanda saba za Wakala; kukarabati majengo 149; kutengeneza barabara zenye urefu wa kilomita 35 na kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 4,249.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Misitu Tanzania unakadiriwa kukusanya jumla ya Sh. 4,561,000,000/= kutokana na vyanzo vyake. Mfuko utatoa ruzuku ya Sh. 1,776,511,831/= kwa ajili ya miradi 161 ya wadau mbalimbali wa misitu na ufugaji nyuki, kati ya miradi hiyo 69 itakuwa mipya. Wadau watakaonufaika na mpango huu ni pamoja na watu binafsi, vikundi vya jamii, Asasi za kijamii, Taasisi mbalimbali na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mbegu bora za miti unakuwa endelevu Wakala wa Mbegu za Miti utakusanya mbegu za miti kilo 12,500, kukuza na kuuza miche 60,000 ya aina mbali mbali za miti. Aidha, Wakala utaanzisha vyanzo viwili vya mbegu bora za miti ya Mkaratusi na Mtiki.

Mheshimiwa Spika, vile vile, vyanzo vitano vya mbegu za miti ya kienyeji aina ya Mvule, Mkongo, Mtakowima, Mwiluti, Mninga, na Mpingo vitatambuliwa na kusajiliwa. Wakala pia utaendelea kutunza vyanzo 31 vya mbegu za miti ya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mfudufudu, Msindano, Mkangazi, Mtiki, Mwerezi, Mvule, Mninga, Mti kivuli, na Mwarobaini. Aidha, Wakala utaendesha mafunzo ya muda mfupi kuhusu kuanzisha bustani na kutunza miche ya miti kwa wadau mbalimbali humu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania itaendelea kuboresha mazingira na miundombinu ya utafiti kwa kuweka samani, vitendea kazi, vifaa vya utafiti na kujenga uwezo wa rasilimaliwatu. Aidha, Taasisi itaendeleza tafiti kuhusu uoteshaji wa miti asili iliyo katika hatari ya kutoweka (Mfano, Mloliondo) kwa kutumia biotekinolojia na kuboresha Mitiki kwa kutumia teknolojia ya *tissue culture*.

Mheshimiwa Spika, tafiti nyingine zitakazofanyika ni kuhusu mahusiano ya watu na misitu kufuatia mabadiliko ya mifumo ya usimamizi wa misitu nchini pamoja na vifanahisabati (*Mathematical Models*) za ukadiriaji wa hewa ukaa katika aina mbalimbali za misitu ya asili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ndogo ya utalii. Sera na Sheria; katika kukuza na kuendeleza utalii nchini Wizara itaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 kwa kujumuisha maoni ya wadau wa sekta. Vile vile, Wizara itaendelea kuhamasisha wakala wa biashara ya utalii kuhusu Kanuni zinazosimamia maendeleo ya utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezaji utalii; katika kuimarisha usimamizi na kuwa na mipango mizuri ya sekta ya utalii, Wizara itaendelea kufanya ukaguzi wa biashara za utalii na kutoa elimu juu ya uendeshaji wa biashara katika Kanda ya Ziwa, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Pwani, Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Magharibi.

Mheshimiwa Spika, pia, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kukusanya takwimu na kufanya soroveya zitakazohusu watalii wanaoondoka nchini na Wakala wa Biashara za Utalii.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii Tanzania. Bodi itaendelea kushiriki kwenye maonesho sita ya ndani ambayo ni Sabasaba, Nanenane, Karibu *Travel Fair*, Siku ya Utalii Duniani, Tamasha la Kimataifa la Filamu la Zanzibar na Tamasha la Sauti za Busara ili kuitangaza utalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, aidha, Bodi itashiriki Maonesho ya Utalii ya Kimataifa na misafara ya utangazaji utalii itakayofanyika Uholanzi, Hispania, Ujerumani, Uturuki, Uingereza, China, Urusi, Afrika ya Kusini, India, Brazil, Nchi za Ghuba na Italia.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara itaendelea kutumia mitandao ya kijamii kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii. Mikakati mingine itahusisha kuandaa Tamasha la Utalii wa Utamaduni kwa kushirikiana na Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo litakalokuwa likifanyika kila mwaka; kuandaa safari mbili za kupanda Mlima Kilimanjaro; kutangaza utalii kupitia michezo; kuendesha onesho jipya la Kimataifa la Utalii (*Swahili International Tourism Exhibition*).

Mheshimiwa Spika, Wizara itafungua ofisi za uwakilishi kwa ajili ya kutangaza utalii nchini India na Ujerumani na kuendelea kuimarisha ofisi ya uwakilishi iliyoko nchini Marekani (*the Bradford Group*) pamoja na kuteua Mabalazi wa Hiari watatu nchini Marekani.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii. Katika mwaka 2013/2014, Chuo kitadahili wakurufunzi 312. Kati ya hao, wakurufunzi 240 katika fani ya ukarimu na 72 katika fani ya utalii. Vile vile, wakurufunzi 216 ni katika ngazi ya Astashahada na 96 katika ngazi ya Stashahada.

Mheshimiwa Spika, aidha, Chuo kitaendelea na ukarabati wa hosteli mbili katika Kampasi ya Temeke na kuanza kutekeleza rasmi mpango wa biashara ambapo kutokana na mpango huo mapato ya Chuo yanatarajiwa kuongezeka kutoka Sh. 1,317,817,600/= mwaka 2012/2013 hadi Sh. 1,874,892,000/= kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale: Sera na Sheria; Wizara itaendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333; kuandaa miongozo ya utafiti na uhifadhi wa malikale katika maeneo ya kihistoria ya Kilwa Kivinje, Mikindani na Mji wa kihistoria Pangani; kuandaa orodha ya maeneo ya wapigania uhuru katika Mkoa wa

Mtwara na kuendelea kushiriki katika mikutano ya Kimataifa ili kunufaika na fursa zilizopo.

Mheshimiwa Spika, uhifadhi na uendelezaji wa Rasilimali za Malikale; Wizara kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje itaendelea kusimamia zoezi la ufukuaji wa nyayo za Laetoli. Vile vile, Wizara itakarabati Boma la Pangani; kujenga vituo vya taarifa na kumbukumbu kwenye Mapango ya Amboni katika Mkoa wa Tanga na Kimondo cha Mbozi Mkoa wa Mbeya; kuendelea na ujenzi wa uzio na kuboresha mandhari katika vituo vya Kunduchi, Ujiji na Kaole.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania. Katika kuenzi utamaduni wa Mtanzania Shirika litaendelea kuratibu Tamasha la siku ya Utamaduni wa Mtanzania. Pia, Shirika litashirikisha jamii ya Wapangwa na Wanyakusa kutoka Mikoa ya Mbeya na Njombe. Aidha, Shirika litaendelea kuboresha vyumba maalum kwa ajili ya utunzaji wa mikusanyo na kumbi za maonesho. Vile vile, Shirika litahamasisha wananchi hasa vijana kutembelea Makumbusho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya uratibu, utawala na maendeleo ya rasilimali watu; Wizara itawezesha watumishi 142 kuhudhuria mafunzo. Kati ya hao 80 watahudhuria mafunzo ya muda mfupi na 62 mafunzo ya muda mrefu. Aidha, katika kukabiliana na changamoto za ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa, Wizara itaajiri watumishi 1,091, kati ya hao 930 ni wa kada ya Wahifadhi Wanyamapori na Misisitu.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ustawi wa watumishi, Wizara itaendelea kuratibu upatikanaji wa mikopo kwa watumishi wake kwa ajili ya kununua vyombo vya usafiri, samani na ujenzi wa nyumba. Vile vile, Wizara itaendelea kutoa huduma ya lishe kwa watumishi wake wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, aidha, watumishi wa Wizara wataendelea kushiriki michezo ya SHIMIWI na Mei Mosi. Pia,

Mazingira ya kazi yataendelea kuboreshwa kwa kuongeza vitendea kazi na kukarabati jengo la Makao Makuu ya Wizara na Ofisi za Dodoma.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Naibu Waziri na Mbunge wa Singida Kaskazini; Bibi Maimuna Kibenga Tarishi, Katibu Mkuu na Bibi Nuru H.M. Millao, Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara, Mashirika, Taasisi na Vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ujumla wao kwa ushirikiano walionipa na wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu ya usimamizi wa Wizara. Vilevile, napenda kutoa shukurani kwa wadau wengine wa sekta kwa juhudi wanazoonessa katika utekelezaji wa kazi mbalimbali za Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imetekeleza majukumu yake kwa ushirikiano na wadau wa maendeleo kutoka nchi na asasi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa pamoja na sekta binafsi, hususan mashirika ya Ndege ya Kimataifa kama vile *Qatary Airways, Turkish Airlines, KLM, Emirates* na *Ethiopian Airlines* kwa kukubali kuongeza idadi ya viti na safari za kuja nchini kutoka masoko yetu ya utalii duniani. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa mashirika mengine ya ndege yanayoboresha huduma ya usafiri kwa watalii wanaokuja nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nichukue fursa hii kuwashukuru wote na kutaja baadhi ya wadau kama ifuatavyo:-

Serikali za Marekani, Ujerumani, Sweden, Ufaransa, Uholanzi, Ubelgiji, Japan, Norway, Finland, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha nayashukuru pia Mashirika ya *DANIDA, JICA, UNDP/GEF, FAO, UNWTO, World Bank, KfW, GIZ, IUCN, UNESCO, ICOMOS, ICCROM, LATF, WMF, SPIDER, SADC, BTC, HSF, Gatsby UK, WWF, FINNIDA, FZS, AWF, AWHF, SNV, AFD, USAID, NORAD, WHF* na *Sida*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza malengo

30 APRILI, 2013

yake kwa mwaka 2013/2014, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 75,681,745,000/= . Kati ya hizo, Sh. 64,033,579,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 11,648,166,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Sh. 25,739,948,000/= kwa ajili ya Mishahara ya watumishi na Sh. 38,293,631,000/= kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na fedha za Maendeleo zinajumuisha Sh. 10,648,166,000/= fedha za nje na Sh. 1,000,000,000/= fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitamuita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii, Mheshimiwa James Lembeli!

MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11), nachukua nafasi hii kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati hii yameainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, Kifungu namba 6(8) na 7(1) kuwa ni pamoja na kusimamia shughuli za Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na kuchambua Bajeti ya Wizara hii, kuisimamia na kuishauri kuhusu utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake,

mnamo tarehe 2 Aprili, 2013, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na wataalam wa Wizara hiyo na kujadili kwa kina Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Mwaka wa 2012/2013, mafanikio na changamoto; pamoja na Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali katika maeneo mbalimbali ya msingi. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imezingatia ushauri uliotelewa na Kamati, japokuwa yapo baadhi ya maeneo ambayo juhudi zaidi zinahitajika katika utekelezaji wake. Maeneo hayo ni pamoja na:-

(a) Mgawanyo wa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii ulenge kuziwezesha Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori;

(b) Serikali ichukue hatua za kupunguza migogoro ya mipaka kati ya jamii na maeneo yaliyohifadhiwa; na

(c) Operesheni maalum ziendeshe mara kwa mara ili kukabiliana na tatizo la ujangili wa wanyamapori hususan ujangili wa tembo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inahimiza Serikali kuzingatia na kuyafanyia kazi maoni yanayotolewa na Kamati hii ili kuwa na uhifadhi endelevu kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014; mafanikio na changamoto; Mafanikio, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ya Maliasili na Utalii iliidhinishiwa jumla ya Sh. 77,249,692,390/= . Kati ya fedha hizo sh. 64,537,010,000/= zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 12,712,682,390/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2013 Wizara ilikuwa imepokea sh.

30 APRILI, 2013

31,539,736,793/= sawa na asilimia 40.83 ya fedha iliyoidhinishwa. Kiasi hiki cha fedha zilizotolewa kinajumuisha sh. 31,179,734,693/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizopatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida, zimeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kufuatilia na kuhakiki ukusanyaji wa maduhuli katika vituo 125. Vilevile operesheni mbili za ukusanyaji wa maduhuli zimefanyika kwa nchi nzima kwa muda wa wiki mbili kila moja;

(b) Kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na uwindaji wa kitalii na kuanza kutumika rasmi mwezi Julai, 2012;

(c) Kuanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ambapo Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Randilen imetangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali (1/2/2013, *GN No.* 22) na Jumuiya nyingine mbili za Kilombero na Mahenge zipo katika hatua za mwisho za kutangazwa katika Gazeti la Serikali;

(d) Doria 60,117 (*mandays*) zilifanyika ndani na nje ya mapori ya akiba ambapo watuhumiwa 1,215 walikamatwa kwa kuhusishwa na makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009;

(e) Kesi 398 zenye watuhumiwa 897 zilifunguliwa katika Vituo mbalimbali vya Polisi na Mahakama ambapo kesi 252 zenye watuhumiwa 247 zilikwisha kwa watuhumiwa kulipa faini ya sh. 147,002,420/= na kesi 20 zilikwisha kwa watuhumiwa 71 kufungwa jela; na

(f) Kufanya utafiti wa mwenendo wa biashara ya utalii nchini pamoja na kukusanya na kuainisha takwimu za utalii wa ndani na wa Kimataifa ambapo takwimu za watalii walioingia nchini kwa mwaka 2012 zimeonesha kuongezeka

kwa idadi ya watalii kwa asilimia 6.7 kulinganisha na Mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ilipanga kutekeleza Mirada saba ya maendeleo kwa jumla ya Sh. 12,712,682,390/= ambazo zote ni fedha za nje na mpaka kufikia Februari 2013 sh. 360,002,000/= tu zilikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, miradi minne ya *Selous-Niassa Wildlife protection Corridor, Wetlands Management and Sustainable Development Project, Support to National Forest Programme* na *National Forest Resources Monitoring and Assessment* ilitekelezwa kwa kutumia Sh. 3,648,837,548/= zinazojumuisha sh. 3,288,835,448/= kutoka katika fedha za maendeleo za Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyoonekana, Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake. Changamoto hizo ni:-

(i) Uhaba wa fedha hasa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, sh. 360,002,100/= tu ndio zilitolewa ikiwa ni asilimia 2.8 ya sh. 12,712,682,390/= zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu;

(ii) Uhaba wa watumishi na vitendea kazi kama vile magari ya kufanyia doria na silaha za kisasa hasa katika sekta za Wanyamapori, Misitu na Malikale;

(iii) Uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za maliasili na mali kale;

(iv) Ushirikiano hafifu wa wadau katika uhifadhi wa maliasili;

(v) Kubomolewa kwa majengo ya kale yanayostahili kuhifadhiwa hasa mijini;

30 APRILI, 2013

- (vi) Ubovu wa miundombinu katika maeneo yaliyohifadhiwa;
- (vii) Ujangili uliokithiri wa wanyamapori;
- (viii) Uharibifu wa misitu; na
- (ix) Mwamko mdogo wa Watanzania wazawa kutembelea vituo vya utalii vya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia kwa kina mikakati ya namna Serikali ilivyojipanga kukabiliana na changamoto hizo na kuona itafaa endapo itasimamiwa na kutekelezwa. Mikakati hiyo ni:-

- (a) Kuendelea kuajiri watumishi wapya kulingana na ikama iliyopitishwa;
- (b) Kuongeza ushiriki wa wadau mbalimbali katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili, malikale na shughuli za utalii;
- (c) Kukuza utalii wa ndani kwa kuhamasisha wananchi kutembelea vivutio vya utalii;
- (d) Kufanya mapitio ya Sera na Sheria;
- (e) Kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji maduhuli; na
- (f) Kuongeza bajeti ya ulinzi, uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za maliasili na malikale.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii, Fungu 69, inaomba kuidhinishiwa Sh. 75,681,745,000/= kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Jumla ya sh. 64,033,579,000/= zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo kati ya hizo sh. 38,293,631,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na sh. 25,739,948,000/= ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, Bajeti inayoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni sh. 11,648,166,000/= kati ya hizo fedha za ndani ni sh. 1,000,000,000/= tu kwa ajili ya mradi wa Utalii *House* hatua ya pili.

Hatua ya kwanza imekamilishwa na Serikali ya Marekani kulingana na makubaliano yaliyowekwa hapo awali kwamba, kila nchi itachangia nusu ya gharama ya jengo hilo litakalotumika kama kitega uchumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitika kuona kwamba hakuna mradi mwingine wowote uliopangiwa fedha za ndani licha ya uzoefu kuonesha kuwa fedha kutoka kwa wahisani huwa hazitolewi kwa wakati na wakati mwingine hazitolewi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara na Taasisi zake inategemea kukusanya maduhuli ya jumla ya sh. 148,420,317,425/=, ikiwa ni ongezeko la asilimia tisa ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati inasikitika kuona Wizara imetenga shilingi bilioni moja tu kutoka fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo licha ya kwamba makusanyo ya maduhuli yanatarajiwa kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Awali ya yote Kamati inaipongeza Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (*TANAPA*) kwa kushinda vivutio viwili kati ya vivutio vya ajabu vya asili saba barani Afrika. Vivutio hivyo ni Mlima Kilimanjaro na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kwa kazi nzuri ya uhifadhi iliyopelekea hifadhi hiyo pia kupata tuzo ya kuwa moja ya vivutio saba vya ajabu vya asili barani Afrika. Kamati inaamini vivutio hivyo vitakuwa chachu ya kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, Sekta ya Maliasili na Utalii ni mhimili wa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu kwani ina mchango mkubwa katika pato la Taifa kwa kuchangia wastani wa asilimia 17.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mchango huo ni mdogo ukilinganisha na fursa nyingi zilizopo hasa katika Hifadhi za Taifa, Wanyamapori na Malikale. Endapo Sekta hii itasimamiwa vizuri na kuendelea kupewa kipaumbele na Serikali katika kutangaza vivutio tulivyonyavyo, ni dhahiri kwamba, uchumi wa Taifa utaimarika na hatimaye kuondoa kwa kiasi kikubwa tatizo la umaskini nchini.

Kwa mfano, katika nchi ya Ufilipino, ambayo haina vivutio vingi vya wanyamapori ukilinganisha na Tanzania, ilipata watalii milioni 4.7 kwa mwaka 2012 na kutoa ajira kwa watu milioni 3.8 ikiwa ni asilimia 10.2 ya ajira kwa mwaka 2011. Nchi hii imefanikiwa kuwa na idadi kubwa ya watalii kutokana na kuwekeza katika kujitangaza ndani na nje ya mipaka yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, biashara ya utalii. Idara ya Utalii kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii (*TTB*), Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (*NCAA*) kwa pamoja wameonesha juhudi za wazi za kutangaza utalii wa Tanzania. Takwimu zinaonesha kwamba idadi ya watalii wanaoingia nchini imeongezeka kwa asilimia 6.7 kutoka watalii 867,994 mwaka 2011 hadi kufikia 930,385 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kamati inasikitika kuona kwamba lengo lililowekwa na Wizara hii mwaka 2002 la kufikisha watalii milioni moja ifikapo mwaka 2010 halijafikiwa mpaka sasa. Hali hii imechangiwa na sababu mbalimbali kama inavyoelezwa hapa chini:-

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipofanya ziara

katika Hifadhi za Kusini (Katavi, Kitulo na Ruaha) ilibaini kwamba hifadhi hizi hazijatangazwa vya kutosha, hivyo kuwa na idadi ndogo ya watalii ukilinganisha na Hifadhi za Kaskazini. Kamati ilijulishwa kwamba, kutotangazwa kwa hifadhi hizi kunachangiwa na fedha ndogo zinazotengwa kwa ajili ya utangazaji wa Hifadhi.

Aidha, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini ubovu wa miundombinu kuelekea katika hifadhi, jambo ambalo ni kikwazo kikubwa kwa biashara ya utalii. Barabara nyingi hazipitiki kwa urahisi, kwa mfano, barabara ya kutokea Mbeya kwenda Rukwa na hatimaye Katavi na ile ya kutokea Iringa Mjini kuelekea katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ubovu huo wa miundombinu, gharama za usafiri mpaka hifadhini zimekuwa ni kubwa mno kiasi cha kuwakatisha tamaa watalii kutembelea maeneo hayo. Kwa mfano, gharama ya usafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kupitia Pori la Akiba la Selous na kurudi, humgharimu mtalii mmoja dola za Marekani kati 700 -1000 kiwango hiki ni sawa na gharama ya kumtoa Mtalii London Frankfort Berlin kuja Kilimanjaro au Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri ni vyema sasa Serikali ikaongeze juhudi katika kuboresha miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege vilivyopo ndani na nje ya hifadhi hasa katika Mikoa ya Kusini, ili kwanza kupunguza gharama za usafiri na pia kuwezesha shughuli za kitalii kufanyika katika msimu wowote wa mwaka tofauti na sasa ambapo shughuli hizo husimama wakati wa masika;

Mheshimiwa Spika, aidha, *TANAPA* ifanye jitihada za ziada katika kutangaza vivutio vya utalii katika Hifadhi za Taifa zilizopo katika Mikoa ya Kusini kwani kuna hazina za kipekee katika hifadhi hizo ikiwa ni pamoja na bustani ya Mungu ya Kitulo na Tembo weusi wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine inayochangia idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi zetu kuwa ndogo,

ni uchache wa vyumba vya kulala watalii katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, Kamati imegundua kwamba uchache huu wa mahoteli katika maeneo ya Hifadhi unachangiwa na baadhi ya wafanyabiashara waliopewa maeneo ya kujenga, kutoyaendeleza maeneo kwa muda mrefu. Kwa mfano, katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Makampuni 11 ambayo yalipewa maeneo ya kujenga kuanzia mwezi Juni, 2009 ikiwa ni miaka takribani minne iliyopita, hayajaanza ujenzi hadi hivi sasa.

Makampuni hayo ni pamoja na *ASB Tanzania Limited, Ruhuji (T) Limited, Antelope Safaris Limited, Pongo Safaris Limited, Kwihala Camp, Tourism Promotion Service Tanzania Limited na Indian Ocean Hotels*. Kamati inaona hatua hii ni hujuma dhidi ya maendeleo ya utalii nchini na inaitaka Mamlaka husika kufuta vibali hivyo kama makampuni hayo hayataanza ujenzi katika kipindi cha miezi sita (6) ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile inashauri kwamba, kwa kuwa Mwaka 2002 Serikali ilijiwekea lengo la kufikisha watalii milioni moja ifikapo mwaka 2010 na kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kufikisha lengo hilo kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Serikali ijiwekee lengo jipya la idadi ya watalii watakaolingia nchini hasa kwa kuzingatia mazingira ya sasa ambapo matangazo ya vivutio vya utalii nchini yamefika katika nchi nyingi zaidi duniani ukilinganisha na mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Kamati inawapongeza Watanzania kwa kuanza kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii nchini. Hata hivyo, kasi hii ya utalii inakwamishwa na gharama kubwa za malazi hasa katika Hifadhi za Taifa. Gharama hizi zinachangiwa kwa kiasi kikubwa na ukweli kwamba hoteli nyingi katika hifadhi za Taifa zinamilikiwa na Kampuni za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara kutoa kipaumbele kwa Watanzania wenye uwezo wa kuwekeza

katika ujenzi wa maeneo ya malazi ndani ya hifadhi kwa maana ya hoteli za kitalii, mabanda (*cottages*), maeneo ya kupiga mahema kwa watu wote (*public campsites*) na kwa watu maalum (*Special campsites*).

Mheshimiwa Spika, Idara ya Wanyamapori, taarifa ya Kamati ya mwaka uliopita wa 2012/2013, kuhusu bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ilizungumzia ujangili wa wanyamapori kama changamoto kubwa katika Idara hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitika kuona kwamba, bado ujangili umeendelea kuwa changamoto kubwa katika mapori yote ya akiba na hakuna dalili yoyote inayoonesha kupungua kwa changamoto hii kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kuchelewa kuhukumiwa na kuharibiwa kwa kesi za ujangili;

(b) Upungufu wa rasilimali watu hasa Askari wa Wanyamapori;

(c) Upungufu na ubovu wa magari ya doria; na kubwa zaidi ni; na

(d) Kukosekana kwa silaha za kisasa kwa ajili ya kukabiliana na majangili ambao wengi hutumia silaha za kisasa za kivita.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kwamba pamoja na nchi yetu kubarikiwa kwa kuwa na hazina kubwa ya wanyamapori, bado Serikali haijaipa kipaumbele na umuhimu unaostahili. Kamati inaona kwamba, japokuwa Wizara ya Maliasili na Utalii imeonesha nia ya wazi ya kukabiliana na ujangili, hivyo kununua silaha kwa ajili ya kufanikisha hilo, Serikali hiyo hiyo kupitia Wizara ya Fedha (*TRA*) imezuia silaha hizo bandarini ikidai kodi kwa ajili ya silaha hizo.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza kwani pamoja na wanyamapori ambao ni mali ya Serikali kuingizia

Taifa pato kubwa bado Taasisi kama TRA haioni wala kutambua jitihada za mkono mwingine wa Serikali za kuokoa rasilimali hii ya Taifa inayoendelea kupotea siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, kwa lugha nyingine, *TRA* kuendelea kushikilia silaha hizo kwa zaidi ya miezi ya mitano kwa kigezo cha fedha kwanza, ni kushawishi majangili yaendeleo kuteketeza tembo wa Taifa hili. Kamati inaishauri na kuitaka Serikali kuruhusu mara moja silaha hizo kuondolewa bandarini japo kwa masharti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuajiri Askari wa Wanyamapori wa kutosha. Idadi iliyopo haitoshi na wala haikidhi mahitaji na changamoto zilizopo. Kwa mfano, Pori la Akiba la Rukwa/Lukwati/Lwafi lenye ukubwa wa kilomita za mraba 9568.26 lina jumla ya watumishi arobaini na tano (45) tu. Hali ni mbaya zaidi katika mapori karibu yote ya akiba ikiwa ni pamoja na Pori la AKiba la Selous ambalo lina ukubwa wa zaidi ya kilomita za mraba 50,000 likiwa na watumishi wasiozidi 250.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba, ili kurejesha hali ya utulivu katika mapori yote ya Akiba, Serikali inatakiwa kuajiri Askari wa Wanyamapori wasiopungua 1000.

Mheshimiwa Spika, aidha, ili kuimarisha ulinzi katika Mapori ya Akiba nchini ni vyema Serikali ikatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kununua magari ya doria kwani yaliyopo sasa ni machache ukilinganisha na ukubwa wa mapori.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kufanya Operesheni maalum kama ile ya Operesheni Uhai ambapo uzoefu umeonesha operesheni hiyo ilimaliza kabisa ujangili na kwa zaidi ya miaka kumi (10), hali katika mapori ya akiba iliendelea kuwa shwari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala kuchelewa kutoa hukumu na wakati mwingine ushahidi wa kesi za ujangili kuharibiwa ni changamoto kubwa katika mapori ya akiba na Hifadhi za Taifa, Kamati inatoa rai kwa vyombo vya Serikali

kama vile Jeshi la Polisi na Mahakama kushirikiana na Idara ya wanyamapori kuhakikisha watuhumiwa wa kesi za ujangili wanashtakiwa kwa kupewa adhabu kali kwa mujibu wa Sheria. Kamati haipendi kuamini kuwa kesi hizi zinahujumiwa kutokana na Askari Polisi na Mahakimu wachache kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha utaratibu kwa Pori la Akiba la Selous kubakiza asilimia 50 ya mapato yake (*retention*). Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa *retention* ya asilimia 100 kwa mapori yote ya akiba ili yaweze kujiendesha kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuimarisha doria katika mapori. Kiwango hicho cha *retention* ya asilimia 50 hakitoshi kuyaweka mapori ya akiba katika hali nzuri hasa ya ulinzi na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati imeridhishwa na hatua ya Serikali ya kukamilisha kuandaa rasimu ya Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Wanyamapori na rasimu ya muundo na uendeshaji wa Mamlaka hiyo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato huo hatimaye Muswada uletwe Bungeni ili Mamlaka hiyo ianze kufanya kazi mara moja. Kamati inaamini kwamba Kuanzishwa kwa Mamlaka hii kutapunguza kwa kiasi kikubwa mianya ya rushwa, ufujaji wa mapato na ufisadi uliopo katika idara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ujangili wa tembo umekuwa ni janga la kitaifa. Ni ukweli usiofichika kwamba leo hii si tu tembo wanauawa bali wanateketezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori hapa nchini na nchi za nje, takwimu zinazoshabihiana na za taarifa za utafiti wa Kimataifa zinaonesha kwamba tembo wasiopungua 30 wanauawa kwa siku, 850 kwa mwezi na tembo 10,000 kila mwaka (*TAWIRI*, 2011)

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasi kubwa ya kuuawa kwa tembo, taarifa za kitaalam kutoka *TAWIRI*

zinathibitisha kwamba idadi ya tembo imepungua kutoka tembo 109,000 mwaka 2009 na kufikia tembo chini ya 70,000 mwaka 2012. Endapo kasi hii ya ujangili wa tembo itaendelea bila kudhibitiwa mara moja, ni wazi kuwa tembo watakuwa wametoweka nchini katika kipindi cha miaka saba ijayo.

Mheshimiwa Spika, hali hii ni ya hatari na ni albu kwa nchi yetu ambayo ni ya pili barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya tembo. Kinachosikitisha ni kwamba, Wizara imekuwa na kigugumizi katika kuitikia kauli ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete iliyoitaka Wizara kuomba msaada kwake kama tatizo la ujangili limewashinda. Jambo hili linaweza kutafsiriwa kuwa ni hujuma inayofanywa na baadhi ya watendaji wa Wizara ambao wamepuuza kauli ya Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kunusuru tembo wa Tanzania kutoweka katika mapori yetu kama walivyotoweka faru katika miaka ya 1980, Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua stahili ikiwa ni pamoja na kufanya Operesheni Uhai nyingine kwa nchi nzima. Aidha, Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009, ifanyiwe marekebisho kwa kuweka adhabu kali kwa watu wote watakaothibitika kuhusika na ujangili wa tembo.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mambo ya Kale; Tanzania ni moja ya nchi maarufu zenye hazina kubwa ya malikale. Malikale zilizopo ni pamoja na majengo ya zamani yaliyojengwa kwa matumbawe katika miji ya Pwani, Michoro ya kale, mapango ya Amboni, Nyayo za zamadamu aliyeishi miaka milioni 3.6 iliyopita na nyingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba nchi nyingi duniani hupata mapato makubwa kutokana na utalii unaotegemea vivutio vya kitalii. Hata hivyo, Serikali yetu bado haijafanikiwa kuliingizia Taifa letu pato la kuridhisha kutokana na utalii wa malikale.

Maeneo mengi yenye vivutio vya aina hii ya utalii ni kama yamesahauliwa kwani hayatangazwi vya kutosha, hayana usimamizi unaotakiwa na sehemu nyingine

yanaharibiwa kwa ajili ya matumizi binafsi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Serikali ifanye juhudi za ziada za kuvitangaza vivutio hivi kwani itaongeza idadi ya watalii wa ndani na wa nje pia. Aidha, ni vyema Serikali ikatekeleza mkakati wake kwa mwaka 2013/2014 wa kuendeleza vivutio vya mambo ya kale ikiwa ni pamoja na kukarabati Jengo la Kalenga, Boma la Pangani na kujenga Kituo cha kumbukumbu na taarifa cha Amboni.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa lilianzishwa kwa Sheria Na. 7 ya Mwaka 1980. Shirika hili ni taasisi ya kielimu na kiutamaduni yenye jukumu la kukusanya, kuhifadhi, kutafiti na kuelimisha jamii kwa kutumia maonesho na machapisho kuhusu urithi wa asili na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona Taasisi hii inashindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

(a) Kutokuwepo kwa Bodi ya Shirika kuanzia Novemba 2011 ambayo inapaswa kusimamia utendaji wa Shirika;

(b) Upungufu wa rasilimali watu;

(c) Uhaba wa vifaa vya kuhifadhia makusanyo ya makumbusho mbalimbali; na

(d) Bajeti/ruzuku inayotengwa kutopatikana kwa wakati; kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 jumla ya sh. 2,026,664,000/= ilitengwa kama ruzuku kutoka Serikalini, lakini hadi kufikia Disemba, 2012 Shirika lilikuwa limepewa sh. 481,884,228/= ikiwa sawa na asilimia 24 tu ya kiwango kilichotengwa.

Mheshimiwa Spika, ulimwenguni kote, hasa katika nchi zilizoendelea, makumbusho ya Taifa (*museums*) ni moja kati ya vivutio vikubwa vya watalii. Ni jambo la kusikitisha kwamba Serikali yetu bado haijaona umuhimu wa kuyafanya

makumbusho ya Taifa kuwa ni moja ya vivutio vya utalii hapa nchini. Kamati inashauri Wizara kupitia Idara yake ya Utalii na Bodi ya Utalii kuitangaza makumbusho ya Taifa sambamba na sekta nyingine za utalii.

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuteua Bodi ya Shirika la Makumbusho ambayo Kamati inaamini kuwa itaweza kushughulikia kwa ufanisi changamoto zote zinazolikabili Shirika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchimbaji wa Madini katika Mapori ya Akiba; tangu kupitishwa kwa Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009 inayoruhusu uchimbaji wa madini (*Strategic Minerals*) kufanyika katika mapori ya akiba, tayari Serikali imeruhusu Kampuni ya *Mantra Tanzania Limited* kuanza maandalizi ya uchimbaji wa madini aina ya Urani katika Pori la Akiba la Selous.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba uamuzi huu una tija kwa Taifa, Kamati inashauri Serikali kuwa makini katika kushughulikia suala hili, hivyo kuepusha madhara makubwa yanayoweza kujitokeza baadaye, sio tu kwa binadamu bali pia kwa rasilimali ya asili iliyopo katika eneo hilo la hifadhi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba urani itachimbwa na itakwisha, lakini maliasili iliyopo katika Pori la Akiba la Selous kama ikitunzwa itakaa pale milele na mapato yatakayopatikana japo kwa kiwango kidogo yataendelea kunufaisha vizazi vya sasa na hata vya watoto wa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na kitendo cha Wizara ya Nishati na Madini kutokuihusisha Kamati hii katika hatua muhimu zinazoendelea katika suala la uchimbaji wa urani, hivyo kuashiria kuwepo kwa vitendo visivyo vya kawaida.

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuleta Azimio hapa Bungeni la eneo la Mkuju lililoko ndani ya Hifadhi ya Pori la Akiba la Selous, kutumika kama eneo la hifadhi na ambalo pia litatumika kwa uchimbaji wa madini ya urani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la mipaka kati ya Vijiji na Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu; tatizo hili limeendelea kuwa changamoto katika sekta ya maliasili na utalii, hivyo kuongeza migogoro kati ya jamii na maeneo yaliyohifadhiwa. Kwa mfano, migogoro inayoendelea katika Pori tengefu la Loliondo; wakulima/wafugaji wa Kijiji cha Kikondo na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo; wahamiaji katika ghuba ya Speke na wafugaji wa lhefu na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, migogoro hii ya mipaka inachangiwa na wananchi ama kwa kutojua mipaka ya maeneo yao au kutumiwa na *NGOs* na wanasiasa ili kuendelea kuyatumia maeneo hayo ilihali mipaka inajulikana wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuchukua hatua za ziada na za haraka ili ufumbuzi wa migogoro hii upatikane na hatimaye kuendeleza mahusiano mema kati ya vijiji na Mamlaka zinazosimamia maeneo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaitaka Serikali kusimamia na kutekeleza kwa hali na mali wajibu wake wa kikatiba wa kusimamia, kuendeleza na kulinda maeneo yote yaliyohifadhiwa yenye umuhimu wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, suala la uharibifu wa misitu limeendelea kuwa changamoto kubwa inayoikabili sekta ya misitu Tanzania. Uharibifu huu unatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na :-

(i) Uvamizi wa misitu hasa wafanyabiashara haramu wa kuni, mkaa, mbao na nguzo; na

(ii) Uhaba wa rasilimali watu kuweza kusimamia hifadhi za misitu kwa ufanisi na uaminifu.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi za misitu ya Mkungunero, Kazimzumbwi na Ruvu Kusini ni mifano halisi ya misitu inayoendelea kuharibiwa kwa kasi na wavamizi hasa wafanyabiashara haramu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa misitu katika kutunza mazingira, vyanzo vya maji na kupunguza hewa ukaa ni muhimu Serikali ikasimamia Sheria zake na kuhakikisha misitu haivamiwi na kuharibiwa ovyo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na Asasi mbalimbali zinazoanzishwa ili kukabiliana na uharibifu huu wa misitu. Jambo la kushangaza ni kwamba, Asasi hizi zimekuwa hazipati ushirikiano wa kutosha kutoka Serikalini katika kupambana na ujangili wa Misitu. Kwa mfano *Independent Monitor for Forest Law Enforcement and Governance (IMFLEG)* ni chombo kilichopendekezwa kuanzishwa baada ya kutokea kwa ujangili mkubwa wa misitu ya Pwani mwaka 2005. Pamoja na umuhimu wake, mpaka leo chombo hiki hakijapewa meno licha ya Serikali kuona umuhimu wa chombo hiki kuanzishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wakala wa Misitu kuchukua hatua za haraka kudhibiti ujangili wa misitu kwa kushirikiana na vyombo binafsi ikiwa ni pamoja na *IMFLEG*.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa hapo awali, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara imetengewa jumla ya fedha za maendeleo sh. 11,648,166,000/=, Kati ya fedha hizo, shilingii bilioni moja tu ndio fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambazo zitatumika kwa ajili ya Mradi mmoja wa Nyumba ya Utalii, hatua ya pili. Mradi huu ni ubia kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Marekani.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikiishauri Serikali

kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kuacha kutegemea fedha za wahisani ambazo upatikanaji wake huwa mgumu. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ilitengewa jumla ya sh. 12,712,682,000/= zote zikiwa fedha za nje. Mpaka kufikia Februari, 2013, sh. 360,000,000/= tu ndio zilikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba miradi muhimu kama ya kuziwezesha jamii kupata mafunzo ya usimamizi shirikishi wa misitu, MKUHUMI na tabia nchi haitatekelezeka kama tukiendelea kutegemea fedha za nje. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenga fedha za ndani kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa miradi muhimu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, yapo masuala mbalimbali ambayo Kamati inaona ni muhimu kuyazungumzia ili kuimarisha sekta ya Maliasili na Utalii. Masuala hayo ni pamoja na:-

(1) Kumekuwa na matumizi yasiyo endelevu ya maji katika mito inayoingiza maji katika Mto Ruaha Mkuu kutokana na shughuli za umwagiliaji kwenye mashamba ya mpunga katika Wilaya ya Mbarali. Hali hii imepelekea Mto Ruaha Mkuu ambao ni tegemeo kubwa kwa wanyamapori, kupungua maji kwa kiasi kikubwa. Kamati inaishauri Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Wizara ya Maji (hususan Rufiji *Water Basin*) kuona namna bora ya kuwa na usimamizi thabiti wa vyanzo vya maji na rasilimali maji;

(2) Kumekuwa na changamoto ya kujaa kwa tope kunakohatarisha uwepo wa baadhi ya maziwa nchini ikiwa ni pamoja na Ziwa Manyara na Ziwa Katavi. Kamati inaishauri TANAPA kuweka mikakati ya kuyanusuru maziwa haya ikiwa ni pamoja na kuelimisha jamii kuhusu athari za matumizi ya ardhi yasiyo endelevu kama vile kilimo cha kwenye miinuko;

(3) Serikali ioneshe juhudi za wazi za kufungua

ushoruba wa mapito ya wanyamapori wa Ngorongoro-Ziwa Manyara- Tarangire ili wanyama waendeleo kupita katika njia zao za asili;

(4) Kwa kuwa wananchi wameendelea kufanya shughuli za kiuchumi kama vile kilimo na ujenzi wa makazi ya kudumu kwenye Ghuba ya Speke na kwa kuwa eneo hili ni pori tengefu Kisheria kwa ajili ya mapito ya wanyamapori kwenda kunywa maji hususani wakati wa kiangazi; Serikali ione namna bora ya kuwahamasisha wananchi kuridhia kuhama kutoka katika eneo hilo na ikibidi maamuzi magumu yafanyike;

(5) Kwa kuwa maslahi ya *tour guides* na wabeba mizigo wanaofanya kazi katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro (*KINAPA*) ni madogo, Kamati inashauri Serikali ione ulazima wa kuboresha maslahi yao kwa mujibu wa Sheria kulingana na ugumu wa kazi wanazofanya;

(6) Kwa kuwa Bodi ya Utalii ndio mtangazaji mkuu wa utalii ndani na nje ya nchi, ili kuiwezesha Bodi hii kumudu majukumu yake, ni vema Serikali ikatambua umuhimu wa kuifanya Bodi kuwa Mamlaka ili iweze kujikusanyia mapato yake yenyewe. Hii itasaidia Mamlaka kujiendesha bila kutegemea bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo mara nyingi imekuwa haitoshelezi;

(7) Kwa kuwa Pori la Akiba la msitu wa Pande (*Pande Forest Reserve*) linaweza kuboreshwa na kuwa kivutio kingine cha utalii, Serikali ione umuhimu wa kuboresha na kuliendeleza Pori hili kuwa hifadhi ya wanyama pori mjini;

(8) Kwa kuwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani kuna Kiwanda cha Chumvi cha *Sea Salt Company Limited* na kwa kuwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (*TAM*) inathibitisha uwepo wa shughuli za kiwanda hicho ndani ya hifadhi unahatarisha uhifadhi endelevu na kwa kuwa uchimbaji wa chumvi hifadhini ni kinyume cha Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009 inayoruhusu uchimbaji wa *strategic minerals* tu, Kamati inaishauri Serikali kutokuingia

mkataba na kiwanda hicho mara mkataba wa sasa utakapomalizika mwaka 2017;

(9) Serikali ione umuhimu wa kuharakisha uteuzi wa Bodi za Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Chuo cha Wanyamapori Mweka; na

(10) Mwisho lakini si kwa umuhimu, ni rai ya Kamati kuwa Wabunge na viongozi wa nchi katika ngazi mbalimbali kutembelea vivutio vya utalii nchini ikiwa ni pamoja na kupanda Mlima Kilimanjaro. Kwa kufanya hivyo si tu tutakuwa tumetangaza utalii ambao utaliongezea Taifa letu mapato, bali pia kuenzi hazina aliyotupa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati namshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Balazi Khamis Sued Kagasheki, Waziri akisaidiwa na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Maimuna K. Tarishi na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Nuru M. Milao, kwa kutoa ushirikiano kwa Kamati hii wakati wa kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2012/2013 na Makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni, busara na ushauri uliofanikisha kuwasilishwa kwa taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba niwatambue Wajumbe hao wa Kamati kwa majina:-

Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdulkarim E. Hassan Shah, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mjumbe; Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, Mjumbe; Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mjumbe; Mheshimiwa Muhamad Amour Chomboh, Mjumbe; Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mjumbe; Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mjumbe; Mheshimiwa Esther Amos Bulaya, Mjumbe;

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mjumbe; Mheshimiwa John John Mnyika, Mjumbe; Mheshimiwa Salim Hassan Turkey, Mjumbe; Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mjumbe; Mheshimiwa Kisyeri Werema Chambiri, Mjumbe; Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyr, Mjumbe; Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mjumbe; Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mjumbe na Mheshimiwa Waride Bakar Jabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge hasa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashillah...

SPIKA : Tumeacha hayo maneno siku hizi.

MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA: na Makatibu wa Kamati Ndugu Grace Bidya na Ndugu Evelyne shibandiko wakisaidiwa na Ndugu Lukindo Choholo, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati mpaka kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Fungu 69 kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, jumla ya shilingi bilioni 77, 249, 692,390/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge ahsante sana. Sasa nitamwita Msemaji wa Kambi wa Upinzani. Lakini hotuba aliyowasilisha hapa ndani tarehe 29 na ambayo imegawiwa kwa taarifa nilizopewa ni kwamba, wameibadilisha, hiyo nyingine iko wapi? Msemaji wa Kambi ya Upinzani, nadhani itabidi tubadilisha utaratibu, siyo kubadili dakika ya mwisho.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA – MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri wa Maliasili na Utalii ilianzishwa kwa mujibu wa kipengele cha 21 cha Nyongeza ya Waraka wa Rais uliochapishwa kama Tangazo la Serikali Na. 494 la tarehe 17 Desemba, 2010. Majukumu ya Ofisi hii yameainishwa katika Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la *mwaka 2010 (The Ministers (Assignment of Ministerial Functions) Notice, 2010)* lililochapishwa katika *Gazeti la Serikali* kama Tangazo la Serikali Na. 494A la tarehe 17 Desemba 2010.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali (TS) Na. 494A, majukumu hayo ni pamoja na ufugaji nyuki, wanyamapori, malikale, makumbusho na sera za utalii na utekelezaji wake. Katika utekelezaji wa majukumu haya, Ofisi hii ina Idara mbalimbali kama vile Wanyama Pori, Utalii, Mambo ya Kale, Usimamizi wa Rasilmali Watu, Sera na Mipango.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ofisi ina taasisi zinazojitegemea kama vile Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) na Mamlaka ya Uhifadhi wa Eneo la Ngorongoro (*NCAA*). Vile vile, Ofisi ina Wakala na Mifuko ya Uhifadhi kama vile Wakala wa Misitu Tanzania (*Tanzania Forestry Agency*) na Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Tanzania (*Tanzania Wildlife Conservation Trust Fund*) na Mfuko wa Hifadhi ya Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki (*The Eastern Arc Mountains Forests Conservation Trust Fund*). Mwisho, Ofisi ina vyo mbalimbali kama vile Chuo cha Misitu Olmotonyi, Vyo vya Wanyamapori Mweka na Pasiansi.

Mheshimiwa Spika, ni hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba, Ofisi ya Waziri wa Maliasili na Utalii imeshindwa kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Tangazo la Serikali tajwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, sababu kubwa ya kushindwa huko kutekeleza majukumu ya kisheria ya Ofisi hii ni ufisadi na matumizi mabaya ya madaraka ambao umetapakaa katika kila sehemu ya Ofisi hiyo ukiwahusisha

30 APRILI, 2013

watendaji wake wakuu pamoja na watendaji wa ngazi za juu za Chama cha Mapinduzi (CCM) na wafanyabiashara makada wa chama hicho.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, kushindwa kwa Ofisi hii kutekeleza majukumu yake hayo kumehatarisha utajiri mkubwa wa maliasili za nchi yetu kama vile wanyamapori, misitu na malikale na kulitia albu kubwa Taifa letu kwamba ndio chanzo kikubwa cha ujangili wa Kimataifa na biashara haramu ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Maliasili kama wanyamapori hai na nyara nyingine za Serikali zimeporwa na kusafirishwa nje ya nchi yetu kwa kupitia viwanja vyetu vya ndege vya Kimataifa pamoja na bandari zetu bila hatua stahiki kuchukuliwa na vyombo vya ulinzi na usalama vya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limepitisha maazimio mengi kuhusu kashfa mbalimbali zilizogubika utendaji wa Ofisi ya Waziri wa Maliasili na Utalii na utekelezaji wa majukumu yake kisheria. Aidha, Bunge lako limeunda Kamati za Uchunguzi ili kuchunguza tuhuma za ukiukaji sheria na matumizi mabaya ya mamlaka katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitika kuliambia Bunge lako Tukufu, maazimio ya Bunge yamepuuzwa na taarifa za Kamati zake za Uchunguzi kuzimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili lawama za kwanza lazima zitupiwe katika Ofisi yako mwenyewe kwa kuwa ndio limekuwa kaburi kubwa la kuzika taarifa za Kamati za Bunge ambazo pengine Ofisi yako inaona zinaonesha udhaifu katika utendaji wa Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Spika, tarehe 27 Aprili mwaka 2006

30 APRILI, 2013

aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii Anthony Diallo, aliunda Kamati ya Maalum ya Uchunguzi Kuhusu Uboreshaji wa Tasnia ya Uwindaji wa Kitalii Tanzania. Lengo la kuundwa kwa Kamati hiyo...

KUHUSU UTARATIBU

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, kwa heshima zote ningepomba kutumia Kanuni ya 63. Kwanza, nieleze ninachotaka, hatuathiri hapa mambo ya Ibara ya Katiba, lakini ni sahihi kusema Ofisi ya Spika ni kaburi, ndani ya Bunge hili jamani! Hiyo siyo kumdhalilisha hata Spika. *(Makofi)*

SPIKA: Nashukuru kwa taarifa hiyo. Kwanza, naomba ukae Mheshimiwa Msigwa. Nikisimama wewe unakaa.

Unajua saa nyingine unasoma vitu halafu unaacha wafanye kwa sababu kila Kamati ya Sekta ina wajibu wa kusimamia Sekta yake. Sasa kaburi lililopo kwa Spika itabidi aende akalichimbe hilo kaburi akaone. Kwa sababu kama kila Sekta ina wajibu wa kusimamia sekta yake, unajua ni maneno ya kurundika bila sababu.

Endelea Mheshimiwa Msigwa. Yako mengi mtayasikia na naomba mtulie kwa sababu fujo zozote ni pande mbili, waache waseme tuendelee tutayaona. Haya yako mengi. Mheshimiwa Msigwa endelea! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba na muda wangu uulinde!

Mheshimiwa Spika, tarehe 27 Aprili, 2006 aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii – Mheshimiwa Anthony Diallo, aliunda Kamati ya Maalum ya Uchunguzi Kuhusu Uboreshaji wa Tasnia ya Uwindaji wa Kitalii Tanzania. Lengo la kuundwa kwa Kamati hiyo lilikuwa ni kuchambua na kubaini matatizo yanayoikabili tasnia ya uwindaji wa kitalii na namna ya kuyatatua matatizo hayo na kuboresha tasnia hiyo.

Kamati ya Mheshimiwa Diallo iliwasilisha Taarifa Kuhusu Uboreshaji wa Tasnia ya Uwindaji wa Kitalii Tanzania mwezi Juni, 2006. Pamoja na mambo mengine, Kamati hiyo iligundua kwamba licha ya biashara ya uwindaji wa kitalii kutakiwa kuwa ni chanzo kikubwa cha mapato ya fedha za kigeni, (biashara hiyo) inaingiza fedha kidogo, wastani wa dola za Kimarekani milioni tisa tu kwa mwaka, wakati wenzetu wa Zimbabwe, (biashara) hii inawaingizia dola milioni thelathini kwa mwaka.

Aidha, Kamati iligundua kwamba, makampuni mengi ya uwindaji hayaajiri wataalam wa ndani, ila huwatumia wananchi kwa kazi ndogo ndogo wakati wa msimu wa uwindaji. Makampuni haya pia yanawatumia wawindishaji kutoka nje ya nchi badala ya kutumia wawindishaji bingwa wa Kitanzania.”

Vile vile, Kamati ilibaini kwamba licha ya kuwepo Makampuni mengi yanayomilikiwa na raia wa Tanzania, Makampuni machache ya kigeni yanamiliki idadi kubwa ya vitalu vya uwindaji ambavyo vina wanyama wengi ukilinganisha na vitalu vya makampuni ya wananchi ambavyo viko kwenye maeneo ambayo hayana wanyama wengi.

Mwisho, Kamati ilibaini kwamba idara ya Wanyamapori haisimamii kikamilifu tasnia hii kwa maana haina taarifa muhimu kuhusu vitalu na thamani halisi ya vitalu hivi. Kwa kadri ya taarifa za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Taarifa hii ya Kamati ya Mheshimiwa Diallo haijawahi kutolewa hadharani na wala kuwasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, inaelekea Kamati ya Mheshimiwa Diallo ilitokana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 - 2010, iliyokuwa imewaahidi Watanzania kwamba Serikali ya CCM itaendelea kuelekeza nguvu zake katika kuhifadhi, kulinda, kuendeleza, kudumisha na kuvuna maliasili kwa manufaa ya Taifa letu. Ahadi hiyo ilirudiwa kwa karibu maneno hayo hayo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015. Aidha, tuliambiwa na CCM katika Ilani yake ya 2005 kwamba Serikali yake itahimiza Miji ianzishe bustani za ufugaji wa wanyamapori (*zoos*) kwa maonyesho. Hakuna bustani ya wanyamapori hata moja iliyoanzishwa katika kipindi hicho na ndiyo maana ahadi hiyo ilipotea kabisa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2010!

Mheshimiwa Spika, kama tutakavyothibitisha, Serikali ya CCM imeshindwa kabisa kutekeleza mapendekezo ya Kamati ya Mheshimiwa Diallo. Badala yake, Serikali hii imeelekeza nguvu zake katika kudidimiza na kudhoofisha uhifadhi, ulinzi na uendelezaji wa maliasili za nchi yetu. Aidha, Serikali ya CCM siyo tu imeelekeza nguvu kubwa katika uvunaji haramu wa maliasili za nchi yetu, bali pia imefanya hivyo kwa manufaa ya wafanyabiashara wa kigeni wakishirikiana na wafanyabiashara wachache ndani ya nchi na viongozi waandamizi wa CCM na makada waandamizi wa Chama hicho.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 Bunge lako Tukufu liliunda Kamati ya Uchunguzi ili kuchunguza matukio ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu za wananchi wa Loliondo katika Wilaya ya Ngorongoro ambapo wananchi walidaiwa kuchomewa nyumba zao na wanawake kudhalilishwa na Jeshi la Polisi.

Taarifa ya Kamati hiyo, iliyoongozwa na Naibu Spika wa sasa wa Bunge lako Tukufu - Mheshimiwa Job Ndugai, haikuwasilishwa Bungeni, na kwa kadri ya ufahamu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, imezikwa kwenye kaburi la Ofisi ya Spika. Matokeo yake, mgogoro kati ya wananchi wa Loliondo kwa upande mmoja, na Serikali ya CCM na Kampuni ya *Orthello Business Corporation (OBC)* inayomilikiwa na

mfanyabiashara kutoka Oman kwa upande mwingine, umezidi kuwa mkubwa kama inavyohibitishwa na maasi ya wananchi wa Loliondo dhidi ya CCM yaliyoshuhudiwa mwezi uliopita na viongozi na makada wa CCM waliopo ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012 Kamati Ndogo ya Kamati ya Kudumu ya Maliasili, Utalii na Mazingira iliwasilisha taarifa ndani ya Bunge lako Tukufu kuhusu utoroshwaji wa wanyamapori hai. Kufuatia kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, Bunge lilipitisha azimio, pamoja na mambo mengine, kwamba Serikali itengeneze kanuni za uwindaji ili iweze kubana mianya ya rushwa inayoikosesha mapato (na kanuni hizo) ziwe tayari ndani ya mwaka mmoja kuanzia sasa. Bunge lako liliazimia pia kwamba, wale wote waliohusika na utoaji wa kibali cha kutorosha wanyama hai wachukuliwe hatua za kinidhamu. Aidha, Bunge liliitaka Serikali kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya watumishi waliohusika kutoa kibali hicho.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Bunge lako lilirudia mapendekezo ya Kamati ya Mheshimiwa Diallo ya kuunda mamlaka maalumu kwa ajili kushughulikia masuala ya biashara ya wanyamapori na uwindaji wa kitalii. Bunge lako liliipa Serikali kipindi cha mwaka mmoja kutekeleza maazimio hayo. Hadi wakati wa kuwasilisha maoni haya, Serikali imepuuza utekelezaji wa maazimio ya Bunge lako Tukufu kuhusu jambo hili.

Aidha, licha ya Mheshimiwa Waziri kutoa ahadi kwa Bunge lako Tukufu kuwa wanyamapori hai waliotoroshwa nje ya nchi watarudishwa nchini, hadi leo ahadi hiyo haijatekelezwa na Bunge hili halielekei kutaka kuchukua hatua stahiki kwa Mheshimiwa Waziri kwa kupuuza kutekeleza ahadi ya Serikali ya CCM kwa Bunge.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012 Mheshimiwa Waziri alichukua vielelezo kutoka kwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Masuala ya Ardhi - Mheshimiwa Halima Mdee juu ya Kampuni ya Uwindaji ya *Game Frontiers*

kukodisha kitalu chake cha uwindaji kwa ajili ya utafutaji wa madini ya urani katika eneo la Mbarang' andu katika Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba atachukua hatua stahiki kuhusiana na suala hilo. Hadi ninapowasilisha maoni haya, Serikali haijaeleza hatua zozote kama zipo, ilizochukua kumnyang'anya mmiliki wa kampuni hiyo ya uwindaji leseni ya uwindaji katika eneo hilo kwa kukiuka masharti ya leseni hiyo. Aidha, hadi sasa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado inasubiri majibu ya Serikali kuhusiana na ujangili wa tembo unaohusisha Watendaji wa Serikali kwa kushirikiana na makada wa CCM.

Mheshimiwa Spika, tarehe 28 Julai, 2007, aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe alipatiwa taarifa ya kitafiti juu ya Uwindaji Haramu Katika Pori Tengefu la *Selous* na maeneo yanayolizunguka iliyoandaliwa na Bwana Baruani Mshale wa Shule ya Masomo ya Misitu na Mazingira ya Chuo Kikuu cha Yale cha Marekani. Pamoja na mambo mengine, taarifa ya Bwana Mshale ilidai kwamba kumekuwa na 'maslahi haramu' (*vested interests*) kati ya Serikali na wafanyabiashara wa uwindaji wa kitalii wa nje ambayo yamesababisha Serikali kufanya maamuzi yasiyofaa yanayowanyima wananchi vijijini faida zitokanazo na utajiri wao wa maliasili.

Mtafiti huyo anataja viashiria vya maslahi hayo haramu kuwa ni pamoja na mvutano kati ya Mkurugenzi wa Wanyamapori na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii na uamuzi wa Mheshimiwa Rais kufanya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri ambapo Waziri wa Maliasili na Utalii aliondolewa kwenye Wizara hiyo. Katika kile kinachoonekana kwamba, maslahi haya haramu ya kisiasa kwa faida ya kiuchumi ya watu wachache, yanajulikana Serikalini; Mtafiti Mshale alimwambia Mheshimiwa Waziri kwamba: "Inawezekana nakukumbusha kitu ambacho tayari unakifahamu!"

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba maslahi haramu ya kisiasa kwa faida ya

kiuchumi ya watu wachache katika sekta ya uwindaji wa kitalii imekithiri ndani ya CCM na Serikali yake na inawahusisha viongozi na Watendaji waandamizi wa Chama hicho na Serikali yake. Kwa mfano, mwaka 2009 shehena ya pembe za ndovu zenye uzito wa tani nne kutoka nchini Tanzania na Kenya zilizoripotiwa kukamatwa na vyombo vya usalama vya Vietnam ilisafirishwa na Kampuni ya Wakala wa Meli itwayo *Sharaf Shipping Co. Ltd.* Taarifa za Wakala wa Usajili wa Biashara na Makampuni (*BRELA*) zinaonyesha kwamba Katibu Mkuu wa CCM Abdulrahman Kinana anamiliki robo tatu ya hisa za *Sharaf Shipping Co. Ltd.*, wakati robo iliyobaki ya hisa hizo inamilikiwa na mtu aitwaye Rahma Hussein. Kwa mujibu wa taarifa ilizonazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Rahma Hussein ni mkewe Abdulrahman Kinana, Katibu wa CCM! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyo tu kwamba Kampuni ya Katibu Mkuu wa CCM na mkewe imehusishwa na usafirishaji haramu wa pembe za ndovu kutoka Tanzania, Kampuni hiyo inaelekea kutoa ajira haramu kwa wageni. Wakati shehena ya meno hayo tembo inakamatwa nchini Vietnam, nyaraka zilizoambatana na shehena hiyo zilionyesha kwamba kibali cha kusafirisha shehena hiyo kilisainiwa na raia wa India anayeitwa Samir Hemani mnamo tarehe 13 Novemba, 2008. Hemani alikuwa Meneja wa Fedha na Utawala wa *Sharaf Shipping Co. Ltd.* Hata hivyo, nyaraka za Idara ya Uhamiaji ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imezipata zinaonyesha kwamba wakati Hemani anasaini kibali cha kusafirisha shehena ya meno ya tembo kwa niaba ya wateja wa Kinana na mkewe, kibali chake cha kuishi Tanzania kilikuwa kimekwisha tangu tarehe 7 Mei, 2008.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM itoe kauli rasmi mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu kushiriki kwa Katibu Mkuu wa CCM katika kusafirisha kiharamu nyara za Serikali ambazo kwa vyovyote vile zinathibitisha kuwepo kwa ujangili wa kutisha unaohusu maliasili wanyamapori wa nchi yetu. Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM itoe kauli mbele ya Bunge lako Tukufu juu ya kuhusika kwa Katibu Mkuu

wa CCM katika kuajiri wafanyakazi wageni ambao walikuwa wanaishi nchini kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Tume ya Rais ya Kuchunguza Kero ya Rushwa Nchini ya mwaka 1996 iliyoongozwa na Waziri Mkuu Mstaafu – Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba ililalamikia kile ilichokiita “ukaribu wa wafanyabiashara na viongozi wa kisiasa,” ulioanza kujitokeza mwanzoni mwa kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu Pili ya Mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi. Taarifa hiyo ilitoa mfano wa Makampuni ya Kigoma *Hill Top Hotel, Shenis Commercial Ltd., Tile and Tube Ltd., Royal Frontier (T) Ltd., Game Frontier (T) Ltd. nee MNM Hunting Safaris Ltd.*, ambayo yalikuwa yanamilikiwa na mfanyabiashara Mohsin Abdallah, mkewe Nargis Abdallah na washirika wao wengine wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Mohsin Abdallah ni kada maarufu wa CCM na Mjumbe wa zamani wa Halmashauri Kuu (*NEC*) ya Chama hicho. Inaelekea kuwa mfanyabiashara na kada huyu maarufu wa CCM ameendelea kuwa na ushawishi mkubwa ndani ya Serikali ya CCM na hasa hasa katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Zaidi ya hayo, inaelekea kwamba, kama ilivyokuwa kwa Tume ya Warioba miaka 17 iliyopita, ushawishi mkubwa alionao kada huyu wa CCM unatoa uvundo na harufu mbaya ya ufisadi.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati Ndogo ya Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira iliyotolewa ndani ya Bunge hili Tukufu, Kampuni tatu zenye majina yanayoelekea kufanana na zina Ofisi katika jengo moja, *Royal Frontiers of Tanzania Ltd., Game Frontiers of Tanzania Ltd.*, na *Western Frontiers of Tanzania Ltd.*, zinaonyesha kuwa wanahisa wa Kampuni hizo wana nasaba za kifamilia, hivyo kuleta hisia kuwa lengo la Sheria na Kanuni kuzuia mtu mmoja kumiliki vitalu zaidi ya vitano linapuuzwa kwa ujanja wa kusajili Kampuni mpya kwa malengo fulani.

Kamati ilipata ushahidi wa maelezo ya Kampuni zinazofanya biashara ya uwindaji wa kitalii kuwa mmiliki wake ni mmoja, na hata maelezo ya baadhi ya Wajumbe wa

Kamati ya kumshauri Mheshimiwa Waziri kuhusu ugawaji wa vitalu yanaashiria kuwa kampuni zote hizo zinamilikiwa na mtu mmoja, hali inayoweza kusababisha mtu huyo kupata vitalu vingi kinyume cha Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli mbele ya Bunge hili Tukufu juu ya mahusiano yake na mfanyabiashara na kada huyu wa CCM ambayo yamepigwiwa kelele kwa karibu miaka 20. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kama huu siyo mfano wa wazi wa maslahi haramu ya kisiasa kwa faida ya kiuchumi ya watu wachache, basi Serikali iliambie Bunge lako Tukufu kuna maslahi gani ya umma katika mahusiano haya?

Mheshimiwa Spika, Mohsin Abdallah sio mfanyabiashara na kada pekee wa CCM mwenye maslahi yenye mashaka katika sekta ya uwindaji wa kitalii. Kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ya Mheshimiwa Diallo, makada waandamizi wa CCM wenye maslahi ya aina hii ni wengi na baadhi yao wako humu ndani ya Bunge lako Tukufu. Taarifa hiyo inayataja Makampuni ya *Coastal Wilderness (Tz) Ltd.*, ambayo Wakurugenzi wake wanatajwa kuwa Naponi Edward Moringe Sokoine na Namelok Edward Moringe Sokoine; Enzagi *Safaris (Tz) Ltd.*, yenye Wakurugenzi Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Muhamed Seif Khatib; Said Kawawa *Hunting Safaris* yenye Wakurugenzi Chande Kawawa na Hassan Kawawa; na *M.S.K. Tours & Hunting Safari Co.* ya Mheshimiwa Muhamed Seif Khatib.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati Ndogo ya Kamati ya Maliasili na Mazingira, mengi ya Makampuni haya yalipewa vitalu vya uwindaji wakati hayana uzoefu wala mtaji wa kuendesha biashara ya uwindaji wa kitalii katika vitalu hivyo. Matokeo yake ni kwamba Makampuni hayo yalishindwa kusimamia uhifadhi wa wanyamapori katika vitalu vyao na kusababisha tatizo la ujangili kushamiri katika vitalu hivyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli mbele ya Bunge lako Tukufu, ni kwa nini Serikali hii ya CCM imekuwa ikitoa vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa makada waandamizi wa CCM ambao wanajulikana kuwa

hawana weledi wala uwezo wa kibiashara wa kuendesha biashara ya uwindaji wa kitalii na hivyo kusababisha tatizo la ujangili kuwa kubwa zaidi na kuleta hasara kwa Taifa letu?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeanza kufedheheshwa katika Mikutano ya Kimataifa ya Uhifadhi kwa sababu ya Serikali hii ya CCM kukumbatia makada waandamizi wa CCM wanaojihusisha na ujangili. Kwa mfano, katika Mkutano wa 16 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Biashara ya Kimataifa ya Wanyama Walio Hatarini Kutoweka (*CITES*) uliofanyika Bangkok, nchini Thailand mwezi uliopita, Mohsin Abdallah alitajwa na Shirika la Upelelezi wa Masuala ya Mazingira (*Environmental Investigations Agency, EIA*) kuwa ni mmoja wa majangili wakubwa wanaojihusisha na biashara haramu ya meno ya tembo, lakini Serikali ya Tanzania imeshindwa kumchukulia hatua za kisheria kwa sababu ya ushawishi wake mkubwa katika siasa za ndani ya Chama Tawala na Serikali hii ya CCM.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni fedheha ya aina gani Kimataifa itakayoiamsha Serikali hii ya CCM katika usingizi wake wa pono ili iweze kuchukua hatua za kisheria dhidi ya makada wa CCM wa aina hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro na Loliondo ni moja ya maeneo ya asili ya jamii za Wamaasai. Kwa mujibu wa taarifa za kitafiti za ekolojia ya maeneo haya, Wamaasai wameishi katika maeneo hayo tangu karne ya 18. Kabla ya mwaka 1959 eneo hili lilikuwa ni sehemu ya maeneo ya Serengeti - Ngorongoro ambayo yalikuwa yakikaliwa na wafugaji wa Kimaasai. Mwaka 1959 Serikali ya kikoloni iliigawanya Serengeti - Ngorongoro baada ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti upande wa magharibi, na Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro upande wa milima ya mashariki ya eneo la ekolojia la Serengeti - Ngorongoro.

Wafugaji wa Kimaasai waliokuwa wakiishi katika maeneo ya Seronera, Moru na Sironet katika upande wa magharibi, waliondolewa katika maeneo hayo na

kuhamishiwa Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro na Loliondo. Hata hivyo, Serikali ya kikoloni iliahidi kwamba haki za Wamaasai juu ya ardhi za maeneo walikohamishiwa zitapewa kipaumbele na kulindwa na Serikali. Kwa mujibu wa Taarifa Rasmi ya Kikao cha Baraza la Kutunga la Sheria (*LEGCO*) cha siku ya Jumatatu ya tarehe 17, Novemba, 1953, Gavana wa Tanganyika wa wakati huo alisema yafuatayo:-

“Wakati eneo hili lilipotangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa, ilitambuliwa kwamba kulikuwa na watu waliokuwa na haki za asili za machungio ya mifugo na maji ndani ya mipaka yake na kwamba haitawezekana kuwaondoa watu hawa kwa nguvu.”

Kauli hii ya Serikali ilitiliwa nguvu na Waraka wa Serikali Na. 1 wa 1956 (*Government Sessional Paper No. 1 of 1956*) uliochapishwa kufuatia kuongezeka kwa shinikizo la Mashirika ya Uhifadhi ya Kimataifa yaliyokuwa yanataka Wamaasai wafukuzwe katika maeneo ya Serengeti - Ngorongoro: “Kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti chini ya Sheria ya Wanyamapori na baadaye kuundwa kwake upya chini ya Sheria ya Hifadhi za Taifa hakukuathiri kwa namna yoyote haki zilizokuwepo za mtu yeyote ndani au juu ya ardhi za Hifadhi, badala yake, haki hizo siyo tu kwamba zililindwa wazi wazi, bali pia Wamasai waliokuwa tayari wanaishi ndani ya eneo la Hifadhi walipewa ahadi chanya na Serikali kwamba haki zao hazitavurugwa bila ridhaa yao.”

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuchapishwa kwa Taarifa ya Tume ya Uchunguzi juu ya Ngorongoro iliyoongozwa na Sir Barclay Nihill aliyekuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki, iliyopendekeza Wamaasai wafukuzwe Serengeti na pia katika maeneo ya Kreta za Ngorongoro na Empakaai, Serikali ya kikoloni ilirudia msimamo wake kuhusu haki za Wamasai wa Serengeti-Ngorongoro katika Waraka wa Serikali Na. 6 wa 1956 (*Government Sessional Paper No. 6 of 1956*): “Mapendekezo ya kuwa na maeneo tengefu katika Kreta hizo mbili hayakukubalika. Yanaashiria kuondolewa kwa Wamasai kutoka kwenye maeneo haya mawili. Haikuonekana sawa sawa kuomba ridhaa ya Wamasai

kuachia haki zao ndani ya Kreta hizo mbili wakati huo huo wakiwa wanaachia haki zao ndani ya Hifadhi yenyewe.”

Mheshimiwa Spika, ahadi za kulinda haki za ardhi za Wamaasai wa Serengeti-Ngorongoro ziliendelea kutolewa kwa nyakati tofauti na viongozi wa ngazi za juu wa Serikali ya kikoloni ya Tanganyika. Hivyo basi, katika kikao cha Baraza la Kutunga Sheria cha tarehe 25 Aprili, 1956, Gavana Sir Richard Turnbull aliliambia Baraza hilo kwamba: “Wakati Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ilipoanzishwa mwaka 1940, ahadi rasmi zilitolewa na Serikali hii kwa Wamasai. Hii haimaanishi kwa kabila lote la Wamaasai bali wale waliokuwa na haki za kisheria au za asili katika eneo hilo. Nina uhakika kabisa kwamba hakuna mtu yeyote anayeweza kutegemea Serikali hii, au Serikali yoyote ya Kiingereza kuvunja ahadi zake rasmi. Imekuwa ni lazima, kwa hiyo, kupata ridhaa ya Wamaasai kwa ajili ya mabadiliko yanayopendekezwa.”

Miaka miwili baadaye Gavana Turnbull alirejea kauli yake hiyo wakati akifungua Mkutano wa 34 wa Baraza la Kutunga Sheria tarehe 14 Oktoba, 1958: “Nadhani ni lazima nichukue fursa hii kusisitiza kwamba kwa misingi yote ya haki na nia njema, hakuna Serikali itakayofikiria kuwaondoa Wamasai kutoka maeneo yote ya hifadhi za wanyama za Serengeti na Nyanda za juu za Kreta.” Kama inavyojulikana, baadaye Serikali ya kikoloni iliingia Mkataba na Wamasai ambapo Wamaasai walikubali kuhama kutoka maeneo yao ya Sironet, Moru na Seronera ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na kuhamia eneo jipya la Hifadhi ya Ngorongoro. Kwa maneno ya Gavana Turnbull: “Uhifadhi wa eneo la Ngorongoro utajengwa kuzunguka nguzo ya maslahi ya wenyeji wa eneo hilo.”

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ambao Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ilianzishwa, yaani 1959, Gavana Turnbull alisisitiza msimamo wa Serikali yake juu uhifadhi wa Ngorongoro kujengwa kwa kuzingatia maslahi ya wakazi wake katika hotuba aliyoitoa mbele ya Halmashauri ya Wilaya ya Maasai mwezi Agosti, 1959: “Nataka kuweka wazi kwenu wote kwamba ni nia ya Serikali kuendeleza *Crater* kwa

maslahi ya watu na matumizi yake; wakati huo huo Serikali inakusudia kulinda hifadhi ya wanyama katika eneo hilo; pamoja na kuwepo kwa mgongano wa jamii na Serikali, bado Serikali inathamini na kuheshimu shughuli za jamii na haitaingilia shughuli za wafugaji wa Kimaasai.”

Mheshimiwa Spika, makubaliano kati ya Serikali ya kikoloni na Wamaasai wa Serengeti-Ngorongoro yalikuwa ndiyo msingi wa kutungwa kwa Sheria ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ya mwaka 1959. Sheria hiyo iliweka msingi kwamba eneo hilo litakuwa ni eneo la matumizi mseto wa rasilimali ambako Wamasai wataruhusiwa kuishi na kutumia maeneo ya Ngorongoro kwa ajili ya malisho ya mifugo yao. Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (*Ngorongoro Conservation Area Authority, - NCAA*) ilipewa majukumu ya kisheria ya kuhifadhi maliasili za eneo hilo na pia kuwaendeleza Wamasai kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa misingi hiyo, Serikali ya Tanzania imeshiriki katika ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu za Wamasai wa Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro na Loliondo katika Wilaya ya Ngorongoro. Serikali pia imekiuka wajibu wake wa kuwaendeleza Wamasai wa Ngorongoro kama ilivyotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 1995 na Shirika la Misaada la Denmark (*DANIDA*), licha ya *NCAA* kupokea mamilioni ya fedha za kigeni kutokana na utalii unaoendeshwa katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, umaskini katika familia za Kimasai ulifikia hatua ambayo 50% ya kaya zao zilikuwa na chini ya mifugo saba kwa kaya, ambacho kinachukuliwa kuwa chini ya kiwango cha kujikimu kiuchumi, wakati 40% ya kaya hizo zilichukuliwa kuwa ni fukara kwa maana ya kuwa na chini ya mifugo miwili kwa kaya.

Mheshimiwa Spika, miaka karibu 20 baadaye, hali ya kiuchumi na kijamii ya Wamasai wa Ngorongoro imekuwa ni mbaya zaidi kuliko ilivyokuwa wakati wa utafiti huo wa *DANIDA*. Ushahidi wa suala hili ni Taarifa ya Tume ya Uchunguzi ya CCM iliyoundwa na Katibu Mkuu wa CCM Abdulrahman

Kinana na kuongozwa na Naibu Katibu Mkuu, Tanzania Bara, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba iliyosambazwa jana tarehe 29 Aprili, 2013. Wajumbe wengine wa Tume hiyo ni pamoja na Mbunge wa Longido Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Simanjiro Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mbunge wa Viti Maalum na Katibu wa CCM Mkoa wa Arusha - Mheshimiwa Mary Chatanda. Ukimwacha Mheshimiwa Chatanda, Wajumbe wengine wa Tume hiyo ni Wajumbe wa *NEC* ya CCM. Kwa vyovyote vile, Taarifa ya Tume hiyo ya uchunguzi inahitaji kupewa uzito na umuhimu wa kipekee kutokana na uzito kichama wa Wajumbe walioiandaa.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Tume ya Mwigulu Nchemba: "Kutokana na ukosefu wa ardhi ya kuendeshea shughuli za kiuchumi, umaskini umekithiri miongoni mwa wakazi wa Ngorongoro kiasi cha kupelekea wakuu wa familia kukimbia familia zao." Ukosefu wa ardhi unaopelekea umaskini kukithiri ni wa kutengeneza na Serikali hii ya CCM, kwani kati ya km² 14,036 ambazo ndiyo eneo lote la Wilaya ya Ngorongoro, km² 8281 au 59% zimechukuliwa na eneo la Hifadhi ya Ngorongoro wakati km² 870 au 6% zimechukuliwa na Hifadhi ya Misitu ya Nyanda za Juu Kaskazini. Maeneo ya wanyamapori na malisho ya mifugo ni km² 3916 au 30%, wakati maeneo ya kilimo ni km² 435 au 3% ya eneo lote la Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya mwanzo 2000, *NCAA* ilipiga marufuku kilimo cha mazao ya chakula katika maeneo ya Nainokanoka na Endulen ambayo yako ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Matokeo ya sera hizi za kuwanyang'anya wananchi wa Ngorongoro ardhi kwa ajili ya mifugo yao na kupiga marufuku kilimo yamekuwa, kwa mujibu wa Taarifa ya Tume ya Mwigulu Nchemba, ni "tatizo sugu la njaa isiyokwisha katika Tarafa ya Ngorongoro." Taarifa hiyo inafafanua zaidi: "Wananchi wa Ngorongoro wana njaa ya muda mrefu ambayo haijapatiwa ufumbuzi. Wananchi hawa hawaruhusiwi kulima ndani ya Hifadhi, hivyo hutegemea mgawo wa chakula toka Mamlaka ya Hifadhi." Ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Kikwete kuwa Serikali ya CCM itashughulikia suala la kilimo cha kujikimu ambacho

kingewasaidia Wamasai kujipatia chakula, ahadi hiyo haijatekelezwa licha ya ukweli kwamba, "Mamlaka ya Hifadhi imeshindwa kuwapatia chakula."

Hivyo, kama walivyosema Profesa Issa G. Shivji na Dkt. Wilbert Kapinga katika kitabu chao, *The Maasai Rights in Ngorongoro, Tanzania*, Serikali ya Tanzania, kwa kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, imekiuka siyo tu haki za binadamu za Wamaasai wa Ngorongoro, bali pia imeshindwa kutekeleza wajibu wake wa kuwaendeleza Wamaasai hao kama inavyotakiwa na sheria. Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, hiki ndiyo chanzo cha migogoro ya ardhi ya muda mrefu na isiyomalizika kati ya Wamaasai na Serikali ya CCM na Mashirika yake ya Uhifadhi wa Wanyamapori.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba njia pekee ya kutatua matatizo ya kiuchumi na kijamii ya Wamasai na migogoro juu ya haki zao za ardhi na rasilimali, ni sharti Serikali iweke utaratibu mpya utakaoruhusu Wamasai kufaidika na rasilimali za wanyamapori katika maeneo yao kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko ilivyo sasa. Kama inavyosema Taarifa ya Tume ya Mwigulu Nchemba, kuwapatia wananchi wa Ngorongoro mgawo wa Shilingi bilioni moja wakati mapato ya Mamlaka ya Hifadhi ni zaidi ya Shilingi bilioni 51 kwa mwaka, ni dhihaka na kuwapuuza.

Mheshimiwa Spika, aidha, utaratibu wa uhifadhi unaosisitiza binadamu na mifugo yao kuondolewa katika maeneo ambayo wameishi pamoja na wanyamapori kwa karne nyingi hauna msingi wowote kisayansi na umepitwa na wakati. Kama walivyowahi kusema watafiti, *Homewood* na *Rodgers* katika kitabu chao *The Maasailand Ecology: Pastoralist Development and Wildlife Conservation in Ngorongoro, Tanzania*, hakujawahi kuwa na sababu za msingi za kisayansi za kuwakataza wafugaji wa Kimasai kutumia rasilimali asili za Serengeti-Ngorongoro kwa ajili ya mifugo yao. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu kama bado kuna sababu zozote za kuendelea kuwazuia wafugaji wa Kimasai wa

Ngorongoro na Loliondo kutumia maeneo ya malisho ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na maeneo ya Kreta za Ngorongoro, Olmoti na Empakaai na vile vile katika Hifadhi ya Msitu wa Nyanda za Juu za Kaskazini ili kukabiliana na matatizo ya ukosefu wa malisho na maji ya mifugo hasa hasa wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa ardhi katika eneo la Loliondo ni taswira nyingine ya jinsi ambavyo Serikali ya CCM imekiuka haki za wafugaji wa Kimasai kwa manufaa ya wawekezaji wa kigeni katika Sekta ya Uwindaji wa Kitalii. Kama tulivyoeleza mwanzoni, kufuatia Wamaasai kuondolewa Serengeti mwaka 1959, baadhi yao walihamishiwa katika Tarafa za Loliondo na Sale na wengine walihamishiwa katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Licha ya ahadi za Serikali ya kikoloni kwamba haki za ardhi za Wamasai zitaendelea kulindwa katika maeneo hayo, miaka ya uhuru ilishuhudia Serikali ya Tanzania ikianza kuhujumu haki hizo. Hivyo basi, mwaka 1975 Serikali iliwaondoa kwa nguvu wafugaji waliokuwa wakiishi ndani ya eneo la Kreta ya Ngorongoro. Miaka tisa baadaye, kati ya 1983/1984, Serikali ilitwaa eneo la Sukenya lenye ukubwa wa ekari 10,716 na kuligawa kwa Kampuni ya Bia Tanzania (*Tanzania Breweries Ltd.*)

Aidha, mwaka 1990 Serikali ilipima vijiji vyote vya Tarafa ya Loliondo na Sale na kuvipatia hatimiliki ya ardhi ikiwa ni pamoja na kuvitambua kisheria. Hata hivyo, mwaka huo huo Serikali hiyo hiyo ilitwaa sehemu ya ardhi ya vijiji hivyo na kuimilikisha kwa Kampuni ya *Orthello Business Corporation (OBC)* inayomiliwa na Brigadia Mohamed Abdulrahim al-Ali anayesemekana kutoka katika familia ya kifalme ya Oman.

Mwaka 1992 Serikali hii ya CCM ilipanua wigo wa umiliki wa ardhi wa Kampuni ya *OBC* na kuiruhusu Kampuni hiyo kuwinda katika Vijiji vyote 19 vya Tarafa ya Sale na Loliondo. Ilipofika mwaka 2003, mkataba wa *OBC* na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kwa niaba ya vijiji ukaisha, lakini *OBC* ikaendelea na uwindaji mpaka sasa. Licha ya Kampuni hiyo kutokuwa na Mkataba halali na wananchi

wa Loliondo, mwaka 2009 *operation* kubwa ilifanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii kuwaondoa wafugaji katika maeneo ya Sale na Loliondo na kupelekea wananchi kuchomewa nyumba zao. Mwaka 2011 Serikali ya CCM ikavitangazia vijiji vyote kurudisha hatimiliki za ardhi na pia vijiji vyenye vyeti vya usajili vikaamriwa vivirudishe. Inaelekea kwamba amri hii ilikuwa ni sehemu ya mwisho ya maandalizi ya kuwanyang'anya wananchi wa Loliondo na Sale ardhi zao, kwani mnamo tarehe 26 Machi, 2013 Waziri wa Maliasili na Utalii aliitembelea Wilaya ya Ngorongoro na kuwatangazia wananchi na wakazi wa Loliondo kwamba, ameagizwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kugawa eneo la Loliondo *Game Controlled Area* ya zamani katika sehemu mbili, yaani km²2500 zimeachwa kwa ajili ya matumizi ya watu kwa kilimo, ufugaji, makazi, na kadhalika; *square kilometer* zimechukuliwa na Serikali ili eneo hilo liwe *Game Control (sic!)* mpya ya Loliondo.

Mheshimiwa Spika, maelezo yote haya yanatoka katika Taarifa ya Tume ya Mwigulu Nchemba. Kwa mujibu wa Taarifa hiyo, Serikali hii ya CCM imeamua kumega eneo la Loliondo *Game Control (sic!) Area* ya zamani na kulifanya *Game Control (sic!) Area* mpya, na kwamba eneo hilo sasa litakuwa mali ya mwekezaji *OBC* kwani analimiliki kisheria. Aidha, kwa mujibu wa taarifa hiyo, endapo eneo hilo litamegwa kama ilivyotangazwa na Mheshimiwa Waziri Kagasheki: "Wakazi wa Tarafa (ya Loliondo) watakuwa wamebakiwa na eneo la km² 265 tu. Eneo hili ni dogo sana kwa wakazi 60,000 wa Tarafa hii."

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Tume ya Mwigulu Nchemba inasema wazi kwamba kauli ya Waziri Kagasheki kuhusu unyang'anyi huu wa wazi wazi wa ardhi ya wananchi ndiyo iliamsha hasira za wananchi. Hii ni kwa sababu, eneo wanalonyang'anywa ndilo eneo pekee wanalolitegemea kwa maji ya mifugo na matumizi ya kibinadamu. Kuwaondoa ndani ya eneo hilo ni sawa na kuwaua. Hivyo wako tayari kufa wakipigania eneo hilo. Aidha, eneo hilo ndilo eneo pekee walilolitenga kwa ajili ya malisho ya mifugo hasa wakati wa

kiangazi panapokuwa na uhaba wa malisho. Kuwaondoa hapa ni sawa na kuiua mifugo yao, jambo ambalo hawako tayari kulishuhudia, bora wafe.

Mheshimiwa Spika, mgogoro kati ya wananchi wa Loliondo na Sale kwa upande mmoja na Serikali na *OBC* kwa upande mwingine umekuwa ukitokota kichini chini kwa zaidi ya miaka 23. Mgogoro huu ni mali binafsi ya CCM na Serikali zake za awamu ya pili, ya tatu na ya nne ya Mheshimiwa Rais Dkt. Kikwete. Ni mtoto wa ndoa haramu ya CCM na wawekezaji wa kigeni katika Sekta ya Uwindaji wa Kitalii. Mtoto alizaliwa na Serikali ya Mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi, akalelewa na baba wa kufikia, Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa na sasa amefikisha umri wa mtu mzima chini ya baba wa kambo Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete!

Mheshimiwa Spika, licha ya Serikali ya CCM kuwatukana wananchi wa Loliondo kwa kuwaita Wakenya, ni wazi kama inavyohibitishwa na Taarifa ya Tume ya Mwigulu Nchemba kwamba, waathirika wa *landgrab* hii ni Watanzania wapatao 59,536 wanaoishi katika Vijiji vya Ololosokwan, Soit Sambu, Oloipiri, Oloirien/Magaiduru, Arash, Losoito/Maaloni na Piyaya.

Vijiji hivi vina Shule za Msingi na za Sekondari zenye wanafunzi 2,302; zahanati nne na nyumba kadhaa za Wahudumu wa Afya; mashine za maji tatu; na mabwawa ya maji mawili. Maelfu ya wananchi hawa na miundombinu iliyojengwa kwa nguvu zao na kwa fedha za walipa kodi wa Tanzania inatakiwa kutolewa kafara katika hekalu la urafiki wa Serikali ya CCM na mwekezaji huyu wa Kiarabu! Huu ndiyo uso halisi wa Serikali hii sikivu na inayotaka maisha bora kwa kila Mtanzania!

Mheshimiwa Spika, kutokana na hoja na ushahidi ambao tumeueleza hapa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM itoe kauli rasmi mbele ya Bunge lako Tukufu juu ya mambo yafuatayo:-

(1) Kama Kampuni ya *OBC* ina haki zozote za ardhi katika maeneo ya Kata za Loliondo na Sale licha ya ukweli kwamba maeneo hayo yalikuweshapimwa na wananchi kumilikishwa kihalali, na vijiji vyao kupatiwa usajili halali kwa mujibu wa sheria za nchi yetu;

(2) Kama ni halali kwa Kampuni ya *OBC* kuendesha shughuli za uwindaji wa kitalii katika vijiji vyote 19 vya Tarafa ya Loliondo na Sale wakati eneo lililopewa kwa ajili mwaka 1990 lilihusu sehemu ndogo tu ya maeneo ya vijiji hivyo;

(3) Kama Kampuni ya *OBC* inaendesha shughuli za uwindaji wa kitalii katika maeneo ya Loliondo kihalali licha ya ukweli kwamba Mkataba wake na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kwa niaba ya wananchi wa Loliondo ulikwisha muda tangu mwaka 2003;

(4) Kama ilikuwa halali kwa Serikali kuwahamisha wananchi wa Loliondo kwa nguvu na kuwachomea nyumba zao moto mwaka 2009, na baadaye kudai wananchi hao ni raia wa Kenya. Kama Serikali hii ya CCM itakiri kwamba vitendo hivyo vya kinyama havikuwa halali, basi itoe kauli kama iko tayari kuwaomba radhi na kuwalipa fidia kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, wananchi wote wa Loliondo na Sale waliodhalilishwa kwa kuitwa raia wa Kenya na kuathirika na unyama huo;

(5) Kama Serikali hii ya CCM iko tayari kuwachukulia hatua za kisheria, au kiutendaji au kinidhamu wale wote walioamuru na/au kushiriki katika vitendo vya kuwaondoa kwa nguvu wananchi wa Loliondo na Sale na kuwachomea nyumba zao moto pamoja na kuwatendea vitendo vya udhalilishaji au ukiukaji wa haki zao za kibinadamu;

(6) Kama ni kweli kwamba kitendo cha hivi karibuni cha Mheshimiwa Waziri Kagasheki kutoa amri ya wananchi wa Loliondo na Sale kunyang'anywa maeneo yao mengine na maeneo hayo kukabidhiwa kwa Kampuni ya

OBC kilitokana na maagizo au maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete au yalikuwa na Baraka zake kama inavyodaiwa na Taarifa ya Tume ya Mheshimiwa Mwigulu Nchemba;

(7) Kama huu siyo wakati muafaka kwa Mheshimiwa Waziri Kagasheki kuwajibika kwa kujiuzulu kwa hiari yake au kama atashindwa kufanya hivyo, kuwajibishwa kwa kufukuzwa kazi kwa kusababisha mgogoro wa sasa katika maeneo ya Loliondo na Sale;

(8) Kama, licha ya ushahidi wote ulioibuliwa na Taarifa ya Tume ya Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na licha ya upinzani mkubwa wa wananchi, bado kuna sababu ya kuendelea kuiruhusu Kampuni ya *OBC* kuendesha shughuli zake katika maeneo ya Loliondo na Sale.

(9) Kama, licha ya ushahidi wote ulioibuliwa na Taarifa ya Tume ya Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwamba chanzo cha migogoro ya ardhi katika Wilaya ya Ngorongoro ni sera za Serikali hii ya CCM, ni halali kwa Serikali na CCM yenyewe kuendelea kuyalaumu mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ya kutetea haki za binadamu na za wafugaji wa Kimaasai kuwa yanachochea vurugu za wananchi wa Loliondo na Ngorongoro; na

(10) Kama, baada ya mambo yote yaliyoelezwa hapa, Serikali hii ya CCM iko tayari kusitisha uamuzi wake wa kuwanyang'anya wananchi wa Loliondo na Sale maeneo yao na kuyamilikisha kwa Kampuni ya *OBC* au Kampuni nyingine yoyote katika siku za mbeleni;

Mheshimiwa Spika, kama alivyopata kusema Dalai Lama: "Lengo letu kuu katika maisha haya ni kuwasaidia watu wengine; na kama hatuwezi kuwasaidia, basi angalau tusiwaumize." Serikali hii ya CCM ilikuwa na bado ina wajibu kisheria kuwasaidia Wamasai wa Wilaya ya Ngorongoro kwa kuwaendeleza kiuchumi na kijamii. Kama imeshindwa kufanya hivyo, kama ilivyoonyeshwa katika maoni haya, basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM

angalau iache kuwaumiza wananchi hawa kwa kuwaachia ardhi zao!

Mheshimiwa Spika, madhara makubwa ya ujangili inawezekana kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na mfumo wa kiuwajibikaji ambao hauko wazi, kwani mtu anayetoa vibali au anayejua ni mnyama gani anatakiwa kuwindwa ni Afisa Wanyamapori wa Wilaya (*DGO*), ambaye kiuwajibikaji yupo chini ya Mkurugenzi wa Halmashauri. Taasisi inayowajibika kwa wanyamapori ni Wizara ya Maliasili na Utalii. Tunaweza kuona mfumo ulivyo na nani anatakiwa kuwajibika kwa nani na mazingira gani wanafanyia kazi na wawindaji wana uzito gani kifedha.

Mheshimiwa Spika, ujangili pia unazidishwa na kutokuwepo kwa Askari wa kutosha. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni kwamba: "Idara ya Wanyamapori inasimamia *Game Reserves 28*, inasimamia *Game Controlled Areas* zaidi ya 40, kwa ujumla inasimamia maeneo yenye zaidi ya kilomita za mraba 200,000. Vigezo vya Kimataifa kwa ajili ya ulinzi peke yake vinasema kwamba, Askari mmoja wa Wanyamapori anapaswa alinde eneo lisilozidi kilomita za mraba 25. Kwa hiyo, kwa kilomita za mraba 200,000 unajikuta kwamba Askari tuliopaswa kuwa nao ni karibu 8,400. Hivi tunavyozungumza Askari tulionao hawafiki 1,700 kwa Tanzania nzima."

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri hii ni kwamba ni rahisi kwa Askari waliopo kukaa kwa muda mrefu katika eneo moja na matokeo yake ni kuwapa majangili ratiba nzima ya mfumo wa ulinzi na mienendo ya wanyama. Kwa mfano, hifadhi nzima ya Katavi ina wafanyakazi 45 tu, eneo lake ni karibu ha.10,000. Eneo hilo halina mawasiliano ya aina yoyote na ratiba ya tembo kutoka eneo moja kwenda lingine inajulikana kwa majangili. Hapa ni dhahiri kuwa mauaji ya tembo yanayofanyika ushiriki wa Watendaji hauwezi kuepokwa?

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi toka kwa Watendaji kuwa majangili wanatumia silaha za kivita katika kutimiza azma yao. Kambi Rasmi ya Upinzani

inaliona hili kuwa ni jambo la kimtandao zaidi, kwani tunaamini kuwa Taasisi zenye uwezo wa umiliki wa silaha hizo ni Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa silaha hizo kwa majangili ni lazima kuwe na uhusiano wa moja kwa moja na baadhi ya Watendaji katika majeshi hayo mawili. Hili linazidisha hofu kutokana na ukweli kwamba tembo wanazidi kuuawa na *TANAPA* hawana silaha za kukabiliana nazo. Silaha zilizoagizwa zimezuiwa kwa ajili ya kulipiwa ushuru, na hilo linawezekana ni kosa la makusudi la kimtandao ili kukwamisha upatikanaji wa silaha za kukabiliana na ujangili. Utaratibu wa kuagiza silaha unajulikana kuwa jeshi ndilo lenye jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa ujangili ni mkubwa sana, kwani upo katika uuaji, usafirishaji, masoko, Polisi, *TRA* na Mahakama. Uchunguzi umebaini kuwa baadhi ya Mahakimu wa Mahakama za Wilaya katika Mikoa ya Mara, Simiyu, Shinyanga, Katavi na Kigoma ni sehemu ya mtandao huo, kwani watuhumiwa wengi wanaokamatwa na nyara zikiwemo silaha hupewa dhamana na hawarudi Mahakamani. Mfano, mtuhumiwa aliyekamatwa kwa tuhuma za kuwinda faru, nyani na ngiri ndani ya hifadhi ya Serengeti mwaka 2010, madubu Masunga Dusara (33) mkazi wa Ng'walali haonekani Mahakamani baada ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Shinyanga - Mheshimiwa Lydia Ilunda kumpa dhamana kwa masharti nafuu.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe taarifa, kwanini wale waliotajwa katika ripoti ya ujangili wameweza kupewa nafasi kubwa ya uongozi wa nchi hii? Biashara ya pembe za ndovu inamilikiwa na nani? Usafirishaji wa pembe hizo na nyaraka nyingine unaratibiwa na magenge gani katika bandari na viwanja vya ndege? Ni kwa kiasi gani vyombo vya Serikali kama Jeshi la Polisi, Usalama wa Taifa na Mamlaka ya Mapato nchini (*TRA*) vinahusika?

Mheshimiwa Spika, Mwezi Desemba, shehena yenye tani 1.3 ya meno ya Tembo iliyofichwa kwenye magunia ya

Alizeti ilikamatwa na Maafisa wa Forodha wa HongKong. Shehena hii ilikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni moja na nusu. Pia wiki mbili kabla ya hapo, takribani tani nne za meno ya tembo zilikamatwa huko huko Hong Kong. Kwa matukio haya mawili, hawa ni sawa na tembo 900 waliouawa.

Aidha, katika mwezi Desemba, 2012 Polisi Mkoani Arusha walikamata nyara nyingi za Serikali katika eneo la Kisongo, zikiwemo ngozi za Simba na wanyama wengine, pembe za ndovu na wanyama wengine na vichwa vya wanyama. Nyara hizi zilikuwa tayari kwa kuuzwa nje ya nchi. Vivyo hivyo Mkoani Katavi walikamatwa majangili kadhaa na kuachiwa huru kwa amri kutoka juu kwa mujibu wa taarifa za Maafisa wa Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika mjadala wa makadirio ya bajeti ya mwaka 2012/2013 ilizungumza sana juu ya hali tete iliyopo katika usalama wa wanyamapori kwa ushahidi wa kutosha ili kuweza kuisaidia Serikali katika kulinda rasilimali asili ya wanyamapori. Kambi Rasmi ya Upinzani ilichoambulia kwa Serikali ni kubezwa na kudhalilishwa na siyo kupokea maoni yetu na kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa hivi karibuni nchini Kenya, Watetezi wa Hifadhi waliishinikiza Serikali kuanzisha sheria kali dhidi ya ujangili ili kuwepo na adhabu stahiki. Pili, Idara ya Wanyamapori ya Kenya (*KWS*) na wahifadhi maliasili kutangaza teknolojia mpya ambayo itasaidia kupambana na ujangili kama ilivyotangazwa na *Daily Nation* ya tarehe 26 Machi, 2013, na tatu Serikali ya Kenya kuongeza Askari zaidi ya 1,000 ili kukabiliana na ujangili. Haya yote yakifanyika Kenya kukabiliana na ujangili, Serikali ya Tanzania inaendelea kulinda majangili ambao taarifa zao zimekuwa zikizifikia Mamlaka zilizo chini ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kutoa rai kwa Serikali, pamoja na kejeli na udhalilishaji kwa Kambi yetu ya kuashiria kuwa na chuki ya wazi na CHADEMA, hili halina tija kwa wananchi

waliowachagua. Ni vema wakarejea kuwa na uzalendo kwa nchi yetu na kuona umuhimu wa kulinda rasilimali zetu na kuwafanya Watanzania wanufaike na rasilimali hizo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa za kanzidata ya Mfumo wa Taarifa za Biashara ya Tembo, yaani *Elephant Trade Information System (ETIS)* kwa kipindi cha mwaka 2002 hadi 2012, Tanzania katika matukio ya kukamatwa kwa shehena za pembe za ndovu kwa matukio 23 sawa na asilimia 28 ya shehena zote kubwa duniani, kwa takwimu hizo imethibitika kuwepo mauaji ya tembo 24,000 kwa shehena zilizokamatwa za pembe za ndovu, hivyo Tanzania kuwa ni nchi inayotoa pembe za ndovu kwa wingi duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2012 tu, shehena zilizokamatwa nchini Hong Kong zenye uzito wa kilo 1,330 pia kwa mfululizo, kuwepo kwa shehena zilizokamatwa kwa nyakati tofauti nchini *Vietnam* kilo 6,232 mwezi Machi, 2009 na 2005; 6 Agosti, pia nchini Ufilipino (*Philippines*) kilo 3,346, mwaka 2011, Malaysia, na nchi nyingine duniani. Kwa matukio haya baadhi na kutokuwepo kwa hatua zozote zinazochukuliwa ni dhahiri Dola imekuwa ni mhusika mkubwa wa kulinda tatizo hili la ujangili na hivyo kuendelea kuwa na walakini na kutokuhusika kwa dola kuchochea tatizo la ujangili kuendelea kuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio hasi kwa nchi kwa takribani miaka saba ijayo Tanzania itakuwa na historia ya kuwa na akiba ya tembo, ikiwa tafiti za mwenendo wa mauaji ya tembo kuonesha kukua na kuashiria mauaji kufikia 10,950 kwa mwaka huu wa 2013, ni dhahiri juhudi za kutokomeza ujangili zilizopo zitatufikisha mwaka 2020 tukiwa hatuna akiba ya tembo hata mmoja tena.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kutoa rai kwa Serikali kama ilivyotoa katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2012, kwamba kuna haja ya kuangalia upya mfumo mzima wa ulinzi wa wanyamapori kama kweli Serikali inayo nia ya dhati ya kukabiliana na tatizo la ujangili nchini.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabla ya kuanza kuchukua hatua dhidi ya tatizo la ujangili kwa nia ya kizalendo kwa nchi, ni vyema sasa Serikali ikaanza kujitathmini yenyewe na viongozi ndani ya Serikali na Chama cha Mapinduzi juu ya tuhuma zilizopo kwa viongozi wake kuhusishwa na ujangili ili kuweza kutoka nje kwa ujasiri kushughulikia tatizo hilo baada ya kuwajibisha viongozi wahusika na kuacha Watendaji na viongozi safi ndani ya Serikali na Chama watakaoshughulikia pasipo kuwa na haya.

Mheshimiwa Spika, pia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuona umuhimu wa kurejea Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009 kifungu cha 103 kinachohusu adhabu kwa makosa ya yanayohusu umiliki wa silaha zinazotumiwa na shughuli za ujangili kuifanyia marekebisho ili adhabu kali zaidi zitolewe kuliko sheria inavyosema kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia inaitaka Serikali kushirikisha wadau wa ulinzi hususan Jeshi la Wananchi (JWTZ) kushiriki katika ulinzi wa wanyamapori kutokana na Mamlaka za Hifadhi na Jeshi la Polisi kuzidiwa nguvu na mitandao ya ujangili ambayo imekuwa ikitumia silaha kubwa za kivita katika shughuli za ujangili.

Mheshimiwa Spika, Shoroba (*corridor* za wanyama – Mapitio ya Wanyama) zote za wanyama ni lazima zilindwe kikamilifu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa wanyama huwa wanaendelea kupita njia ile ile wakati wote wa maisha yao na katika mapito hayo ndiyo pia hupata muda wa kuzaliana. Mbali na hilo, ni pia katika shoroba hizo majangili ndipo hutumia mwanya huo kuwaua.

Aidha, pamoja na umuhimu wa Shoroba hizi za wanyama, Serikali imekuwa ya kwanza kuziharibu na mfano ni ushoroba uliopo Mvomero ambako yalikuwa ni mapito ya Tembo. Serikali imejenga jengo la Mkuu wa Wilaya na Halmashauri kwenye eneo hilo, na ni hivi majuzi tu tembo aliyekuwa anapita eneo hilo, iliamriwa auawe na Maaskari wa Wanyamapori baada ya kukwama njiani kutokana na

kukosa njia eneo hilo. Pia upo mfano wa shoroba iliyopo kati ya Tarangire na Manyara inayopitia njia ya Mijingu, nayo imevamiwa na kaya za watu wasiozidi 22 na kufunga njia hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ambayo inasema kuwa inahifadhi uhalisia wa mazalia ya wanyamapori wetu, inakuwaje wataalam wetu na Serikali badala ya kulinda, wanakuwa ndio waharibifu wakubwa? Hifadhi ya Taifa Rubondo ni hifadhi ambayo ni Kisiwa kinachoundwa na visiwa tisa vidogo vidogo ambapo kisiwa hiki cha Rubondo ni makazi na mazingira muafaka ya kuzaliana Samaki wakiwemo Sato na Sangara wenye ukubwa wa uzito wa kilo hadi 100. Wanyama wanaopatikana katika hifadhi hiyo ni pamoja na Viboko, Pongo, Nzohe, Fisi maji, Mamba na Pimbi, wanabadilishana makazi na wanyama wengine waliohamishiwa katika hifadhi hii kama Sokwe, Tembo, Mbega weusi na weupe na Twiga.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa shoroba za kuwafanya wanyama waweze kutoka na kurudi katika hifadhi ni tatizo kubwa *kijenetik*. Kutokana na utafiti uliofanyika unaonyesha kuwa kitendo cha wanyama kukaa eneo moja kwa muda mrefu na kuzaliana wenyewe kwa wenyewe kunaweza kuadhiri wanyama hao. Hili linatokana na ukweli wa kibailojia kuwa uzaliano wa kindugu (*in breeding*) una madhara makubwa kwa jamii, kwani kama kwenye familia kuna magonjwa, ni dhahiri kuwa familia nzima itakuwa na magonjwa hayo na vivyo hivyo, kwa hifadhi ambazo wanyama wake wametengwa na kufungiwa sehemu moja. Hii ni hatari kwa mwendelezo mahiri wa hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika tafiti umeendelea kuwa ni vigumu kwa Serikali yetu hususan katika Sekta ya Wanyamapori kutokana na kutokuwa moja ya vipaumbele vya Serikali. Hii ni kutokana na dhana ya Serikali kutotambua umuhimu wa rasilimali hizi kwa maendeleo ya uchumi wa nchi, Taasisi ya utafiti wa Wanyamapori ambayo ni *TAWIRI* na inafanyakazi zake lakini kutokana na kutokupatiwa fedha za kutosha za kufanya tafiti zake kwenye Sekta ya

Wanyamapori kumepelekea taarifa muhimu na za maana kutokupatikana hapa kwetu kwa maendeleo ya Sekta ya Wanyamapori, badala yake tafiti muhimu kwenye sekta hii zinafanyika kwa ufadhili toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa, huu ni udhaifu kwa nchi ambayo inapata mapato mengi kupitia sekta hii na kutowekeza zaidi katika utafiti wa sekta hii. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 makusanyo Sekta ya Wanyamapori yalikuwa kiasi cha Sh. 15,074,053,972.10 na kwa mwaka wa fedha 2012/2013 makisio yalikuwa Sh. 25,175,381,917/=. Hizi ni fedha nyingi kwa sekta ambayo uwekezaji katika sekta hiyo ni karibu na hakuna. Kuna haja ya Serikali kuona umuhimu wa kujitathmini zaidi na kuona ni muhimu zaidi kwa maendeleo ya Sekta ya Wanyamapori kuwa na fungu maalumu kwa ajili ya kuwezesha tafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuna Taasisi ambayo imepewa dhamana ya kuratibu na kuwezesha tafiti mbalimbali hapa nchini ambayo ni *COSTECH*, lakini cha ajabu ni kwamba Taasisi hii imekuwa haitoi kipaumbele kwa watafiti ambao wanafanya utafiti kwenye sekta hii ya wanyama na badala yake utafiti unaegemea sana fedha za mashirika ya nje ambayo yanakuwa na haki zote za tafiti husika. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka vipaumbele kwa kuangalia mchango wa sekta kwenye uchumi husika ambako tafiti zitafanyika.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaozunguka Mbunga za Hifadhi ndio wenye jukumu kubwa la kuhakikisha ulinzi wa wanyama. Hivyo basi, mahusiano kati ya mbuga na wananchi ni muhimu sana. Mipaka ya hifadhi iliyowekwa miaka hiyo wakati idadi ya wananchi katika vijiji mbalimbali ilikuwa ni ndogo na hivyo mipaka ya hifadhi ilikuwa ndani ya vijiji na shughuli za vijiji hazikuwa na madhara katika hifadhi hizo. Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wananchi katika maeneo hayo na shughuli zao za kiuchumi kuwa kubwa, kulipelekea maeneo ya hifadhi kutumiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha uhifadhi wa wanyama wetu unaendelea vyema, ni lazima ushirikishwaji wa wananchi katika zoezi lolote la kuweka mipaka ya hifadhi au kuchukua mipaka iliyokuwepo miaka ya 1960 ni muhimu. Pia ni bora kama nchi tuangalie jukumu letu la msingi ni nini kati ya kulinda raia wake au kulinda wanyama?

Mheshimiwa Spika, Mbuga ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha inapakana na jamii kubwa na kwa sasa kuna mgogoro wa ardhi baina ya *TANAPA* na wananchi wa Ruaha kwa kuwanyang'anya ardhi yao hasa kwenye Kata ya Rwembe, na hivyo kuwafanya wananchi kushindwa kufanya shughuli za maendeleo kama vile kilimo na wakati hawana njia nyingine ya kupata kipato chao cha kujikimu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa kauli kuhusiana na madhira haya wanayopata wananchi wa Kata ya Rwembe ambao vijiji vyake vinne wamezuiliwa wasifanye shughuli yoyote ya maendeleo na uongozi wa *TANAPA*.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa jamii zinashiriki na kunufaika na maliasili zetu, hasa Wanyamapori na Kukuza Uhifadhi wa Wanyamapori nje, na maeneo ya makazi yao, hivyo kuanzisha maeneo ya Jumuiya ya Usimamizi Wanyamapori (*WMA*). Kazi kuu za *WMA* ilikuwa ni kuhamishia usimamizi wa maeneo ya Jumuiya ya Usimamizi Wanyamapori kwa wananchi vijijini na hivyo basi kuulinda ushoroba wa wanyama, njia za uhamaji, maeneo ya usalama wa wanyama, na kuhakikisha kwamba jamii zilizo katika maeneo hayo ya wanyama zinafaidika vilivyo kutokana na uhifadhi wanyamapori. Kuzuia matumizi haramu ya wanyamapori nchini kote kwa kuchukua hatua endelevu za usimamizi, ulinzi na kutekeleza sheria.

Mheshimiwa Spika, kitendo chochote kitakachofanyika cha kuzifanya hizi *WMA* kushindwa kufaidika na uwekezaji wa wananchi katika hilo ni hujuma kwa wananchi na kinapelekea wananchi badala ya kuwa wasimamizi wanakuwa wahujumu.

Mheshimiwa Spika, MBOMIPA ni kifupi cha chenye maana ya “matumizi bora maliasili”. IDODI na PAWAGA inaundwa na vijiji 21 kama wanachama waanzilishi. Vijiji vyote vipo katika Tarafa za Idodi na Pawaga Wilaya ya Iringa. Ilianziwa mwaka 1998, iko Mashariki ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Asasi ya MBOMIPA inasimamia eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 773. Eneo hili lina aina na idadi kubwa ya wanyama wakubwa, wadogo, ndege na mandhari nzuri ya kuvutia kandokando ya Mto Ruaha ambao ndiyo mpaka na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayoikumba asasi hii ya *WMA* yanaakisi asasi nyingine za uhifadhi za wananchi. *MBOMIPA* ilipata mwekezaji tangu mwaka 2008 anayeitwa *Kilombero North Safari (KNS)* kwaajili ya ujenzi wa hoteli na lodges za kitalii. Mwekezaji huyu hajajenga hoteli yoyote hadi sasa na amekuwa akiwadanganya wananchi na Jumuiya juu ya ujenzi wa hoteli kulingana na makubaliano na *MBOMIPA*. Mwekezaji huyu pia amekuwa akilazimisha kufanya shughuli ya uwindaji kwenye kanda hiyo na kukiuka Sheria ya Uwindaji na *Resource Zone Management Plan (RZMP)* ambayo imepitishwa na *MBOMIPA* kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, ujangili ni mkubwa sana hasa wa tembo kwenye kanda ambayo inasimamiwa na Mwekezaji huyu, na hata tarehe 20 na 21 Aprili, 2013 wameuawa tembo wanne wakubwa karibu kabisa na Kambi ya Mwekezaji (*KNS*) na meno yote kuchukuliwa na majangili. Hili suala linajulikana kwa Watendaji karibu wote wa Serikali. Hii inatokana na maslahi na mahusiano binafsi kati ya wahusika na wamiliki wa *Kilombero North Safari*.

Taarifa zilizopo ni kwamba, Kampuni ya *Kilombero Hunting* ina wanahisa ambao baadhi yao ni Wajumbe wa Bodi ya asasi ya *MBOMIPA* ambao pia ni wafanyabiashara wawili maarufu Iringa, Mbunge mmoja na mfanyabiashara maarufu nchini ambaye mdogo wake Acram Aziz ni msimazi

wa karibu kwa niaba ya kaka yake. Hii ndiyo siri ya ubabe wa Kampuni ya *Kilombero North Safari* katika eneo la LUNDA ndani ya eneo la MBOMIPA.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa eneo la Asasi ya MBOMIPA unakabiliwa na changamoto kubwa kutokana na vitendo vya rushwa vinavyofanywa na kampuni zinazotaka kupata maeneo ya uwindaji hasa Kampuni ya *Kilombero Hunting Safari* na nyingine ambayo inatoa rushwa kwa baadhi ya Wajumbe wa Bodi ya MBOMIPA, Afisa Wanyamapori (W) Iringa, baadhi ya Viongozi wa Vijiji na Wajumbe wa Vijiji kwenye Asasi.

Mheshimiwa Spika, kiini cha mgogoro na migongano inayotokea kwenye eneo la asasi linasababishwa na maslahi ya Wawindaji na siyo suala la Uhifadhi endelevu wa eneo husika. Kwa kuwa lengo ni uhifadhi wa wanyamapori na mazingira yao, mgogoro huo utakwisha pale tu ambapo Jumuiya hii itaondokana na kuachana kabisa na shughuli za uwindaji katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa, eneo la MBOMIPA kuendelezwa kwa shughuli za Utalii wa picha ambazo ni endelevu, na ipige marufuku shughuli zote za uwindaji. Aidha, ifanye ukaguzi maalum kwa WMA hiyo ili kubaini mwenendo wa asasi hiyo kama unazungatia maslahi mapana na uanzishwaji wake, hatua za haraka zichukuliwe ili kunusu raslimali za nchi kuishia kwenye mifuko ya wahujumu uchumi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa taarifa ni kwa kiasi gani makubaliano kati ya WMA na Kampuni ya *Kilombero North Safari* yametetelezwa kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Spika, katika ukusanyaji wa maduhuli ndani ya Idara mbalimbali, kumekuwepo na baadhi ya takwimu zinazoashiria ubadhirifu wa rasilimali za umma kwa kuzingatia viwango vinavyotajwa kwenye makadirio ya makusanyo. Ukisoma katika randama ya Wizara

iliyowasilishwa ndani ya Kamati, kifungu namba 1001- Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu kinatoa kiasi cha fedha zinazotarajiwa kukusanywa kutokana na vyanzo vya mapato kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, taarifa inaonesha makusanyo katika mauzo ya vifaa chakavu ni Sh. 1,000/=, mapato yatokanayo na mauzo ya vifaa Sh. 1,000/=, masurufu ambayo hayajarejeshwa Sh. 1,000/=, pia katika kifungu cha 2001 mapato mengine Sh. 1,000/= kwa kutokuwa makini na Watendaji wa Wizara na kutumia mbinu chafu kuiba rasilimali za Umma kwa kuweka viwango vidogo vya makadirio ya ukusanyaji huku takwimu hizi kutokuakisi uhalisia, ni dhahiri Taifa litaendelea kutafunwa na baadhi ya Watendaji wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, kwa akili ya kawaida, Wizara haiwezi kufanya kazi ya kukusanya Sh. 1,000/= kwa mwaka mzima na huu ni mfano wa maeneo machache kwa kuonesha tabia hii kukithiri ndani ya Serikali kwa wahujumu na kujificha katika mgongo wa Serikali kutopata mapato ya kutosha huku mapato yakipatikana kwa kiwango kikubwa na bila taarifa zake kuwekwa wazi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutolea ufafanuzi hujuma hii inayofanywa na Watendaji na ni kwa vipi Wizara inadhibiti taarifa za makadirio ya maduhuli kwa kuhakiki ili ziwe na uhalisia zaidi kuliko hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2012, Serikali imeendelea kutoa vibali vya kuendelea na uwindaji kwa Kampuni zilizokuwa na malimbikizo ya madeni, mfano kampuni saba za uwindaji: *M/S Malagarasi Hunting Safaris, Mwanahuta & Company Limited, Usangu Ltd, Rana Tours & Safaris Ltd, Coastal Wilderness (T) Ltd, Kilimanjaro Game Trails Ltd na Said Kawawa Hunting Company Ltd*. Kampuni hizi kwa jumla zikidaiwa na Wizara jumla ya dola za kimarekani 973,493.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina juu ya sababu za kutoa vibali pamoja na Kampuni hizi kushindwa kulipa maduhuli kwa wakati na kuendelea kuruhusiwa kufanya shughuli za uwindaji.

Mheshimiwa Spika, pia wawindaji halali waliopewa leseni wamekuwa wakifanya shughuli za uwindaji na kufikia mwisho wa mwaka 2012, bado Serikali haikukusanya maduhuli yenye jumla ya dola za Kimarekani 216,000 na kuisababishia hasara Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inachelea kulithibitishia Bunge kuwa ni vitendo vya rushwa vinavyoifanya Serikali ikose mapato na mapato hayo kuingia mifukoni mwa Watumishi wasio waaminifu ndani ya Wizara. Hivyo basi, Serikali itoe ufafanuzi wa kina, nini tafsiri yake kama siyo ruhusa?

Mheshimiwa Spika, Taarifa za Upotevu wa Mapato ya Serikali imeendelea kuonekana katika Sekta ya Utalii kupitia ada ya Utalii isiyokusanywa. Dola za Kimarekani 158,000 kwa mujibu wa Kanuni Na. 4 ya Kanuni za Utalii (ada na tozo) za mwaka 2009 inaeleza kuwa "ada ya leseni kwa kila daraja italipwa kila mwaka kwa kiasi ambacho kimeainishwa katika jedwali la pili la Kanuni hizo".

Mapitio ya makusanyo ya mapato yatokanayo na Leseni za Uendeshaji wa Huduma za Utalii katika Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2011/2012 yameonyesha kuwepo kwa Kampuni zilizojiingiza kwenye biashara ya kutoa huduma ya utalii lakini hawajalipa ada ya Leseni za Utalii yenye jumla ya Dola za Kimarekani 158,000.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano, malengo ya kiutendaji ni kuboresha mfumo wa makusanyo ya mapato yatokanayo na shughuli za utalii. Kambi ya Upinzani inauliza kama mambo yaliyo wazi ya ukusanyaji yanashindikana, huo mfumo utaboreshwa vipi wakati hujuma inafanywa kwa ushirika na Watendaji?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina, ni kwa jinsi gani imehakiki ili kutorudiwa kwa matatizo haya ya kupoteza mapato? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuchukua hatua kwa Watendaji wasiozingatia sheria na kanuni katika kutimiza majukumu yao, maana utaratibu huu ni hujuma inayofanywa na wafanyabiashara na Watendaji wasio waaminifu kwa Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mpango wa maendeleo, unaonyesha kuwa kwa mwaka huu wa fedha uwekezaji kwenye Sekta ya Utalii ni Shilingi bilioni 43.968 wakati kitabu cha bajeti fedha zilizotengwa za maendeleo katika Sekta ya Utalii inaonyesha Shilingi bilioni moja tu sawa na asilimia 2.2 tu ya fedha zilizotengwa kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza kwa nini hili limekuwa hivi? Nini tafsiri ya kuwa na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kama hatuwezi kuutekeleza? Ni kweli sekta hii itaweza kuwa shindani na wenzetu katika jumuiya ya Afrika ya Mashariki au tupo tukisubiri miujiza? Kama siyo dharau kwa Ofisi ya Rais, Idara ya Mipango, ni nini hiki?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kitabu cha *Transforming the informal Sector, How to Overcome the Challenges (ESAURP)* kinaainisha takwimu za ukubwa wa eneo la misitu Tanzania ikiwa ni hekta milioni 33.5 za misitu ambayo ni sawa na asilimia 38 ya eneo la ardhi yote nchini, pia kinaainisha mchango mkubwa unaoweza kutolewa na Sekta ya Misitu katika uchumi kwa kuirasimisha sekta hiyo kuweza kuweka mazingira bora ya ajira kwa wananchi ikizingatiwa shughuli za misitu ni moja ya chanzo kikubwa cha kipato kwa wananchi wa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za *TRAFFIC 2007* zinaainisha kuwa ni asilimia nne tu ya mazao ya misitu huvunwa kihalali na asilimia 96 huvunwa bila kupata vibali rasmi na Serikali kukosa mapato kwa uvunaji mkubwa unaofanywa kutokana na kutorasimisha biashara ya mazao ya misitu na kuwa na utaratibu ulio rasmi wa kufuatilia

uvunaji wa mazao haya ya misitu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuona umuhimu wa kuona asilimia kubwa ya wananchi wanaotegemea bidhaa za misitu kuendesha maisha yao kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika hizo asilimia 96 ambazo huvunwa bila ya kupata kibali, kuna miti ambayo inavunwa kwa ajili ya uchomaji wa mkaa. Kwa mujibu wa tafiti zilizokwisha fanyika, Sekta ya Mkaa huingiza zaidi ya dola milioni 650 sawa na zaidi ya Shilingi trilioni moja kwa mwaka na kuajiri mamilioni ya Watanzania hususan waishio vijijini. Ni wazi kuwa sekta hii imeachwa bila mikakati na sheria unganifu. Kama nilivyoeleza kwa kina katika hotuba yangu ya Wizara ya Mazingira, Tanzania tunapaswa kujifunza kutoka Brazil ambayo inazalisha mkaa asilimia 11 na Tanzania pekee inazalisha asilimia tatu ya mkaa wote unaozalishwa duniani. Sekta hii ikiwekewa mikakati mizuri ya makusudi itaweza kuzalisha mikaa kwa njia ya kisasa huku ikipunguza hewa ya ukaa na kuifanya sekta hii kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, Brazil huzalisha asilimia 11 ya mkaa wote unaozalishwa duniani. Kwenye miaka ya 1990 asilimia 60.3 ya uzalishaji wa mkaa Brazil ulifanywa kutoka kwenye uvunwaji wa misitu ya asili.

Baadaye mkakati wa makusudi ulifanywa ili mkaa uzalishwe kutoka katika misitu ya kupandwa. Ingawa matumizi ya mkaa nchini Brazil ni kwa ajili ya viwanda vya kufua chuma, jambo la msingi ni kwamba uvunaji wa mkaa kwa misitu asili ilipungua kwa asilimia 82 kati ya mwaka 1989 hadi 1996. Makampuni makubwa yalipewa jukumu la kupanda miti, kuzalisha na kusambaza mkaa kwa ajili ya kuifanya iwe endelevu. Hapa nchini upo uwezekano kabisa wa kuboresha ubora wa mkaa kwa kuwajengea uwezo wazalishaji na kuifanya kuwa sekta rasmi huku tukiendelea kuboresha mazingira yetu. Hali hii ikiwezekana, itasaidia sana katika kuboresha na kuhifadhi misitu katika Tanzania.

Ikiwa Sekta ya Mkaa itafanywa kuwa endelevu, ni dhahiri kuwa athari zitokanazo na mkaa kama vile uharibifu

wa mazingira, hewa ya ukaa iharibuyo tabianchi na gesi ya *ozone* kupunguzwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuanzisha mikakati ya makusudi ya kuweza kuifanya Sekta ya Mkaa iwe sekta rasmi na endelevu kwani ni nishati tegemewa na asilimia kubwa ya wananchi wa Tanzania. Pia, mchango wake wa zaidi ya Shilingi trilioni moja katika ukuaji wa pato la Taifa ni mkubwa ukilinganisha na mazao mengine yatokanayo na misitu. Hivyo haiwezi kupuuzwa na kuachwa bila mkakati wowote.

Mheshimiwa Spika, badala ya kuacha Serikali iendelee kupoteza mapato kupitia Watendaji katika Halmashauri ambao wamekua wakitoza faini kwa bidhaa za misitu na mapato yake kutoingizwa katika Mfuko wa Serikali, na ukweli ni kwamba hata tusiporasimisha, mkaa utaendelea kutumika na itaendelea kuwa ni biashara ya wakubwa tu, na kama Taifa, misitu itaendelea kukatwa na mapato tutaendelea kuyakosa. Kwani ukweli ni kwamba hatuna chanzo mbadala cha nishati kwa Watanzania wa kipato cha chini. Hivyo basi, ni wakati muafaka kwa Serikali kurasimisha biashara za misitu na kuwafanya wananchi waendeleo kufanya kwa utaratibu maalumu na kuweza kuipa Serikali sehemu ya mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, mwanamazingira mmoja duniani aliwahi kusema hivi, naomba kunukuu: *"To be poor and be without trees, is to be the most starved human being in the world"*, Hakuishia hapo, na akasema tena: *"To be poor and have trees, is to be completely rich in ways that money can never buy."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la uharibifu wa misitu bado limeendelea kuwepo nchini na kuathiri juhudi za utunzaji wa misitu nchini. Itakumbukwa mnamo tarehe 19 Aprili, 2013, ilizungumzwa ndani ya Bunge hili kuwa magogo yamekuwa yakisafirishwa nje ya nchi kupitia bandari ya Dar es Salaam katika maswali kwa Mawaziri, huku tatizo la madawati kwa wanafunzi likiwa halijapata suluhu. Swali linakuja: Je, pamoja

na majibu ya Waziri kuwa Serikali imekwishapiga maruku usafirishaji wa magogo nje ya nchi, ni sahihi kuwa hali iliyopo sasa inathibitisha utekelezaji wa katazo hilo la Serikali?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haihitaji kujua nani alitoa taarifa zilizo sahihi kati ya Mbunge na Waziri, lakini jambo kubwa hapa ni kusimamia sera na taratibu rasmi za Serikali katika kulinda misitu nchini. Itakumbukwa kuwa takwimu zinaonesha kuwa ni asilimia nne tu ya misitu yetu ambayo huvunwa kwa vibali halali na asilimia 96 ni kwa njia isiyo halali. Hii ni kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (*JET*) - "Biashara haramu ya mazao ya misitu yaisumbua Serikali."

Mheshimiwa Spika, kutokana na ubadhirifu huo katika Sekta ya Misitu, Serikali inakosa mapato yatokanayo na uvunaji wa misitu. Pia wananchi wa pembezoni mwa misitu wanashindwa kujikwamua katika umaskini. Kwa kurejea taarifa ya Shirika la Mazingira la *TRAFFIC* ya mwaka 2007, ilitoa takwimu zilizoonesha hasara inayoipata Serikali kwa mwaka kutokana na biashara haramu ya misitu ikiwa ni Shilingi bilioni 75. Pamoja na kuonesha hasara hiyo ya mapato ya Serikali, pia ilieleza uhusikaji wa viongozi wa Serikali katika ubadhirifu huo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuona umuhimu wa misitu katika kukuza uchumi na kuwaondoa wananchi katika wimbi la umasikini, hivyo kuweka kipaumbele katika suala la usimamizi wa misitu iliyopo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu, aliainisha moja ya vipaumbele vya Ofisi yake ikiwa ni pamoja na ufugaji nyuki, na kueleza mwenendo wa Sekta ya Nyuki nchini. Pamoja na maelezo ya Waziri Mkuu, bado sekta hii ipo nyuma ikilinganishwa na matamshi ya kuonesha kuwepo kwa juhudi kubwa katika kuiwezesha sekta hii kukua na kuwa na tija kwa uchumi wa nchi na jamii husika. Ufugaji wa nyuki ni shughuli ya kiuchumi inayoweza kuwaongezea wananchi wetu kipato na kuwaondolea umaskini. Katika kipindi cha

miaka minne iliyopita 2009 - 2012, uzalishaji wa asali ulifikia wastani wa tani 8,747 na nta tani 583 kwa mujibu wa taarifa ya Waziri Mkuu Bungeni katika hotuba ya makadirio ya bajeti ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, suala la kipaumbele chochote cha Serikali siyo kufanya kwa malengo ya kutangaza nia kwa wananchi kwa maslahi ya kisiasa, kuna haja ya Serikali kuhakiki inatekeleza vipaumbele kwa kuonesha utendaji halisi hasa kuifanya Sekta ya Nyuki kuwa na manufaa kwa wananchi wanaoingia katika biashara hiyo. Takwimu zinazotolewa na taarifa za Serikali juu ya kuiwezesha Sekta ya Ufugaji Nyuki siyo za kuridhisha kutokana na rasilimali nyuki tulionayo nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Serikali juu ya uwekezaji katika Sekta ya Nyuki kwa kuendeleza sekta hiyo kuweza kuwafanya wananchi waweze kuuza bidhaa za nyuki na siyo bidhaa ghafi.

Mheshimiwa Spika, taarifa za mauzo yatokanayo na bidhaa za misitu, licha ya ukweli kwamba bidhaa za misitu zimekuwa kianzio kikubwa cha mapato kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara inaendelea kukiri katika taarifa zake kwa uwazi kwamba hakuna udhibiti wa kutosha kwenye eneo la misitu. Hivyo kusababisha makusanyo ya maduhuli sawa na asilimia 40 kutokusanywa kwa kutokana na changamoto mbalimbali hususan kuingiliwa na wanasiasa, maslahi madogo kwa Watumishi, Wasimamizi wa Misitu, ulegevu katika usimamizi wa sheria na kutoeleweka vizuri kwa vianzio vya kodi na wakusanyaji mapato kama vilivyoainishwa kwenye kifungu 49 cha Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 (*Act No 14 of 2002*).

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuona umuhimu wa kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma ili kuwapa motisha na kulinda rasilimali za Taifa, pia kuzingatia sheria katika utekelezaji wa mipango ya Serikali, hivyo itaweza kudhibiti siasa kuingilia utendaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na nguvu hadi wakati huu. Napenda kushukuru viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo kwa msaada mkubwa ambao wamekuwa wakiniipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya kibunge na Uwaziri Kivuli wa Maliasili na Utalii.

Napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Iringa Mjini kwa kunipa nguvu, msaada na ushirikiano tangu wanichague niwe Mbunge wao hadi wakati huu. Nawaambia kwamba nawapenda na nitaendelea kuwatumikia kadri ya uwezo wangu wote.

Mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, ni kwa familia yangu, kwa uvumilivu mkubwa kwa kipindi chote ninachokuwa sipo nyumbani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani naomba kuwasilisha. *(Makoff)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa muda tulionao, tunaweza kuwa na wachangiaji watano na hao ni kama wafuatao: Mheshimiwa Emanuel Nchimbi, Mheshimiwa Professor Juma Kapuya, Mheshimiwa Fatma Abdalah Mikidadi, Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Nianze kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea sana, niitumie nafasi hii kuipongeza sana Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa ambayo inafanya nchini. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri imejdhahirisha wazi kwamba katika kipindi kifupi wameweza kukamata watuhumiwa 354 wa matukio ya ujangili. Ziko Mahakamani kesi 283, bunduki 535

zimekamatwa na risasi zaidi ya 1,129. Vilevile Askari wetu wenye mapenzi na nchi yetu wa Wanyamapori 17 wameuawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna maelezo unayoweza kuweka yakaonyesha ni jinsi ambavyo Wizara hii inafanya kazi kubwa katika nchi yetu. Ukiona mtu anasimama anasema hakuna Wizara inachofanya katika mapambano na ujangili, ni wazi kuwa upeo wake wa kuelewa una utata mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze sasa kwenye baadhi ya hoja zilizojengwa dhidi ya Katibu Mkuu wa Cham cha Mapinduzi Mheshimiwa Abdulrahamani Kinana.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni amelieleza Bunge lako kuwa Mheshimiwa Kinana amehusika na biashara ya kusafirisha pembe za ndovu nje ya nchi. Nimejaribu kufuatilia kwa makini kujua hiki alichokisema alikimaanisha, alikielewa, alikitafakari, au ameandikiwa tu akaenda kusoma? Baada ya kutafakari kwa kina, nimegundua kuwa hakuwa na nia mbaya, ameandikiwa tu na amekwenda kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli wa jambo hili ni nini? Ziko tofauti za majukumu ya *shipping agent* na *clearing and forwarding*, na jambo hili Viongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni wanalijua vizuri mno. Hawajasahau na wala hawajafanya makusudi kulipotosha.

Kampuni ya *Shipping Agency* wajibu wake duniani kote ni kumwakilisha mwenye meli. *Agent* hawezi kuwa mwenye meli, ila anamwakilisha mwenye meli. Kuna shughuli ndogo ndogo zinazofanyika katika eneo zinahusu meli inapofika kwenye nchi, nani anamwakilisha mwenye meli?

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ya kuhudumia Watumishi wa Meli, kupeleka vyakula kwenye meli, kupeleka mahitaji muhimu, kufanya usafi, lakini wako watu wanaitwa *clearing and forwarding*; Kiswahili chake ni kupeleka na

kutoa. Mchungaji Msigwa, *Clearing and Forwarding* ni kupeleka na kutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa ndio wanaopeleka mizigo bandarini. Wakipeleka mizigo bandarini kule ndiyo kuna utaratibu wa upekuzi. Katika utaratibu wa upekuzi, hahusiki mtu wa *Shipping Agency*. Sina mashaka hata kidogo kuwa Mchungaji Msigwa analijua hili ninalolisema, ila amelifumbia macho kwa makusudi kwa maslahi yasiyokubalika katika Taifa. *(Makofi)*

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, taarifa!

SPIKA: Naomba uendelee! Mnanyamaza kama walivyonyamaza wenzenu. *(Kicheko/Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kumekuwepo uvumi ambao umekuwa ukifanywa kwa makusudi kwamba Mheshimiwa Kinana anamiliki meli iliyohusika na kusafirisha pembe zile. Uvumi huu ni uzushi. Meli iliyobeba mizigo ile inaitwa *Delmas Nakala*. Mmiliki wake ni Bus Herman Redray. Jambo hili jambo hili, Kambi ya Upinzani Bungeni inalijua, ila kwa maslahi yasiyokubalika katika Taifa wameamua kudanganya Bunge lako. *(Makofi)*

Baada ya uchunguzi wa kutosha kuhusu kesi hii, wahusika walibainika na ndiyo ikafunguliwa kesi ya Uhujumu na Uchumi Na. 3 na Na. 4 ya mwaka 2009 na watu wakapelekwa Mahakamani. Kwa kibali chako nitawataja waliopelekwa Mahakani. Wa kwanza anaitwa Ladius Tesha, ni Mkurugenzi wa Kampuni ya *Team Fright Tanzania LTD*; Gabriel Chambo Barua - Meneja wa *Import and Export* Kampuni ya *T. Fright Tanzania LTD*; Shaaban Yasin Yabura - Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kigoma *M.N Interprises LTD*; Erick Kileo Moran - Mfanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Bandari ya Dar es Salaam, Issa Ahmed Reno - Wakala wa Kampuni ya Kigoma *M. N. Interprises*; Nelbert Kiwale - Wakala wa Kampuni ya *T. Fright Tanzania LTD*, Abubakar Omar Hassan - Wakala wa Kampuni ya *T. Frighters*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa ndio waliopelekwa Mahakamani, uchunguzi ulijidhihirisha kuwa ndio watuhumiwa wa jambo hili. Jambo hili Kambi ya Upinzani Bungeni inalijua.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kusema kwamba ukishafanya upelelezi unaupeleka Mahakamani. Kesi hii imekwenda Mahakamani, Mahakama ya Kisutu. Ikatokea kuwa umebakiza ushahidi kutoka nchi ya Vietnam. Vietnam wamesema hawana Mkataba na Tanzania kwenye ushirikiano wa mambo ya Jinai, Ubalazi wetu wa China unaendelea kufanya mawasiliano tupate ama Mkataba wa Ushirikiano au wakubali kwa mpito watupatie kibali cha kupata ushahidi kutoka kwao ili kesi iweze kuendelea. Kwa msingi huo wa kukosa ushahidi kutoka Vietnam, Mahakama ya Kisutu iliagiza kesi hiyo iondolewe, ukipatikana huo ushahidi iletwe tena Mahakamani. Jambo hili Wapinzani wanalijua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilichojidhihirisha siku za karibuni ni kwamba Kambi ya Upinzani imeamua kwa makusudi kuanza kutazama kwa makusudi maono yao kwa mtazamo mfupi usiojali maslahi kwa siku za usoni ya Taifa letu. Wameamua kutumia siasa za kupakana matope, siasa za kuchafua watu, siasa za kutunga uongo, siasa za uzushi, siasa za kutoana kucha na kila aina ya siasa ambayo inachafua nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako lazima likatae utaratibu huo. Haya ni maono mafupi. Ni maono ya watu wasiotazama mbele. Hivi leo tukiwakabidhi Serikali, kama mchezo wao ni huu, tukiwakabidhi Serikali watafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mkristo. Kwenye Biblia inasema, ni bora mchawi kuliko mwongo. Ukitaka kuiweka katika tafsiri sahihi, maana yake nini? Wachawi wanatuhumiwa kuua, lakini hawau kwa halaiki kama hivyo, ila mwongo, uongo wake unaweza kusababisha mauaji ya halaiki! Ndiyo msingi wake uko hapa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Bunge lako tumekaa na genge la waongo ambao wanaweza kusababisha maafa zaidi ya uchawi katika nchi yetu. Kila Mtanzania lazima afike mahali aanze kuwachambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulifika mahali tukaanza kuwa na imani. Mtu mwenye nia njema na nchi, anasema tunataka Vyama viwili, vitatu hivi ambavyo vyote vinaweza kupewa madaraka vikaongoza nchi yetu vizuri. Watu wa heshima walishawahi kusema; alishawahi kusema Baba yetu wa Taifa, Mwalimu Nyerere kuwa hii CHADEMA naiona inakuja vizuri. leo angekuwapo angesema CHADEMA haiji vizuri. imejizuia ilipoanzia. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, lazima Bunge lako lisimamie ukweli katika nchi, huu ni ushauri wa bure tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia niseme kuwa, katika matatizo yangu madogo madogo ya kiimani, huwa wakati mwingine namwomba Mchungaji Msigwa aniombee. Leo nimwombe rasmi kuwa amwombee Mheshimiwa Kinana aache kutungiwa uongo. Lakini pia aliombee Taifa liwe lina mkakati wa kwenda mbele, lakini pia aiombee Kambi ya Upinzani Bungeni itokwe na mapepo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Profesa Kapuya.

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Dkt. Nchimbi kwa uchangiaji wake mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa kweli ni nzuri, sina tatizo na utekelezaji wa Wizara hii na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Tatizo langu

liko katika maeneo Fulani fulani tu, kwa mfano suala moja ambalo nataka nizungumzie hasa kwa kuhusisha Jimbo langu la Uchaguzi ni mipaka. Suala la mipaka bado halijazingatiwa sawasawa kama Mheshimiwa Waziri alivyokuwa akizungumza hapa. Katika maeneo ambayo tunaishi sisi mipaka iliyopo bado ni ile ile iliyochwa na Mwingereza wakati wa Ukoloni ndiyo ambayo wananchi tunaitambua na matokeo yake inaleta vurugu kubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa idadi ya watu imeongezeka, ukija kuangalia Jimbo la Urambo Magharibi kwa maana ya Kaliua, wakazi wa asili pale tuko kama 10%, 15% mpaka 20% na wageni ni karibia 80%. Kuendelea kung'anga'ania kwamba wageni hawa wanafanya makusudi kukiuka mipaka hii, siyo kweli. Wageni hawa wakati mipaka inaundwa, hawakuwepo. Sasa Mheshimiwa Waziri ametoa mfano wa Moyowosi Kigosi, labda kama ameweka mpaka huu upande wa Kahama au upande wa Kibondo, lakini kwa upande wa Jimbo langu Mheshimiwa Waziri mpaka huu napenda kukuhakikishia kwamba hauonekani. Kwa hiyo, nakuomba sana, hii mipaka katika eneo hili uje utusaidie sana.

Mheshimiwa Spika, mipaka hii inazua utata sana, imeleta hata mgogoro wa kijamii kwa sababu wageni hawa wanapokuja na hasa kwa kuhamasishwa na baadhi ya Viongozi wa Siasa wenye mlengo usiokuwa na maslahi kwa Taifa hili, wanakwenda kukaa katika maeneo hayo. Wale ambao ni wakazi wa asili wanapoona kwamba wenzao wageni ndio wamekwenda kukaa kule, inaleta matatizo ya kutokuelewana kati ya jamii hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Msemaji wa Kambi ya Upinzani akisema kwamba Mheshimiwa Waziri awajibike kwa kujiuzulu kwa kupotosha, lakini nataka nimrejeshe Mheshimiwa Msigwa kwamba, akiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Maliasili, alipata nafasi ya kutembelea Jimbo langu la uchaguzi, na alishiriki katika kupotosha mipaka ya hifadhi ya misitu kule kwangu. Matokeo yake ametuachia mgogoro mkubwa wa kijamii. Sasa kama hoja ni kujiuzulu, mimi nadhani yeye ndiye anatakiwa awe wa kwanza kujiuzulu. Kwa sababu

ametuletea matatizo makubwa kule. Watu hatuelewani, na ubishi wake anasema mipaka ya mwaka 1949 itawezekanaje uendeleo kuheshimika mpaka leo? Tatizo ni tarehe? Nikamwuliza, kama hiyo ni hoja, basi mipaka ya Tanganyika isiheshimike kwa sababu uliwekwa zaidi ya mwaka 1949. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge hili kama alivyosema Mheshimiwa Nchimbi jamani, hebu tulitumie kuwaelimisha Watanzania. Bunge ni Taasisi inayoheshimika sana. Tukiwapotosha Watanzania kwa kutumia Taasisi hii, tunawaangamiza! *(Makofi)*

MHE. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, taarifa!

SPIKA: Ngoja amalize hotuba yake. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Hakuna taarifa!

MBUNGE FULANI: Kaa chini!

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Spika niko mmoja tu. Mimi ndio Spika! Siyo kila mtu anatoa amri. Nimesema Mheshimiwa Kapuya atamaliza hotuba yake.

MHE.PROF. JUMA A. KAPUYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunilinda. Kwa sababu ninayoyasema ni kweli, na yeye anajua!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisa ilikuwa kwamba, pale Kijiji cha Shela, kuna Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji ambaye ametokana na Chama cha Upinzani. Kwa hiyo, akaacha kuangalia misingi ya mipaka, akazungumza misingi ya kisiasa na hii ndiyo inatuletea vurugu. Mpaka leo pale mahali hapajatulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie suala letu la mipaka.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ningemwomba Mheshimiwa Waziri, yapo maamuzi ambayo yalishapitishwa na Mawaziri waliopita, sasa kwa sababu sisi tunaamini Serikali ni endelevu, Serikali ni ile ile, maamuzi yaliyopitishwa na Mawaziri waliopita akiwemo Mheshimiwa Zakhia Meghji, hebu myaheshimu ili kuweka amani katika Vijiji ambavyo tayari vipo katika maeneo yetu. Vipo Vijiji vya Mbaga *line* vile vyote ni Vijiji halali, vipo Vijiji vya Kata ya Kashishi, Seledi na Sasi vyote ni vijiji halali kutokana na maamuzi ambayo tulipewa na Mheshimiwa Zakhia Meghji alipokuwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Sasa kila Waziri akija na maamuzi yake, haiteti utengefu katika maeneo ya wananchi wanayoishi. Wananchi wanaishi kwa hofu kwamba hatujui Waziri atakayekuja atakuwa na maamuzi gani. Huwezi ukaendesha nchi kwa misingi hiyo! Kwa hiyo, naomba sana Waziri maamuzi ya Mawaziri wenzako hawa, yawekee utaratibu wa kuyaheshimu ili wananchi hawa waweze kuishi kwa amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile suala la *WMA*, Mheshimiwa Waziri ameziorodhesha hapa zipo kama tano ama sita hivi. *WMA* ya eneo langu ambayo inaitwa Isawima siioni. Sasa sijui kama ameisahau au vipi! Nadhani amesahau kwa sababu, sisi vile vijiji ambavyo vimezunguka pale vimejitahidi kujiunda kwa nguvu zake vyenyewe hamjawapa msaada. Leo imeshaundwa, bado tuna mgogoro, hatupati msaada wowote kutoka Serikalini. Tufanyeje ili Isawima na yenyewe iweze kuingizwa katika utaratibu wa kupata misaada kama jinsi ambavyo mmezungumza katika maeneo mengine?

Mheshimiwa Spika, tumesikia habari za Wakala wa Misitu. Wakala wa Misitu mimi namsikia kwingine tu, lakini katika Mkoa wa Tabora eneo langu ndiyo lina karibuni asilimia 70 mpaka 80 ya misitu ya hifadhi. Hao Mawakala wanazunguka wapi? Matokeo yake mnatuachia sisi tunahangaika na Halmashauri zetu tu na Halmashauri hazina rasilimali za kutosha. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba kule

sasa katika misitu hii kuna mgogoro mkubwa kati ya wakulima na wafugaji, kati ya wafugaji na wananchi warina asali.

Wale wafugaji kwa sababu hawakwenda pale, na wakati mwingine wanahisi wananyanyasika, kwa hiyo, wanajitengenezea utaratibu wa kujilinda wenyewe. Matokeo yake wanaathiri hata shughuli za warina asali. Naomba Waziri unisaidie kuliangalia sawasawa, pamoja na kutambua kuwepo kwa Isawima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulinzi naona umejikita sana katika ujangili, lakini ulinzi wa hifadhi ya misitu bado ni mdogo sana. Matokeo yake mnatuachia sisi na Halmashauri zetu ndiyo tunahangaika kule, na rasilimali hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, nilizungumza mwaka jana mwezi Machi, 2011, tulipeleka baadhi ya viongozi pale kwenda kutoa tangazo kwamba huu msitu mliokaa hapa wafugaji ni eneo la hifadhi ya msitu, mnaombwa kuondoka, na wakavamiwa wakauawa. Nikasema, Mheshimiwa Waziri kama mnaweza mkalipa fidia kwa sababu watu wanauawa na wanyamapori, hawa ni watu ambao wameuawa kutokana na kufanya kazi ambazo mlikuwa mnapaswa kuzifanya ninyi; hivi hamwalipi hata fidia au kifuta machozi? Mtu akiliwa na chui, au akiliwa na simba mnamlipa angalau Shilingi milioni moja; hawa wameuawa wakati wakifanya kazi ambayo mmekosa kuzifanya ninyi kutokana na walinzi wenu kutokutosha, na niliwataja hapa akiwemo Ndugu Yasini Nkwabi, Ndugu Makenzi Mlangira, Ndugu Ali Mwangira na Ndugu Emmanuel Gabriel. Wote hawa, mmoja akiwa ni Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, Mmoja ni Mtendaji wa Kijiji (VEO) na hawa wawili wakiwa ni mgambo. Mpaka leo sijapata jibu!

Mheshimiwa Spika, nimesoma majibu ya Mheshimiwa Waziri katika hotuba iliyopita sijaona majibu yoyote kuhusu wananchi hao. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri hawa watu familia zao zinahangaika sana, mnipe kifuta machozi tuweze kuwapelekea kama jinsi mnavyofanya kwa watu wanaoliwa na wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachonishangaza zaidi ni kwamba, wakati mimi nazungumza habari za watu walioaawa na leo nitakukabidhi hata picha za maiti hizi; lakini wapo wazushi ambao huwa wakizua mambo katika Bunge hili. Mwaka 2011 walizua kwamba Mkuu wa Mkoa Tabora amesimamia uvamizi wa watu waliopo katika misitu ya hifadhi na watu karibuni 26 wameuawa. Mkaunda Tume kwenda kupeleleza uwongo huu, matokeo yake mkakuta hakuna ushahidi na hakuna hatua zilizochukuliwa juu ya mtu mwongo kama huyu. Ndiyo maana Mheshimiwa Nchimbi amesema, afadhali ya mchawi kuliko mwongo. Serikali imetumia hela nyingi kwenda kufuatilia kitu ambacho hakipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 vilevile ikatokea uzushi mwingine hapa, kwamba kule Shela mahindi yamechomwa, mama mmoja kauawa na mtoto alikuwa anacheza na maiti ya mama yake, ananyonya matiti ya mama aliyekufa, mkaunda Tume ya Maliasili ikaenda kule, uwongo mtupu! Sasa mimi naleta ushahidi hapa, hata *attention* hatupati!

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nasikitika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu mambo ya kale. Kulikuwa kuna mradi unaohusu mambo ya *Slave Route*, njia ambayo walikuwa wakipita watumwa, kwamba walikuwa wanataka kujenga kituo. Pale kwetu kuna kituo pale Usinde, kuna kituo Ulyankhulu nadhani haya nayo mngeyazingatia.

Mheshimiwa Spika, mwisho zaidi ni kwamba ndani ya Bunge tunajitahidi sana kujenga mazingira ambayo wananchi wetu wataingia katika maisha bora. Maisha bora hatuwezi kuingia kama hatujazingatia kilimo au biashara. Sasa inapotokea kwamba tenda zinapotangazwa, wananchi wanapoomba na wakapata tenda hizo, Bunge linasimama hapa kuwalaani wananchi hao, tunawakatisha tamaa kabisa. *(Makofi)*

Kwa mfano, imezungumzwa hapa kwamba kuna wananchi ambao wamepata vitalu, hawa ni watu ambao

wanapaswa kulaaniwa wakati humu humu Bungeni tumezungumza kwamba vitalu mara nyingi walikuwa wakipewa watu wa nje...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Muda umekwisha. Sasa namwita Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Antony Gervas Mbassa.

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya tatu ya kuzungumza kuhusu suala zima la Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, ningependa kutoa salamu za pole kwa jamaa na marafiki wa Marehemu Sheikh wa Wilaya ya Lindi Said Mussa Mbala. Imebidi niombe radhi niseme hayo, kwa kweli nampa pole sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende kwenye masuala ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, suala la maliasili na utalii katika nchi mbalimbali kwa kweli inachukua nafasi kubwa sana kuendeleza jamii na kuendeleza nchi. Kwa mfano, nchi ya Namibia, Swaziland, Afrika ya Kusini na Kenya wanaendeleza uchumi wao kwa kupitia utalii. Ningeomba sana Wizara kwanza ichambue ione vipengele vyake vyote, kama ni kuongeza Mawaziri waongezwe, badala ya wawili wawe watatu; awepo Waziri mwenyewe, Manaibu Mawaziri wawili kwa sababu ina mambo mengi sana kiasi mengine hayafanyiwi kazi.

Mheshimiwa Spika, pili, mimi nimeamua hapa kuja kuitangaza Lindi katika utalii kwa sababu nimeona kuna mambo mengi ya utalii Lindi lakini hayafanyiwi kazi. Ningeomba Wizara basi, iende Kusini Lindi, Mtwara na Ruvuma ichambuliwe kwa umakini kabisa, viangaliwe

vipengele mbalimbali ambavyo vingeweza kuendeleza utalii Kusini.

Mheshimiwa Spika, kuna utalii unaoitwa *Cultural Tourism*, au utalii wa kiutamaduni. Nimeangalia katika kitabu hiki, nimeona umesemwa kidogo sana, lakini kuna utalii mkubwa kabisa Kusini wa *cultural tourism*; utalii wa mambo, utalii wa vitu, utalii wa jamii na utalii wa vitu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ukichukua Lindi peke yake, nimeamua nisimame hapa niviseme vitu hivyo ili jamii isikie, Umma usikie ili waje Kusini waangalie utalii wa Kusini ni upi ili tuweze kupata uchumi wa kuendeleza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, watu wanasema kwamba mtu asipokusikia ukisema wakati umesimama, basi panda hata juu ya meza useme watu wakusikie. Kwa hiyo, mimi nimepanda juu ya meza kuutangaza utalii Kusini badala ya kufanya malumbano ndani ya Bunge. Nawaomba sana wenzangu wanaofanya malumbano ndani ya Bunge, hakuna tija yoyote. Wewe omba msaada, omba maendeleo katika Jimbo lako.

Mheshimiwa Spika, ninaanza kuitangaza Lindi sasa na nimesimama hapa juu ya meza sasa, sijasimama kawaida, nimesimama juu ya meza; kwanza, fanyeni utafiti Lindi, kuna mambo zaidi ya 21 ambayo yataleta tija. Kuna maboko 3,000 wanaosema na binadamu; mmewaona hao? Sikuona popote katika eneo hili. Maboko, yaani wanyama 3,000 ndani ya Mto Nyange, kwa Mzee Mambo, yale maboko yanasema na binadamu. Huu ni utalii wa vitu mbalimbali. Mmewiangalia hivyo? Bado! Hilo ni moja.

Mheshimiwa Spika, pili, kuna Mji Mkongwe unaitwa Mji Mkongwe wa Kilwa. Nimeona sehemu ndogo sana katika kitabu hiki cha Waziri wa Utalii leo. Mji huu Mkongwe wa Kilwa ni Mji wa zamani kwa miaka ya nyuma kabisa AD. Mji ule ni kati ya Miji mitano iliyopo Afrika Mashariki ambayo ni Lamu-Kenya, Mombasa -Kenya, Mogadishu-Somalia, Sofala - Msumbiji, Kilwa - Lindi. Mji huu wa Kilwa unaendelezwaje?

Kwa sababu *UNESCO* walisema kwamba watatoa pesa katika Miji hii mikongwe kwa ajili ya kuendeleza Miji. Je, fedha hizi zimetolewa? Kama zimetolewa, zimefanya nini? Kama hazikutolewa, zimefuatiliwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waziri katika majumuisho yake atuelezee kati ya Miji mikongwe hii mitano, Mji wa Lindi umeendelezwaje katika sifa yake ya kuwa Mji Mkongwe.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, mimi nikitaja suala la mjusi watu wanacheka. Sasa hivi nimebaki na jina tu, mjusi. Mama Mjusi, Mama Mjusi. Wengine wadiriki kusema kwamba mijusi nenda kule wanakojenga nyumba ya Waziri Mkuu utaikuta milimani imajaa. Siyo hivyo! Huyu mjusi ni wa pekee, ni wa Tanzania, amechukuliwa, yupo Ujerumani. Ni mkubwa analindwa na watu 373 na anaongeza utalii Ujerumani badala ya kuongeza utalii Lindi au Tanzania. Sisi Watanzania tunafaidika nini na mjusi yule? Hivi kweli Serikali haifahamu suala hili?

Mheshimiwa Spika, tunataka Serikali ituambie, katika kitabu hiki sikuona popote ambapo imeelezea masuala ya *dinosaur*, mnyama wa zamani aliyeweza kuishi duniani. Wanyama hao waliishi nchi tatu; aliishi Marekani, Afrika Kusini na Tanzania na hawa wote watatu mabaki yao yapo kule Ujerumani. Ukienda Ujerumani mbele kabisa unamkuta *dinosaur*. Wale waliokwenda Ujerumani nafikiri wamemwona. Mjusi yule ni mkubwa, anaongeza utalii kule Ujerumani. Sisi Tanzania tunafaidika nini?

Mheshimiwa Spika, tunaomba leo tuelezwe Watanzania tunafaidika nini au tutafaidika na nini au Ujerumani wana mpango gani wa kutusaidia sisi Watanzania kumtengeneza mjusi mwingine Tanzania? Kwa sababu tumeambiwa kwamba kuna mijusi mingine ipo pale Lindi, mingi sana: Je, tumewaomba Ujerumani waje wafanye utafiti na wao waweze kuendeleza suala zima hili? Kwa sababu ni kitu ambacho kinaleta uvumi nchi nyingine badala ya kuleta uvumi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nikiacha suala la mjusi, (wengine wanasema mjusi hawajui maana yake, ni *dinosaur*) kuna suala lingine la kumbukumbu ya Vita vya Maji Maji. Vita hivi vilianza Lindi vikaenda Ruvuma, Songea vikaishia kule. Pale Lindi - Kilwa kuna wajukuu wa Mzee Kinjekitile, Kilwa kuna familia ya Mzee Kinjekitile, sasa badala ya kuliendeleza eneo hili la Kilwa Kinjekitile sherehe zote zinakwenda wapi? Ruvuma Songea. Hatukatai, ni jirani zetu! Lakini ni kwanini tusiunganishe na Lindi? Kwa sababu vita vilianza Lindi vikaishia Ruvuma, Songea.

Tunaomba kabisa maeneo haya mawili yote yaweze kuendelezwa badala ya kuendeleza Ruvuma peke yake. Sherehe zinapofanywa, basi zifanywe kwa zamu. Mwaka mwingine wafanye Ruvuma na mwaka mwingine wafanye Lindi. Lindi vile vile paendelezwe!

Mheshimiwa Spika, hapana dalili yoyote ya kuendeleza pale Kinjekitile. Huu ni utalii wa vitu mbalimbali. Sasa hivi watu wamechoka kuona Mlima Kilimanjaro, Mlima Meru; waje Kusini waone mambo vile vile! Hatukatazwi kwenda kule, lakini na huku kuna vitu ambavyo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, nafikiri hata Mheshimiwa Telele atafikiwa.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja iliyopo hapa mbele yetu. Lakini nianze tu kwa kuunga mkono Kambi ya Upinzani kwa maoni iliyowasilisha.

Mheshimiwa Spika, kama kweli imetajwa na imeeleweka kabisa kampuni ile iliyosafirisha huu mzigo na Wakurugenzi wake wametajwa na aliyesaini nyaraka bado ni Meneja wa Fedha na Utawala, mimi nafikiri Serikali itupe kauli kuhusiana na suala hilo ni jinsi gani itakavyoweza kulitokomeza.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kujikita zaidi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala zima la migogoro. Katika hotuba iliyosomwa, suala zima la mipaka kati ya vijiji, hifadhi na mapori tengefu ni tatizo kubwa sana.

Naomba niende kwanza kwenye hoja ya Kamati ukurasa wa 21, nitasoma kipengele kidogo tu kuhusiana na migogoro hii. Tatizo la mipaka limeendelea kuwa changamoto katika sekta ya maliasili na migogoro hii ya mipaka inachangiwa na wananchi ama kwa kutokujua mipaka ya maeneo yao au kutumiwa na wanasiasa ili kuendelea kuyatumia maeneo hayo ilhali mipaka hii haijulikani.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kwanza nitofautiane na hii hoja, lakini nikubaliane na pendekezo walilotoa kwamba sasa Wizara hii kwa sababu suala hili ni suala mtambuka wakae chini na walifanyie kazi haraka sana.

Mheshimiwa Spika, suala la migogoro kati ya vijiji vinavyopakana na hifadhi limekuwa suala sugu sana. Leo hii hatujui na tunaomba Serikali itupe majibu na Waziri atueleze, wakati vijiji hivi vinatengwa, wakati vijiji hivi vinasajiliwa, vijiji hivi vinapata hatimiliki, haya masuala ya hifadhi yalikuwa katika mazingira gani? Mipaka hii ipi ilianza? Vijiji au hifadhi?

Mheshimiwa Spika, ni juzi tu hapa wakati likijibiwa swali ulitolewa mfano wa Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi. Katika Kata ya Kaniha, Kijiji cha Kaniha, Kijiji cha Mpago, leo hii wananchi wale wanaambiwa kwamba wanaishi ndani ya Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, kidogo haiji akilini kuona wananchi hawa sasa hivi wanaanza kufurushwa, wanaambiwa wasilime, wanaambiwa waondoke kwamba wako ndani ya Hifadhi, wakati Kijiji hiki kimesajiliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, namba ya usajili wa Kijiji hiki ninayo. Kijiji hiki kimesajiliwa kwa Namba *KGR/KIJ/695* na Kijiji cha Mpago kimesajiliwa kwa Namba ya usajili *KGR/KIJ/695*.

Mheshimiwa Spika, hii inasikitisha sana! Leo hii wananchi hawa wamefurushwa, wamefukuzwa, wananchi hawa wanaambiwa wasilime, mifugo yao imeondolewa kwamba wako ndani ya Hifadhi. Hivi hii mipaka ya Hifadhi imeanza lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama kweli, Wizara ipo, wananchi wameishi miaka yote nenda-rudi, umri huo wana wajukuu na vitukuu, leo hii ndiyo wanaambiwa wako ndani ya Hifadhi! Ni nani mwenye mamlaka ya kuonesha hiyo mipaka? Na wananchi iweje kwamba, waishi kwenye eneo ambalo hawalijui?

Mheshimiwa Spika, hapa kuna walakini mkubwa sana. Naomba Wizara irudi katika mipango yake. Najua Serikali ni moja, labda kama kuna Serikali mbili. Serikali iliyokuwa inatenga Vijiji na Serikali iliyokuwa inatenga mipaka ya Hifadhi. Hapo labda tutapata jibu sahihi. Kwamba, hawa walikuwa na *document* tofauti na hawa nao walikuwa na *document* tofauti. Lakini kama Serikali ni ileile moja, Watendaji wapo wa sehemu zote mbili, tafadhali migogoro isiyo ya lazima kwa wananchi tunaomba iepukwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii watu wanakosa imani na Serikali. Leo hii miaka yote nenda-rudi, wanaambiwa wananchi hawa wako ndani ya Hifadhi! Cha kusikitisha ni kwamba, Serikali imetengeneza miundombinu mizuri, barabara ipo, uongozi upo, shule imejengwa katika Kijiji cha Mpago na mwaka huu Darasa la Saba wanahitimu. Leo hii wanaambiwa kwamba wanaishi ndani ya Hifadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012 mwezi wa Kumi na Moja, zoezi hili liliendelea la kusafisha maeneo ya hifadhi au kufanya *operation* maalum, *Operation* Okoa Mazingira, ambayo ilikuwa chini ya Serikali ya Mkoa. Watu hawa wanajua kabisa mipaka jinsi ilivyo, lakini watu hawa wamekuwa ndiyo wa kwanza kubahudhi hawa wananchi. Mimi nimekwenda kutembelea kule, nimekuta wazee wanalia. Wazee wanasema sasa tumekuwa watu wa kupokea matatizo kila mara. Mifugo yao imepelekwa,

nyumba zao zimechomwa, wanaambiwa wako ndani ya Hifadhi. Miaka yote hiyo Serikali ilikuwa wapi kuwaangalia hawa wananchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga maeneo hayo miaka mingapi? Kama walikuwa ndani ya Hifadhi, ilikuwaje? Kwa nini wananchi hawa wasiondolewe wakaoneshwa eneo mbadala sehemu la kuishi?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya amewaambia hapa, leo hii sensa ya wananchi wa Tanzania imeongezeka. Kila siku tunapanga tupime maeneo ya Mijini, Vijijini hatujawahi kupata mtetezi wa kupima yale maeneo; hivi vijijini hawaongezeki? Hawa wananchi wanaoongezeka vijijini, wanaishi wapi? Hawa wananchi tunaowahimiza wafuge vijijini, watafugia wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ije na jibu. Wakati Mheshimiwa Waziri anakuja ku-*wind up*, anipe maelezo ya kina kuhusu wananchi wangu wa Kata ya Kaniha, Kijiji cha Mpago, tuelewe ni nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu doria zinazofanyika. Doria zinazofanyika sasa hivi zimekuwa doria tofauti kabisa na tunazozielewa za Askari Wanyamapori. Kwa watu ambao tunaishi karibu na maeneo ya hifadhi, doria hizi zimekuwa ni doria za kufukuza mifugo kutoka ndani ya Vijiji kupeleka ndani ya Hifadhi ili wapate pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wamekuja wafugaji hapa mara nyingi wanalalamika na juzi walikwenda kwa Mheshimiwa waziri Mkuu.

Mara nyingine wameshawahi kufika hapa, kilio chao ni suala la jinsi wanavyonyanyaswa, lakini inaonekana kauli yao inapoletwa hapa hakuna anayeisikiliza; hakuna kinachoendelea! Mheshimiwa Balozi Suedi Kagasheki, alifika Jimboni kwangu tukakaa naye kikao ndani ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, tukaeleza hali halisi ya matatizo ya wafugaji wanavyonyanyaswa na Askari Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, tumekwenda kwenye Mkutano wa Hadhara, akapewa na risiti za tozo zisizokuwa halali zinazofanyika kule ndani ya Hifadhi. Taarifa imekuwepo ya ng'ombe waliopigwa risasi na Askari Wanyamapori ndani ya Hifadhi, lakini hakuna sehemu yoyote inapoonekana ni hatua gani Serikali imechukua dhidi ya watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana. Leo hii hawa wananchi tunawapeleka wapi? Hawa wananchi wanaonyanyasika tunawaweka katika kundi lipi? Hawana mtetezi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba tupate jibu, wananchi wa Biharamulo, maeneo ya kufugia, maeneo ya Hifadhi, kama Serikali inaweza ikaja ikaonesha mipaka iliyopo, wananchi waache kusumbuliwa. Leo hii mtu inaonekana kufuga inakuwa tatizo, kwa sababu ya watu wa Hifadhi. Badala ya kwenda kufanya kazi ndani ya Hifadhi kama inavyoelekezwa kwa mujibu wa Sheria na taratibu zao, wao wanaingia kwenye biashara nyingine.

Mheshimiwa Spika, watumishi hawa ambao sio waaminifu, tunaomba Serikali, iwaangalie. Tunaomba Serikali, iliangalie hili.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la fidia kati ya watu wanaoishi kwenye mipaka ya maeneo ya Hifadhi. Suala hili nimeliuliza mara nyingi, lakini hakuna jibu lolote linalopatikana. Inaonekana Serikali imetenga fedha, Serikali imetenga Waraka, lakini hakuna kinachoundelea. Matokeo yake, ndiyo maana inafika mahali wanakata tama, kama wanavyoelekea kukata tamaa hawa wafugaji ambao sasa na wao sijui wataelekea wapi! Hili nitaliongelea huko mbele. Lakini naomba tafadhali, Serikali ilete Waraka na sisi Wabunge tupewe tuone hizo nyaraka zinasemaje juu ya fidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii mwananchi ikionekana kamdhuru hata tumbili tu, Sheria inachukuliwa. Yeye akidhuriwa na huyo ngedere, basi ni kitu cha kawaida. Tunakwenda wapi? Wanajitahidi kulima kwa jembe lao la

mkono, mazao yao yakiharibiwa, basi. Fidia hakuna! Hawa waishije? Maisha yao yaweje?

Mheshimiwa Spika, tunaomba tupate ufafanuzi wa kina juu ya suala hili. Suala hili, niiombe kabisa Wizara inayohusika, najua ni Wizara mtambuka, ikae chini na watu wa Ardhi na Makazi, waje wapime waangalie maeneo haya, warudi kwenye taarifa zao, ili kusudi wananchi wote hawa waweze kuishi kwa amani. Wanayo haki ya kuishi ndani ya nchi yao vizuri na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa. Sasa nimwite msemaji wa mwisho asubuhi hii, Mheshimiwa Kaika Telele.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara ya Maliasili na Utalii. Namwomba sana Mwenyezi Mungu aniongoze, anisaidie nizungumze kwa utaratibu bila jazba, lakini ujumbe ufike kunakohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba suala la Loliondo limechukua muda mrefu, miaka 20. Lakini bado naamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi haijashindwa kutatua mgogoro huu. Lakini ikishadumu pia kwa miaka 20 inatia mashaka, lakini nashukuru pia hatua ambayo amechukua Mheshimiwa Waziri kutenga zile Kilometa 1,500 ambazo kwa kweli imelalamikiwa na wananchi na hata mimi mwenyewe nalalamikia, lakini kwa maana hii, Mheshimiwa Waziri maana yake ni kwamba, alitaka jambo hili sasa lifikie mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Jeshini, Kamanda wa Jeshi ni lazima afanye maamuzi. Hata kama uamuzi huo utakuwa umekosewa, yule ambaye anaitwa 2/C anaweza akachukua nafasi ya Kamanda aliyekuwepo. Lakini jambo hili mimi nashukuru kwamba sasa ni kama moto umewashwa na kwa hiyo, jambo hili sasa litaangaliwa upya na litafikia mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitambue juhudi ambazo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya katika kujaribu kumaliza mgogoro huu. Tume mbalimbali zimekwenda huko, tumejaribu kufikiria kama *WMA* inaweza ikawa ni *alternative* katika jambo hili. Tumefanya mikutano kadhaa ya wadau na wawekezaji na wananchi katika jambo hili, lakini hadi sasa haya mambo hayajazaa matunda.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe mwaka 2009 nilikuja na Hoja Binafsi, lakini wakati tunaandaa hiyo hoja, nikashauriwa na Wanasiasa na Wanasheria kwamba, badala ya kuwa Hoja Binafsi iwe ni Maelezo Binafsi. Sijaelewa tofauti kati ya Hoja Binafsi na Maelezo Binafsi mpaka leo, lakini imefika kwenye *Caucus* ya Chama chetu na Waziri Mkuu, nakumbuka wakati ule aliniahidi kwamba, kwa sababu mgogoro huu unagusa sekta mbalimbali, unagusa mifugo, unagusa maji, unagusa kila kitu na ile *operation* iliyofanyika kule Wizara mbalimbali zilikusika, kwa hiyo, akaniambia kwamba nitawatuma Mawaziri watano waende Loliondo wakaangalie mgogoro huu; Waziri wa Ardhi, Waziri wa Maliasili, Waziri wa Mambo ya Ndani na Mawaziri wengine, lakini bahati mbaya Waziri pekee aliyekuwa ni aliyekuwa Waziri wa Ardhi. Sasa na yeye amekuja amejaribu kuzungumza na wale watu, lakini hili jambo bado halijapata msukumo.

Mheshimiwa Spika, kwanza niwashukuru pia Wabunge wenzangu wote walionipa pole katika suala la Loliondo, lakini wakanipa pia pole kwa sababu, kulikuwa na kauli ya kwamba, Viongozi wa kule wote tujiuzulu. Lakini hajiuzulu mtu katika jambo hili. Kwa sababu, tukijiuzulu, hawa watakuwa kama kondoo wasiokuwa na mchungaji na *after all* ningejiuzulu mimi Mbunge, ni nani angewasemea katika Bunge hili kama ninavyosema sasa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini wanasema Waswahili kwamba, baada ya Mwenyezi Mungu ni Serikali. Serikali, iliyopo madarakani ni ya Chama cha Mapinduzi. Sasa Chama cha Mapinduzi ambacho ndicho kimeunda Serikali hii, naomba kabisa kwa unyenyekevu sana iweze kumaliza sasa tatizo hili la mgogoro huu wa Loliondo. Sina mashaka kwa

sababu wakati ule tulilifikisha kwenye *Caucus* ya Chama kwa Waziri Mkuu, akiwa Mwenyekiti wetu, lakini sasa limerejea tena suala hili. Wananchi wa Ngorongoro, Viongozi wa Ngorongoro, walikuja wakamwona Waziri Mkuu hapa Dodoma na bahati nzuri wamemwelewa na yeye amewaelewa, amewapa matumaini makubwa na hivi sasa Loliondo kule kumetulia, wanasubiri Kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, jambo hili sasa na wewe ulitolee tamko, kwa sababu Mheshimiwa Kagasheki na yeye amesema kikombe hiki ikiwezekana kimwepuke, basi kimetua kwa Waziri Mkuu, ambaye ndiye Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali, Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka kupendekeza kwamba, kwa sababu katika jambo hili la Loliondo, Bunge hili halijawahi kuunda Tume Maalum ya Bunge ya kushughulikia jambo hili, nafikiri kwamba, pengine kama mambo yote haya yatashindikana, basi iundwe Kamati Maalum, Tume Maalum ya Bunge na ilete Taarifa baadaye katika Bunge hili, kuhusu mgogoro wa Loliondo.

Mheshimiwa Spika, lakini matatizo ya Tume hizi zinaweza kuanza kuchukua muda mrefu, zinatimia *resources*, lakini wananchi wangu sasa hivi wanakusanyika, wanasikiliza ni nini kinaendelea katika Bunge hili na kwa hiyo, mimi nitaiachia Serikali, kama nilivyosema mwanzo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi bado haijashindwa kumaliza mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumze jambo lingine la watu wa Ngorongoro. Watu wa Ngorongoro kwa muda mrefu nao wamekuwa na matatizo. Kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukitusaidia kugawa haya Majimbo, itatusaidia sana kwa sababu, ninavyohangaika Ngorongoro ni dunia nyingine na Loliondo kule ni dunia nyingine na sehemu zote mbili zina tofauti, zina matatizo ya aina tofauti. Sasa Napata shida kweli, kama Mbunge.

Mheshimiwa Spika, lakini nizingumzie Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na majukumu yake makuu matatu; Uhifadhi, Utalii pamoja na Kuendeleza Wenyeji, Wamasai, kwa mujibu wa Sheria walioko eneo lile.

Naomba rasilimali fedha inayopatikana katika Shirika la Mamlaka, kama haiwezekani kuigawa sawa kwa sawa kulingana na haya majukumu, basi angalau igawanywe kulingana na asilimia kwa jinsi ya umuhimu wa majukumu yote matatu kati ya Uhifadhi, Kuendeleza Utalii na Kuendeleza Wenyeji.

Mheshimiwa Spika, lakini nashukuru kwamba mwaka huu kidogo katika suala la chakula kwa sababu, Wizara ilikuwa imepiga marufuku kilimo cha bustani, ingawa tunaendelea kuomba kwa sababu chakula cha kulishwa nacho kina matatizo yake, kinaweza kisije kwa wakati; lakini nashukuru kwamba Mamlaka ya Chakula wametenga Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya chakula safari hii na Baraza la Wafugaji wametenga Shilingi milioni 700.

Ninachoomba tu ni kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaomba kibali tupate kuchukua hicho chakula kutoka maghala ya Serikali, yaliyoko Mjini Arusha kwa maana ya *SGR*.

Mheshimiwa Spika, naomba mimi nihitimishe kwa kuomba kwamba, ni aibu sana kwa eneo la Ngorongoro ambalo ni eneo la Urithi wa Ulimwengu, bado limepata heshima juzi juzi hapa ya kuwa ni *Natural Wonder of The World*, bado ni *Man and Biosphere, International Man and Biosphere Reserve*, yaani ni eneo la Kiulimwengu, dunia nzima inalitizama.

Sasa Serikali yetu ilitizame pia eneo hili kwa macho ya huruma sana. Ni aibu watu wa pale kuendelea kuwa na

30 APRILI, 2013

njaa wakati mapesa mengi yanaingia pale, lakini mgawanyo wa rasilimali hizo hauendi sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe waliosaidia kwenda huko, namshukuru kwanza Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, ameunda Tume ya Waheshimiwa Wabunge wa Halmashauri Kuu ya Chama chetu ambao wamekwenda huko Loliondo, wameangalia hali halisi, wamewasiliza wananchi, wamepeleka taarifa kwenye Chama na Chama ambacho ndicho kina Serikali hii, kinafanyia jambo hilo utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu hao ni kweli kwamba, waliongozwa na Mheshimiwa Mchemba, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Ndugu yangu Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana, nashukuru. Sasa jioni nitawaita wafuatao: Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Missanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Grace Kiwelu. Wengine watatajwa wakati utakapofika.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kusitisha shughuli za Bunge, mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.55 mchana, Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 jioni)

30 APRILI, 2013

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, habari za jioni.

WABUNGE FULANI: Nzuri.

MWENYEKITI: Tunaendelea na ratiba ya kikao chetu kwa jioni ya leo, majadiliano yanaendelea na kwa mujibu wa Mwongozo wa Mheshimiwa Spika alipokuwa anasitisha shughuli hizi alisema mchangiaji wetu wa kwanza jioni hii atakuwa Mheshimiwa Anastazia Wambura atafutiwa na Mheshimiwa Brigedia Hassan Ngwilizi, naona hawapo, namwita Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali.

MHE. MBAROUK SALIM ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Maliasili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk, hapa taarifa zangu zinaniambia una dakika tano tu.

MHE. MBAROUK SALIM ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama changu cha CUF kinaamini kwamba sekta ya Maliasili ni sekta muhimu sana kimazingira, kiuchumi na kijamii na kwa kweli ingekuwa inasimamiwa sawasawa basi ni uhakika kwamba Tanzania ingeokoka au ingetoka katika mashimo ya umaskini kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Serikali ya CCM wamefanya wachofanya lakini wamefika mahali wamekwama na tunategemea kwamba sisi Wapinzani tuwashauri vilivyo ili waweze kurekebisha vile ambavyo tunahisi ni makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha ni kwamba tulitegemea hotuba zetu za Upinzani zitatoa maelekezo mazuri na ushauri mzuri kwa Serikali iliyopo ili tuweze kwenda

30 APRILI, 2013

vizuri na kuokoa maisha ya jamii na Watanzania kwa ujumla lakini siyo hivyo. Kwa sababu hiyo, nathubutu kusema kwamba kama kitabu kitakatifu cha Quran kilivyosema kwamba *lakumd hukum waliadin*, kwamba CHADEMA na upinzani wao na sisi CUF na upinzani wetu. Naomba Watanzania waelewe kwamba CHADEMA ni kama CHADEMA na CUF ni kama CUF na upinzani wao, kwa hiyo wajue jinsi ya kutuhukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende moja kwa moja kwenye mada. Ujangili na uharibifu wa misitu kwa kweli umekithiri kama hotuba ya Kamati ya Maliasili ilivyosema na kwa kweli kama hapakutafutwa mifumo mizuri ya kuzuia ujangili huu na kusimamia rasilimali zetu hizi, tunaweza tukafika mahali tukawa hatuna tena rasilimali za maliasili. Hii inachangiwa na mambo mengi. Moja, ni ukosefu wa wafanyakazi. Kuna wafanyakazi ambao kwa kweli ni wazee, ukienda kwenye maliasili za misitu utakuta walinzi walioko pale wengi ni wazee na wengi wameshafariki lakini hakuna *replacement* yoyote ambayo inafanyika. Hili ni tatizo, huwezi ukamkuta mlinzi mmoja analinda zaidi ya hekta thelathini, kwa kweli hapo hapana ulinzi wowote unaofanyika isipokuwa ni ubabaishaji tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine wenzetu majangili wanatumia silaha za moto, silaha za kisasa lakini walinzi wetu wanakuwa na silaha za kienyeji, angalau kwa hifadhi za mbuga za wanyama unaweza ukakuta wana magobore lakini pia hayawezi kupambana na majangili. Ukienda kwa upande wa misitu, unaweza ukakuta mtu ana bakora, kwa kweli sidhani kama unaweza ukapambana na jangili ambaye ana silaha ya moto kwa bakora. Kwa hiyo hilo nafikiri Serikali wangeliangalia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine labda nizungumzie kwenye Sera ya Misitu. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake alisema kwamba wanajipanga mwaka huu wa fedha kufanya mapitio ya Sera ya Misitu na Nyuki. Ninavyokumbuka Sera hizi ni za mwaka 1998 na hii Sera ya Misitu ilifanyiwa

30 APRILI, 2013

mapitio mwaka 2008 na wadau wakatoa maoni yao na michango yao lakini la kusikitisha ni kwamba hakikueleweka kilichoendelea na mpaka sasa hivi ni kimya leo hii ndiyo namsikia Waziri akisema kwamba kuna mchakato mwingine unataka kuanza wa kufanya mapitio ya Sera hiyo. Kwa hiyo, labda atakapokuja Mheshimiwa Waziri kuhitimisha hoja yake atuambie huu mchakato uko vipi.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Tayari Mheshimiwa dakika zako tano zimeisha, nakushukuru sana Mheshimiwa.

MHE. MBAROUK SALIM ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa nitamwita Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, wamegawana dakika tano tano na Mheshimiwa Salim, kwa hiyo sasa atafuatia Mheshimiwa Kuruthum na Mheshimiwa Maria Hewa ajiandae.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nitakwenda moja kwa moja katika ukurasa wa 11 wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri, kipengele cha tano, hapa amezungumzia juu ya ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi wa wanyamapori. Hapa ameongelea kuhusu *WMA* ambazo zipo katika mchakato wa kukamilika. Sisi kwetu Rufiji kuna hii *WMA* ameitaja hapa Juhiwangumwa. *WMA* hii imeanza tangu mwaka 2006, Mheshimiwa Waziri kama kweli tunataka kuwashirikisha wananchi wanaokaa kandokando ya Pori la Akiba ya Selou ambalo lipo katika kijiji cha Mloka, Nyaminywili, Mtanzamsona na kwingine, tunaomba sana hii *WMA* yetu ikamilike kwa sababu ni muda mrefu sasa tangu mwaka 2006 mpaka sasa 2013 kwenye taarifa inaonyesha yenyewe bado ipo katika mchakato. Tunasaidiaje hawa watu ili wasipate tamaa ya kuingia kwenye hifadhi?

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu kule sisi Rufiji kumekuwa na matatizo makubwa sana baina ya watumishi wa hifadhi na wananchi hususani wananchi ambao wanakaa kandokando ya Pori hili la Selou kule Rufiji. Watu wanapoteza maisha, nimelalamika hapa katika bajeti ya mwaka jana, vijana wanakufa sana. Vijana wanaingia kule kwenda kuvua samaki lakini watu wanapita pale na magari ambayo yana meno, vijana wanafahamu, majangili wanakwenda kule wanaua tembo, hata juzi kule Ngarambe kuna tembo karibu watatu wameuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watu wanafahamu kwamba watu wanakwenda wanaua ndovu na wanatoka na meno lakini wao wakienda kwenye mabwawa ambayo yapo karibu na kijiji na hii inatokana na tatizo la mpaka, sisi kule wakati lile pori linawekwa ule mpaka ilikuwa ni takribani kilomita tano kutoka kwenye kijiji lakini kila siku zinavyokwenda watu wa hifadhi wamekuwa wakijiongezea mpaka sasa hivi imekuwa mtu akitoka tu miguu miwili kijijini tayari anaambiwa ameingia kwenye hifadhi, anakamatwa, anapelekwa Morogoro. Vijana wengi wanapewa kesi za kubambikizwa lakini majangili wanaachwa. Historia inaonyesha wazi kwamba Pori la Selou lilikuwa na takribani tembo karibia 100,000 lakini sasa hivi Selou kuna tembo 30,000 tu lakini wanaokamatwa na kunyanyasika ni wananchi wetu wanyonge. Ukimkuta kaenda kwenye bwawa kavua samaki mmoja anapigwa risasi anakufa lakini watu wanaondoka na meno, tembo laki moja sasa wapo thelathini elfu tu wanafanya nini, lakini ndiyo hao wafanyabiashara wakubwa wenzetu ambao wanafahamika hawachukuliwi hatua, wanaonewa dagaa, papa wanaachwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtandao wa ujangili ni mkubwa sana inabidi nguvu za dharti ziongezwe kwa sababu watu wanaohusika tunaona wazi kesi zinapelekwa Mahakamani, kwa mfano Tunduru, kuna kesi ilipelekwa Mahakamani lakini Hakimu wa Wilaya kesi ile akaiacha. Ilikamatwa *Mark II* na meno kabisa ya uthibitisho lakini kesi ikaenda mtu akaachiwa. Sasa wale wananchi

30 APRILI, 2013

ambao wanazunguka yale mapori, mnawaambiaje washiriki katika kutunza zile hifadhi wakati wanaona watu wanachukua rasilimali, wanaondoka nazo, sasa nao wanashindwa kuwa na uvumilivu, kwa hiyo inabidi nao waingie kule lakini wakiingia kule wao wanapata matatizo, wanauawa, wanakwenda kubambikiwa kesi kubwa lakini watu ambao wanachukua zile rasilimali kubwa sana wanaachwa, wanaendelea kupeta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mgogoro huu wa Mloka, ilikuja Kamati ya Ulinzi na wale wananchi wakahaidiwa kwamba sasa patajengwa mabwawa lakini ahadi hii ya mabwawa mimi tangu nasimama katika Bunge hili kila siku naiongelea, mabwawa yatajengwa, kumi/kumi na moja, kumi na mbili mpaka leo hakuna hata bwawa moja. Walisema watajenga mabwawa mbadala ili sasa watu wafuge samaki kisasa, waache kuingia kwenye hifadhi lakini mpaka sasa hivi imekuwa ni hadithi, mabwawa hayapo. Naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie, ni lini sasa mabwawa yale yatajengwa ili wale wananchi waache tamaa ya kuingia kule kwenye hifadhi kwenye mabwawa ambayo wanakwenda kupata kitoweo tu cha samaki? Wajenge haya mabwawa ili na wao waweze kunufaika na rasilimali ambazo zinazozunguka pale kwao maana wanakula kwa kuona sasa hii inakuwa ngumu watu kuvumilia, hawawezi kuona samaki wako pale lakini watu wengine wapo ndani ya hifadhi wanavua na wanawauza, wanakaushwa na wanaondoka, watu wanawaona lakini wao hawaruhusiwi kuvua. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunakuomba, huu utaratibu wa mabwawa basi ufanyike ili watu waache kuingia kwenye hifadhi na wanusuru maisha yao na familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongee kidogo upande wa misitu. Kwetu sisi kule Pwani misitu kwa kweli inavunwa kwa kiasi kikubwa sana. Misitu inavunwa kwa ajili ya mkaa, mingine ndiyo hizo mbao. Serikali kule inakusanya maduhuli yote inarudisha asilimia tano lakini asilimia tano sasa inakidhi nini kwa sisi kule, ukiangalia tatizo ni kubwa sana

30 APRILI, 2013

katika Wilaya ya Mkuranga, Wilaya ya Rufiji, Wilaya ya Kisarawe misitu inaisha, sasa hivi kunakuwa jangwa. Kuna mkakati gani wa makusudi wa Serikali utakaoweza kurejesha ile hali ya uoto wa asili, hakuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu waliingia kule Rufiji wengine kwa hofu ya wafugaji, sisi hatukatai watu, tunapenda watu wote, kwa kuhofia wafugaji ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuruthum, dakika zako tano zimekatika, nakushukuru sana.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nilisema nitamwita Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Maria Hewa naona bado hajaingia ukumbini. Waheshimiwa Wabunge labda ningewataja Wabunge kama watano hivi ambao watachangia kusudi kama wako nje ya ukumbi wa Bunge wangerudi ndani ya ukumbi wa Bunge kuweza kunisaidia kuendeleza mpango wa uchangiaji kama walivyoomba.

Orodha yangu hapa inamhitaji Mheshimiwa Mama Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Salehe Pamba, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Betty E. Machangu na Mheshimiwa Ole Sendeka. Sasa kwa sababu hawa wengine siwaoni, ninaomba nimpe nafasi Mheshimiwa Betty Machangu atafuatiwa na Mheshimiwa Ole-Sendeka.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa nafasi niliyopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze moja kwa moja kwa kwenda katika Mkoa wa Arusha. Katika Mikoa

30 APRILI, 2013

inayolipa kodi kubwa ni Mkoa wa Dar es Salaam unafuatiwa na Mkoa wa Arusha, *I stand to be corrected* lakini nadhani ndiyo hivyo. Mkoa huu una wafanyabiashara wengi ambao wanafanya biashara ya utalii, *tour operators* na wafanyabiashara wengi wanalima maua na watalii wengi wanaokuja na *foreign institution* nyingi. Cha kusikitisha wafanyabiashara hawa hawana mtu wa kuwasemea lolote kwa Serikali yao kwa sababu Mbunge wao siku zote yuko kwenye vurugu, siku zote yuko kwenye maandamano, naomba niwaambie watu wa Arusha tafakarini tafadhali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye mada niliyokuwa nataka kuiwasilisha, niipongeze *TANAPA* na Wizara kwa ujumla, wanafanya vizuri, yapo mapungufu ndiyo lakini ukweli ni kwamba wanajitahidi. *TANAPA* mwaka 2007/2008 walikuwa wamepata shilingi bilioni 71.9 lakini kwa miaka mitano tu wamepata shilingi bilioni 118, wameongeza asilimia kama arobaini hivi, kwa hiyo ni pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato hayo ya *TANAPA*, hifadhi ya Kilimanjaro inachangia asilimia 38% ikifuatiwa na Serengeti 33%, ikifuatiwa na Manyara 11% na nyinginezo. Kwa hiyo, mtu wa kale alisema ukiona vinaelea vimeundwa, kuna mtu mahali anafanya kazi pamoja na *TANAPA* yenyewe na *KINAPA* lakini kuna Halmashauri za Wilaya tano zinazozunguka huu Mlima. Inapotokea ni moto, inapotokea ni matatizo, wananchi wa Wilaya hizi ndiyo wanaenda kufanya kazi kuhakikisha kwamba mlima unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlima Kilimanjaro ukiambiwa mapato yake hayatoki tu kwenye Mandara *Hut* na Kibo *Hut* na pale kwenye *Crater* hapana! Mapato haya yanatokana na kwamba mlima huu unatunzwa kuanzia huku chini, miti inapandwa kuanzia chini kwa ajili ya kuendelea ku-*attract* ukungu pale ile barafu isiyeyuke ndiyo maana tunapata watalii wengi. Kwa hiyo, naomba Serikali ilifikirie hili kwamba hizi Halmashauri zinazozunguka mlima huu angalau

30 APRILI, 2013

zipate fungu kidogo kwa ajili ya kuweza kuendeleza mazingira yake yaweze kuwa mazuri kwa kupanda miti na kuitunza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio ya *TANAPA* zipo changamoto nyingi ambazo zinawakabili na kama walivyosema wenzangu ni tembo kuuawa. Kwa mfano tunasema tembo 110 waliuawa lakini nimeona kwenye taarifa ya *CAG* anasema Idara ya Wanyama Pori ilipunguza doria na wakasema Katavi, doria ilipungua kwa 43.2% wakauawa tembo 15, Mikumi wakapunguza kwa 29.9% wakauawa tembo 10, Nkomazi wakapunguza kwa 43.3% wakauawa tembo watano. Mimi naomba Serikali ituambie hawa watu waliopangua mpango wa doria mzuri, walipata adhabu gani au Serikali imechukua hatua gani kwa sababu tumepoteza tembo 35 kwa kupunguza huo mpango wa doria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kuwoko na angalizo kwamba katika hifadhi ya Mkomazi, Same, tuna faru wanyama ambao ni wachache na wako karibu kutoweka duniani na katika Afrika. Kwa hiyo, niombe sana, *TANAPA* na Serikali iangalie mpango wa doria katika hifadhi hii ili faru hawa wasije wakauawa kama tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko changamoto nyingine ya *concession fee* inayoipata *TANAPA* kwamba kuna hifadhi 14 kubwa ziko kwenye hifadhi za Taifa yaani mahoteli yamejengwa kule kwenye hifadhi za Taifa. Licha ya kile wanachokilipa kama *corporate tax*, kuna *concession fee* ambayo wawekezaji hawa wanatakiwa kulipa lakini wanalipa asilimia kidogo sana, wanalipa 10%. Kwa mfano, kwa mahesabu niliyonayo, Seronera *Wildlife* ilipata wageni 3,292 ikalipa *concession fee* ya wastani wa dola nne, wengine wanalipa wastani wa dola tatu. Ukifanya basi 10% ni dola nne, *fee* kamili ni dola 40 na mimi ukiniambia kuna hoteli iliyoko kwenye hifadhi inachaji dola 40 haiwezekani yaani haiingii akilini kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kuna

30 APRILI, 2013

mahali udanganyifu unatokea lakini inawezekana pia mikataba iliyowekwa tangu mwanzo, tunakumbuka kwamba hizi hoteli zilinunuliwa kutoka Serikalini lakini nakumbuka Serikali ilisema ina-*review* mikataba ya madini kwa nini tusi-*review* mikataba ya hizi hoteli? Haiwezekani mtu kama Grumate au Seronera alipe dola 40 kwa kitanda au kwa kichwa. Naomba Serikali ilianganalie hili na ikiwezekana kama ni sheria basi iletwe hapa tuweze kuisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine *TANAPA* wanakabiliwa na uvamizi wa wakulima walioko kwenye maeneo yanayozunguka mlima, kwa sababu tumekuwa na matukio mengi, tembo wanaingia kwenye makazi na wamekuwa wanafanyiwa uharibufo mkubwa. Hii ni kwa sababu ile korido yao kutoka hifadhi ya Kilimanjaro kwenda Hifadhi ya Kenya Mboseli na kwenda Hifadhi ya Arusha inazibwa kutokana na wakulima kufanya *activities* zao kule. Mimi naomba, ili hawa tembo wasije wakaingia kwenye makazi ya watu na kuleta madhara, Serikali ianganalie ni namna gani basi hawa wakulima waelimishwe umuhimu wa hizi njia kuwa wazi ili hawa wanyama waweze kuwa na *free movement* ambayo haitaleta madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine la *KINAPA*. *KINAPA* wana wafanyakazi, wapagazi lakini na wakala na ipo taarifa kwamba wanalipa mawakala shilingi 20,000 kwa siku. Kwa hiyo, huyu wakala anamlipa *potter* shilingi 5,000, nasikia ndiyo kuna mazungumzo lakini niseme tu shilingi 5,000 kwa *potter* anayebeba kilo 25 ni kiasi kidogo sana. Wakati mwingine wanalazimika kubeba kilo nyingi zaidi ya 25, kwa hali hii tutazalisha magonjwa ya mgongo na magonjwa ya *nerve*. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifuatilie hili kwa ajili ya kuwalinda Watanzania hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapagazi hawa wanaenda mpaka mlimani, hawana bima ya aina yoyote. Kuna baridi sana wanaweza kugua *pneumonia* lakini pia na *muscles dislocation* kwamba wanapanda mlima kila siku, inawezekana kabisa misuli yao ikawa imepata matatizo lakini

30 APRILI, 2013

hawana bima hata kidogo. Naiomba Serikali iangalie ni namna gani inaweza kuwasaidia, *in case* wamepata matatizo weweze kutibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha pia ni kwamba hakuna *helicopter* ya kufanya *rescue* kule mlimani. Kwa hiyo, watalii au wafanyakazi wakipatwa na tatizo haliwezi kufumbuliwa ni mpaka wapige simu Kenya wakodishiwe *helicopter* ije ikamchukue huyo mtu mwenye matatizo. Kwa tukio moja, Kenya wanatoza Watanzania shilingi milioni sasa. Sasa nikajuliza *TANAPA* wanakusanya hela nzuri na pengine labda tukiwapa *rentation* kwa muda kidogo wanaweza wakanunua *helicopter* yao. Naiomba Serikali ifanye hima kuangalia ni namna gani wanaweza kununua *helicopter* kwa ajili ya kufanya *rescue* zake bila kutegemea *helicopter* ya kukodisha kutoka nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nichangie ni hali ya madhari ya *Kibo Hut*. *Kibo Hut* ni kile kibanda cha mwisho ambacho sasa mtalii huyu akitoka chini anakuwa amechoka na sasa anatulia akijiandaa kupanda juu. Wakati mwingine unakuta watalii wako wengi pale *Kibohut*, kama watakuwa wamepanda wengi. Hapa *Kibo Hut* eneo halitoshi, lakini hata madhari yake haipendezi. Mtalii akiangalia amelipa kitu kama dola 1700 au 1800 kupanda mlima, halafu anafika mahali hapo panakuwa na madhari kama ile, hali hiyo haipendezi na inaweza kusababisha tukose biashara. Naiomba sana Serikali ifanyie kazi hili tatizo la *Kibo Hut*, ili kuwe na madhari nzuri na kuondoa manung'uniko ya watalii.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa kengele ya pili.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahasante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Betty E.

30 APRILI, 2013

Machangu. Waheshimiwa Wabunge nilimwita Mheshimiwa Ole-Sendeke na nimemwona Mheshimiwa Selehe Pamba amerejea ukumbini. Kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Sendeka, tutafuatiwa na Mheshimiwa Pamba. Mheshimiwa Sendeka tafadhali!

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu sana ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima nikiri na kukubali kwamba kwa muda mfupi ambao nilipata nafasi ya kuingia kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, nilipata kujionea mwenyewe kwa macho yangu na kwa kusoma taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na *TANAPA* kwa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa kutembelea baadhi ya Hifadhi za Taifa. Nimeridhishwa na jitihada kubwa zinazofanywa na wahifadhi wetu katika hifadhi hizo za Taifa, lakini nimeridhishwa pia na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nianze pia na suala alilogusia ndugu yangu, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Dkt. Nchimbi. Hili halina maana kabisa kwamba sitambui kazi nyingine nzuri zilizomo kwenye ripoti ya Kambi ya Upinzani baadaye nitazitaja sehemu ambazo utafiti wao ni wa kina na wakati mwingine unaweza kuwa na tofauti ya maneno ya namna ya kutumia lakini ukweli unabaki kuwa ni ukweli katika maeneo muhimu waliyoyagusia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hili la *allegory* ya jina la Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, sijui matokeo yake kama ni mkutano wa Morogoro, maana suala la pembe za ndovu ilikuwa ni mwaka 2009 na washtakiwa wake ni wale mliowasikia wako saba, bwana Tesha, bwana Lelo, bwana Lweno, bwana Kiwale, bwana Abubakari na bwana Yabula na wote hawatoki katika Kampuni inayomilikiwa na Kanali Abraham Omar Kinana. Kampuni inayomilikiwa na ndugu Abraham Omar Kinana, baada ya Ripoti ya *Interpol* iliyopelekea *DPP* kufungua mashtaka kwa watu hao saba ili-

30 APRILI, 2013

clear Kampuni ya Sharaf inayomilikiwa na Abrahman Kinana kwamba imetimiza wajibu wake kwa misingi ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonishangaza pamoja na Kambi ya Upinzani kutouona ukweli huo, bado inageuza hata jina la kampuni na kusema kwamba makosa ya kampuni yanaweza kuwa ni makosa ya mmliki bila kujua kwamba kampuni yenyewe ni *legal entity*. Ni kama leo unakwenda *Club* Bilicanas, kwenye burudani pale, halafu mle ndani chooni akakutwa kijana mmoja anakula unga, huwezi kumshtaki Mheshimiwa Freeman Mbowe wala wamiliki wa Bilicana, utashughulika na mhalifu kwani ile ni kampuni. Suala hili Wapinzani wanajua na Mchungaji wangu anajua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kana kwamba hiyo haitoshi, *allergy* nyingine inaingia kwa viongozi waasisi wa Taifa hili, majina ya Nyerere, Sokoine na Kawawa. Kampuni inayomilikiwa na familia ya Sokoine, hivi leo tunavyozungumza haimiliki hata kitalu kimoja cha uwindaji. Iliwahi kumiliki kati ya mwaka 2000 na 2009 mpaka mabadiliko ya juzi na katika muda wote huo, haijawahi kuwa na kashfa ya ujangili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata watoto wa viongozi kufanya kazi ya uwindaji na kumiliki makampuni ya uwindaji siyo kosa. Familia ya Kawawa ina historia ya uwindaji na Saidi Kawawa aliwahi kufanya kazi *TANAPA* na kabla ya hapo alishiriki kuhifadhi pori la Selou na Longido kule. Makosa yao ni kuitwa Kawawa, kuitwa Nyerere au Sokoine? Mnataka kuwalisha hawa? Mbona wengine hamuwataji? Mbona kwenye makampuni ya *tours*, wako hawa ndugu zangu akina Lucy Owenya na Ndesamburo wanamiliki kampuni za *tours*, mbona hawa hamuwataji kama wanafanya biashara za utalii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nachosema hii ni biashara halali, Ndesamburo anafanya biashara halili, familia ya Sokoine anafanya biashara halali, familia ya Kawawa wanafanya biashara halali, Kinana anafanya biashara halali.

30 APRILI, 2013

Kazi ni kutaja majina, mnafikiri itafuta hoja za Morogoro! Nendeni kule jukwaani Morogoro mkajibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Loliondo na suala la Ngorongoro. Mimi nalijua suala hili kwa kina. Siyo tu kwa sababu ya kuingia kwenye Tume iliyoundwa juzi na Kanali Abraham Kinana, Katibu Mkuu wa CCM. Nimekwenda huko mara kwa mara na nimekutana na wananchi wa Ngorongoro na nimekutana na viongozi wa Ngorongoro pia, akiwemo Mheshimiwa Mbunge Kaika Samingo Ole-Telele, akinieleza matatizo ya Ngorongoro. Eneo la Ngorongoro, kama mng'ebaki tu kwenye hoja, Msemaji wa Upinzani ameeleza matatizo ya wananchi wa Ngorongoro, ni matatizo ya kweli. Mimi nasema katika sehemu ambayo mmefanya utafiti ni kubainisha historia ya Wamasai wa Loliondo na Wamasai Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti ya Tume yetu, sina haja ya kuisema leo hapa maana siyo mali ya Bunge, lakini nataka niwaambie kwamba wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro wana matatizo ya msingi, hawamiliki ardhi, hawaajiriwi na kiasi cha fedha wanachotengewa na mamlaka ni kidogo na hili tumemweleza Mheshimiwa Waziri Balozi Khamis Kagasheki ameelewa na nimeambiwa katika bajeti ya mwaka huu wametengewa shilingi bilioni tisa tofauti na ilivyokuwa kule nyuma. Bado ni rai yangu kwamba Serikali hii iongeze ili makusudio matatu ya kuanzashwa kwa Mamlaka ya Ngorongoro Uhifadhi, Utalii na kuendeleza Wamasai iweze kutimia kama sheria yenyewe ilivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la Loliondo kama Tarafa ya Loliondo, kilometa za mraba 1500, ndugu zangu sisi wengine tumefanya utafiti na nashukuru Kambi ya Upinzani kwa taarifa iliyozikotaokota imerejea kama nukuu yao. Nataka niwaambie, tumeleta taarifa ya wananchi wa Ngorongoro siyo kwa kilometa 1500 tu peke yake, tumechambua kilometa zote 14,000 zinatumikaje. Tumeona wazi kwamba katika kilometa za mraba 1500, uko ukweli wa

30 APRILI, 2013

wazi kabisa kwamba wananchi wa Tarafa ya Loliondo bila kuitumia eneo lile hawana maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uko ukweli pia kwamba kuna wanyama waliopo pale ambapo Mheshimiwa Waziri Balozi Khamis J. Kagasheki kwa dhamana aliyopewa kama hataweka utaratibu pamoja na wananchi walioko katika eneo lile, ni dhahiri kwamba utalii na wanyama wale tutakuwa tumewaweka rehani. Tumependekeza mapendekezo mazuri ya kuhakikisha kwamba maslahi ya wananchi wa Loliondo yanapewa kipaumbele lakini uhifadhi pia kwa namna ya kushirikisha jamii unapewa kipaumbele stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nataka niseme wazi na bayana kwamba mkiona Mbunge wa Ngorongoro amezungumza kwa upole kiasi kile, ni baada ya Ripoti ya Tume ya Mheshimiwa Mwigulu L. Madelu tuliyoiwasilisha kwa Katibu Mkuu wa CCM na kwa Waziri Mkuu, kwa Mheshimiwa Waziri Balozi Khamis Kagasheki, tukakaa kwa pamoja tukaafikiana. Tunachotaka sasa hivi na kitakachofanyika ni kwamba Serikali itakaa na wadau wale kama wale waliokuja Madiwani wote wa Ngorongoro na wadau wote wa Tarafa ya Loliondo na kuja na uamuzi wenye maslahi kwanza kwa wananchi lakini pia kuzingatia eneo lile ambalo wanyama wanazaliana, bila kuathiri ufugaji katika Tarafa ya Loliondo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, msione kama Mheshimiwa Mbunge Kaika Saningo Ole-Telele mori umepungua, ndiyo maana alikuwa anamwomba Mwenyezi Mungu kabla hajaongea kwamba ampe hekima ya kuongea katika jambo hili maana ana uchungu lakini anaujua pia ukweli kuwa Serikali imeshasikia taarifa ya Tume ya Mheshimiwa Mwigulu L. Madelu na imekubaliana na mapendekezo yetu na itatoa uamuzi utakaokuwa na maslahi kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la migogoro ya mipaka katika Hifadhi ya Taifa (*Game Reserves*)

30 APRILI, 2013

na maeneo ninakotoka ya Simanjiro. Kijiji cha Kimotoro katika Wilaya ya Simanjiro na kijiji katika Wilaya ya Kiteto...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha k
wa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole Sendeka kengele ya pili!

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Hiyo siyo ya kwanza? *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Kengele ya pili!

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii, nikitegemea kwamba suala la mpaka huo litatatuliwa, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Sendeka na makofi hayo uliyopiga inatakiwa taratibu huwa hatuyaruhusu sana, kwani mmepongezana hapo kwa nguvu kubwa sana lakini nakushukuru sana kwa mchango wako Mheshimiwa Sendeka, nilisema nitamwita Mheshimiwa Saleh Pamba. Tafadhali Mheshimiwa Saleh Pamba!

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nitangulize kusema kwamba naunga mkono hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu hawa wa Wizara ya Maliasili na Utalii wanafanya kazi katika mazingira magumu sana lakini kutokana na uchache wao, kutokana na moyo walio nao wa kizalendo, wa nchi yetu, bado wameeendelea kufanya kazi bila kukata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano. Hifadhi ya Selou peke yake ina ukubwa wa *squre* kilometa 50,000 ni sawasawa na ukubwa wa nchi ya Ubeligiji, ni sawasawa na

30 APRILI, 2013

ukubwa wa nchi ya Uholanzi, ni sawasawa na ukubwa wa nchi ya Denmark. Mataifa hayo makubwa matatu ni sawasawa na hifadhi moja tu! Watumishi wetu kwa moyo kabisa wameendelea kufanya kazi, wameendelea kupambana na majangili na ndiyo maana hifadhi hii na hifadhi nyingine hapa nchini bado zimebaki katika hadhi yake ileile ya kimataifa. Wanafanya kazi nzuri sana, msikatishwe tamaa na maneno hayo, muendeleo kabisa na Serikali itawasaidia katika kuhakikisha kwamba mnapata wafanyakazi wa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo yametajwa na Kambi ya Upinzani. Kwa bahati nzuri ni kwamba mimi nimepata nafasi ya kufanya kazi katika Wizara hii kwa takribani miaka 34. Mambo mengi yaliyomo humu yanatakiwa yatolewe ukweli ili kusudi wananchi waweze kuelewa yale yanayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa hii ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, amezungumzia juu ya Ripoti ya mwaka 2006 ambayo Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani anasema ripoti hii ilikuwa ni Ripoti ya Bunge. Ukweli wenyewe ni kwamba wakati Serikali ya Awamu ya Nne inaingia madarakani; moja kati ya maeneo iliyotaka kuyafanyia kazi kwa haraka, ni kuhakikisha kwamba sekta ya uwindaji inaleta mafanikio yanayotakiwa. Kwa misingi hiyo, pale sisi ambao tulikuwa Wizarani, tuliunda Kamati ambayo kwa bahati nzuri sana iliongozwa na Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina ambaye ni Mbunge wa Ngara. Kamati hiyo ilifanya kazi nzuri sana na lengo kubwa tulitaka tujue ukweli kwamba, je, mapato ya utalii hasa katika sekta ya uwindaji yanasaidia nchi? Kwa hiyo, Kamati hii ilitembelea maeneo mbalimbali, ilikwenda Mozambique, ilienda Botswana, ilienda Zambia, ilienda South Africa. Kutokana na Kamati hii, Wizara ilitekeleza mapendekezo yote ya Kamati hii na siyo kweli kwamba Wizara ilikalialia au iliyaweka kampuni mapendekezo ya taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo Wizara iliyafanyia kazi, la kwanza ni bei za wanyama.

30 APRILI, 2013

Wawindaji walikuwa wanatupa bei ndogo sana ya wanyama. Kwa mfano, simba tulikuwa tunachaji dai dola 3000, Serikali ilipandisha kutoka dola 3000 mpaka dola 10,000. Hayo ni mafanikio makubwa ya Kamati hii na Serikali imeyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, katika Kamati ile waligundua, idadi ya vitalu vilivyopo ni vikubwa mno kulinganisha na wenzetu katika nchi nyingine. Vitalu vilikuwa 42 tu lakini Wizara ilifanyia kazi na ikaongeza vitalu kutoka 42 mpaka 96, kwa kuvigawa ili watu wengi waweze kufaidika. Hayo yote yalifanyiwa kazi na Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo ni la msingi kabisa. Wizara katika kipindi kile ilikuwa inapata dola milioni 14 tu kutokana na biashara ya utalii wa uwindaji lakini sasa hivi kutokana na taarifa ile ambayo Serikali ya CCM, Wizara inayoongozwa na Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki hivi sasa, wanapata dola bilioni 28 kutokana na utalii wa uwindaji peke yake. Kwa hiyo, ni kwamba taarifa hii imefanyiwa kazi na haikuwekwa kapuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie kidogo katika suala ambalo taarifa hii imelisema kuhusu Ngorongoro. Mimi nataka niweke mambo sawa, ni kwamba Ngorongoro ilianzishwa mwaka 1959 wakati wa enzi za Ukoloni na wakati walipoanzisha hifadhi hii, mambo matatu makubwa, walisema watalinda maslahi ya wenyeji wa pale. Serikali ya CCM ilibadilisha sheria hii mwaka 1978 lakini kutokana na kulinda haki za wenyeji pale, bado katika sheria hii mpya, moja ya majukumu ya Ngorongoro ni kuhakikisha kwamba wananchi wanalindwa na maslahi yao yanalindwa. Kwa hiyo, kazi kubwa zinazofanyika pale ni kazi tatu. Kazi ya kwanza, ni utalii, kazi ya pili ni uhifadhi na kazi ya tatu ni kulinda maslahi ya wananchi pale na bado inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi ambayo Hifadhi ya Ngorongoro inawafanyia wenyeji pale. Masuala ya mifugo, majosho na kadhalika na masuala yanayohusu kilimo. Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

30 APRILI, 2013

imetumia zaidi ya shilingi bilioni 10 kutafuta eneo katika eneo la Oldonyosambu kuhakikisha kwamba wananchi wa pale wanaondokana na adha ya kupewa chakula cha misaada. Yote haya yanafanyika kwa sababu CCM kinaheshimu wananchi wake na hasa wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro, kama wananchi wengine ambao ni sehemu ya jumuia ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende harakaharaka, kwenye suala moja tu lililobaki, ni hili suala la misitu. Napenda niwapongeze sana Wizara kwa kuanzisha Mamlaka ya Misitu (*Tanzania Forestry Services*) wamefanya kazi nzuri na waendeleo kufanya kazi nzuri. Wameanzisha kuanzisha mfuko, sisi ambao tuko kule Wilayani, tunaomba fedha hizi ambazo mmezianzisha kwenye Mfuko wa Misitu, fedha hizi sasa zitumike kupeleka Wilayani katika Halmashauri zetu ili tuweze kupanda miti. Fedha ni nyingi mmeanzia lakini mtafute vyanzo vingine vya kuhakikisha kwamba mfuko huu unatuna ili kusudi tuweze kupanda miti. Tusibaki tu kusherekea siku ya kupanda, kitu muhimu ambacho tunatakiwa kufanya sisi na Wizara ifanye, ni kuhakikisha kwamba, miti milioni 288 ambayo imepandwa mwaka jana peke yake, kwamba miti hii inatunzwa, inakua ili kuiondolea nchi yetu hatari ya kugeuka jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ambalo ningependa kuzungumzia, ni suala la ujangili. Nimeona jitihada za Wizara hii na wanafanya kazi ngumu sana. Ninataka waendeleze jitihada na kuhakikisha kwamba wanapambana na majangili popote walipo, wahakikishe kwamba majangili ambao sasa wamepiga kambi katika hifadhi zetu wanaondoka kwa kufanya *operation* maalum ya kuwaondoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tufanye kazi ya kuwaondoa majangili ambao wako kule, halafu tuweze kujipanga vizuri. Tumepoteza wanyamapori wengi katika kipindi cha miaka 30. Tanzania tulikuwa na tembo 300,000 sasa hivi tuna tembo 150,000 peke yake na hatuwezi

30 APRILI, 2013

tukaendelea katika hali kama hii. Sisi tutajitahidi na kutokana na *influence* zetu kama Wabunge, tuhakikishe kwamba Wizara hii kwa sasa hivi inapata bajeti ya kutosha ya kuhakikisha kwamba inapambana na majangili ili kusudi hifadhi zetu ziweze kuendelea, ziweze kupata heshima kama ambayo tumeipata kwa Mlima Kilimanjaro, heshima tuliyoipata kwa ajili ya Serengeti, Ngorongoro na hifadhi zote nyingine ambazo zina sifa ya kipekee hapa Duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwasaidie katika kuongeza bajeti ya utalii...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saleh Pamba nakushukuru.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saleh Pamba nakushukuru kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Rebecca Mngodo atazungumza kwa dakika tano na dakika tano zinazobaki zitatumwa na Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kabla sijatoa mchango wowote, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Betty Machangu ya kwamba Mkoa wa Arusha haujakosa mtu wa kuwasemea kwa vile eti Mbunge wao yuko katika maandamano. Humu ndani niko mimi, yuko Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Joyce Mukya na tumewahi kuzungumzia masuala ya wanawake wanaoteseka na watoto wanaotumikishwa katika mashamba ya maua na hata yeye pia Mheshimiwa Betty ni mwanamke ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum ambaye pia anaweza akawasemea wanawake na watoto katika mashamba ya maua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa sababu ametupa nchi nzuri yenye wanyama pori

30 APRILI, 2013

wazuri, ambao ni urithi tuliopewa tangu babu zetu mpaka leo na vizazi vyetu vijavyo ambavyo vinaweza vikafaidika na mbuga za wanyama endapo uangelizi na uendelevu mzuri utawekwa katika mbuga zetu za wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, nasikitika Serikali ya CCM imeshindwa kuweka *priority* katika mbuga za wanyama. Ukiangalia fedha ambayo imeombwa katika mwaka huu ni shilingi bilioni 11, tunaambiwa shilingi bilioni 10 ni fedha za nje ambazo mimi nasema fedha ikiwa ya nje naiona ni fedha hewa, kwa sababu hatuna uhakika kwamba fedha hiyo itatolewa. Aidha, shilingi bilioni moja ambayo ni ya ndani, ninahesabu pia kwamba ni hewa, kwa sababu hatuna uhakika kwamba hiyo fedha itatolewa kwa sababu katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, kinasema kwamba, katika mwaka wa fedha 2012/2013, fedha iliyokuwa imetolewa kwa miradi ya maendeleo ilikuwa shilingi milioni 360 tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli ni aibu kwamba katika sekta muhimu kama hii ambayo inachangia pato la Taifa karibu asilimia 17, tusingekuwa leo na watoto ambao wanakaa chini kwa kukosa madawati, tusingekuwa leo na hospitali ambazo hazina dawa, tusingekuwa na wanawake ambao wanazalia chini eti kwa sababu hakuna vitanda, ni ukosefu wa kuweka *priority* katika mbuga za wanyama ambazo mimi ninahakika kama wangeweka *priority* kwa kutangaza, kwanza ningependa kujua ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya kutangaza mbuga zetu. Wakenya hapa kila siku tunalia tunasema wametuzidi, kila mara wanaendelea kutushinda kwa kusema kwamba Milima iko kwao, wanyama wako kule kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa pale Mkoani Arusha katika hoteli fulani, naona mbuga za wanyama zikitangazwa wakisema Serengeti iko kwao, Seronera iko Kenya na sisi bado tuko kimya, hatusikii kwamba Wizara hii inachukua hatua gani. Hatufahamu wana mtazamo gani, hatuelewi, mimi nashindwa kuelewa. Sasa tutakuwa kila siku tunazungumza

30 APRILI, 2013

ni yaleyale jamani na huku wenzetu wa Kenya wanazidi kufaidika, tunahitaji kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuona Wizara hii ikichukua hatua, tunahitaji kuona changamoto zile zilizoko katika sekta hii ya Maliasili na hasa katika mbuga za wanyama, zinafanyiwa kazi. Kama ni kuajiri Maafisa kazi wa kutosha, tuone wanaajiriwa. Kama ni kutenga fedha za kutosha tuone ile fedha inatolewa na siyo kwamba fedha inatolewa inatengwa na inaombwa hapa inaidhinishwa na Bunge halafu hakuna chochote kinachofanyika. Tunaona kwamba ni pesa kidogo tu inatengwa, shilingi milioni 360, hiyo ni fedha kidogo sana ambayo ilitengwa katika mwaka uliopita. Sasa hivi Mheshimiwa Waziri atasimama tena hapa kuomba fedha iidhinishwe na hatujui kama hiyo fedha itatolewa kama ilivyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo naomba nizungumzie biashara inayofanyika Loliondo. Mzungumzaji wa Kambi ya Upinzani alielezea kuhusu *OBC* inayofanya biashara ya uwindaji Loliondo lakini nataka kusema pamoja na hayo kuna makampuni mengine yanayoshughulika na utalii wa picha katika hilo eneo hilo bila kibali cha Serikali. Kampuni inayoitwa *Clens Camp* inafanya biashara katika eneo la hekta 25,000 katika kijiji cha Ololosenkwan kinyume na Sheria, samahani Wamasai kama nimekosea kutamka lakini najua kuna Kampuni ya aina hiyo ambayo inafanya kazi katika kijiji hicho kinyume na sheria. Aidha, kampuni hiyo ina kiwanja cha ndege, watalii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rebecca dakika zako zimekwisha. Mheshimiwa Susan Kiwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

MHE. SUSAN L. A KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza...

30 APRILI, 2013

MWENYEKITI: Una dakika tano.

MHE. SUSAN L. A KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi kwanza ni Mjumbe wa Kamati, kwa hiyo, sina budi ya kuungana na yale yote yaliyowasilishwa na Mwenyekiti wetu wa Kamati kwa sababu mimi ni sehemu ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mimi niko kwenye Kambi ya Upinzani, kwa hiyo, sina budi kuunga mkono maelezo yote yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani kwa sababu ndiyo msimamo wa Kambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza kwa kusema hivi, kwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM na Kampuni yake amehusishwa na masuala mbalimbali katika kupeleka meno ya tembo ya Tanzania ambayo yalikamatwa China, hiyo haina ubishi, ni vema Serikali ikapokea hoja na ikazifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vema Serikali ikapinga hoja ambazo zimesambaa duniani kote. Kusema kwamba yeye ni kampuni mambo yanayofanyika mle siyo yeye anayehusika, je, huyu mtumishi wake katika Idara ya Fedha na Utawala anayelitwa Samiy Rehman ambaye aliishi hapa nchini na kibali chake killiisha, ilikuwaje asiondolewe nchini akaendelea kuishi hapa nchini bila kibali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo hamwezi kubisha, ukweli lazima muuchukue na muufanyie kazi. Tuko hapa vilevile kuwasaidia angalau mbakie madarakani lakini mkifanya mchezo, yatawakuta yaliyowakuta Ruaha, Kinana kaenda, Nape kaenda, jana tumebeba, juzi tumebeba, Kijiji na Kitongoji, mmebaki hoi, chali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo salamu za Watanzania kwenu, pamoja na kwamba mmetumia nguvu kubwa lakini tumewabwaga chali. Mwenyekiti wa Mkoa wa CCM alikuwa kule, ndugu yangu huyu hapa Mbunge wa

30 APRILI, 2013

Kusini na Mkuu wa Wilaya alikuwa kule, yule Tarimo wa Kilosa, mimi nilikuwa hapa Bungeni, nimewaacha, nimepanga majeshi yangu, chali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo CHADEMA na hizo salamu za CCM kwamba lazima mchukue mambo ambayo tunawaambia na myafanyie kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko natoka, katika suala zima la maliasili, lazima tukubali kujipanga vizuri kulinda maliasili zetu, maliasili zinaondoka, wanaoonewa ni watu wadogo, wale wakubwa wanaachwa. Haiwezekani Serikali ikaweka mapori ya akiba, hayana ulinzi, tembo wanatembea wanaenda kule, majangili wanajua kwamba tarehe fulani tembo wanakwenda, kunakuwa machinjio ya tembo, Serikali haiweki Askari, haiweki ulinzi. Haiwezekani! Serikali mnajua na ninyi ndiyo mnaopanga mbinu ya kwenda kule kuchinja wale tembo wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tembo wanazunguka kwenye ule Mlima wa Udzungwa, wanaingia kwa wananchi Wilaya ya Kilombero, wananchi wa Kilombero siku hizi hatuui tembo, kama tembo tulikuwa tunaua zamani, hata uhujumu uchumi ulivyofika, wananchi waliokuwa wanafanya kazi hiyo wakaamua kuacha, sasa hivi wanaohusika na uhujumu uchumi ni watu ambao wako kwenye mamlaka, wenye silaha za kivita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie Wizara hii kwamba, hebu muwasaidie wananchi wanaozunguka katika maeneo hayo, muwashirikishe katika kulinda maliasili na wao waone faida moja kwa moja wanavyolinda, nyama mnatukataza kula, samaki mnatukataza kuvua, sasa tunafaidika nini tuliozaliwa katika maeneo hayo? Lazima tuone faida za moja kwa moja, tulinde ili na sisi tufaidike. Shule tunajenga wenyewe, barabara hazipitiki. Tumekwenda Ruaha, barabara ya kilometa 130 mmeshindwa kujenga! Kazi yenu kwenda tu kuchukua fedha kule, kwa hiyo, Serikali

30 APRILI, 2013

lazima iwajibike. Hizo njia zinazolingia katika hizo hifadhi za kitaifa, jengeni barabara watu waende wakatalii, fedha zizidi kuongezeka, boresheni miundombinu. Hamwezi mkakubali kukamua maziwa wakati ng'ombe hamjampa majani, haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilombero katika ile migogoro ya mipaka, kesi iko Mahakamani lakini leo wakati huu wa mafuriko eti kuna mtu pale na *team* imetoka Wizarani, inakwenda kurekebisha ile mipaka. Sasa hivi kuna maji, naomba ile *team* Waziri airudishe, wakati wa kiangazi iende ikarekebishe ile mipaka. Sasa hivi wakienda hawatafika, watatumia fedha za Serikali bure. Nimesikia wako pale Kilombero eti wanakwenda kwenye maji watafikaje? Watafikaje wakati wenyewe tunashindwa kuingia kule? Hayo ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali, naomba ile *team* isimamishe mara moja kama kwenda kurekebisha mipaka waende wakati wa kiangazi siyo wakati wa masika kwa sababu hawatafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida zipatikane, wananchi wa Kilombero wameteseka sana na hii *TANAPA*, mpaka sasa wanazidi kuteseka. Tembo wanaingia katika vijiji, kwa mfano Mkula pale, Ulayaulaya kule Kilosa, wanaharibu mazao lakini hamna fidia. Ukimpigia Mkuu wa Wilaya nitakwenda, sijui Maasikari hakuna, *Game* hakuna, naomba Serikali iweke *ma-game* kulinda tembo wasiingie kwa wananchi. Wananchi wanavumilia sana na wanateseka.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. SUSAN L. A KIWANGA: Nashukuru, naona ujumbe umefika ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Beatrice Shellikindo atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kebwe.

30 APRILI, 2013

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa sababu ya muda nakwenda moja kwa moja kwenye hoja zangu. La kwanza ni *WMA*. *WMA* Kilindi inapita kwenye vijiji 11 na hili jambo tumeahidiwa takribani miaka nane iliyopita. Kinachonishangaza kila mwaka ukipita hatumo ndani. Tuliwaandaa wananchi kwa ajili ya semina kama tulivyoambiwa, walifika kule wataalam, bwana Masanja walikwenda na watu wengine, walifika wakaona eneo na wakatoa tathmini. Kila nikiuliza naambiwa iko mezani kwa Katibu Mkuu. Sasa naomba niulize, wananchi wanasubiri, leo naona tena vijiji vingine vimetajwa Kilindi haipo. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba sana, hata lile gawio la asilimia 25 kwa miaka minne hakuna kitu, sasa tujeleweje sisi watu wa Kilindi? Mimi naomba sana tupate majibu Waziri atakapohitimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Kilindi, niwashukuru sana *TANAPA*. *TANAPA* wamekuwa wakitusaidia kwa mambo mbalimbali ya kijamii na hususan hata kwenye *post* yetu. Kwa hiyo, nimeombwa niwashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyuki, tuna vijiji 15 na zaidi ya Kata tano ambazo zinashughulika na nyuki, lakini nashangaa hapa nikisoma, sioni mahali popote ambapo Kilindi imo hata mafunzo, hata nini, hakuna. Sasa sijui Maliasili wana mpango gani na hivi vijiji vya Kilindi ambavyo vina nyuki. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana kwa upande huo, hawa ambao wanashughulika na ufugaji wa nyuki na wenyewe watazamwe kwa sababu wanafanya kazi kubwa na inatupatia kipato kikubwa ndani ya Kilindi, wanahitaji msukumo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilitaka kuuliza tu, napenda sana kufuatilia mijadala na mara nyingi sasa hivi nimekuwa msikilizaji, lakini ninaona sasa hivi hapa, mimi sidhani kama Kinana asingekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, jina lake lingetajwa humu ndani. Naona linatajwa kwa sababu ni Katibu Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme na niwaombe

30 APRILI, 2013

Watanzania mnaosikiliza, hapa ndani hatuji kushindania vyama vyetu, tuna majukwaa kama alivyosema Mheshimiwa Kiwanga huko nje, hiyo ni sahihi, lakini hapa ndani tunaongelea maslahi ya wananchi. Hasa mambo ya kuongelea ushindani wa vyama, kutaja majina ya vyama kwa sababu hiyo, kwa kweli mimi napata uchungu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kwa muda mfupi tulongao twende na haya masuala ambayo ni kweli, kwa sababu pia nimeongea na watu wa huko Loliondo, wenyewe hawana matatizo na *OBC*, *OBC* hawajamilikishwa, wale wanaishi mle ndani, wanaishi nao, wanasema jamani mbona mnasema *OBC*, sisi hatuna tatizo, sisi tuna tatizo na *GCA* mbona siku zote tuko na hawa watu? Sasa jamani, mimi naomba sana, tunapongea haya mambo, niombe tu Serikali itumie busara zake, siasa nyingi pia imekwenda. Naibu Katibu Mkuu wa Chama kwenda kule ilikuwa ni sahihi! Sisi hawa watu wametupa kura, ndiyo maana tuko madarakani. Tukisikia jambo lao tunakwenda, mimi Kilindi nikisikia jambo sijali kuna Serikali, sijali kuna nini, niko pale kwenye tatizo, kwa sababu ndiyo walionipa kura. Sasa Naibu Katibu Mkuu kwenda ni jambo la kawaida kabisa na tunafanya kazi zetu kwa utaratibu wa Chama chetu kama ambavyo tumeambiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi kwa kweli, nilikuwa nasema tu, mimi nasikitishwa sana, wananchi wenyewe tunazidi kuwatia chonjo nyingi kutokana na mambo ya kwetu ya kisiasa. Niombe Serikali itumie busara zake, iende ikajaribu kuamua hili jambo kwa upole. Watu wale wanataka *WMA*, *simple*. Kwa hiyo, ni jambo ambalo la kuliangalia kwa busara badala ya kulikuza na kujenga hisia tofauti badala ya kuleta maendeleo kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa kweli mimi niombe tu kumpongeza Waziri kwa safari za nje anazokwenda kutangaza utalii. Mara nyingi tunapata taarifa mbalimbali jinsi anavyozunguka pamoja na Naibu wake kutangaza utalii. Kuna jambo moja tumepata malalamiko,

30 APRILI, 2013

Bodi ya Utalii, mara nyingi wanakwenda wao, wenyewe Wajumbe wa Bodi na watalaam, lakini tulikuwa tunaomba sasa na wale wafanyabiashara, wadau waende. Kwanza wanajigharamia wenyewe hamna *cost* yoyote, ni ile kuongeza nguvu. Kwa hiyo, naomba niliseme hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile la mwisho kabisa, tuliwahi kusema kuwa kwenye Balozi zetu waende Maafisa Utalii. Sasa sujui hili limefikia wapi. Badala ya watu kutoka hapa, gharama kubwa kuzunguka tungekuwa na Maafisa pale *permanent* ambao wanafanya kazi hizo, kwa kweli gesaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimwa Beatrice Shellukindo nakushukuru sana kwa kutusaidia kutunza dakika kadhaa ambazo zitatumwa na Mheshimiwa Peter Serukamba kama mliyokubaliana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Dkt. Kebwe.

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii kuchangia Wizara hii muhimu katika mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana Serengeti wamenituma hivi, nilete salamu kwa Serikali. Nasimama leo hii kuwawakilisha ni mara ya tatu katika Wizara hii tangu Bunge hili la kumi. Salamu zenyewe, wametoa onyo, wamevumilia vya kutosha kwa kero ambazo zipo. Kero ya kwanza ni *CITES*, *CITES* kwa kazi zake kubwa za msingi ni kuangalia na kuweka mazingira, wanyama hawa ambao wanatishiwa kutoweka wasitoweke, lakini *CITES* kazi inayofanyika pale Serengeti wamekuwa ni wakusanya ushuru kwa wawekezaji ambao wako ndani ya Serengeti, hususan maeneo yale ya *WMA* pamoja na vikundi mbalimbali, kwa mfano pale kijiji cha Ikomarobanda. Fedha ambayo inaletwa hajjulikani ni kiasi gani, vile vikundi vinapunjwa, fedha ambazo

30 APRILI, 2013

zinapelekwa ukijaribu kuangalia gawio lile, linakwenda katika Serikali Kuu, inapelekwa Halmashauri, pamoja na *WMA*. Mazingira haya ya *CITES* nimeyazungumzia tangu mwaka 2011, lakini Serikali yetu sikivu ya Chama cha Mapinduzi masiko yamekuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wameshatembelea Wilaya ya Serengeti, labda safari zile zilikuwa ni za dharura ikiwemo mauaji ambayo yalitokea katika ile *camp* ya wenzetu pale lkomarobanda. Sasa Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho, naomba baada ya kuhitimisha, twende ziara Serengeti, tukae, tuzungumze na wenyewe mjionee, wanasema, *to see is to believe*, naomba katika majumuisho nipate majibu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mipaka, ukijaribu kuangalia Tangazo la Serikali la mwaka 1968 limeeleza, labda wakati ule hapakuwa na *GPS* hapakuwa na *GIS*. Katika kufuatilia, timu za Wizara wamekwenda mara kadhaa lakini wakienda wanabishana, kwa mfano, timu ilikwenda mwaka 2008 na baadaye ikaenda mwaka 2010 timu nyingine ya Wizara wakaanza kubishana kwamba aah, hawa wenzetu waliokuja hawakufanya sahihi, utaratibu ni huu. Mwaka 2012 mwezi Novemba mpaka Desemba timu ya Wizara ilikuwa inazungukia maeneo kulingana na hoja ambazo tulileta hapa Bungeni. Inasikitisha nao wamekwenda maeneo mengine ya vijiji, fikiria tangu tamko la Serikali la mwaka 1968 leo wanaambiwa kwamba eneo hili lipo katika hifadhi, mnaombwa muondoke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni kuwanyanyasa na kuwatesa wananchi kwa sababu miaka yote hiyo Serikali ilikuwepo na hali ya mipaka ilikuwa inajulikana. Naomba hili kama tulivyokubaliana katika kikao cha wadau wa utalii pale Mwanza tarehe 25 na 26 Machi, utaratibu na ushauri ule Wizara muuchukue na muufanyie kazi haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala hili la mipaka, ukiangalia upande wa Mashariki wa Wilaya ya Serengeti mpakani na Ngorongoro kulingana na Sheria ya

30 APRILI, 2013

mwaka 1959 ya kuanzisha *National Park* wakati wa ukoloni, bado kuna mzozo mkubwa kati ya Wilaya ya Ngorongoro pamoja na Serengeti. Kwa hiyo, naomba suala hili lifanyiwe kazi mapema iwezekanavyo ili kuepusha migogoro ambayo si ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nikijaribu kuangalia adha ya tembo imekuwa ni karaha kubwa kwa sababu, wenzetu Zanzibar najua tembo ni suala lingine wao wanaita ndovu, wenzetu wa Zanzibar mtuelewe huku Bara sisi tunasema tembo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ndovu ni tatizo kubwa lakini kwa wana Serengeti tunaomba Serikali itusaidie, sisi hatuwauwi tembo tunawaabudu. Kwa mfano, ukienda lkomorobanda, ni mnyama ambaye anaabudiwa kwelikweli na ni kijiji ambacho kiko karibu na *National Park* na kutokana na mazingira yale tembo wenyewe kwa hisia wameshajua wakienda hawabughudhiwi. Wanakwenda kwenye maeneo kama ya Machochwe, wanakaa vizuri na hawauawi, wananchi wanawaabudu. Ushahidi uliopo mwaka 2012 mwishoni kuna mwananchi ambaye ametengwa na jamii ya wenzetu wa Kira pale Machochwe kwa sababu ya kushiriki katika ujangili wa tembo. Kwa hiyo, unaweza kuona ulinzi huu wa asili jinsi ambavyo unasaidia kuendeleza maliasili hii. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali iyachukue mawazo haya mazuri kwa ajili ya kujenga uhusiano na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikijaribu kuangalia suala zima la uhusiano hivi likoje? Ukijenga uhusiano, unasaidia kuongeza nguvu ya kiulinzi. Naomba watumishi wachache wale ambao wanaipaka matope Wizara, washughulikiwe kwa ajili ya kuimarisha vizuri suala la uhusiano. Kwa sababu wakati wengine unakuta mifugo iko mbali kabisa na hifadhi hata haijafika kwenye *buffer area* lakini wanaswagwa wanapelekwa kwenye *National Park* wanawasulubu, wanawatesa halafu wanachukua na fedha kinyume na utaratibu. Watumishi hawa wachache Wizara fanyeni kazi, kazeni kamba ili kusudi wasizidi kuwapaka matope na kujenga uhusiano mbovu.

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 wakati nachangia katika Wizara hii, niliwasilisha risiti ambazo walitoa kwa huyu Mzee Mwita Tahimaha shilingi milioni mbili. Sasa yule mkulima maskini anachajiwa fedha nyingi kiasi hiki lakini mpaka leo sijapata majibu kutoka Wizarani. Niliwasilisha risiti ile kwa ajili ya utendaji wa kazi, si hata barua ingekuja basi, kwani ni sehemu ya kujenga uhusiano mzuri na kuonyesha kwamba Serikali inafanya kazi hoja hizi ambazo tunazileta Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mapato, katika swali namba 33 ambalo nililuliza katika Bunge hili, tarehe 12/4/2013, niliambiwa kwamba mapato ambayo Serengeti tumepata mpaka sasa ni shilingi milioni 13 katika mwaka huu wa fedha lakini katika makisio ilikuwa ni shilingi milioni 59, sasa fedha nyingine zipo wapi? Kwa hiyo, ni vizuri katika mapunjo haya ambayo tunayapata, Serikali ikae vizuri ili iendane sambamba na suala la kuondoa gharama hizi za ushuru wa vitanda, *bed fee* imeondolewa, ni sehemu ambayo Halmashauri zetu zingeweza kupata fedha za kutosha kwa ajili ya maendeleo ya Wilaya kwa sababu tunachangia kwa kiasi kikubwa katika ulinzi wa maliasili hii. Je, *bed fee* iko wapi? Sheria Namba 5 ya mwaka 2009 hadi sasa Kanuni zipo wapi ili kusudi Halmashauri ziweze kujipanga kutumia sheria kwa ajili ya kuinua mapato kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kero nyingine ambayo tunaiona imekithiri na naomba Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii wachukue hatua haraka iwezekanavyo. Wana Serengeti wapo wengi wenye uwezo wa kifedha na uzoefu wa kibiashara, hivi inakuwaje bidhaa zinatoka Mkoa wa Mara kwa mfano, samaki wanatolewa Ziwa Victoria wanapita palepale Serengeti, wanapelekwa mpaka Arusha. Samaki haohao hutolewa Arusha na kurudishwa kwenye hoteli za Serengeti, hili halikubaliki kwa wana Serengeti. Ndiyo maana nimesema leo tunatoa onyo hatua inayofuata tutachukua hatua kali zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msingi ambalo naliona ni kuhusu fidia. Kuna madhara yanayofanyika ya

30 APRILI, 2013

mifugo kuuawa na wanyama wa porini, kuna mifugo ambayo inapotea katika mazingira ambayo siyo ya kawaida lakini fidia ile ambayo inadaiwa na nyaraka kupelekwa Wizarani, majibu hayapatikani. Hivi kuna nini ambapo kwa utaratibu nyaraka hupitia kwa Mkuu wa Wilaya na Halmashauri halafu zinakuja Wizarani lakini hakuna majibu. Ukijaribu kuangalia wananchi wengi ambao wako kandokando ya vijiji vile ambavyo vipo jirani na *National Park*, mashamba imekuwa ni tatizo, wakilima kidogo mazao ya chakula na biashara yanaharibiwa na wanyama hawa lakini inakuwaje majibu ya fidia hayatoki Serikalini? Tatizo ni nini? Kwa hiyo, suala hili ni la msingi lifanyiwe kazi kwa umadhubuti ili kusudi kuondoa adha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la misitu limezungumzwa katika kitabu hiki lakini sijaona sehemu ambayo Wizara imejipanga kuchukua Mto Mara kwa ajili ya kulinda ile misitu ambayo ipo. Mto Mara kwa eneo lake, ni ombi tunaleta Mkoa wa Mara ili mto ule uwe chini ya Maliasili na Utalii kwa sababu pale kuna misitu mizuri, miti mizuri, kuna viboko, nyatimaji na mamba pia. Mazingira kama hayo huwezi kuachia Vijiji eti wasimamie ulinzi huo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge.

DKT. KEBWE S. KEBWE: Nashukuru sana na ninaunga mkono kwa mara ya mwisho. *(Makofi)*

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. HALIMA J. MDEE: Mwongozo wa Spika!

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Halima lakini nitakupa nafasi baadaye. Tunaendelea na wachangiaji wanao fuata, nitamwita Mheshimiwa Lucy Owenya kwa dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu.

30 APRILI, 2013

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Ni dakika tano tano!

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Kipekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka kwa kutambua kwamba *Keys Hotel and Travel* zinafanya biashara ya kihalali na ni mfano wa kuigwa kwa viongozi wengine kwamba CHADEMA tunafanya biashara halali na ndiyo maana Kambi ya Upinzani haikuweza kututaja katika hotuba yake. Aelewe kwamba kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani wale waliotajwa inatokana Kikosi Kazi cha Mheshimiwa Diallo alichokiunda mwaka 2006. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika sekta ya utalii kama nilivyoeleza kwamba mimi ni mdau. Sekta ya utalii inachangia kwa 17.5% kwenye pato la Taifa na Mlima Kilimanjaro unachangia fedha nyingi sana, inaonyesha kwamba Kilimanjaro imeingiza zaidi ya shilingi bilioni 80 ambayo ni takribani dola 50,000. Hizi ni fedha nyingi sana lakini wana Kilimanjaro wanauliza Halmashauri zinazozunguka mlima ule zinafaidikaje na mapato haya? *KINAPA* imekuwa ikitoa msaada kwa kujenga choo au darasa, hii haitoshi kwa watu wanaozunguka Mlima Kilimanjaro kwa sababu sisi ndiyo tunaoulinda mlima ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiongea mara nyingi kuhusu Mlima Kilimanjaro kwamba fedha zinaweza zikapatikana zaidi, kuna *route* ya *Old Moshi*. Nimekuwa nikiizungumzia mara nyingi, ni *route* fupi na miundombinu tayari ipo. *Route* ile inaweza kutumika kwa ajili ya ku-*achromatize* au kwenda kupiga picha kwani kuna *water falls*, inaweza kutumika kwa *day trip* lakini mpaka sasa hivi Serikali inasuasua kufungua *route* ile. Mimi naomba tu Wizara ya Ujenzi pamoja na Maliasili basi mtengeneze ile barabara inayoanzia Kiboriloni kupitia Kikarara, Kidia mpaka Gate. Barabara ile ikitengenezwa, nina hakika *route* ile itaazika na sisi kama wadau tupo tayari ku-*market* ile barabara na watalii watakuwa wengi tu. (*Makofi*)

30 APRILI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hilo, sijaona Waziri akizungumzia kuhusu michezo na utalii. Kilimanjaro tumekuwa tukifanya *Kili Marathon* na *Kili Marathon* hii ilianzishwa na Mheshimiwa Ndesamburo na sasa hivi imekuwa ni ya kitaifa na watu wengi wanakuja na ni mfano mwingine pia wa kuigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa mwaka 2014 hoteli zote Moshi na Arusha zimeshajaa. Hivyo basi, naomba Mheshimiwa Waziri achanganye michezo na utalii kwa sababu watalii wengi wanakuja kutembelea nchi yetu kwa kupitia michezo na imeshajidhirisha katika *Kili Marathon*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kilimanjaro, kuna ile barabara inayozunguka mlima, inanzia Rombo mpaka Ngarenanyuki, barabara ile bado hajakamilika na tumeshaanzisha *tours* kwa ajili ya watu wanaokwenda kwa baiskeli na imefanikiwa. Kinachotukwamisha ni barabara siyo nzuri na usalama bado siyo mzuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba uliangalie hili ili uweze kuiimarisha barabara ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Mheshimiwa Beatrice ambaye ameelezea kidogo kuhusu *Tanzania Tourist Board*. Ni jambo la kusikitisha, juzijuzi wamekwenda Beijing kutangaza matangazo ya utalii, lakini wameondoka wao na Wenyeviti wa Bodi. Mimi nimekuwa nikizungumza mara nyingi hapa mnawapeleka Wenyeviti wa Bodi wa nini? Wapelekeni wataalamu, Wenyeviti wa Bodi mnawalipia tiketi *business class* siyo zaidi ya dola 4,000 wanakwenda kulala kwenye *Five Star Hotel*, hata kule kwenye maonyesho hakuna kitu wanachokifanya, mnawaacha wadau ambao wanalipa fedha zao, wanachangia ile *boots* ya maonyesho, wanalipa tiketi zao, wanalipa hoteli na bado wanatafuta...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

30 APRILI, 2013

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Lucy Owena, sasa ni Mheshimiwa Grace Kiwelu, atafuatiwa na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru lakini na mimi niungane na msemaji aliyemaliza kuzungumza kwamba ninaunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani na niombe Serikali ya Chama cha Mapinduzi iifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ninaunga mkono hotuba ya Kamati kwani mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo, ninampongeza Mwenyekiti wangu kwa hotuba aliyoitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Mheshimiwa Lucy Owena kuhusu Mlima Kilimanjaro. Kwenye hotuba ya Mazingira nilisema kwamba Kilimanjaro imeingia kwenye maajabu saba ya dunia lakini niombe *TANAPA* kwamba tunaomba mgawo kwa zile Halmashauri zinazozunguka mlima kwa sababu moto unapotokea wananchi wa Kilimanjaro na hasa Halmashauri zilizopo jirani ndiyo wanaokwenda kuuzima. Sasa ifike wakati tuzisaidie Halmashauri zote zinazozunguka Mlima Kilimanjaro tuachane na misaada ya vyoo na madarasa, tunahitaji fedha ya kutosha ambayo tunaweza kupanda miti na kustawisha msitu wetu wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la ujangili. Mwenyekiti kwenye hotuba ya Kamati ameelezea kwamba tulifanya ziara ya kutembelea Hifadhi ya Katavi pamoja na Pori la Rukwa. Mimi nitaeleza matatizo tuliyoyakuta kwenye eneo lile, moja ya matatizo waliyoyasema wafanyakazi wa mapori yale pamoja na hifadhi ya Katavi ni kwanza wana upungufu wa wafanyakazi. Wafanyakazi ni wachache hasa kwa Kitengo cha Ulinzi, Askari ni wachache, hawana magari na magari yaliyopo ni mabovu, barabara ni mbovu, hawana

30 APRILI, 2013

mawasiliano ya simu, huwezi kufanya kazi kwenye mazingira kama yale ambapo mnaweza mkavamiwa lakini mawasiliano ya simu hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia walitoa changamoto nyingine kwamba kumekuwana na ucheleweshaji wa kesi au kufutwa kwa kesi. Walitutolea mfano wa kesi moja kwamba kuna watu waliokamatwa na meno ya ndovu, kesi ile ilipelekwa Mahakamani lakini cha kushangaza kesi ile ilifutwa na kibaya zaidi watu wale walioshtakiwa walirudishiwa yale meno pamoja na gari walilokuwa wanatumia. Mungu alivyo mwema, watu wale walipata ajali katika eneo la Chamwino Mkoa wa Dodoma na meno yaleyale 75 yaliyokamatwa Katavi yalikutwa kwenye gari lile pamoja na hati ya mashtaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi napenda kujua tumesema tuna dhamira ambapo sina hakika kama tuna hakika ya kweli ya kupambana na ujangili kwa sababu mtandao wao ni mkubwa upo mpaka kwenye Serikali. Sasa ninapenda kujua, Hakimu aliyeifuta kesi ile na kuwafutia mashtaka watu wale amechukuliwa hatua gani mpaka sasa? Namwomba Waziri pamoja na Waziri wa Sheria na Katiba wamfuatilie huyo Hakimu pamoja na Mwendesha Mashtaka ambaye aliwafutia kesi watu wale na kuwaambia hawana kesi ya kujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni kwamba tunapokea wageni na tunajivuna kwamba nchi yetu ni ya amani na utulivu lakini tulipewa taarifa ya kesi nyingine kwamba yupo raia mwingine wa Kichina aliyekamatwa na meno ya Simba, kesi hii ilikuwa inataka kufutwa lakini Mwenyekiti wa Kamati nimpongeze kwani alizungumza na Mkuu Mkoa na kumwomba afuatilie suala hili. Niiambie Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba hawa wageni tunaowaingiza aidha ni kwa nia njema au vipi lakini tusiwaachie bila kuwafuatilia. Sina hakika aidha simba huyu kama alichomwa sindano ya usingizi ndiyo akang'olewa meno au aliuawa. Kwa hiyo, mimi ninachotaka ni kuitahadharisha Serikali kwamba wachukue hatua na

30 APRILI, 2013

kufuatilia wageni wote wanaoingia nchini kuhakikisha wanafanya zile kazi ambazo zimewaleta. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni kuhusu suala la silaha zilizopo bandarini. Tulikutana na *TANAPA* nao wakaeleza kwa masikitiko makubwa kwamba wanashangaa *TRA* kuzuia silaha hizo bandarini. Ikiwa Majeshi mengine kama Jeshi la Polisi au Jeshi la Wananchi wanaweza kuingiza silaha hizo bila kulipia kodi ni kwa nini hawa *TANAPA* wanadaiwa kodi? Hawa wanakuja kufanya kazi ya kulinda rasilimali zetu na kulinda wanyama wetu wasiuawe na hao majangili. Kwa hiyo, tuiombe Serikali na mimi naamini kwamba Serikali ni moja, Wizara hizi pia zinafanya kazi pamoja zichukue hatua za haraka ili silaha zile ziweze kutoka bandarini zirudi kwenda kulinda wanyama wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia lipo jambo lingine ambalo walilizungumza Askari wa Wanyamapori kwamba wamekuwa wakipata matatizo makubwa pale wanapopambana na majangili, wanapotokea kuwau majangili wale kwa sababu wale majangili wanakuwa wanatumia silaha za moto lakini Askari wetu hawana *tshirt* za kuzuia risasi au *bullet proof*, kwa hiyo Askari wetu wamekuwa wakiuawa na tumeona kwenye taarifa ya Waziri wameuawa Askari 17 lakini Askari wale wakitokea kuwau majangili huwa wanashtakiwa. Sasa napenda kujua Sheria hii ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Grace na sasa nitamwita Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura akifuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu na Mheshimiwa Ali Khamis Seif ajiandae.

30 APRILI, 2013

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana lakini ili nisisahu mwishoni naomba nitamke tu mwanzoni kabisa kwamba nasikitika kuwa Mbunge wa kwanza ambaye siungi kabisa mkono hoja hii iliyopo mezani mpaka pale Serikali itakapotoa ufafanuzi juu ya yale masuala yote yaliyojiri katika katika Jimbo langu la Tunduru Kusini na Kaskazini kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Maliasili ilifanya *operation* ya malihai mwezi Novemba 2012. Katika *operation* ile, kwa kiwango kikubwa ilikuwa ni uvunjifu wa haki za haki za binadamu na kulikuwa na kutokuwa na utekelezaji wa utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu imetamka wazi rasmi kwamba mtu hawezi kuhukumiwa bila kufikishwa katika vyombo vya kutafsiri sheria ambayo ni Mahakama na vyombo vile vitoe fursa ya mtu yule kuweza kujitetea lakini *operation* hii haikuendeshwa katika misingi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *operation* ile, yalitolewa matangazo katika vijiji mbalimbali kwamba kila anayemiliki bunduki aiwasilishe ili iweze kukaguliwa. Wananchi kwa kuheshimu sheria na mamlaka zilizopo mbele yao, walikubali na wakazifikisha bunduki zile ili ziweze kukaguliwa. Cha kushangaza kile aliyepeleka bunduki ile kwenda kukaguliwa alisainishwa kwamba bunduki hii anaikabidhi Serikali na yeye mwenyewe kuwekwa Mahabusu na matokeo yake anapelekwa Mahakamani na alipofikishwa Mahakamani hakupewa hata fursa ya kujitetea, anahukumiwa kwamba akitumike kifungo miaka miwili nje ya jela. Zaidi ya wananchi 200 sasa hivi wanatumikia kifungo cha nje ilihali hawakupata fursa hata dakika moja ya kujitetea. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri atafute muda, aje Tunduru, najua alifika Tunduru lakini alidanganywa na Kamanda ambaye alikuwa anaongoza kikosi kile ambaye ni Kamanda Tossi.

Alimdanganya kwamba, amekusanya bunduki zaidi ya 300 za majangiri, ilihali bunduki zile Wananchi wamezipeleka wenyewe kwa mikono yao ili zikakaguliwe. Matokeo yake bunduki zile zikawa *confiscated*, zimekamatwa na Serikali na athari kubwa sasa hivi inatokea kwa Wananchi wa Tunduru. Wananchi wengi sasa hivi wameshauawa kwa Tembo, mazao yao mengi sana yameshaliwa, vijiji vingi mwaka huu vitakumbwa na baa la njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii haiwezi kuvumiliwa. Nashukuru nilipozungumza na Mheshimiwa Waziri, ameonesha utayari wake wa kuja Tunduru na kufanya kazi hiyo ya tathmini ili kuweza kujua nini kilichojiri katika eneo lile la Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wamiliki hawa wamenibandikia barua mbalimbali wakileta malalamiko. Kitu cha kushangaza zaidi, imefikia hata wanaomiliki bunduki za kujilinda wenyewe na bastola zimechukuliwa. Sasa sielewi kama bastola nayo inaweza ikaua Tembo ambaye wao wanamkusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache tu nitasoma baadhi ya Wananchi ambao wameniletea barua zao kuilalamikia Serikali juu ya vitendo vibaya vilivyofanywa na kikosi kile kinachoongozwa na Kamanda Tosi. Mmoja wao ni Hashim Ndeka, Rajab Ali Tumu, Hausi Hakimu Ndalamila, Gasi Mohamed Gasi, Shaibu Mussa Chande, Omari Rajab Shamri na Ahmed Khalifa Mshangama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni baadhi tu ya Watanzania wachache ambao wamedhulumiwa nafsi zao, wamefungwa kifungo cha nje bila kupata fursa ya kujitetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipouliza swali la nyongeza mwaka jana katika Wizara hii kwamba kuna baadhi ya Wananchi wa Tunduru wanapigwa, wananyang'anywa mali zao na hata wengine ambao wamekwenda kuvua samaki kwa ajili ya kitoweo wanadhalilishwa. Naibu Waziri kwa masikitiko makubwa

kutokana na majibu ambayo amepewa na wataalam kutoka Tunduru, alisema kwamba, hakuna Mwananchi yeyote ambaye amewahi kufanyiwa vitendo hivyo. Nikamwuliza je, endapo kutatokea ushahidi utakuwa tayari kuwajibika? Alichosema ni kwamba, niko tayari kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Mbunge na ikibidi niende Tunduru nikajionee mwenyewe. Kwa masikitiko makubwa mpaka leo hajafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache tu nimpe taarifa kama ifuatavyo: Tumekusanya orodha ya watu wachache tu ambao wamepigwa, wamevunjwa mikono na wengine wameuawa na operesheni hizi mbalimbali ambazo zinafanywa katika eneo letu la Tunduru Kusini.

Katika Kijiji cha Michesela kuna Wananchi zaidi ya 16 na waliopigwa mpaka kufa ni wawili; Mohamed Hesabu kwa jina la *a.k.a.* Nangukule; na Hausi Twalibu jina la utani anaitwa Mchicha. Halafu Kijiji cha Meyamtwaru ni Wananchi 16 na mmojawapo aliuawa kwa kupigwa anaitwa Jafari Amir Chikombola. Kijiji cha Kumbo ni watu kumi ambao walipigwa na kunyang'anywa mali zao. Kijiji cha Amani ni watu 12 na mmojawapo alipigwa mpaka kufa, ambaye anaitwa Hussein Salum Pasietu. Kijiji cha Nasia ni watu watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakabidhi majina haya na baadhi ya barua ambazo nimekabidhiwa na Wananchi hawa ili Mheshimiwa Waziri aweze kuzifanyia kazi.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtutura endelea, hebu Mheshimiwa Kange subiri.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sasa hivi nitaje athari chache ambazo zimetokea kutokana na operesheni hii ya mali hai ambayo Wananchi kwa ujumla hawailaani, ila namna ilivyoendeshwa ndicho wanachokilaani, kwa sababu hakuna Mwananchi yeyote wa Tanzania ambaye atakubali maliasili zetu ziporwe kwa tamaa

tu ya kibinadamu, haiwezekani. Tunacholaani ni namna oparesheni hii ilivyoendeshwa, haikufuata mfumo wa Utawala Bora na wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Wananchi kunyang'anywa silaha zao ambazo walikuwa wanazitumia kujilinda wao na mali zao kama Katiba inavyowaruhusu kwamba una haki ya kujilinda pamoja na mali zako pale tu inapoonekana Vyombo vya Serikali haviwezi kuwafikia Wananchi wale. Kijiji cha Marumba, Mzee Daudi Rashid ameuawa kwa tembo. Kitongoji cha Nakatete bwana mmoja anaitwa Mmomo ameshauawa kwa tembo na taarifa tumekuwa tukitoa kwenye Idara ya Maliasili. Matokeo yake wanafika baada ya siku tatu au nne, wanakuta yule tembo ambaye ameuwa binadamu ameshatoweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba ya watu wa vijiji mbalimbali katika Jimbo la Tunduru Kusini yameathirika vibaya sana na mwaka huu njaa kubwa itaingia katika Jimbo langu la Tunduru Kusini. Kijiji cha Mischela, Liwanga, Meyamtwaro, Chiungo, Lipepo, Chilundundu, Lukumbo, Marumba pamoja na Molani, hivi vijiji vyote mwaka huu hali ni mbaya kwa sababu Tembo wamekula mazao. Tumetoa taarifa Maliasili, lakini hakuna hata mtaalam mmoja ambaye amekwenda kufanya tathmini na kuwapa pole Wananchi wale. Wananchi wanakosa imani kabisa na Idara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hofu kama vita hii dhidi ya majangiri itaweza kufanikiwa kwa sababu licha ya silaha kuwepo au kitu gani, ninachoamini mimi uwepo wa Wananchi ambao wakishirikishwa na wakakubali kushiriki kikamilifu, naamini ujangiri utaangamia. Kitendo cha wanyama hawa kuathiri binadamu halafu Serikali ikakaa kimya isichukue hatua zozote za kuwahami wanadamu hawa, ujio wa majangiri kwao itakuwa ni ukombozi. Ndiyo maana nasema kwamba, vita dhidi ya ujangiri itashindikana kwa sababu Wananchi wanadhaliishwa sana na wanyama hawa na Serikali inakaa kimya bila kuchukua hatua zinazostahili.

Suala la Tembo kwenda kushambulia Mashamba ya Misechela, mashambulizi haya yameanza tarehe 14 lakini mpaka kufikia tarehe 27 ndipo Askari wa Maliasili wamekwenda baada ya siku 14, nusu mwezi. Wakiulizwa wanasema risasi hamna. Siku hiyo hiyo wakisikia kwamba tembo ameuawa kijiji fulani wanakuwa na risasi na mafuta ya kwenda kumhami yule tembo. Sasa kipi chenye thamani kwa Serikali, yule tembo aliyeuawa au wanadamu ambao wameiweka madarakani Serikali hii?

MBUNGE FULANI: Tembo. *(Kicheko)*

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninajibiwa kwamba tembo ndiye mwenye thamani, sasa sijui kama ni ukweli. Sera ya CCM inasema kwamba, wanadamu wana thamani zaidi kuliko mnyama. Sasa kama Wizara hii peke yake inasema kwamba tembo ana thamani kuliko wapiga kura, naomba niambiwe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii itufafanulie na ituambie ni lini bunduki za Wananchi wale ambao hawana hatia zitarudi?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Haya, tunakushukuru Mheshimiwa Mtutura, kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema sasa nitamwimta Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, lakini simwoni ndani ya Ukumbi wa Bunge. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Ali Khamis Seif, halafu Mheshimiwa Rosweeter Kasikila ajiandae.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na uzima kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaliwa utajiri mkubwa wa wanyamapori wengi na wa aina mbalimbali. Wanyamapori hawa wanaonekana katika maeneo ya

hifadhi zetu ambazo kwa sasa hivi zimefikia Hifadhi za Taifa 16 katika maeneo ya Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kuwa, pamoja na utajiri au hazina yote ambayo nchi imejaaliwa, kuna hatari kubwa ya baadhi ya wanyama kutoweka kutokana na ujangiri. Tumefikia mahali hivi sasa hata twiga ambao ni nembo ya Taifa wanauawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa wanyama ambao wako hatarini ni tembo. Katika miaka ya sitini inaeleweka kuwa Tanzania ilikuwa na tembo kati ya 250,000 mpaka 300,000. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kuna tatizo gani? Tembo ni Tatizo? Mheshimiwa Mbunge endelea, sidhani kama Tembo ni tatizo. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sensa ambayo imefanywa mwaka 2009, Tanzania ina karibu tembo 110,000. Ninavyoona mimi katika suala zima la ujangiri, Serikali nayo inasaidia suala hili kwani bado haijaamua kuondoa tatizo zima la ujangiri wa wanyamapori na hususan tembo na jamii inataka niite ndovu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Idara ya Wanyamapori iweze kuendeleza uhifadhi na kuweka doria katika sehemu za mapori ya akiba na mapori tengefu, kwa wastani inahitaji shilingi bilioni 31 kwa mwaka. Serikali kwa wastani inatoa shilingi bilioni sita kwa mwaka. Sasa ni dhahiri kuwa, Serikali nayo inachangia suala hili la ujangiri, kwa sababu tunaelewa kuwa rasilimali fedha ina nafasi kubwa katika kuweka doria katika maeneo haya ambayo ni makubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali fedha kama nilivyosema, wanahitaji shilingi bilioni 31, lakini wanapewa shilingi bilioni sita. Pia kuna rasilimali watu, ili mapori haya ya akiba yalindwe ipasavyo yanahitaji wafanyakazi 4,588. Leo wafanyakazi ambao wako katika Mapori ya Akiba na Mapori

Tengefu ni 1,155. Sasa hapa pana suala la msingi kabisa na Serikali iamue, kwell inataka kulinda wanyama hawa au vipi? Kwa sababu haiwezekani mahali panapohitajika wafanyakazi 4,588, kuna wafanyakazi 1,155, halafu tuseme Serikali iko makini katika suala zima la ulinzi wa wanyama wetu.

Hii maana yake nini? Kwa kawaida inatakiwa kila kilomita 25 za mraba zilindwe na askari mmoja, hapo inaonekana ndiyo ufanisi utapatikana. Leo kwa idadi ya wafanyakazi hawa ni kwamba, kila kilomita za mraba 157 ndiyo zilindwe na askari mmoja. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba, Serikali nayo inachangia katika suala zima la ujangiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba Idara ya Wanyamapori haizalishi fedha katika mapori haya; inazalisha, lakini Serikali wanazichukua na kile ambacho wanarejsha ni kidogo sana. Kwa mfano; katika mwaka wa 2009/2010, Idara ya Wanyamapori ambayo sehemu kubwa ya fedha zinatokana na mapori ya akiba na mapori tengefu, ilipata shilingi bilioni 28.34, hizi ndiyo fedha ambazo zimezalishwa. Matokeo yake walichobakiziwa *retention* ni shilingi bilioni 3.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010/2011, Idara ya Wanyamapori ilizalisha shilingi bilioni 31.10, walichorejeshewa ni shilingi bilioni 2.3, hata kile chao hakirejeshwi. Kwa hiyo, bado hoja yangu inabakia pale pale kuwa Serikali inachangia kabisa katika ujangiri kwa wanyamapori wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu wa magari. Doria haiwezi kufanyika kwa miguu kwa sababu ni eneo kubwa. Kuna karibia kilomita 25,000 za urefu wa barabara katika mapori ya akiba, kwa hiyo ni dhahiri huwezi kwenda kwa miguu. Wanahitaji magari 283, wanayo magari 53, wapewe na nani hawa kama siyo Serikali? Kwa hiyo, nasema ni dhahiri bado Serikali inachangia katika suala zima la ujangiri wa wanyamapori. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuwa kesi zinazohusiana na wanyamapori zinahujumiwa kwa kweli. Mifano imetajwa mingi, nami nitaje mfano mmoja; katika Kituo Kikuu cha Polisi Kilwa, kulifunguliwa kesi yenye Na. KLM/IR/498 ya mwaka 2007, yalikamatwa meno ya Ndovu kwa usalama wa kikao hiki, 46. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kesi ya uhujumu uchumi, lakini cha kusikitisha ni kwamba, meno haya 46 yalitoweka katika Kituo cha Polisi. Sasa hii inadhihirisha kuwa hawa askari wachache waliopo na kazi wanayofanya, hizi kesi zipo nyingi, meno yanatoweka. Leo kwa mfano angeliwekwa mpinzani ndani akatoweka ingelikuwa kasheshe kubwa, lakini meno ya tembo haya... *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taaluma ya wanyamapori ni maalum; hivyo, inahitaji watu maalum au waendesha mashitaka maalum. Wanyamapori wameenea nchi nzima, makosa yanafanywa nchi nzima, lakini hawa wanahitaji waendesha mashitaka wasimamie kesi hizi. Huko nako kuna upungufu vilevile. Wanahitaji waendesha mashitaka 70, lakini walionao nao ni 48. Kwa hiyo, hawa ambao hawana taaluma hiyo wanafungua kesi kwa sababu hawana utaalum huo, kesi zinavurugwa na majangiri wanakuwa hawapatikani na hatia. Kwa hiyo, inaonekana pamoja na matatizo au changamoto zote zilizopo bado Serikali ina mkono wake. Naishauri Serikali isichangie ujangili, lakini ipambane na majangili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapomalizia ni kuwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Seif, nakushukuru, muda wako umeshakatika.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nashukuru kwa nafasi hii uliyonipa ili nami niweze kuchangia mada hii. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya kawaida, tunapozungumzia maliasili, utalii, misitu na wanyamapori, huwa tunafikiria Serengeti, Ngorongoro, Lake Manyara, Mlima Kilimanjaro, Selous na Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama mbele yako nikitaka kusema kwamba, Mkoa wa Rukwa ni mzuri sana. Kwanza, kwa hali ya hewa ni mkoa mzuri sana, hali ya hewa yake ni baridi. Pia ni mkoa ulio na misitu inayovutia. Misitu hiyo Wanarukwa wanaitumia vizuri kwa ufugaji wa nyuki. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi ambavyo amehamasisha na anavyoendelea kuhamasisha juu ya ufugaji wa nyuki. Kwa kweli Katavi wanafuga sana nyuki, lakini hata Sumbawanga Vijijini na Kalambo wameanza kufuga nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia kuhusu Ziwa Rukwa; Ziwa Rukwa lina kina kifupi sana kuliko maziwa yote duniani, lakini lina mamba wengi sana kuliko maziwa mengine yote duniani. Sasa sielewi kama Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Wizara hii, walipokuwa wanafanya sensa sijui kama walienda kuhesabu wale mamba kwenye Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Ziwa Rukwa lina samaki wazuri aina ya kambale, ni samaki ambao hata minofu yake ingeweza kuuzwa mpaka nchi za nje. Ukienda sehemu ya Ziwa Rukwa, Wananchi wanasema sana kwamba wale kambale minofu yake inaweza kutumika hata kwa kutibu ugonjwa wa kansa. Kwa hiyo, ninasema ni changamoto kwa Taasisi ya Utafiti ili waende kufanya utafiti kama kweli wale kambale wanaweza kutibu ugonjwa wa kansa *then* itakuwa imetusaidia sana Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiachana na Ziwa Rukwa; Wilaya ya Kalambo ina msitu mzuri sana wa Mbizi. Ule msitu

umesheheni mbega wekundu kwa wingi sana. Kwa hali ya kawaida, tumezoea kuona mbega weupe, weusi waliochanganyika na rangi nyeusi na nyeupe, lakini ukienda Kalambo kwenye Msitu huu wa Mbizi utawakuta mbega wekundu. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kulitangaza eneo hili kama halikufahamika tusiwe tunafikiria tu Ngorongoro labda na Lake Manyara na Mikumi, lakini Kalambo pia kuna vivutio vizuri sana vya utalii, ambavyo kama Serikali itachukulia maanani basi vitasaidia kuiingizia nchi yetu Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo msitu tu lakini kuna maporomoko mazuri sana ya Kalambo, kuna maporomoko ya Lwanji, kuna maporomoko ya Kibwe, ambayo ni mazuri sana. Yakitengenezwa vizuri itakuwa ni vivutio na tutapata watalii wengi sana kule Wilaya ya Kalambo, Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kalambo kuna eneo zuri sana, ardhi yake ni kama ya lhefu, ukitembea mwenyewe utashangaa. Ni eneo ambalo ukikanyaga ni kama unakanyaga zulia, ardhi inadidimia na kupanda. Kwa hiyo, ni kivutio kimojawapo ambacho kama kitatiliwa maanani na Serikali, basi kitauingizia Mkoa wetu wa Rukwa na nchi yetu kipato kizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo Manyara kulipo na chemchemi ambayo ni ya maji moto ambayo hata unaweza ukachemsha yai ukitaka, lakini kule Kalambo kuna eneo linatoa maji ya moto ambapo unaweza hata ukaweka kiasi baada ya dakika 15 kikawa kimeshaiva na watu mkala. Kwa hiyo, vivutio katika Mkoa wa Rukwa vipo vingi sana. Ninachotaka kusema ni kwamba, labda kumesahaulika hakufanyiwi kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ombi Wizara iende mpaka Mkoa wa Rukwa, Wilaya ya Kalambo, kwenda kushuhudia vivutio hivi vya utalii. Ni vivutio ambavyo vingeweza kutuingizia pato kwa Mkoa wa Rukwa, vikatuinulia uchumi, lakini na kwa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna misitu huko Kalambo ambayo ina sokwe mtu, hakuna asiyemfahamu mnyama sokwe mtu, kila mtu anamfahamu, lakini maeneo mengi wanyama hawa wameanza kupotea. Sokwe mtu ni wengi sana, kiasi ambacho sasa hifadhi yake ipo lakini ulinzi siyo makini kwamba, Wananchi wameanza kuwaua watapotea, watatoweka kwenye uso wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naleta ombi tu kwa Wizara husika kwamba, tunaposhughulikia utafiti na kutangaza maeneo ya utalii, tusipofikiria kwamba Kilimanjaro labda na Manyara na Ngorongoro, Mikumi, lakini Rukwa kuna vivutio vingi sana na vizuri sana ambavyo vingeweza kutuingizia Pato la Taifa. Ukiangalia ni vivutio ambavyo vipo mpakani. Kwa hiyo, tusipoangalia kama Maporomoko ya Kalambo yanatembelewa sana na watalii kupitia Zambia, lakini upande wa kwetu Tanzania bado hakujashughulikiwa vizuri na hakujatengenezwa vizuri ili watu waweze kwenda kuangalia na maeneo yale yakaendelea kutangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ila nilikuwa najaribu kutangaza vivutio vilivyoko kwetu Rukwa kwamba nako watu wanaweza wakafika na wakaweza kutembelea na wakafurahi, wakatuachia fedha tukainua uchumi wa Mkoa wetu na kwa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii muhimu ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naanza kwa kuunga mkono hoja. Kwa sababu katika ukurasa 41 katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imenifurahisha sana. Nimeona kwamba amekusudia kukusanya bilioni 4.7, makusanyo ambayo yatasaidia Miradi mbalimbali katika Mfuko wa Misitu. Pamoja na hilo, nimeunga mkono hoja hii katika fedha hizi naomba nitoe maombi kwa Mheshimiwa Waziri kwamba, katika shilingi bilioni nne, namwomba atenge shilingi bilioni

moja kwa ajili ya matumizi ya madawati katika Wilaya ya Mufindi. Sisi kule watoto wanakaa chini na ni aibu kubwa sana hata kwa Serikali na hata kwa sisi Wabunge kuona mbao zinatoka pale msituni halafu watoto wanakaa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi kama Mbunge, ninawakilisha Wananchi na bahati nzuri katika mahesabu yako umeshatenga shilingi bilioni nne kwa ajili ya matumizi mbalimbali; naomba utenge shilingi bilioni moja kwa ajili ya madawati tu. Unaweza ukatuletea madawati sisi tukagawa katika mashule. Nimefanya hesabu ndogo ya haraka haraka, maana yake tunaweza tukapata madawati kama 24,000 hivi, yale madawati yatasaidia sana katika shule zetu za msingi katika Wilaya ya Mufindi kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, sidhani kama Mfuko huu ndiyo umeanza sasa hivi, kwa sababu Mheshimiwa Waziri amesema watafaidika na watu binafsi. Mimi katika Wilaya yangu kuna watu wengi sana wanapanda misitu, sasa kwa sababu umelenga kwamba utasaidia, nadhani katika bajeti hii tutakapokuja mwakani watu wengi watakusifu kwa kuwasaidia kutokana na Mfuko huu ambao fedha hizi umeshatenga hapa kwa ajili ya kuwasaidia wale watu wanaopanda misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda niliongelee ni kwamba, nadhani Mheshimiwa Waziri ulikuja kule Mufindi, tukaongea sana masuala ya ardhi kuhusiana na mipaka. Bahati nzuri katika Hotuba yako ulieleza vizuri sana na Wananchi wakulielewa vizuri sana. Sasa katika vile vijiji ambavyo Serikali ilikubali na tulitembelea ile sehemu tukaona kuna sehemu inabidi Wizara iwaachie Wananchi. Naomba Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ya kuhitimisha hoja, awaambie wale Wanamufindi maana wanamsubiri kwa hamu sana, ile mipaka aliyoiangalia; kwa mfano, Kijiji cha Ihomasa, Kijiji cha Kilolo, Kijiji cha Udumka na Kata ya Kibengu, Serikali imesema waendeleo kulima tu wasiwe wanapata njaa na mifugo waendeleo. Wananchi wanamsubiri sana Mheshimiwa Waziri wakati anatakupokuwa ana-*wind up* hapa watamsikiliza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Serikali ilifanya tathmini na sisi tukiwepo pale na tukaona ni heri Serikali iwaachie Wananchi kwa sababu Sheria ya mwaka 1972, sijui mwaka 1974, wakati watu hawajaongezeka, sitaki kuelezea sana Wabunge wengine hapa wameeleza kwamba, watu wameongezeka. Bahati nzuri kwetu sisi Wilaya ya Mufindi kuna maeneo makubwa ambayo imeachiwa Wizara ya Maliasili na Utalii, kuna sehemu nyingine hata miti haijapanda, sasa itakuwa ajabu kung' angania sehemu wanayokaa watu wakati kuna sehemu nyingine hata miti hamjapanda. Sasa sisi tunategemea wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha hoja atatoa kauli nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kuna *mission* moja pale Kibengu, wakati tupo kwenye mkutano, *sister* alisimama alieleza vizuri sana. Sasa itakuwa ajabu maana kazi ya *sister* ni kutuombea sisi Wabunge na Watanzania wote, ndiyo maana tunasimama tuna afya. Itakuwa ajabu sana Serikali inaenda kunyang'anya maeneo ya masista wakati masista kazi yao ni kutuombea sisi na wanatoa huduma ya hospitali kwa ajili ya watoto wetu na sisi tunaugua tunakwenda kutibiwa pale, halafu leo badala ya kwenda kuomba anaenda kuongea na Serikali kwa ajili ya ku-*bargain* mipaka. Hicho kitakuwa kitu cha ajabu, nadhani wale masista unawaambia wasiwe wanaenda kusali. Wewe unawaambia waendeleo tu kusali ile mipaka umeshawaachia, ile ni sehemu ya miaka mingi na wanatoa huduma kubwa sana kwa Wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka niliongelee hapa ni kuhusiana na upasuaji wa mbao. Bahati nzuri msitu ule sawa na Msitu wa Serikali, hilo tunakubaliana, lakini unamilikiwa na watu wa Mufindi. Kwa sababu msitu hauwezi ukafumuka tu, msitu una *process* ndefu sana mpaka upate msitu nadhani mvua zinanyesha sehemu nyingine, lakini watu wengi wanashindwa kupanda misitu. Mwitikio wa watu wa Mufindi wameshapanda misitu kule, pamoja na kwamba ni mali ya Serikali. Huwezi kusema hii ni mali yako, tunasema ni mali ya wote, pamoja na wale waliopanda kwa sababu nao ni Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kusema hapa, tukipiga hesabu ya haraka haraka, kwa sababu msitu unakatwa mbao halafu unapanda mti na unaendelea kukua, unatunzwa ndani ya miaka 20 mpaka ufikie umri wa kuvuna. Sasa ninachomwomba, Mheshimiwa Waziri, afanye hesabu ndogo sana, wale wenyeji wanaotunza misitu kule wapate asilimia 70 ya upasuaji. Halafu wale ambao hawatunzi wanakuja tu kwa ajili ya kupata masilahi, wapate asilimia 30. Nadhani siku ile tuliongea vizuri sana na bahati nzuri ulitoa hotuba nzuri sana. Kuna jambo lingine linataka kujitokeza ambalo siyo zuri, mimi kama Mbunge naomba nikushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, mwaka huu Mheshimiwa Waziri anataka kuja na *format* mpya, *si-discourage format* yako, lakini amesema kwamba, atatoa kwenye vikundi. Sikatai asitoe kwenye vikundi, lakini nataka nitoe ushauri kwamba, watu ambao wameji-*organize* kwenye vikundi, wapo kwenye vikundi, kuna wengine ni matajiri wapo pale Mafinga wanapasua misitu, wana mashine zao hawawezi kujiunga na mtu mwingine. Kwa hiyo, aseme kwamba, kuna vikundi, kuna watu binafsi, kuna viwanda vikubwa, kuna viwanda vidogo vidogo, watu wawe huru wapatiwe wafanye kazi. Akisema vikundi; je, yule ambaye hana kikundi na ana mashine na ameshaajiri watu itakuwaje? Hili litaleta mgogoro mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iwe *fair* tu, hii ya kujibana bana mara sheria hizi sijui mnaokota wapi inaleta sheria. Hebu tengenezeni msimamo kwamba wapasu mbao, utaratibu ni huu. Wale watu watoe kodi siyo bure, hiyo italeta mlolongo mzuri sana. Ukisema ni vikundi, kumbe unataka watu wajitoe wenyewe halafu unasema hajaunda kikundi halafu hujampa mgao wake, italeta tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, ile ya kusema vikundi aachane nayo, kama kuna watu wameji-*organize* sawa wape kwenye vikundi, lakini kama kuna watu binafsi wameomba wape. Kuna watu wanategemea kuishi kwa njia ya biashara ya msitu, sasa usipowapa pale italeta shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishasema kwamba, kuna vijana walishajunga katika vikundi, wale waliotoka kwenye vikundi wanaleta shida kubwa sana, kwa sababu mpaka leo wengine wameandika maombi miaka mitano hawajapata. Mheshimiwa Waziri, naomba hilo uliangalie vizuri sana kwa sababu isije ikatuletea shida tena katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu jambo lingine ambalo napenda niliongelee ni shida ya misitu. Naomba Waziri wakati anahitimisha hoja yake hebu aweke *format* nzuri, siyo kila mwaka tunapoingia ndani ya Bunge tunaongelea vibali. Kila mwaka tukija vibali, hii inakuwa siyo nzuri sana. Kwa nini msitengeneze *system* ambayo kila Mwananchi anaridhika na pale inapoleta shida kubwa sana kwa Wananchi wanavyolalamika wanasema kwanza waliacha maeneo ambayo ni *reasonable* waliichia Wizara iendelee kupanda misitu. La pili, wenyewe ndiyo wanaopanda ile miti. La tatu, wenyewe ndiyo wanaolinda mti ile mpaka inafikia umri wa kuvuna siyo kazi ndogo ni kazi kubwa sana. Sasa kwa nini Serikali isiwafikirie?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri; nilisema kuna vijiji vimezunguka msitu pale, hivi katika kijiji chenye watu 800 ukatoe kibali kimoja au viwili kuna tatizo gani? Kwa mfano, mwaka jana vimepewa vijiji 12, sasa vijiji ambavyo vimezunguka pale vipo kama 50 hivi, ukisema katika vibali 600 ukatoa vibali 50 kwenye vijiji vinavyozunguka msitu hakuna tatizo; kwa sababu utakuwa umewasaidia watu wengi sana.

Sasa ninakuomba Mheshimiwa Waziri mwaka huu vijiji ambavyo vinazunguka msitu wapewe vibali tena, hata ukitoa kibali kwa kwa kila kijiji kimoja kimoja inasaidia, ingawa mimi katika mapendekezo yangu nilikuwa nasema vibali viwili viwili. Kufuatana na ufinyu wa vibali, ninakuomba hebu toa kibali kimoja kimoja kwa vijiji vinavyozunguka msitu, utakuwa umesaidia vijiji vile. Vile vijiji siyo kwamba wanafanya biashara, wakipata zile fedha ambazo zinatokana na msitu wanaanza kujenga shule, wanajenga zahanati, kuna matumizi mengi sana yanasaidia pale kwenye jamii.

Namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo kwa umakini sana, ndiyo maana nimesema kwa leo ninaunga mkono hoja bila tatizo, kwa sababu ninajua ukisimama hapa kwanza hotuba yako lazima uongeele Mufindi, usipoiongelea Mufindi maana yake sisi tunaanza upya mjadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Kigola. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Felister Bura na naomba Mheshimiwa Dunstan Mkapa ajjandae.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza, natoa masikitiko yangu makubwa sana kwa Bunge hili, kumjadili mtu ambaye hayana uwezo wa kuingia humu ndani kujitetea, huku ni kumwonea. Kwa kweli Mheshimiwa Kinana, ameonewa vya kutosha, lakini anaonewa hivyo kwa sababu hana uwezo wa kuingia humu ndani ya Ukumbi na kujitetea kwa yale yote yaliyozungumzwa dhidi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja hii. Naomba ku-*declare interest* kwamba, mimi ni mdau katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, kuwapongeza sana Wafanyakazi wa Maliasili, kwa kazi kubwa wanayoifanya na kwa Maaskari wa Wanyamapori kufanya kazi katika hali ngumu, isiyoweza kuelezeka kwa sababu fedha hazitoshi zinazopelekwa katika hifadhi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wachache hawana vitendea kazi, hawana magari ya kutosha, magari yaliyopo ni chakavu, wanapambana na majangili wenye silaha za kivita na wao wenyewe hawana silaha za kivita. Pamoja na hayo, hata silaha ambazo Serikali imejitahidi ikanunua, bado

TRA wakaona kwamba haiwezekani kutolewa Bandarini pasipo kulipiwa ushuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namsihi Waziri wa Fedha, kabla hatujamaliza Kikao cha Bunge, atuambie kama silaha hizo zimeruhusiwa kutoka Bandarini au bado hazijaruhusiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu wanafanya kazi katika hali ngumu sana. Nadhani Waheshimiwa Wabunge wengi wetu hatujapata muda wa kutembelea hifadhi zetu au mapori ya akiba tukaona hali halisi ya wafanyakazi, maaskari wa wanyamapori katika maeneo yao ya kazi. Mngeona hata bajeti hii isingepita bila kuongezewa fedha. Hiyo *retention* ambayo inatakiwa kurudi kule wanatafuta fedha wanapeleka Hazina, lakini hiyo *retention* inayotakiwa kurudi kama inarudi ni robo. Mara nyingi *retention* hiyo inachelewa kwa muda mrefu sana. Maslahi ya maaskari wa wanyamapori hayazingatiwi, lakini siyo kwamba ni Wizara hapana, ni Hazina ambao hawajali hali halisi ya wafanyakazi wa wanyamapori katika maeneo yao ya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Sekretarieti ya Utumishi, Wizara ya Afya, wamepewa kibali cha kuajiri watumishi, Wizara ya Elimu na Mafunzo pia wamepewa nafasi ya kuajiri watumishi, lakini sijasikia kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii na wana upungufu mkubwa wa askari wa wanyamapori. Kuna Chuo cha Pansiasi pale Mwanza, kuna vijana wengi tu ambao wamemaliza chuo pale hawana ajira. Kuna vijana ambao wamemaliza JKT hawana ajira. Nilitegemea Wizara hii kutokana na hali halisi ya upungufu wa wafanyakazi katika maeneo yao, wapewe nafasi za ajira hasa kwa maaskari wa wanyamari. Tusitegemee kwamba, tutapata asilimia 17 ya *GDP* kama tembo wataendelea kuuawa katika mapori yetu, wanyama wataendelea kutoroshwa katika mapori yetu, ndovu wataendelea kutoroshwa katika mapori yetu, na kama hawatakuwa na magari, hawatakuwa na silaha za kisasa kama majangili walivyo na silaha za kisasa. Ipo siku hii asilimia 17 itashuka kama hawataangaliwa watumishi hawa ambao wapo katika maeneo ya hifadhi ya wanyamapori. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahamasishe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kuingia kwenye hifadhi ni shilingi 1,500, sidhani kama kuna anayeweza kukosa shilingi 1,500 akaenda kuangalia mambo mzuri, vivutio vizuri ndani ya hifadhi zetu. Nawahamasisha Wabunge wenzangu hebu twende tukaangalie vivutio tulivyonavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze *TANAPA* na Ngorongoro kwa kazi kubwa walizofanya maana bila matangazo yao wala tusingeingia kwenye maajabu saba ya dunia. Ngorongoro, Serengeti na Mlima wa Kilimanjaro, isingeweza kuingia kwenye maajabu saba ya dunia. Imeweza kwa sababu ya juhudi kubwa zilizofanywa na wenzetu wa *TANAPA*, Ngorongoro na Bodi ya Utalii. Pamoja na juhudi hizo Ngorongoro hawana Bodi. Ngorongoro hawana Mhifadhi Mkuu, Mhifadhi Mkuu aliyepo anakaimu na ameshakaimu karibu zaidi ya mwaka, kama hafai muwekeni mwingine, kama anafaa mpeni hiyo nafasi. Mnawapa kazi ngumu kufanya kazi bila ya Uongozi wa Bodi, bila Mhifadhi Mkuu ni kuwaonea. Ninaiomba Serikali ione namna ya kupata Bodi ya Ngorongoro na pia Mhifadhi Mkuu aweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makumbusho ya Taifa sijui wanajitangaza vipi na wao pia hawana Bodi, hawana fedha za kutosha. Makumbusho ya Taifa ni muhimu sana kwa Taifa letu, kuna mambo mengi sana ya kujifunza pale, lakini hawajitangazi, anayewajua ni nani zaidi ya Wabunge na wafanyakazi walioko katika Wizara hiyo? Hata wanafunzi wanatakiwa kwenda pale kujifunza mambo mengi ya Makumbusho, lakini hawawezi kwenda kwa sababu Makumbusho hawana namna ya kujitangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kwa kifupi suala la misitu. Idara ya Misitu sijui kama wanafanya kazi vizuri, sielewi, Mheshimiwa Waziri ataniambia. Mbao zinazokatwa bila vibali ni tani nyingi mno, itafika wakati hatutakuwa na misitu. Kuna siku nilipita Barabara ya Itigi kwenda Tabora, nilishangaa kweli, lakini hata ukienda Rungwa kule utashangaa misitu inavyofyekwa. Sijui Idara ya Misitu

inafanyaje kazi zao, sijui kama wana ufinyu wa bajeti na wao, sielewi? Kama wana ufinyu wa bajeti, Serikali iangalie namna ya kuwasaidia. Tunapanda miti lakini na misitu inakatwa na bado tunalilia mambo ya ukame, ukame hauwezi kwisha kama misitu inakatwa ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala la ufugaji wa nyuki. Idara ya Ufugaji wa Nyuki bado elimu ni ndogo sana kwa Watanzania. Kufuga nyuki kunahitaji utaalam mdogo na fedha kidogo tu, mtaji mdogo sana, lakini Watanzania hawajaelewa faida ya kufuga nyuki, kwa sababu hiyo elimu haienezwi kwa Watanzania, ingekuwa inasemwa Watanzania wengi wangepuga nyuki, lakini hawafugi nyuki kwa sababu hawana elimu ya kufuga nyuki. Hapa Dodoma Mwalimu wetu ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye anafuga nyuki katika Manispaa yetu, anatusaidia. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitakuletea vijana waliomaliza *UDOM*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana naona hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu alishakuwa anakusikiliza sana, basi unaweza tu kumwona ofisini ili kumaliza hiyo hoja ya kupeleka hao wanafunzi wa Vyuo Vikuu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Dustan Daniel Mkapa na Mheshimiwa Sylvester Mabumba ajiandae.

MHE. DUSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote, naomba nitamke wazi kwamba, naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilayani Nanyumbu kuna mgongano mkubwa sana kati ya wanyamapori na binadamu na wanyamapori hawa hasa ni ndovu. Wilaya ya Nanyumbu imekuwa ni mapitio ya ndovu kutoka Selous kwenda Msumbiji na kutoka Msumbiji kwenda Selous. Kwa

hiyo, maafa mengi yanatokea, ndovu hawa wanafanya uharibifu mkubwa na huko nyuma niliwahi kutoa taarifa kwamba, siku moja ndovu hawa katika Kata ya Sengenya waliua watu wawili, lakini vilevile katika Kata ya Masugulu mama mmoja aliuawa wakati anakwenda kutafuta maji. Kwa hiyo, mgongano huo umekuwa mkubwa sana, lakini tatizo kubwa ni Idara ya Maliasili ya Halmashauri ya Wilaya Nanyumbu kukosa vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu haina gari kwa ajili ya Idara hii ya Maliasili. Kuna wakati niliomba gari kwa Waziri aliyepita wakati ule alikuwa Mheshimiwa Shamsa Mwangunga na alinipatia gari moja. Lile gari lilikuwa siyo jipya, lilikuwa limeshaanza kutumika lakini namshukuru lilisaidia kwa kiasi fulani lakini sasa hivi gari lile limeharibika. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, nakuomba unapohitimisha hotuba yako, utamke wazi kwamba, unatupatia gari Wilaya ya Nanyumbu ili Wafanyakazi wale waweze kupata gari la kufanyia kazi na kufanya doria hasa kwa sababu ndovu ni wengi sana Wilayani Nanyumbu. Pia kuna tatizo la uhaba wa Wafanyakazi wa Idara ya Wanyamapori, wako wachache na silaha vilevile ni chache na risasi vilevile ni chache. Naomba sana nimwombe Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu sana, Mheshimiwa Kagasheki utuone kwa jicho la huruma Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna mahusiano ambayo siyo mazuri kati ya Wafanyakazi kwenye hifadhi mbalimbali zilizopo Wilayani Nanyumbu na Wananchi wanaozunguka hizo hifadhi. Sehemu kama Mpombe, Chimika na maeneo mengine, kila mara panatokea tafrani kati ya Wafanyakazi wa hayo maeneo na Wananchi. Kuna wakati Ofisa mmoja wa Maliasili aliuawa na Wananchi kwa sababu ya mahusiano haya haya mabaya. Hivyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri uhimize mahusiano mazuri kati ya Wananchi na Maafisa wanaofanya kazi kwenye hifadhi mbalimbali Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilayani Nanyumbu tuna utalii siyo wa wanyama na wala siyo wa mbuga, kule tuna utalii wa ngoma. Tuna ngoma za asili kule ambazo kama watalii wangukuwa wanaletwa Wilayani Nanyumbu, Serikali au Taifa lingeweza kuingiza mapato. Kuna ngoma nyingi tu, kuna tepete, kuna subira na mashambura na nyinginezo. Tunaomba sana watalii wanapofika wawe wanaletwa Wilayani Nanyumbu waone ngoma zetu za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la wanyama waharibifu; tumbili na nyani. Nimekuwa nikiulizwa na Wananchi wakati nawatembelea kwamba hivi hawa nyani mbona wamekuwa wengi na hatuna zana zozote za kuwapunguza. Huko nyuma tulikuwa na utaratibu wa kupatiwa nyavu za kuweza kuwaua hawa wanyama, sasa hivi nyavu zile hazipatikani na mara nyingi Wananchi walikuwa wakiniagiza niwasaidie nyavu. Mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri, hebu waagize wafanyakazi wako katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii, watembelee Nanyumbu waone ni jinsi gani wanaweza kutusaidia kuwaondoa hawa wanyama waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi kwenye Mto Ruvuma ni tatizo kubwa sana. Wananchi wananyanyaswa, wanapigwa kwa sababu ya kujipatia kitoweo tu ndani ya Mto Ruvuma. Ule mto mbona siyo wetu peke yetu ni pamoja na Msumbiji, wenzetu wa Msumbiji mbona wanavua hawana matatizo yoyote imekuwaje Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu wapate manyanyaso hayo? Naomba sana jambo hili lifikiriwe, Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu waruhusiwe kuvua samaki ili waweze kujipatia kitoweo.

Ndani ya Mto Ruvuma kuna mamba wengi sana. Miaka miwili ya nyuma nafikiri walifanya sensa na wakapunguzwa, lakini bado wanazaliana kwa kwenda mbele. Naomba sana tusaidiwe kupunguza wale mamba wanaua Wananchi, wanawapa vilema vya kudumu Wananchi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atusaidie kupunguza wale mamba kule Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nikiwasiliana mara kwa mara na Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu ahadi ya Serikali, ambayo ilitolewa na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii katika Vijiji vya Masuguru na Chimika. Alipotembelea kule alitoa ahadi ya kuchangia shilingi milioni sita kwa ajili ya uchimbaji wa visima katika maeneo haya niliyoyataja. Ni aibu mpaka leo hii Wizara ya Maliasili na Utalii haijaitimiza ile ahadi, inaonekana kwamba Mbunge amekula au Mkuu wa Wilaya amekula, wakati ahadi hiyo hamjaitimiza ninyi Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kikundi fulani kimeandika barua kwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Kikundi hiki ni wafanyabiashara wa mbao za kutoka Msumbiji kupitia Kituo cha Mtambaswala. Wao wanadai wananyanyaswa sana, wanadhulumwa sana, mbao zao nyingi zimekamatwa na hawajui hatma ya hizo mbao na hatma ya mapato yao. Wanadai kwamba, pale Mtambaswala wananyanyaswa na Maafisa Huduma za Misitu Kanda ya Kusini.

Nadhani barua hiyo ameshaipata Mheshimiwa Waziri na kama hajaipata mimi nimepewa nakala yake hapa naweza kumkabidhi. Naomba alishughulikie suala hili, Wananchi hawa wa Mtambaswala wananyanyaswa sana, mbao zao hawakati huku kwetu Tanzania, mbao zile zinatoka Msumbiji hasa taratibu tu za pale Mtambaswala ndiyo zimekuwa ngumu kama walivyosema kwa sababu ya kunyanyaswa na Maafisa Huduma za Misitu Kanda ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nanyumbu inarina sana asali, lakini katika zana duni na utaalamu duni. Ninaomba sana Wizara itusaidie Wananchi wa Nanyumbu hasa wale wanaofuga nyuki, waweze kupata elimu bora na zana bora ili waweze kujipatia kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nimwite Mheshimiwa Sylvester Mabumba, atafuatiwa na Mheshimiwa John Paul Lwanji.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Naomba niende moja kwa moja kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Nianze kusema kwamba, mchango wangu wote utajikita kwenye Sekta za Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi hapa wameelezea namna ambavyo ujangili unavyoathiri Sekta ya Utalii, namna ambavyo wanyama wetu wanavyoawa na mwisho wa siku huenda Taifa hili likawa halina tembo kabisa hata faru vilevile. Kwa hiyo, ningependa niishauri Wizara kukiri kuzidiwa siyo unyonge, inawezekana askari wa wanyamapori wamezidiwa hawawezi tena kufanya kazi hii ya kulinda wanyama wetu na kwa vile tunaamini wakati huu nchi yetu ipo katika amani na nchi jirani zote ukiachia sehemu ndogo ya Malawi.

Ninashauri Jeshi la Wananchi na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama vitumike kwenye Operesheni Chakaza Majangili ili kulinda wanyamapori wetu. Watalii wengi wanakuja kwa ajili ya kuona wanyamapori ambao ni hai siyo ambao wamehifadhiwa katika *zoo*, kwa vile tunapoachia jambo hili wanyama wakateketea basi huenda sekta nzima ya utalii ikaathirika vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kufanya *comparative studies* kuangalia utalii wa Tanzania na nchi jirani kama Kenya, Mauritius, Seychelles, Namibia na hata Zimbabwe. Ukiangalia nchi hizo Sekta ya Utalii imeendelea sana. Sekta ya Utalii ina mchango mkubwa ambao tunaweza kusema kwa Kiingereza *multiply, effect* yake ni kubwa; ina *backward and forward linkages* na sekta zingine mfano kwenye kilimo kwa sababu watalii wakija watahitaji chakula, barabara nzuri, huduma nzuri za afya na kitoweo kizuri kama samaki na nyama. Kwa vile vitu hivi vyote vinanufaika panapokuwa na sekta iliyoendelezwa ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utalii wa Tanzania, naweza nikasema ni kama ule wa mwaka 1947 wa *Friendship First*, kutafuta marafiki zaidi kuliko kuangalia faida na baada ya miaka 50 ya Uhuru wetu, naamini tungehitaji utalii wa kiuchumi zaidi kuliko utalii wa kirafiki. Sekta hii ya Utalii kwa nchi ambazo nimezitaja, utalii umechangia sehemu kubwa ya Pato la Taifa katika *foreign earnings*, lakini vilevile imechangia kwenye ajira na imeweza kuchangia kuwa na uchumi endelevu na hasa wakati huu tunaposema kwamba mabadiliko ya tabianchi kilimo sasa hakina tija, lakini Sekta ya Utalii kama tutaiangalia kwa makini uchumi wetu utaweza kuwa imara zaidi.

Sekta ya Utalii inasaidia kufanya ile *balance of trade* kwa sababu sisi hatuwezi kuuza zaidi, lakini tunapokuwa na utalii mzuri, watakuja wageni wengi zaidi watachangia kuziba ile *deficit* ya biashara zetu baina ya sisi na nchi za nje. Kwa hiyo, naishauri Serikali kupitia Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwamba, tuachane na utalii wa mwaka 1947.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwamba ukipitia Kitabu cha Hotuba cha Mheshimiwa Waziri, yale malengo waliyokuwa wamejipangia kukusanya maduhuli, unakuta wako chini ya asilimia 50, lakini Wizara haisemi ni kwa sababu gani. Mfano, wamesema walilenga mwaka 2012/13 mpaka mwezi Machi kukusanya shilingi bilioni 11 wakakusanya shilingi bilioni mbili, sawa na asilimia 24; hii ni aibu. Sekta ambayo ingeweza kusaidia nchi yetu leo makusanyo yake yako chini na hatujaambiwa sababu yake ni nini. Naomba Mheshimiwa Waziri akija hapa atuambie sababu yake ni nini hasa makusanyo kuwa kidogo. Aliambie Bunge lako Tukufu kwamba, pengine kwenye Wizara yake kuna mchwa na kama kuna mchwa awaondoe awasafishe. Mimi naamini Mheshimiwa Waziri na Naibu wake ni wachapakazi sana, Wizara hii ina watendaji ambao wamekubuhu kwa rushwa, ni mchwa wanaotafuna fedha za umma awaondoshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Sekta ya Utalii ingechangia kwenye huduma bora za afya, lakini Serikali haikusanyi vya kutosha; huduma za afya ni mbovu, vilevile

kwenye elimu unakuta huduma zake ni mbovu, watoto wanafeli kwa sababu hawana vitabu, hawana maabara za kutosha ambazo zina vifaa, matokeo yake wanafundishwa kwa nadharia bila vitendo, ni kwa sababu Wizara hii ambayo naamini ingeweza kutumia kunyanyua uchumi wetu, haijafanya kazi ya kutosha. Naomba Mheshimiwa Waziri, asimamie kuondoa mchwa kwenye Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii, ukiangalia kwa makini ni Wizara ambayo kwa nchi yetu kuna vitu vingi sana hata watalii wanaweza kuja. Ukiangalia kuna kitu kinaitwa *Conference Tourism*, tunasema Arusha ni Geneva ya Afrika. Mheshimiwa Waziri atatuambia ni wageni wangapi walihudhuria mikutano ambao walifika Tanzania katika Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha na kumbi zingine za Kimataifa, waliingiza fedha kiasi gani? Kama kweli wataalamu wake wanafanya kazi. Vilevile kuna Watalii wanakuja Tanzania kuharibu mazingira yetu, katika ile *package tourism* watu wanalipa Ulaya wanakuja Tanzania kuharibu mazingira tu; ni mikakati ipi Serikali yetu kupitia Wizara yetu hii inafanya uchunguzi kuonesha kwamba watalii wanaokuja Tanzania wanakuja kulipa ipasavyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wengine kwamba, wenzangu tuhakikishe kuwa Maliasili zetu hizi zinalindwa ipasavyo. Nilipata nafasi ya kwenda Butiama kwa Marehemu Baba wa Taifa, ni Watalii wangapi wanaopita Serengeti wanafika pale Butiama na hata kuweza eneo lile likaingizwa kwenye zile *package* za Utalii ili pamoja na kufika kwao pale fedha wanazolingiza zitumike kuhifadhi eneo lile.

Baba wa Taifa jina lake ni mvuto kwa watu, lakini Wizara hii haija-*promote* vya kutosha eneo la Mwintongo na pale pana Maktaba nzuri sana, kazi za Mwalimu ukiingia pale utakuta kuna vitabu kama 8,000 amevisoma na kuvi-*sign* mwenyewe. Sasa ni namna gani tunaweza kuwashawishi Watalii wakafika eneo lile. Vilevile Watalii wanapenda kutembelea Fukwe, tunaposema kuwa Tanzania ni nchi ya Kilimanjaro na Zanzibar ni namna gani tumeweza kutumia kutangaza Zanzibar kwenye Vyombo vya Kimataifa vya

Habari? Unapotumia kipindi cha Zamadamu cha *TBC*, mimi nina wasiwasi kama *TBC* inaangaliwa na watu wengi; ninashauri kuwa tutumie redio na *TV* kubwa za Magharibi, pamoja na magazeti makubwa ya Magharibi. Leo hii utashangaa, Mheshimiwa Waziri au Katibu Mkuu anakwenda kukesha London kui-*promote* Tanzania; huo utaalamu wa ku-*promote* nchi yetu anao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwatumie hawa wataalamu wetu kufanya kazi, kwa sababu ni lazima tuheshimu taaluma za watu. Waziri ni Mwanasiasa, lakini kuna wataalamu ambao wamesomea, wamebobeza, tuwatumie ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, ninaunga mkono hoja ahsante. (*Makofi*)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie juu ya hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Wakati tunapata Uhuru tulikuwa watu takriban milioni tisa, lakini leo tuko zaidi ya milioni 43 au 44 na nchi yetu huwezi kusema kuwa inapanuka mipaka yake ni ileile. Tatizo ni kwamba, hatujaainisha vizuri tuone jinsi tunavyoweza kukaa pamoja na mbuga zetu au Hifadhi zetu tulizonazo. Mimi nina vijiji vingi katika Jimbo langu ambavyo vipo kandokando ya Mpori ya Rungwa, Muhesi na Kizigo.

Katika vijiji hivi kuna Kijiji cha Rungwa, Kintanula, Mwamagembe, Kalangali, Mitundu, Mipalalyu, Makale, Mtakuja, Kayui, Busoswanoni, Mwamatiga, Itagata, Lulanga, Doroto, Msisii, Kahomwe, Kitaraka, Kazikazi, Ibomboda, Itigi, Majengo, Damweru, Mgambo, Mkajenga, Katumba, Ipande, Muhanga na Kianchu. Ninataja Makusudi ili muelewe jinsi sisi tulivyo wadau wa Wizara hii, lakini waliowasilisha mada hapa sijui kama wanafanya kazi au hawafanyi; ninapenda kusema kuwa, miaka mitano sasa inakaribia kufika mwisho, lakini sijawahi kumwona wala kuona nia ya Waziri au Naibu Waziri kufika maeneo haya.

Hiyo mimi kidogo inanipa wasiwasi, vijiji vyote hivi nilivyovitaja, huduma muhimu kwa Wananchi hakuna. Kweli kuna baadhi ya vijiji vichache, lakini vilivyo vingi viko hoi. Pia rasilimali inayotoka katika mapori haya ni mchangiaji wa fedha katika Mfuko wa Hazina, maana hizi zipo chini ya Idara ya Wanyamapori. *Tanzania Wildlife Protection Fund* ipo pale, lakini hatujaona jitihada za kutosha kuweza kusaidia Wananchi wetu. Sichelei kutounga mkono hoja, lakini ninaeleza kilio change, mara nyingine ninachelea kusema niunge mkono hoja kwa kazi gani! Kwa kipi hasa niunge hoja mkono! Kama kuna nia basi tunashirikiana katika kuhakikisha yale yanayowasilishwa na Serikali mbele yetu, tunayafikiria kwa manufaa ya Wananchi wetu ili waweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninasikitika sana kuwa vijiji vyangu nilivyovitaja vyote bado havijafikiwa kupatiwa huduma za kutosha; hakuna shule za kutosha, hakuna maji salama na hata maji ya kawaida kwa ajili ya mifugo na Wananchi wenyewe; na pia hakuna zahanati za kutosha na barabara siyo nzuri. Kwa hiyo, nigeiomba Wizara hii itusaidie.

Kana kwamba haitoshi, mwaka 2007, *Tanzania Wildlife Protection Fund* ilitenga shilingi milioni 250 kwa ajili ya kukarabati Bwawa la Kijiji cha Rungwa, ambalo lilivunjwa na maji. Hao watu, baada ya kutenga hizo fedha waliahidi kutenga fedha kila mwaka ili waweze kukamilisha hili lengo lakini hawakuendelea na bwawa lile mpaka leo liko vilevile. Sura ya kijiji kile imebadilika maana kama kulikuwa na bwawa pale na watu wanavua samaki na wananyama wanakuja kunywa maji, wanyama pori na wanyama wengine, halafu kuna bustani na watu walikuwa wanachota maji ya kunywa pale, leo hakuna bwawa kama lile, *definitely* sura ya kijiji inabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajitahidi sana kwa upande mwingine kupata visima, lakini maisha ya watu wa Rungwa hayawezi kuwa sawasawa kama yalivyokuwa miaka ya nyuma. Watu wa kawaida tulifikiri kuwa sasa tunasonga mbele, lakini bahati mbaya sana tunarudi nyuma. Mimi ningomba kupata majibu juu ya suala hili kuwa hizi fedha

zilikwenda wapi na mikakati gani ipo mpaka sasa ya kuweza kuwarejeshea Bwawa hilo Wananchi wa Kijiji cha Rungwa.

Tuna migogoro ya mipaka kama nilivyosema kwamba, mipaka yetu ni ileile Mwenyezi Mungu alivyoiumba, tuna kilomita za mraba laki tisa na kitu, lakini maeneo yetu hatujayaaainisha vizuri. Mwaka 2000, baada ya kilio kikubwa cha Wananchi wa Kijiji cha Goroto, Tarafa ya Itigi, walikuwa wana tabu kubwa sana, lakini Serikali iliwasikiliza ikaamua kuwa wasogeze mpaka kwa kiasi. Nadhani ilikuwa kama takriban kilomita kumi hivi kufikia Kambi ya Mkaa na Wananchi waliishukuru sana Serikali. Alikuwepo dada yangu Mama Zabein Mhita, wakati huo alikuwa Waziri bahati mbaya nimesahau Wizara, lakini alikuja pale akaona kilio hicho cha Wananchi, alirudi na bahati nzuri wakaja kulimaliza wakati anaingia Mheshimiwa Maige hapa wakawa wametanzua na Wananchi wakafurahi sana, lakini walikuwa na taratibu ya kupita maeneo haya na kujua shida za Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio kikubwa kikabaki kile cha Lulanga, nina kumbukumbu nyingi tu katika Wizara hii ambazo nimeandika kuwaomba watusaidie juu ya hiki kijiji. Kijiji hiki kilikuwa ni Kitongoji halafu kikapandishwa hadhi kuwa kijiji kamili, lakini kipo ukingoni kabisa na hifadhi. Sasa hawa watapanua vipi shughuli za Halmashauri ya Kijiji; watafanya vipi? Ninaomba majibu kutoka Wizara hii ili iweze kutusaidia hawa Wananchi waweze kuishi kama wenzao wa Doroti na hawako mbali.

Sasa wanapoona wenzao wamefanikiwa katika maombi yao halafu hawa wamekwama ndipo wanapoona suala la ubaguzi kuwa kwa nini Serikali inabagua watu wa sehemu moja. Ningeomba hili suala liangaliwe na ningependa kupata majibu wakati wanaainisha suala hili.

Bado tuna kilio cha kulipa fidia kwa Wananchi wetu, kwa wale waliopoteza maisha yao, ndugu zao, fidia ya mimea na mazao yaliyoharibiwa na pia fidia ya mifugo. Ndiyo maana juzi nilisema tukiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori, labda kutakuwa na *authorities*, watakaokuwa

karibu na Wananchi waweze kuona kama watawasaidia. Ninaposikia kilio cha hifadhi zingine katika maeneo ya Kaskazini ya nchi, ninaona labda inaweza kuwa tabu hivyohivyo.

Inasikitisha wafiwa wanapoambiwa wanalipwa shilingi laki tano, sasa ninafikiri kama sikosei na mimea unaambiwa unalipwa shilingi laki moja kwa hekta, maana hekta ni heka mbili na nusu kama sikosei; *is it fair* kwa kazi hasa maana yule mtu utakavyomlipa vile atafanya nini ndiyo kweli fidia halisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri kuwa labda nipendekeze iwe kama ni fidia ya maisha ya binadamu walau shilingi milioni tano, maana pesa nyingi sana zinafujwa kwenye rasilimali hizi. Sasa kwa nini Mwananchi asiweze kulipwa; mtu amepoteza mkewe, amepoteza mumewe, mke alikuwa amekwenda kukata kuni; kwa nini alipwe fedha kidogo shilingi laki tano? Tembo wale kumetokea majangili ndani ya Hifadhi kule wanakimbia na wanakimbilia kwenye vijiji huku wanakuja kuharibu mazao ya binadamu sasa ni kosa la nani?

Ikiwezekana katika mazao wawe wanaangalia hali halisi ya bei ya soko pamoja na mifugo; huyu ng'ombe akipelekwa mnadani ni shilingi ngapi. Katika suala hili la mifugo ndiyo kabisa maana ile *reporting system* pale mpaka huyo bwana aje, ng'ombe ameshaoza na hawezi kuthaminiwa tena.

Mimi yananisibu hayo katika Jimbo langu na siwezi kuacha kusema, nitasema tu kila siku, Wizara hii bado haijatatendea haki. Ninaunga mkono hoja hii huku nikiwaomba kuwa wakimaliza shughuli iliyoko hapa na tukapitisha, basi waje waone maeneo haya kwa nini wenzao walikuwa wanakuja wao hawaji? Kwa nini wajikite kwenye maeneo ya Kaskazini kwenye hoteli kubwa na sisi watu ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Lwanji. Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Missanga.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia ingawa nilikuwa sijajiandaa vizuri, lakini kwa heshima uliyonipa niseme machache.

La kwanza, kwa muda mrefu katika Bunge hili nimekuwa nikieleza tatizo la ndege waharibifu. Ninalazimika kusema hilo kama wenzangu wanavyozungumza pamba, wengine kama wanavyozungumza tumbaku, wengine nazi na mimi ninalazimika kuzungumzia suala la ndege waharibifu.

Viongozi Wakuu wote waliokuja Singida; Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, moja ya kero ambayo wanaambiwa kila siku ni wale ndege waharibifu. Kuna kweleakwelea na kuna wale wa rangi ya kijani wale sisemi kama Yanga hapana, wa kijanikijani hivi ambao wanapendeza, ninadhani Wazungu wanawaita *Lau birds* kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege hawa wanaathiri sana jitihada za Wananchi za kilimo, wanaharibu mimea na hata zile mbegu zikipandwa wanafukua, mtama ukishaanza kuota wanakula, sasa ni tatizo la muda mrefu. Miaka ya 2003, nilikwenda Wizara ya Kilimo nikalieleza hili na Wizara ikakubali kuunda Tume, Tume ambayo ilikwenda Singida katika vijiji mbalimbali na kuangalia ukweli wa jambo hili na kwamba wachukue hatua ambazo wanaweza kuchukua ili kunusuru jitihada za Wananchi ambazo zinafanyika kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalazimika kulizungumzia hili kwa sababu ni kero, mimi nikifika kule hakuna jambo nitakaloulizwa ni hili, pamoja na wanyama wakali. Sasa ile Kamati ilishauri katika hatua za mwanzo, Wananchi waruhusiwe kuwavuna wale ndege kwa sababu ipo *burn* ambayo ilitengenezwa na *International Organization*, inayohusika na mambo haya, Mheshimiwa Waziri na Msaidizi wake watakuwa wanafahamu. Wakasema kuwa, wakati Wizara ikijitahidi kuhangaika na *International Organisation*

kuondoa ile *burn*, Wananchi waruhusiwe kuwavuna. Jambo la kusikitisha, baada kuwaambia Wananchi hali hiyo wakaanza kuwavuna, mwaka jana Mwananchi wangu mmoja Msukuma alikutwa na wale ndege amewavuna akakamatwa na Askari wa Maliasili na kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule akakubali, unajua ndugu zangu hawa tena akaambiwa umekamatwa akasema ndiyo, hana njia nyingine akapigwa miaka mitano, niliona uchungu sana. Nilikwenda nikazungumza na Mkuu wa Mkoa, ikaonekana *process* ni ndefu, nikaamua kulipa *fine* ambayo alikuwa ametozwa ama afungwe au alipe *fine*, mimi binafsi kwa kuona huruma kwa sababu nilishawaambia matokeo ya Wizara kuwa mnaweza mkawavuna, nimewaambia halafu ikatokea wakakamatwa na kufungwa, nimelipa ile *fine* ambayo ilikuwa inatakiwa, shilingi laki tatu au laki mbili na nusu. Ni jambo la kusikitisha; hivi tunapokuja humu Bungeni tunaeleza matatizo ya Wananchi toka mwaka 2003 ninalizungumza hili mpaka leo Serikali kwa sifa hiyo ya Serikali sikivu iko wapi?

Hiyo *burn* ambayo inasemekana inashughulikiwa hajishughulikiwa, sasa Wananchi wanateseka, wanafungwa na kadhalika. Tatizo ni kubwa, kwa sababu linaharibu mazao ya Wananchi, mazao ya biashara, pamoja na mazao ya chakula. Naomba sana, leo iwe mara yangu ya mwisho; vinginevyo na mimi itabidi nije na hoja binafsi kama sitapata jibu la maana kuitaka Serikali ichukue hatua huko. Ninadhani ndiko tutakakoelewana, kwa sababu sisi wengine ni *waungwana rahim*, hatupendi mambo ya vurugu, lakini tukifika mahala kama ni hivi kwa maslahi ya Wananchi wetu ambao wametuleta humu ndani, nitalazimika kuleta hoja binafsi juu ya tatizo hilo.

Burn iliyowekwa ya ndege hawa iondolewe ili Wananchi wasafirisha nje ya nchi, lakini pia *burn* iliyowekwa Wananchi ambao wanawavuna ama ni kwa kula au kwa shughuli yoyote, nayo iweze kuruhusiwa, hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii, baadhi ya Waheshimiwa hapa wamezungumza sana kuhusu Utalii; ni kweli mbuga za wanyama, wanyama sijui na nani, sawa, lakini hatuwezi kuwa *innovative* tukagundua utalii mwingine ambao unaweza kufanyika katika nchi yetu. Tuendeleo tu kuwa na wanyama, tumeona babu zetu wamefanya, baba zetu wamefanya na sisi tunaendelea kufanya na wengine wanaitwa kizazi kipya na kadhalika. Ninadhani kuna haja ya Serikali kuwa *innovative*, ni maeneo gani mengine ambayo tunaweza kufanya katika suala la utalii.

Kwa mfano, kule Singida wale ambao mmefika kule, kuna majabali kwa Kinyaturu tunaita *ng'ongo*, sasa sijui ni nani atanitafsiria hapa; yaani ni milima na majabali makubwa ambayo yamepandana. Mimi nina hakika hawa wenzetu wanaotoka nje hawana kitu kama hicho na wangependa kuona kitu kama hicho. Bahati nzuri sana, Mheshimiwa Naibu Waziri anajua *ng'ongo* maana yake nini, mtafsirie boshi wako na itafsirie Serikali *ng'ongo* maana yake nini. Wewe unazijua zaidi maana hata kule kwako zipo nyingi, mimi kwangu zimejaa, kwa Mheshimiwa Tundu Lissu zimejaa na kadhalika. Ninashauri tubadilike tusing'ang'anie utalii ambao tumeurithi, tuangalie na njia nyingine ambazo tunaweza kupata utalii.

Mimi huwa bado ninakereka sana kuwa bado Serikali yetu ya Tanzania haijajimarisha katika kutangaza vivutio vya utalii. Suala la Kenya bado linatawala kule nje, ukifika kule unaangalia TV unaona wanatangaza habari za Kenya. Mimi sioni kama kuna tangazo la habari ya Tanzania, unakaa pale miezi miwili mpaka mitatu, hakuna lolote linalozungumzwa kuhusu Tanzania wala magazeti hayazungumzi kuhusu Tanzania. Inanikera sana mimi; hivi wataalamu hawa aliokuwa anasema mwenzangu wapo na Serikali yote hii hivi haiwezi kweli kujitahidi kuangalia namna ya kutangaza zaidi habari za utalii nje ya nchi ili tuondokane na hii kasumba ya Kilimanjaro iko Kenya sijui na nini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa sana lakini ninaendelea kuisisitiza kuwa, ni lazima tuwe na mikakati ya kutangaza vyanzo vyetu vya utalii. Mheshimiwa Lwanji,

alikuwa anazungumzia wanyama wakali ni tatizo kama nilivyosema, fidia bado haitoshi, madhara yanayotokana na wanyama hawa wakali; simba, tembo na kadhalika ni makubwa sana. Hiyo ni moja ya kero ambayo Mheshimiwa Rais, alipokuja katika Kijiji cha Mtunduru, Wananchi walimwambia hiyo kitu. Ninasema ni bahati mbaya sana, hakuna *action* ambayo inachukuliwa na Serikali. Sasa ukishamwambia mpaka Rais, jamani akasema nimesikia sasa ninyi wasaidizi wake si ndiyo mumsaidie Rais? Sasa kwa nini hamumsaidii; msaidieni Mheshimiwa Rais na ninyi mtakuwa mmejisaidia wenyewe.

Migogoro ya mipaka ni mingi sana; ipo migogoro ya mipaka kati ya Hifadhi na Wananchi na kadhalika, hili nalo ni kero ya muda mrefu. Naiomba sana Serikali yetu hii, tuondoe migogoro kati ya Wananchi na Wananchi. Sitaki kuzungumzia sana mgogoro huu wa Loliondo ni wa muda mrefu na umesemwa sana, madhara yake mpaka Viongozi wetu Wakuu wameanza kuwa *implicated* na habari kama hizi; hivi kuna tatizo gani la kutokuchukua hatua thabiti ya kuhakikisha kuwa migogoro hii tunaiondoa.

Naomba maeneo yote kwa sababu ni kila mahala, tunayo Arusha ndiyo kabisa, Manyara ndiyo kabisa, kwa hiyo, naomba sana hili suala la migogoro ya mipaka liweze kurekebishwa ili kuwe na amani kati ya Hifadhi na Wananchi katika vijiji vyao na Wananchi walewale ndiyo wanaweza kuwa walinzi wazuri sana wa Hifadhi zetu hizi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Kengele ya pili Mheshimiwa.

MHE. MOHAMMED H. MISSANGA: Ya pili, Yanga oyee ninashukuru kwa kunipa nafasi Yanga Bingwa. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Missanga, sasa unavunja Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja kutoka Ofisi ya Mheshimiwa Spika kuhusu Sherehe za Mei Mosi zitakazofanyika katika Uwanja wa Jamhuri Mjini Dodoma. Nimeombwa niwatangazie na kuomba kuwaalika rasmi Waheshimiwa Wabunge wote, kushiriki katika Sherehe za Mei Mosi zinatakazofanyika Uwanja wa Jamhuri kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa nane mchana.

Katika ratiba hiyo ya shughuli inaonesha mwanzo wa matukio ni saa 12.30 asubuhi na tukio hilo la kwanza ni kukusanyika kwa wafanyakazi katika eneo la Viwanja vya Bunge ili kujipanga kwa mpangilio wa Vyama. Sasa hiyo saa 12.30 asubuhi, kama Wabunge tutashiriki sijui tutajipanga kwa mpangilio wa Chama gani cha Wafanyakazi, ninadhani kwa mantiki hiyo ndiyo maana tumealikwa tuanze kuhudhuria saa mbili katika Uwanja wa Jamhuri. Vinginevyo, ninadhani sherehe zitakazofuata basi Waziri mwenye dhamana aone na Wabunge ni Wafanyakazi bora kwenye Majimbo yao, utaratibu wa kuwatunza Waheshimiwa Wabunge nao uandaliwe.

Hilo ni tangazo la mwaliko, kwa hiyo, watakaokuwepo hapa Dodoma kwa siku ya kesho, tunaalikwa kushiriki katika shughuli hiyo ya Mei Mosi. Baada ya kumaliza shughuli hizi kwa muda uliopangwa kwa siku ya leo, ninaomba sasa niahirishe shughuli za Bunge na niwaombe tukutane keshokutwa msije wengine mkaja kesho, kesho ni siku ya mapumziko kitaifa, kwa hiyo, tutakutana keshokutwa saa tatu kamili katika Ukumbi huu kama ilivyo kawaida ya Kanuni zetu za Bunge.

*(Saa 1.41 Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,
Tarehe 2 Mei, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*